# SIMULIZI ZA VIRUSI VYA UKIMWI/UKIMWI ZINAVYODHIHIRIKA KATIKA NYIMBO ZA JAMII ZA KENYA KIBAADAUSASA

**NA**

**ROTICH, ALEXANDER KIPKEMOI**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Kitivo cha Fani na Sayansi za Kijamii ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamifu katika Kiswahili**
**Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,**
**Chuo Kikuu cha Moi**

**SEPTEMBA, 2018**

# UNGAMO NA IDHINI

## UNGAMO

Hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

…………………………….. ……………………

**Rotich, Alexander Kipkemoi** Tarehe

SASS/DPHIL/KIS/01/2010

## IDHINI

Tasnifu hii ya uzamifu imewasilishwakwa idhini yetu kama wasimamizi wa chuo.

…………………………….. ……………………

**Prof. Issa Y. Mwamzandi** Tarehe

Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Kabianga.

…………………………….. ……………………

**Dkt. Mosol Kandagor** Tarehe

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi.

# TABARUKU

Kwa mjukuu wetu wa kwanza Sydney Kibet, watoto wetu Chepkorir, Chepng'eno na Kiplang'at ninawapokeza mwenge huu wa elimu.

# SHUKRANI

Ningependa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Jalali kwa kunijalia uzima katika kipndi chote nilipokuwa nashughulikia mradi huu. Ninaamini kwamba, bila ya majaaliwa yake singefikia umbali huu. Shukurani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu waadhama, Prof. Issa Mwamzandi na Dkt. Mosol Kandagor. Sitamsahau marehemu Prof. Naomi Shitemi, ambaye alikuwa mmoja wa waelekezi wangu kabla ya ziraili kuitwaa roho yake. Nawashukuru kwa kunielekeza, kunishauri na kunihimiza. Subira na himizo kutoka kwenu zilikuwa msukumo kwangu wa kuendelea na mradi huu, nilipoonyesha dalili za kutamauka. Ahsanteni kwa msaada wa vitabu, makala na kazi nyinginezo nyingi zilizochangia kufanikisha tasnifu hii.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wengine wa Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi wakiwemo Prof. Nathan Ogechi, Dkt. Allan Opijah, Dkt. Vifu Makoti, Dkt. Mbwarali, Kenga Mumbo, Mukuria na Munywa. Mlinipa ushauri ulionifaa. Sitasahau kuwashukuru wahadhiri wenzangu katika Chuo Kikuu cha Kabianga. Nawashukuru Dkt. Simiyu Kisurulia, Dkt. Muindu, Dkt. Salim Sawe, Dkt. Anne Lang'at, Dkt. Benedicta Tabot na Anne Jose kwa kunihimiza katika safari hii ya kiakademia.

Nawashukuru wazamifu wenzangu tuliokuwa pamoja katika darasa la Uzamifu: Nilson Opande, Joy Mocho na Anne Kawa. Safari hii ya usomi tuliianza pamoja, tukafaana kwa hali na mali. Mliniauni kwa mengi yakiwemo vitabu, mawazo na usafiri. Ningependa pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Dkt. Kipng'etich Kirui wa Chuo Kikuu cha Moi kwa kuipitia tasnifu hii na kuifanyia uhariri. Shukurani pia ziwaendee marafiki wangu wa dhati kwa mhimizo, msukumo na ushauri. John Korir, Kiplang'at Chebose, Joseph Marindany na Richard Mibey wa Chuo cha Ualimu cha

Kericho na Shule ya Sekondari ya Wavulana, Chepwagan mtawalia ahsanteni kwa kuwa marafiki wa kutegemewa.

Shukrani za kipekee ziende kwa rafiki yangu Fredrick Keter wa Chuo cha Anuai cha Eldoret kwa kunitengea chamba nyumbani mwake ambamo nilistakimu na kuifanyia kazi hii kila nilipokuja Eldoret. Kwa kufanya hivi, uliniepusha na gharama ya kukodisha vyumba hotelini. Mungu akubariki sana. Shukrani nyingi pia ziwaendee Erick Obade na Charles Ouma kwa kukusanya, kunakili na kutafsiri nyimbo za Kijaluo. Aidha, Irene Olding'di Kitipa na Joseph Nkoitoib shukrani za dhati kwa kushughulikia nyimbo za Kimaasai

Pamoja na hayo, shukurani zingine ni kwa familia yangu. Mke wangu Rachel, umekuwa rafiki wa karibu ahsante kwa kuwa na subira nami. Watoto wangu Chepkorir, Chepng'eno na Kiplang'at shukurani kwa kuwa watoto wazuri, wenye nidhamu. Mlikuwa na subira kwangu, licha ya kutumia muda mwingi kusoma badala ya kuwalea. Chepkirui, nakushukuru mwanangu kwa kunipa msukumo. Tulisoma pamoja hadi usiku wa manane. Wazazi wangu Rebecca Tuei, Ziporah Tuei na Kiprotich Tuei, nawashukuru kwa kunilea vyema na kunipeleka shule. Nawashukuru ndugu zangu John, Alice, Jonathan, Emily, William, Samuel, Hellen, Joseph na Caren kwa mapenzi na mhimizo kutoka kwenu. Yote tisa, ya kumi ni kuwashukuru watu wote ambao kwa njia moja au nyingine, walichangia ufanisi wa tasnifu hii. Mungu awabariki nyote.

# ABSTRACT

It is now over thirty years since the emergence of the Human ImmunodeficiencyVirus/Acquired Immune Deficiency Syndrome, popularly refered to as HIV/AIDS pandemic, an epidemic which has caused untold human suffering globally. Governments worldwide have put in place various measures which aim to control the spread of the disease which, to date, has no cure. The purpose of this study was to investigate the role of cultural and Kiswahili songs in the fight against HIV/AIDS in Kenya. The main aim of the research was to analyze the role of society in interrogating the subject of HIV/AIDS through indigenous knowledge and wisdom. More specifically, the study examined how the song genre is used as a window through which the epidemic is conceptualized and the ensuing narratives that are assigned to it. The study was guided by the theory of postmodernism and in particular Michel Foucault's ideas on discursive formations which have through the ages enabled institutions to wield power and domination by excluding the mad, the poor, the criminal, the deviant and the sick. Similarly, his argumentthat, discourse is always inseperable from power because it is the governing and ordering medium of every institution is applied. Discourse determines what is possible to say, the criteria for 'truth', who is allowed to speak with authority and where such speech can be spoken. Guided by this view, this study analyzed grand andminor narratives inherent in the selected songs hence showing how they speak about deviance, warnings, comfort and stigma. Data was collected through observation, focused groups discussions and interview methods and was drawn from selected artists and media stations.Twenty three song texts are purposely selected, thirteen of which are in Kiswahili, four in Kalenjin, four in Dholuo and two in Maa languages respectively. Kalenjin songs were transalated by the researcher since he belongs to the speech community. Maasai and Luo songs were translated with the assistance of selected speakers from the respective communities. The songs collected were analyzed using explanatory and descriptive methods. The study found out that the songs under examination are a repository of the breath of indigenous knowledge as well as an invaluable source of an alternative way of fighting HIV/AIDS. It is the researcher's belief that the epidemic has been re-constructed by the society since singers have a unique way of rendering the subject. Since scientific methods have not fully succeeded in the fight against HIV/AIDS, the study advocates for such a multi-sectoral approach in combating it. Such an approach advocates for the use of cultural methods, songs included, together with scientific methods. From the findings of this study, it is recommended that further research be done based on songs from other communities and other genres of oral literature so as to bring to the fore narratives on HIV/AIDS and what they portend in the fight against it.

# IKISIRI

Ni zaidi ya miaka thelathini tangu janga la Virusi Vya Ukimwi/ UKIMWI almaarufu VVU/UKIMWI liibuke na kusababisha madhara si haba kwa wanajamii kote ulimwenguni. Serikali za mataifa kote ulimwenguni zimeweka mikakati mbalimbali inayolenga kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu ambao mpaka sasa hauna tiba. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza mchango wa nyimbo za Kiasili na za Kiswahili katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI. Utafiti ulilenga kuchanganua nyimbo husika ili kubainisha namna wanajamii wanavyozitumia lugha kiuimbaji katika kulijadili suala hili huku ukibainisha mtazamo wao kuhusu ugonjwa huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baadausasa hasa mawazo ya Michel Foucault katika kuhakiki jinsi miundo na taratibu za kijamii zilivyowezesha asasi kuwa na mamlaka na udhibiti kwa kuwatenga wanajamii wengine hasa wendawazimu, wangonjwa, wachochole, wahalifu na waliokiuka maadili. Anahoji kuwa, daima diskosi haiwezi kutenganishwa na mamlaka kwa sababu ndicho kinachotawala na kuamuru au kuongoza njia za mawasiliano za kila taasisi. Huamua kile kinachoweza kusemwa, vigezo vya ‘ukweli’, nani ana mamlaka ya kusema na ni wapi usemi wa aina hiyo unaweza kutokea. Kwa kuongozwa na mtazamo huu utafiti huu ulichanganua simulizi kuu na simulizi ndogo za VVU/UKIMWI zilizomo kwenye nyimbo kwa kubainisha namna zinavyoweza kupinga ukiukaji wa maadili, kutoa maonyo na faraja pamoja na kukuza au kuudumaza unyanyapaa. Data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu za utazamaji, mijadala ya makundi teule na usaili wa ana kwa ana kisha kuripotiwa katika tasnifu hii zilitokana na kazi zawasanii walioteuliwapamojana vituo vya utangazaji. Nyimbo ishirini na tatu ziliteuliwa kimakusudi. Nyimbo kumi na tatu zilikuwa za Kiswahili, nne zilikuwa za Kikalenjin, nne zilikuwa za Kijaluo na mbili zikiwa za Kimaasai. Mtafiti alizitafsiri nyimbo za Kikalenjin kwa kuwa yeye ni msemaji wa lugha husika.Aidha, mbinu ya sampuli kimaksudi ilitumiwa kuwateua wasemaji wa Kimaasai na Kijaluo ili kutafsiri nyimbo kutoka jamii husika. Mbinu za uchanganuzi zilihusisha maelezo na ufafanuzi. Matokea ya utafiti huu ni kwamba, nyimbo katika muktadha wa baadausasa zina simulizi kuu na simulizi ndogo zinazolenga kujadili suala la VVU/UKIMWI. Aidha utafiti ulibainisha jinsi nyimbo zinavyoweza kupindua nguvu za awali au zilizokuwa zinatawala kama zile za kisayansi na wanajamii kuhusu VVU/UKIMWI na waathiriwa. Utafiti huu unachangia tafiti zilizotangulia hasa ikizingatiwa kuwa, nyimbo zinaweza kuwa njia mbadala inayoweza kutumiwa kukabiliana na janga la UKIMWI. Ni rai ya utafiti kwamba jamii imehodhi simulizi sadifu za ugonjwa huu kwani waimbaji wana njia zao mahususi za kuujadili. Kwa kuwa mbinu za kisayansi hazijafaulu kabisa katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI, kuna haja ya kutumia mbinu anuwai zikiwemo za kitamaduni kama vile nyimbo pamoja na mbinu za kisayansi. Kutokana na utafiti huu, inapendekezwa kwamba, tafiti zaidi zifanywe katika nyimbo za jamii nyingine pamoja na katika vipera vingine vya fasihi simulizi ili kubainisha simulizi za VVU/UKIMWI zilizomo pamoja na umuhimu wake katika vita dhidi yake.

# YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ..................... ii
SHUKRANI ..................... iv
ABSTRACT ..................... vi
IKISIRI ..................... vii
YALIYOMO ..................... viii
MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO ..................... xiii
MAELEZO YA ISTILAHI ..................... xiv
**SURA YA KWANZA ..................... 1**
**MISINGI YA UTAFITI ..................... 1**
1.1 Utangulizi ..................... 1
1.2 Usuli wa Suala la Utafiti ..................... 1
1.2.1 Nyimbo katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI ..................... 4
1.3 Suala la Utafiti ..................... 8
1.4 Malengo ya Utafiti ..................... 9
1.5 Maswali ya Utafiti ..................... 9
1.6 Umuhimu wa Utafiti ..................... 9
1.7 Upeo na mipaka ya Utafiti ..................... 11
1.8 Mbinu za Utafiti ..................... 11
1.8.1 Utangulizi ..................... 11
1.8.2 Utafiti wa Maktabani ..................... 11
1.8.3 Sampuli ..................... 12
1.8.4 Vifaa vya Utafiti ..................... 13
1.8.4.1 Runinga na Tepu Rekoda ..................... 13
1.8.4.2 Uwasilishaji wa Data ..................... 13
1.8.4.3 Uchanganuzi wa Data ..................... 13
1.9 Hitimisho ..................... 14
**SURA YA PILI ..................... 15**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA** ..................... 15
2.1 Utangulizi ..................... 15
2.2 Vipengele Vielekezi Vinavyochangia Kuenea kwa VVU Nchini Kenya ..................... 15
2.2.1 Umaskini ..................... 15
2.2.2 Maambukizi kupitia kwa Ngono/ Magonjwa ya Zinaa ..................... 16

2.2.3 Athari za Pombe na Dawa za Kulevya ........ 18
2.2.4 Mizozo na Vita vya Kikabila ........ 19
2.2.5 Dhana na Desturi za Kitamaduni ........ 21
2.2.6 Dini ........ 28
2.2.7 Wanajamii Walio katika Hatari ya Kuambukzwa VVU ........ 29
2.3 Athari za VVU/UKIMWI Nchini Kenya ........ 29
2.3.1 Athari za Kijamii na Kiuchumi ........ 29
2.3.2 Mayatima na Watoto wasiokuwa na Usalama ........ 32
2.4 Mikakati ya Serikali katika Vita dhidi ya VVU/UKIMWI ........ 33
2.4.1 Uongozi na Uratibu wa Programu zinazohusu VVU/UKIMWI ........ 33
2.4.2 Mikakati iliyopo Sasa ........ 36
2.4.3 Huduma za Unasihi na Upimaji wa Hiari (UUH) ........ 37
2.4.4 Kuzuia Uambukizaji kutoka kwa Mama hadi kwa Mtoto ........ 38
2.4.5 Tahadhari za Mfumo wa Afya na Usalama wa Damu ........ 39
2.4.6 Kuhimiza Matumizi ya Kondomu ........ 40
2.4.7 Kutibu Magonjwa ya Zinaa ........ 40
2.4.8 Kuhimiza Utambuaji ........ 41
2.4.9 Kuwatibu na Kuwatunza Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI ........ 42
2.5 Hali ya VVU/ UKIMWI Nchini Kenya ........ 44
2.5.1 Maambukizi ya VVU Miongoni mwa Wanawake na Wanaume ........ 45
2.5.2 Maambukizi ya VVU/UKIMWI Kimaeneo ........ 45
2.5.3 Maambukizi ya VVU/UKIMWI na Viwango vya Elimu ........ 46
2.5.4 Maambukizi Miongoni mwa Walio kwenye Ndoa ........ 47
2.5.5 Maambukizi na Suala la Tohara kwa Wanaume ........ 48
2.5.6 Maambukizi Miongoni mwa Walioshiriki Ngono ........ 48
2.5.7 Maambukizi na Matumizi ya Kondomu ........ 49
2.5.8 Maambukizi Miongoni mwa Walio katika Hatari ya Kuambukizwa ........ 50
2.5.9 Maambukizi kutoka kwa Mama hadi kwa Mtoto ........ 50
2.5.10 Maambukizi na huduma za Afya ........ 51
2.5.11 Viwango vya Ufanisi Vilivyoafikiwa ........ 52
2.6 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo na Makabiliano ya UKIMWI ........ 54
2.6.1 Nyimbo kama njia ya Kuwaunganisha Watu ........ 54
2.6.2 Nyimbo kama njia ya kukabiliana na UKIMWI ........ 55
2.6.3 UKIMWI na Ulemavu ........ 58

2.6.4 Uigizaji kama njia ya kukabiliana na UKIMWI ... 59
2.6.5 Dini, Utamaduni na UKIMWI ... 61
2.7 Misingi ya Nadharia ... 65
2.8 Hitimisho ... 70
**SURA YA TATU ... 71**
**MIKAKATI YA KIBAADAUSASA KATIKA NYIMBO ZA VVU/ UKIMWI 71**
3.1 Utangulizi ... 71
3.2 Mikakati Inayopinga Usasa ... 71
3.3 Ukiukiaji kama Kipengele cha Ubaada Usasa ... 73
3.3.1 Ukiukiaji na Kimtindo ... 74
3.3.2 Ukiukiaji wa Kimaudhui ... 74
3.4 Udhihirikaji Wa Mwingilianomatini katika Nyimbo za Kibaadausasa ... 78
3.4.1 Dhana ya Mwingilianomatini ... 78
3.4.2 Mbinu ya Unukuzi/ Kiwango cha Sanaa na Miktadha ... 79
3.4.3 Mbinu ya Urejelezi ... 82
3.4.4 Mwingilianomatini Kiwango cha Sanaa ... 85
3.5 Ukosefu wa Mshikamano katika Nyimbo za Kibaadausasa ... 87
3.6 Kukosekana Kwa Uaushi ... 90
3.6.1 Misimu/Misemo Inayoonyesha Kukosekana kwa Uaushi ... 92
3.7 Hitimisho ... 95
**SURA YA NNE ... 96**
**NYIMBO NA SUALA LA UNYANYAPAA ... 96**
4.1 Utangulizi ... 96
4.2 Maana ya Unyanyapaa ... 96
4.3 Athari za Unyanyapaa ... 97
4.4 Aina za Unyanyapaa ... 98
4.5 Nyimbo na Simulizi kuhusu Unyanyapaa ... 100
4.6 Hitimisho ... 126
**SURA YA TANO ... 127**
**UKIMWI NA SUALA LA MATABAKA ... 127**
5.1 Utangulizi ... 127
5.2 Dhana ya Utabaka ... 127
5.3 Matumizi ya uwezo wa Kifedha ... 128
5.4 VVU/UKIMWI na Suala la Mamlaka/Hadhi ... 135

5.4.1 Tofauti za Kiumri ........ 136
5.4.2 VVU/UKIMWI na tofauti za Kihadhi ........ 141
5.5 Hitimisho ........ 147
**SURA YA SITA ........ 149**
**NYIMBO ZINAZOHUSU UKIMWI NA MIKTADHA MINGINE YA KIJAMII ........ 149**
6.1 Utangulizi ........ 149
6.2 Dhana ya Jinsia ........ 149
6.3 KIMWI na Suala la Ujinsia ........ 150
6.4 Nyimbo na Malalamishi ........ 161
6.4.1 Malalamishi juu Ubaya wa UKIMWI ........ 161
6.4.2 Malalamishi kuhusu Ulevi wa Pombe ........ 166
6.4.3 Malalamishi kuhusu tamaa ........ 168
6.5 Simulizi za Tahadhari ........ 170
6.5.1 Tahadhari kuhusu Ulevi ........ 170
6.5.2 Tahadhari kuhusu Tamaa, Starehe na Anasa ........ 174
6.5.3 Tahadhari kuhusu Ngono bila Kinga au ya Kiholela ........ 176
6.5.4 Nyimbo na njia nyingine za kuepukana na UKIMWI ........ 179
6.6 Hitimisho ........ 182
**SURA YA SABA ........ 184**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 184**
7.1 Utangulizi ........ 184
7.2 Muhtasari wa Tasnifu ........ 184
7.3 Matokeo ya Utafiti ........ 185
7.4 Mchango wa Utafiti ........ 188
7.5 Mahitimisho ........ 189
7.6 Mapendekezo ........ 190
MAREJELEO ........ 191
VIAMBATISHO ........ 199
Kiambatisho 1: Mwongozo wa Mijadala katika Makundi Teule ........ 199
Kiambatisho cha 2: Kidadisi cha maswali kwa Hadhira ........ 200
Kiambatisho cha 3. Wasanii na Nyimbo ........ 201
Kiambatisho cha 4: Nyimbo za Kiswahili ........ 202
Kiambatisho cha 5: Nyimbo za Kikalenjin ........ 223

Kiambatisho cha 6: Nyimbo za Kijaluo........................................................................228
Kiambatisho cha 7: Nyimbo za Kimaasai....................................................................231

# MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ANC** | Antenatal Clinic |
| **ART** | Mfumo wa kimatibabu unaozingatia matumizi ya dawa za kupunguza makali ya Ukimwi. |
| **ARV** | Dawa za kupunguza makali ya Ukimwi. |
| **CACC** | Constituency AIDS Control Committee |
| **KAIS** | Kenya AIDS Indicator Survey |
| **KMK** | Kutoshiriki ngono, kuwa Mwaminifu kwa mpenzi mmoja na kutumia Kondomu. |
| **Mshr** | Mshiriki |
| **NACC** | National AIDS Control Council |
| **NASCOP** | National AIDS Control Program |
| **PLWHA** | People Living With HIV and AIDS |
| **PRSP** | Makala kuhusu mikakati ya kupunguza umasikini. |
| **TY** | Tafsiri Yangu |
| **UKIMWI** | Upungufu Wa Kinga Mwilini. |
| **UMMM** | Uzuiaji wa Maambukizi kutoka Mama hadi kwa Mtoto. |
| **UUH** | Unasihi na Upimaji wa Hiari. |
| **VVU** | Virusi Vinavyosababisha Ukimwi. |

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Ubaadausasa**: Kipindi kinachohusishwa na ukiukaji wa kaida zilizozoeleka. Kwa mfano, katika fasihi andishi, wasanii hupuuza mbinu zilizozoeleka na kujaribu mbinu mpya za uandishi.

**Uhalisiwingi**: Aina nyingi za uhalisi kutokana na mitazamo tofauti tofauti.

**Ukoka**: Aina fulani ya nyasi inayomea na kutambaa ardhini. Huweza kukatika na kuanza kumea tena ilipokatikia.

**Upendelevu**: Utoaji wa fasiri au maana unotokana na kuongozwa na hisia.

**Ushabihikweli**: Ukweli unaotokana na maoni yanayofanana; ukweli ulio sawa.

**Simulizi kuu**: Maelezo yaliyozoeleka na yasiyobadilika. Husisitiza matumizi ya mitndo na mbinu zilizozoeleka. Hupinga matumizi ya mitindo mbinu za kimajaribio.

**Simulizi ndogo**: Maelezo yanayodhihirisha shughuli za kila siku jinsi zilivyo; hukiuka kaida zilizozoeleka na kuhimiza matumizi ya mitindo na mbinu mpya za kimajaribio hivyo kupinga simulizi kuu.

**Uwekaji sambamba**: Uwekaji wa vitu kwa namna inavyofanya vionekane kuwa sawa.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii,nimeangazia vipengele muhimu vya utafiti kwa lengo la kuweka msingi wa sura zitakazofuata. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, umuhimu wa utafiti, azma ya utafiti, nadharia tete, nadharia iliyoongoza utafiti, na hatimaye mbinu na vifaa vya utafiti.

## 1.2 Usuli wa Suala la Utafiti

UKIMWI ni janga ambalo limemhangaisha binadamu kwa zaidi ya miaka thelathini na kuleta machungu na masikitiko si haba. Juhudi nyingi zimefanywa na serikali za mataifa, mashirika yasiyokuwa ya serikali pamoja na watu binafsi ili kukabiliana nalo lakini nyingi zinaambulia patupu. Utafiti umeelekezwa kwenye juhudi hizi za kupigana na hili janga.

Ripoti ya pamoja ya Mpango wa Umoja wa Mataifa (UNAIDS,2008) kuhusu janga la UKIMWI ulimwenguni inabainisha kupungua kwa idadi ya vifo na maambukizi mapya katika mataifa mengi. Aidha ripoti hii inaonyesha kuongezeka kwa idadi ya watu wanaopata tiba ya kupunguza makali ya UKIMWI almaarufu ARVs. Hata hivyo inakisiwa kuwa, watu milioni thelathini na tatu (33) ulimwenguni wameambukizwa Virusi Vya UKIMWI (VVU). Kimaambukizi, mataifa yaliyoko chini ya jangwa la Sahara ndiyo yaliyoathirika zaidi ikilinganishwa na maeneo mengine. Kulingana na Barasa la Kitaifa la Kuzuia UKIMWI (NACC, 2000), mataifa hayo ya Afrika yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara huchangia asilimia 70% ya maambukizi kote ulimwenguni.Kenya nayo haijasazwa na janga hili la UKIMWI kwani ni mojawapo ya mataifa yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara.

Tangu kuibuka kwa ugonjwa huu miaka ya 1980, Kenya imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na VVU/UKIMWI. Kulinganana na (NACC, 2005), nchi hii ilitambuliwa kama mojawapo ya nchi ambazo zilionyesha kupungua kwa idadi ya walioambukizwa. Ripoti ya Kenya iliyowasilishwa kwenye kikao maalum cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu UKIMWI (NACC,2006) inaonyesha kuwa, maambukizi miongoni mwa watu wazima nchini Kenya yalipungua kutoka asilimia kumi (10%) katika miaka ya 1990 hadi asilimia saba (7%) mwaka wa 2003. Kupungua huku kwa viwango vya maambukizi kumehusishwa na sababu kadhaa zikiwemo kubadilika kwa watu kitabia na "maendeleo yasiyo na budi."Kulingana na NACC (2006) maendeleo yasiyo na budi yana misingi katika ukweli kuwa:

i. Wakati janga linapoendelea kukua, idadi kubwa ya watu hufa kutokana na magonjwa yanayohusiana na VVU na kwa hivyo utokeaji wa vifo huwa juu ukulinganishwa na kiwango cha maambukizi.
ii. Katika hatua za mwanzo mwanzo za janga, VVU kimsingi huenea miongoni mwa wanajamii walio katika hatari ya kuvipata na kuvieneza, kwa hivyo vifo vya walioambukizwa huenda vikapunguza kuenea kwa virusi.

Idadi kubwa ya Wakenya walio na VVU/UKIMWI wamo katika kitengo cha watu wazima walio na umri wa miaka 15-49 (NACC, 2005) ingawa kuna ongezeko la maambukizi nje ya watu wenye umri huu, hasa miongoni mwa watoto au wanawake, na wanaume walio na umri wa zaidi ya miaka hamsini (50) (NACC, 2008).

Amuyunzu–Nyamongo (2008) anaeleza kuwa vijana huathiriwa zaidi na ugonjwa huu wa UKIMWI kwa sababu ya kushiriki ngono ya mapema, jambo linalosababishwa na sababu za kiutamaduni, kijamii na kiuchumi. Anaongeza kuwa tatizo hili linafanywa changamano zaidi kutokana na wazazi, viongozi walimu na vijana kutojadili masuala

yanayohusiana na ngono katika miktadha ya mazungumzo ya kawaida. Vijana wamelikwepa tatizo hili la kimawasiliano kwa kuzungumzia masuala husika kupitia kwa nyimbo ambazo zinawasilisha hisia zao. Wasemavyo Barz (2006) na Rafiq (2008) vijana huvutiwa zaidi na nyimbo kuliko maandishi ya magazeti, mabango na mikutano kama vile makongamano au warsha.

Kijitabu cha data kuhusu hali ya VVU/UKIMWI nchini Kenya; Kenya HIV/AIDS Data Booklet, (NACC, 2005) kinabainisha kuwa, uambukizaji miongoni mwa watu wazima hawa ulikadiriwa kuwa katika kiwango cha asilimia sita nukta nne (6.4%) mwaka wa 2004, hii ikiwa upungufu wa asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) wa mwaka wa 2003. Aidha, kijitabu hiki kinaonyesha kuwa, kulikuwepo na wanawake wengi katika kitengo cha umri wa miaka 15-49 waliokuwa na virusi ikilinganishwa na idadi ya wanaume kwenye kitengo hicho. Hata hivyo mitalaa ya hivi punde inaonyesha kuwa, licha ya kupungua kwa kiasi kikubwa kwa maambukizi tangu miaka ya 1990, vita dhidi ya janga hili havijafaulu bado (Nyawira, 2008).

Kupungua kwa maambukizi kunamaanisha tu kuwa idadi ya watu wanaoambukizwa inapungua huku vifo vinavyosababishwa na UKIMWI vikiongezeka. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa, mbinu za kisayansi pekee hazijafaulu katika vita dhidi ya janga hili na hivyo kupelekea haja ya kuzingatia mchango wa mbinu mbadala za kukabiliana nalo. Mbinu hizo ni kama vile drama, ngoma na aina mbalimbali za nyimbo ambazo zinawashirikisha wanajamii wa viwango mbalimbali. Nyimbo, kwa mfano, zimenakiliwa kuwa na sifa ya kutoa tiba ya kisaikolojia kwa wale walioathirika na kuwapa matumaini ya kuendelea kuishi (Barz, 2006; Ahamadi, 2006).

### 1.2.1 Nyimbo katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI

Tangu kuibuka kwa janga hili, tafiti anuai kuhusu mchango wa nyimbo katika vita dhidi yake zimefanywa. Njogu (2003) anapendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa kukabiliana na masuala ya kiafya huku zikiburudisha. Anasisitiza kuwa sanaa huwa na dhima muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa afya nzuri hususan miongoni mwa vijana. Njogu anaendeleza maoni ya Tufte (2002) anayeeleza kuwa, mbinu ya Elimu-Burudani inaweza kutumiwa kwa ajili ya malengo mengi yakiwemo mawasiliano ya kiafya kama njia ya kuitikia uchangamano wa kijamii kiafya na nyanja nyingine za maendeleo zinazohitaji kushughulikiwa.

Shitemi (2012) anaeleza kuwa nyimbo za kuimbwa na kutendwa katika fasihi simulizi hutokea katika miktadha ya kijamii kama vile, kuzaliwa kwa mtoto, tohara, ndoa, mazishi na kazi. Anaeleza kuwa nyimbo zimetumika tangu jadi katika jamii za Kiafrika kwenye miktadha ya aina hii. Utafiti wangu ulichochewa na maelezo haya Shitemi, kwani VVU/UKIMWI ni mada inayohusishwa na jamii. Maelezo ya Shitemi hapo juu, yaliniongoza katika kutafakari kwamba, VVU/UKIMWI ni mada ambayo inaweza kujadiliwa kiuimbaji na kiutendaji katika viwango na miktadha mbalimbali ya kijamii. Katika utafiti huu, nimechanganua nyimbo zilizoteuliwa na kisha kubainisha namna simulizi ndogo ndogo za nyimbo zinavyoweza kutumiwa katika jamii kujadili mada za maonyo, faraja, maadili na unyanyapaa mintaarafu ya VVU/UKIMWI.

Kulingana na Garfias (2004), nyimbo zinazochimbuka kutokana na utamaduni wa wanajamii hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine huku mabadiliko yakifanyiwa nyimbo husika kadri miaka inapopita. Anaeleza kuwa, katika jamii za Kiafrika nyimbo ziliimbwa katika sherehe mbalimbali kwa malengo mbalimbali. Kwa

mfano, nyimbo zilizoimbwa katika mazishi kama vile Tero Buru miongoni mwa Wajaluo zililenga kumsifu aliyekufa, kuwafariji waliofiwa, kuwafanya watu wasilale usiku na kuelezea hisia za uchungu. Aidha, zilitumiwa wakati wa matakaso na kuwafukuza mapepo wabaya.

Garfias (kama hapo juu) anaendelea kueleza kuwa, nyimbo zina nguvu za kimawasiliano zinazoathiri maisha yetu na yale ya watu wengine. Akizungumzia utanzu wa nyimbo za injili, Garfias anadai na ninakubaliana naye kwamba, utanzu huu una hadhira kubwa kutokana na sababu kwamba, nyimbo hizi huchezwa katika idhaa ya taifa, vituo vya redio vya FM pamoja na vituo vya runinga nchini Kenya. Nyimbo za aina hii zinakuwa njia mwafaka ambayo kwayo jumbe nyeti au tata zinaweza kuwasilishwa kwa hadhira bila pingamizi. Utafiti wa Garfias ulinifaa licha ya kujikita katika nyimbo za injili pekee. Hii ni kwa sababu utafiti wangu ulishirikisha nyimbo za injili pamoja na za kitamaduni.

Ahmadi (2005) anaona muziki kama tiba lakini akimrejelea Ruud (1998) anaeleza kuwa tabibu wa kimuziki hutumia muziki kutekenya sehemu ambazo hazijaathiriwa ili kuleta matumaini badala ya utamaushi. Anaeleza kuwa ugonjwa wa UKIMWI ni zao la kijamii na mbali na matumizi ya dawa za kupunguza makali (ARVs), hali ya afya inafaa kuboreshwa. Anasema kuwa muziki, kwa kuwa una sifa ya kidayolojia, una uwezo wa kupunguza upweke na kuwafanya wagonjwa wajieleze na hivyo kujitathmini tena. Sifa hii ya kidayolojia ilibainika katika nyimbo nilizozichanganua ambapo waathiriwa wanajitetea dhidi ya unyanyapaa na lawama kutoka kwa wasio na VVU/UKIMWI.

Barz (2006) anasema kuwa, njia za usimulizi zinachangia katika utunzaji kiafya. Mathalani, matini za muziki aghalabu hupendekeza mikakati inayohimiza na

kuchangia mbinu za kimatibabu. Aidha, muziki huwa kama dawa inayoponya kisaikolojia na kiroho. Hata wanapokuwa katika uchungu, watu hupata hisia za hadhi ya utu na furaha wakichezewa muziki. Kwa hivyo,nyimbo na muziki ni dawa na wakati huo huo huwa elimu ya kuiadilisha jamii. Barz alishuhudia uwezo huu wa muziki na sanaa nyingine za maonyesho na utendaji nchini Uganda. Ni kutokana na ushahidi huo ambapo Barz (2011) anasisitiza umuhimu wa kuvuka mipaka ya matibabu ya Kimagharibi na haja ya kuukabili UKIMWI kama tukio linalopambanuliwa kiutamaduni na kijamii. Hali kama hii inawezekana katika nchi nyingine barani Afrika na hasa Kenya tunapotafakari kuhusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI.

Maelezo ya Barz yanaafikiana na ya Mutembei (2009) anayeeleza kuwa, nafasi ya ushairi katika maisha ya mtu ni kubwa na mchango wake unatambaa katika maeneo mengi ya maisha yake. Anaendelea kuelezea kwamba, dhima ya kuburudishwa na nyimbo, kuliwazwa, kuhamasishwa na zaidi kuelimishwa imekuwa ikionekana kupitia ushairi zikiwemo nyimbo na mashairi. Aidha, akirejelea utafiti wa Mathew J. Bush, Mutembei anaeleza kuwa, ushairi umetumika katika tiba na hasa tiba ya akili ya mwanadamu (*http://www.enterthefreudianslip.com/using-popular-music.*htm). Utafiti huo umeonysha kuwa nyimbo zinaweza kutumika kwa mafanikio makubwa katika tiba inayogusa hisia za mwanadamu. Isitoshe, matatizo ya mihemko, mfadhaiko, kutawaliwa na hali ya kupenda ulevi na ubaya unaoletwa na tabia hizi, yote haya yanaweza kupunguzwa na kumalizwa na ushairi (The Power of Creative Therapy katika EnterTheFreudianSlip.com).

Maelezo haya yalinifaa kwa kuwa, nyimbo zilizoshughulikiwa katika tasnifu hii zinatekeleza dhima ya kuburudisha, kuliwaza, kuhamasisha na kuelimisha. Aidha,

matatizo ya mihemko, mfadhaiko, kutawaliwa na hali ya kupenda ulevi wa pombe na mihadarati pamoja na ubaya wa tabia kama hizi, ni hali inayowakumba waathiriwa wa UKIMWI na huchangia kuenea kwa VVU na unyanyapaa.

Maelezo mengine yaliyonifaa ni yale ya Clive Robins anayesema: "wakati njia za tiba zinaposhindikana, tiba ya muziki huwa na taathira ifaayo kuwaponya watoto wenye matatizo ya mihemko" (Clive Robins 1990) katika Mutembei (2009). Mutembei anaongeza kueleza kuwa, na wala sio watoto tu, bali hata watu wazima kwani tangu zamani za kale muziki na ushairi kwa jumla ulikuwa ukitumika katika tiba. Maelezo haya yalinifaa kwa sababu, katika muktadha wa VVU/UKIMWI, tiba kamili imeshindikana huku watoto na watu wazima wakiathirika sana. Hali hii imepelekea kutazamwa kwa utanzu wa nyimbo, hasa simulizi zake ndogo ndogo kama tiba mbadala kwao.

Rafiq (2008) anaeleza kuwa, ni kupitia kwa Hip-Hop ambapo vijana wanaweza kuchangia kupunguza kwa kiwango kikubwa kuenea kwa janga la UKIMWI nchini Tanzania. Aidha anaeleza kuwa, vijana nchini humo waliweza kumuktadhaisha Hip-Hop na kuitumia kama chombo cha kuwasilisha matatizo yao kwa jamii na serikali. Kwa kiasi kikubwa wamejihusisha sana na mbinu hii katika kujieleza kiasi kwamba baadhi ya watu nchini humo wametambua Hi-Hop kama utamaduni.

Ingawa watafiti wengi waliotangulia walitekeleza tafiti kuhusu Nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI, utafiti huu unaelekea kuchukua mkabala tofauti kwa kuwa nyimbo na simulizi husika zimekitwa kwenye muktadha wa ubaadausasa. Hivyo basi utafiti huu unaibuka kuwa wa kipekee kwa sababu sijawahi kuona kazi kama hii ambazo zimeegemezwa kwenye mkabala wa ubaadausasa, na hata kama zipo ni chache mno.

## 1.3 Suala la Utafiti

Tafiti nyingi za awali zinazohusu nyimmbo na suala la VVU/UKIMWI zikiwemo za Ahmadi (2005), Barz (2006), Nyawira (2008), Mutembei (2009), Barz na Cohen (2011) na Wanyama na Okong'o (2011)zimelenga mtindo na maudhui mengine ambayo ni tofauti na simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo mintaarafu ya VVU/UKIMWI. Hata pale ambapo maudhuiyanahusu VVU/UKIMWI, nyingi ya tafiti hizo zimeegemea isimu, isimujamii, mawasiliano na muziki kama taaluma ya kisayansi. Ingawa nyimbo zinzoimbwa katika jamii za Kenya katika nyakati hizi za kibaadausasa zinaweza kutumiwa kama njia mbadala ya kukabiliana na VVU/UKIMWI pamoja na madhara yake, tafiti hizo za awali hazikubainisha jinsi zinavyotekeleza jukumu hili. Utafiti huu basi umechombezwa na ukweli huo na hivyo kuchanganua simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo katika nyimbo za kibaadausasa na ambazo zinaweza kutumiwa kama njia mbadala ya kuwapa faraja wale walioathirika na pia kuzuia maambukizi zaidi kwa wale ambao hawajaathirika. Nyimbo hizi zinapoimbwa huifikia hadhira kubwa kupitia kwa vyombo habari na uimbaji mbele ya hadhira hai. Simulizi hizo zinahusu maadili au maonyo, unyanyapaa, jinsia, mamlaka na faraja mintaarafu ya VVU/UKIMWI. Aidha, ni simulizi zinazowasilisha jumbe nyeti kuhusu mapenzi, ngono,matumizi ya mipira ya kondomu na sehemu za siri za mwili wa binadamu kupitia vyombo vya habari na uimbaji mbele ya hadhira.

### 1.4. Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

a) Kueleza jinsi mikakati ya kibaadausasa inavyobainika katika nyimbo zinazohusu VVU/UKIMWI.
b) Kuchanganua simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo za unyanyapaa katika nyimbo zinazohusu VVU/UKIMWI.
c) Kujadili namna mamlaka yanavyochangia kuenea kwa maambukizi VVU/UKIMWI.
d) Kufafanua kimuktadhajinsi nyimbo za kibaadausasa zinavyopiga vita VVU/UKIMWI.

### 1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika nadharia tete zifuatazo:

a) Je, nyimbo za kibaadausasa zinadhihirisha mikakati inayohusishwa na nadharia ya Ubaadausasa?
b) Je, nyimbo za kijamii na za Kiswahili zinasimulizi kuu na simulizi ndogo ndogo zinazowasilisha habari zinazohusu unyanyapaa na VVU/UKIMWI?
c) Je, mamlaka yanachangia kuenea kwa maambukizi ya VVU nchini Kenya?
d) Nyimbo zinazoimbwa katika miktadha ya kijamii huchangia vipi katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI?

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unahusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWIna unatarajiwa kuwa na umuhimu katika jamii hasa ikizingatiwa kwamba janga la UKIMWI linaendelea kuleta maafa kila uchao ulimwenguni. Katika mkabala huo, kwanza utafiti huu

ulikusudia kutoa habari muhimu zilizomo katika vipande vya simulizi vya nyimbo na ambazo zinaweza kuchangia katika kukabiliana na au kurutubisha kuenea kwa VVU/UKIMWI na unyanyapaa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu nyimbo katika muktadha wa kibaadausasa huwa na upekee wa matumizi ya mikakati kama vile mwingiliano matini, mwigo, kutokuwepo kwa uaushi na kadhalika. Mikakati hii huwawezesha waimbaji kuwasilisha jumbe kuhusu VVU/UKIMWI bila aibu na pia bila kuzuiliwa na mipaka ya kijamii kama ya kiumri, kijinsia, kitabaka, kielimu na kadhalika.

Aidha, ni muhimu kutaja kuwa, tafiti nyingi za awali ziliegemea taaluma ya muziki na kuwasilisha tasnifu katika lugha ya Kiingereza na hivyo kuwanyima wapenzi wa Kiswahili nafasi ya kupata habari muhimu kuhusu VVU/UKIMWI kupitia lugha waipendayo. Upekee wa utafiti huu umejikita katika nyimbo zilizoimbwa kwa Kiswahili na nyimbo mahususi za jamii maalum pamoja na viwango maalumu na matokeo yake yanawasilishwa kwa lugha ya Kiswahili.

Vile vile, matokeo ya utafiti huu yataenda sako kwa bako na tafiti za awali zikiwemo za Ahmadi (2005), Nyawira (2008), Barz (2006) na Mutembei (2009) katika kuziba mapengo ambayo hayakuzibwa hapo awali. Ninaamini kuwa utafiti huu utakuwa mchango wa kuchochea na kuendeleza tafiti zaidi katika siku za usoni.

Hatimaye, kwa kuangazia umuhimu wa nyimbo katika jamii, matokeo ya utafiti huu yatasaidia serikali katika kubuni sera na mikakati itakayosaidia kukabiliana na kuenea kwa VVU/UKIMWI nchini Kenya, sera na mikakati ya kuwashirikisha waimbaji, vipengele vya tamaduni na wanajamii inavyostahiki.

### 1.7 Upeo na mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijifunga kwenye nyimbo za kijamii na za Kiswahili na ambazo zina mada ya VVU/UKIMWI. Kwa kutumia usampuli wa kimakusudi, nyimbo ishirini (23) ziliteuliwa. Aidha, nyimbo hizi ziliainishwa kama za kidini na zisizo za kidini. Aidha, utafiti ulijifunga kwenye simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo zilizomo katika nyimbo husika na ambazo zinahusu VVU/UKIMWI. Nilichanganua simulizi katika nyimbo zilizosanifiwa na wasanii kama inavyodhihirishwa katika viambatisho vya tatu(3) hadi saba(7).

### 1.8 Mbinu za Utafiti

#### 1.8.1 Utangulizi

Huu ni utafiti wa kimaelezo ambapo nyimbo zilinakiliwa, kutafsiriwa na simulizi kuu na simulizi ndogo kujadiliwa kiufafanuzi. Kwa jinsi hii basi, katika sehemu inayofuatanimejadili mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, nilitumia mbinu na vifaa vifuatavyo: Utafiti wa maktabani, uchunguzi nyanjani na mijadala ya makundi teule. Vifaa vya kukusanya na kuchanganua data vilikuwa: kidadisi, tarakilishi na runinga. Hatimaye nimejadili jinsi data ilivyochanganuliwa.

#### 1.8.2 Utafiti wa Maktabani

Utafiti maktabani uliniwezesha kuyapitia na kuyahakiki maandishi mbalimbali juu ya nyimbo na suala zima la ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Mapitio ya maandishi husika yaliniwezesha kupata habari zaidi kuhusu hali ya VVU/UKIMWI ulimwenguni na pia nchini Kenya. Aidha, mapitio ya maandishi husika yaliniwezesha kupata habari kuhusu juhudi zilizowekwa ili kukabiliana na tatizo hili.Isitoshe, utafiti wa maktabani

ulinimulikia viwango vilivyofikiwa kiutafiti kuhusiana na suala la utafiti. Mapitio haya yalinibainishia mapengo ya tafiti za awali na ambazo zinaweza kuzibwa na matokeo ya utafiti huu.

Aidha, nilitalii tovuti ili kupata habari zaidi kuhusiana na suala la utafiti. Pamoja na hayo, nilizizuru maktaba za vyuo vikuu kama vile ya Chuo kikuu cha Moi na vile vile maktaba za kitaifa ikiwemo ya Kericho. Nilivitembelea vituo vya redio kama vile Kass Fm International, Redio Maa, Ramogi FM na Shirika la Utangazaji nchini Kenya (KBC) ambapo nilipata nyimbo za wasanii walioteuliwa kwa ajili ya utafiti huu.

### 1.8.3 Sampuli

Kwa kutumia uteuzi wa sampuli wa kimakusudi, niliteua nyimbo ishirini na tatu (23). Nyimbo kumi na tatu (13) zilizoimbwa kwa Kiswahili, nne (4) kwa Kikalenjin, nne (4) kwa Kijaluo na mbili (2) kwa Kimaasai. Aidha usampulishaji huu uliniwezesha kuwateua wasemaji wa lugha za Kimaasai na Kijaluo walionisaidia katika kuzitafsiri nyimbo kutoka jamii husika. Uteuzi wa nyimbo hizi ulizingatia kigezo cha kuzungumziwa kwa mada za VVU/UKIMWI kama mada kuu ndani ya nyimbo hizo.

Mbali na kuteua nyimbo, wasikilizaji wa nyimbo hizi waliteuliwa kimaksudi hususan miongoni mwa waumini makanisani, kumbi za kijamii na pia vijijini ambapo mbinu mbili zilitumiwa. Mbinu ya kwanza ilikuwa mijadala katika makundi teule na mbinu ya pili ilikuwa ya usaili wa ana kwa ana iliyotumiwa kuwasaili watafitiwa mmoja mmoja. Wahusika katika makundi teule walitarajiwa kusikiliza na au kutazama nyimbo zikichezwa kwenye CD kisha kubainisha simulizi za VVU/UKIMWI pamoja na masuala yanahusu ngono kwa jumla. Aidha, walielekezwa kubainisha mikakati ya kibaadausasa kama vile mwingiliano matini, mwigo,

kukosekana kwa uaushi na kadhalika. Wahusika waliosailiwa nao walielekezwa vivyo hivyo.

### 1.8.4 Vifaa vya Utafiti

Kuna vifaa kadha wa kadha vinavyoweza kutumiwa katika kukusanyia, kuchanganulia na kuhifadhia data katika utafiti. Uteuzi wa vifaa maalum hutegemea aina na upekee wa utafiti. Katika utafiti huu nilitumia kinasa sauti au tepu rekoda, tarakilishi na runinga kama vifaa vya utafiti.

#### 1.8.4.1 Runinga na Tepu Rekoda

Vyombo hivi vilitumika kuchezesha CD na kanda zenye nyimbo zilizoteuliwa. Kwa kutumia runinga, niliweza kuchanganua nyimbo husika kiutendaji kwani hubainisha miondoko ya kimwili na ishara mbalimbali zinazoambatana na uimbaji. Tepu rekoda nayo ilitumiwa kuchezesha nyimbo zilizorekodiwa katika kanda za kunasia sauti. Aidha ilitumiwa kurekodi mijadala iliyokuwa inafanyika katika makundi teule.

#### 1.8.4.2 Uwasilishaji wa Data

Data ilitokana na nyimbo zilizoteuliwa kisha kunakiliwa. Hatimaye nyimbo hizi zilitumiwa katika uchanganuzi kwa kuzingatia sehemu zinazohusiana na suala. Baadhi ya sehemu hizo ni pamoja na simulizi kuu na simullizi ndogo ndogo kuhusu swala zima la VVU/UKIMWI, mwingiliano wa matini, mwigo, kukosekana kwa uaushi, hadhira za kulengwa na miktadha ya kijamii.

#### 1.8.4.3 Uchanganuzi wa Data

Nyimbo zilizoteuliwa zilinakiliwa. Zile za Kikalenjin, Kimaasai na Kijaluo zilinukuliwa kwanza katika lugha chanzi kisha kutafsiriwa kabla ya kuchanganuliwa.

Mtafiti alizitafsiri nyimbo za Kikalenjin kwa kuwa yeye ni msemaji wa lugha hiyo. Zile za Kimaasai na Kijaluo zilitafsiriwa na wasemaji wa lugha husika walioteuliwa kimakusudi na mtafiti. Nyimbo na hasa simulizi kuu na simulizi ndogo ndogo za nyimbo zilizoteuliwa zilichanganuliwa. Aidha uchanganuzi ulikuwa wa kiufafanuzi au kimaelezo na uliegemea kwenye mwelekeo wa matumizi ya nadharia ya baadausasa kwa kujikita katika matini na miktadha huku ukizingatia uhakiki wa simulizi zinazojitokeza katika nyimbo. Uchanganuzi huu uliegemezwa kwenye mihili ya nadharia ya baadausasa kama vile mwingilianomatini, ukiukaji, urejelezi, kukosekana kwa mshikamano na kukosekana kwa uaushi au uhalisi.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imejadili misingi ya utafiti kama vile usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, azma ya utafiti na nadharia tete. Mambo mengine muhimu yaliyoshughulikiwa kwenye sura hii ni pamoja na umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, mbinu za utafiti zilizotumiwa na namna data zilivyokusanywa, kuwasilishwa na kuchanganuliwa. Katika sura ifuatayo, ninajadili mapitio ya maadishi yanayohusiana na mada pamoja na misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu mapitio ya maandishi ya maandishi na misingi ya kinadharia. Katika sura hii, nimehakiki maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti. Kwa jinsi hiyo, nimeangazia vipengele kama vile vipengele vielekezi vinavyochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI nchini Kenya, athari za VVU/UKIMWI nchini Kenya, mikakati ya serikali katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI, hali ya VVU/UKIMWI nchini Kenya na yaliyoandikwa kuhusu nyimbo na VVU/UKIMWI kwa ujumla. Pamoja na hayo, nimejadili nadharia ya Ubaadusasa ambayo iliongoza utafiti huu. Mikakati ya nadharia hii ilikuwa msingi wa uchanganuzi wa data.

## 2.2 Vipengele Vielekezi Vinavyochangia Kuenea kwa VVU Nchini Kenya

### 2.2.1 Umaskini

Kuna uhusiano mkubwa kati ya umaskini na kuenea kwa VVU/UKIMWI. Hali ya umaskini miongoni mwa wanajamii huchangia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa njia mbili kuu. Mosi, umaskini huwaweka wanajamii katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Pili umaskini huchukua nafasi kubwa katika kuuhimili na kuuendeleza. Kenya, jinsi yalivyo mataifa mengine hasa yaliyo kusini mwa jangwa la Sahara, ni lazima ipambane kuondoa umaskini iwapo vita dhidi ya VVU/UKIMWI vitashindwa. Hii ni kwa sababu umaskini unaweza kumithilishwa na shamba lenye rutuba ambapo VVU/UKIMWI unaweza kusitawi. Kwa mujibu wa Poverty Reduction Strategy Paper (PRSP, 2007), Kenya ina idadi kubwa ya watu wasiolingana kimapato.

Zaidi ya nusu ya wananchi wanaishi katika hali ya umaskini, hali iliyozidishwa na ufisadi ulioenea, VVU/UKIMWI na uharibifu unaotokana na ukame wa mara kwa mara. Hali hii imewafanya watu milioni tatu nchini wawe wenye kutegemea msaada wa chakula kila mwaka. Kwa sasa asilimia hamsini na mbili (52%) ya wananchi wanaishi katika hali ya umaskini kabisa. Hii ni kwa sababu riziki yao ya kila siku ni chini ya dola moja na hivyo hawawezi kupata mahitaji yao ya kimsingi ( PRSP, 2007).

Ingawa athari na utokeaji wa ugonjwa ni sawa miongoni mwa watu maskini na matajiri, ni dhahiri kuwa njia zao za kukabiliana nao hutofautiana kabisa. Huu ni ukweli uliopo kuhusiana na maambukizi ya VVU. Idadi kubwa ya watu maskini hawawezi kugharamia huduma za matibabu katika hospitali za umma sembuse za kibinafsi. Umaskini pia huchangia kutoweza kwao kudhibiti hatari ya kuambukizwa. Huwalazimisha, hasa wanawake, kushiriki ngono bila kinga, kuwa wahamiaji, kuwa katika hali ya utapiamlo, hali ambazo zinawaweka katika hatari ya kuambukizwa magonjwa na pia katika hatari ya kukumbwa na matendo yanayodhuru kama vile ndoa za mapema, urithi wa wajane na ukeketaji. Hali hizi zote huongeza uwezekano wa mtu kuambukizwa VVU (Nyawira, 2008).

### 2.2.2 Maambukizi kupitia kwa Ngono/ Magonjwa ya Zinaa

Magonjwa ya zinaa ni mojawapo ya njia ambazo wanajamii wanaweza kuambukizana VVU. Haya ni maambukizi yanayotokana na usafirishwaji au upitishwaji wa viumbehai vya kikaboni kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine wakati wa ngono. Kuna aina mbili za magonjwa ya zinaa. Aina ya kwanza ni magonjwa ya zinaa yanayosababishwa na bakteria. Magonjwa hayo husababisha malengelenge na chunjua katika viungo vya uzazi na homa ya manjano. Aidha, magonjwa haya

yanaweza kuainishwa kama yenye vidonda na yasiyo na vidonda. Hali hii ya kuwepo au kutokuwepo kwa vidonda ni muhimu hasa tunapotafakari kuhusu nafasi ya magonjwa mengine ya zinaa katika maenezi ya VVU. Kutokana na ukweli kwamba watu huambukizana magonjwa ya zinaa pamoja na UKIMWI sana sana kupitia kwa ngono, mikakati au hatua za uzuiaji huwa sawa. Kulingana na Matengu (2005), mahusiano kati ya UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa hayatokani na njia za pamoja za uambukizaji na uzuiaji tu. Anaeleza kuwepo kwa uhusiano wa utaratibu wenye msingi wa kibayolojia kati yao. Anafafanua kuwa magonjwa ya zinaa huchangia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa kuzidisha uwezekano wa kuambukizwa na wepesi wa kuathirika kwa urahisi. Ameielezea hali hii kama inayotokana na ukweli kuwa, shahawaya mtu aliye na ugonjwa wa zinaa huwa na mkolezo wa hali ya juu ya virusi vya UKIMWI.

Aidha, ongezeko la idadi ya watu wanaoambuzwa magonjwa ya zinaa kupitia ngono ni ithibati kuwa wengi wanashiriki ngono bila kinga. Kulingana na NACC (2006), VVU/UKIMWI ulikadiriwa kuenea kwa asilimia ishirini na tatu (23%) nchini Kenya mnamo mwaka wa 2003 miongoni mwa wanawake waliokuwa na magonjwa ya zinaa. Asilima thelathini na Saba (37%) ya wanawake husika walikuwa na magonjwa ya zinaa yanayohusishwa na vidonda kwenye viungo vya uzazi. Asilimia ishirini na mbili (22%) ya wanaume walioambukizwa VVU walikuwa na hivyo vidonda katika viungo vyao vya uzazi.

Ripoti hii ilibainisha pia kwamba asilimia kubwa ya waathiriwa walitafuta matibabu ya magonjwa ya zinaa huku wengine wakikosa kutafuta huduma za kimatibabu. Kulingana na Baraza la Kitaifa la Kudhibiti VVU/UKIMWI, Kenya (2000), kuna vizuizi kadhaa vinavyotatiza udhibiti au usimamizi unaofaa wa magonjwa ya zinaa.

Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa vifaa vya kimsingi na dawa, uhaba wa wataalamu waliohitimu, usimamizi usiotosheleza wa magonjwa maalum ya zinaa, tabia isiyoridhisha ya kushughulikia masuala ya kiafya, kutoshughulikia kwa dhati mwelekeo wa dalili nyingi za ugonjwa na kadhalika.

### 2.2.3 Athari za Pombe na Dawa za Kulevya

Mataifa ya Afrika hasa yaliyoko kusini mwa jangwa la sahara bado ni kitovu cha zilizala ya VVU/UKIMWI ulimwenguni. Mbali na kukabiliwa na mzigo mzito wa maambukizi ya VVU kupitia kwa ngono, mataifa haya pia yanakumbwa na tatizo kubwa la matumizi haramu ya dawa za kujidungia au zisizo za kujidungia.

Matumizi ya dawa hizi yanahusiana moja kwa moja na uwezekano wa kuenea kwa VVU miongoni mwa wahusika (Needle na wenzake 2006). Kuna data chache mno za kuhusisha UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya katika eneo la Afrika, hususani Kusini mwa jangwa la Sahara. Pamoja na hayo kikundi cha watumiaji wa dawa hizi ni kikundi ambacho pia ni vigumu kufikiwa kwa sababu kimeathiriwa na unyanyapaa na hivyo kujificha katika lindi la matumizi ya mihadarati. Kulingana na Stimson (katika Nyawira 2008), kikundi hiki aghalabu hakishirikishwi katika mifumo ya uchunguzi kidoria.

Heroini ni dawa inayoripotiwa kutumiwa zaidi nchini Kenya. Kuna heroini ya kujidungia na isiyo ya kujidungia. Dawa zingine zinazoripotiwa kutumiwa hasa katika majiji ya Mombasa na Naiorbi ni pamoja na bangi, kokeini, pombe na miraa(Needle na wenzake 2006). Mahojiano yaliyofanywa na Beckerleg katika Deveau na wenzake (2006) yalibainisha kuwa, mjini Malindi, watumiaji wa dawa za kulevya walikuwa na mazoea ya kutumuia sindano moja kujidunga. Isitoshe

watumiaji wengi walitumia mchanganyiko ule ule mmoja wa heroini. Tabia hizi zinazidisha uwezekano wa kuambukizana VVU kwa sababu damu ya watu tofauti inaweza kuchanganyikana kwa urahisi. Pamoja na matumizi ya sindano moja kwa ushirika, mahojiano hayo yalibainisha kuwa wahusika walikuwa na wenzi walioshirikiana ngono bila kutumia mipira ya kondomu. Needle na wenzake (2006) wanaongeza kuwa watumiaji wa dawa za kulevya za kujidungia wa kike na wa kiume hushiriki ngono ya malipo ili kupata fedha za kujidumisha katika mazoea ya matumizi ya mihadarati. Dawa zingine kama vile kokeini husisimua miili ya wanaume kwa wanawake na hivyo kuwazuia wahusika kufanya maamuzi yanayofaa kuhusu ngono salama. Msisimko huu humweka mtu katika hatari kubwa ya kuambukizwa kwani kuna uwezekano wa kushiriki ngono bila kinga. Hali hii huwakumba mabasha na wahusika wa jinsia tofauti (Deveau na wenzake, 2006).

### 2.2.4 Mizozo na Vita vya Kikabila

Mizozo na vita vya kikabila vimekuwa vikiongezeka nchini Kenya. Hali hii ilifikia kilele chake Disemba 2007 baada ya matokeo ya uchaguzi mkuu kutangazwa ambapo kulikuwa na mabishano kati ya pande mbili za kisiasa zilizokuwa zinawania urais. Aidha, vyombo vya habari aghalabu havikosi kurusha matangazo yenye habari za mizozo na vita kati ya makabila mbalimbali katika sehemu mbalimbali za nchi hii. Mathalani, kumekuwa na habari kuhusu kutolewa kwa makaazi kwa wakimbizi wa ndani kwa ndani au wale wanaotorokea Kenya kutoka nchi jirani kama vile Somalia na Sudan Kusini.

Isitoshe, kumekuwa na taarifa kuhusu vitisho vya makundi haramu kama vile Mungiki , Chingororo, Baghdad Boys na kadhalika. Kumekuwa na habari juu ya vita katika eneo la Mlima Elgon, Mai Mahiu, Tana River, Bungoma, Samburu na

kadhalika. Ripoti ya UNAIDS (2004) kuhusu janga la UKIMWI ulimwenguni yaonyesha kuwa viwango vya juu vya UKIMWI miongoni mwa wanajamii na maeneo mbalimbali katika nchi hudhihirika nyakati za vita. Ripoti hii inafafanua njia mbalimbali ambazo zinafanya maambukizi kuenea zaidi nyakati kama hizi.

Kwanza, vita vinapotokea watu hutoroka makwao na huenda wakakimbilia maeneo ambayo kuna hatari na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa virusi vya UKWIMI. Uhamisho mara nyingi huwaweka watu katika hali tatanishi ambapo inakuwa vigumu hata kupata vifaa vya kujikinga kama vile kondomu pamoja na kukosa huduma za kimatibabu. Pili, ripoti hii inaeleza kuwa hali ya mvurugiko inayohusishwa na mizozo husababisha kuvunjika kwa maadili ya kiasili hasa yanayohusiana na ngono. Kuvunjika kwa maadili na kaida zinazodhibiti masuala ya kijamii hususan ngono kunawaweka wanajamii husika katika hali ya hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Tatu, mizozo na vita vya kikabila huwaathiri zaidi wasichana,wanawake na watoto kuliko wanajamii wengine. Kulingana na ripoti hii, wasichana na wanawake wanalazimishwa kushiriki ngono ili kupata pesa, chakula na ulinzi au uhifadhi. Mathalan, askari wengi wanapotumwa mahali fulani kudumisha amani, huwa kuna uwezekano wa kuenea kwa virusi miongoni mwao na wanawake wanaoshiriki ngono ya kutarazaki.

Nne, ripoti hii inaeleza kuwa, kitendo cha ubakaji hutumiwa kama silaha ya kivita. Katika mizozo mingine hususan barani Afrika, wanaume na wavulana wameripotiwa kabakwa. Njia ya tano inayochangia maenezi ya virusi wakati wa mizozo na vita ni kuvunjika kwa mifumo ya kimatibabu. Katika nyakati za mizozo na vita, taasisi za afya huathirika kiutendaji kazi na hata kuvunjika kabisa. Akiba ya damu ya kitaifa pia

huathirika na mikakati ya uzuiaji wa maenezi ya virusi vya UKIMWI pamoja na ile inayolenga utunzaji wa waathiriwa nayo huporomoka.

Hatimaye, ripoti hii inaeleza kuwa, katika hali hii, kuna uwezekano wa baadhi ya wanajamii pamoja na watoto kuzidisha matumizi ya pombe, gundi na mihadarati ili kujipumbaza na kujisahaulisha juu ya dhiki zinazoambatana na mizozo pamoja na vita. Kuna uwezekano wa matumizi ya dawa za kulevya za kujidungia. Hii hutokana na kutatizwa kwa njia za kawaida za kupitishia dawa zingine za kulevya ambazo hutafunwa na kumezwa, zile zinazonuswa ama zinazovutwa ( UNAIDS, 2004).

### 2.2.5 Dhana na Desturi za Kitamaduni

Vipengele vya kitamaduni vinavyochangia kuenea kwa VVU nchini Kenya ni pamoja na utamaduni na dini. Kila jamii ina utamaduni wake; utamaduni ambao una mfumo wa maadili, desturi na imani ambazo hupambanua jamii moja na nyingine. Vipengele hivi vinakuwa kama dira ya kuwaongoza wanajamii kutathmini hatua au kufanya maamuzi juu ya namna wanavyojiendesha katika muktadha fulani. Vipengele hivi huwa na uwezo mkubwa wa kuathiri maamuzi ya wanajamii hata kushinda "ustaarabu", viwango vya elimu au usasa na umji. Janga la UKIMWI barani Afrika ikiwemo Kenya linahusishwa zaidi na tathmini, maamuzi, hatua na dhana zilizochukuliwa na kuamuliwa kiutamaduni. Kwa bahati mbaya, baadhi ya mambo haya huishia kwenye tabia na mwenendo hatari unaowaweka wanajamii katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Chambilecho Umeh (1997: 72):

> UKIMWI/ VVU ni ugonjwa maalum. Ni maalum kwa kuwa umefungamana na suala la jinsia, suala ambalo ni bishani karibu ulimwengu mzima. Mtu hawezi kujadili suala la UKIMWI/VVU pasipo kuzingatia mielekeo ya kijinsia kama sehemu ya tatizo zima. Kote ulimwenguni, kila utamaduni hudhihirisha sifa za kipekee lakini ndani ya kila mojawapo maana ya jinsia kiutamaduni huwa wazi kabisa ( Umeh, 1997:72)

Nchini Kenya, zaidi ya asilimia themanini (80%) ya watu huambukizwa VVU kupitia kwa ngono kati ya mwamume na mwanamke walio na Virusi Vya UKIMWI. Baadhi ya mienendo ya kitamaduni inayowaweka watu katika hatari ya maambukizi ni pamoja na dhana za kitamaduni kama vile: kuoa wake wengi, tohara za kiasili kwa wavulana, ukeketaji wa wasichana na wanawake, ushirika wa wanaume wengi mke mmoja, urithi wa wajane upurukushani na kadhalika.

Dhana za kitamaduni zinazohusu jinsia ya kiume na ya kike zimechangia pakubwa kuenea kwa VVU nchini Kenya. Jinsi ilivyo katika mataifa mengine ya Kiafrika, aghalabu wanawake na watoto ndio wanaoathiriwa zaidi na misiba ya vita, njaa, magonjwa, unyanyasaji wenye misingi ya kijinsia, umaskini, ukosefu wa haki ya kumiliki mali, ubabedume na kadhalika.

Onyango (2007) anadai kwamba, ubabedume ndio msingi mkuu unaosababisha maenezi ya VVU nchini Kenya. Anaeleza kuwa, miundo ya kiitikadi na uwezo katika jamii nyingi nchini Kenya huependelea wanaume zaidi kuliko wanawake. Msimamo wake ni kwamba, kutokana na sababu hizi wanawake huathiriwa zaidi na maambukizi ya VVU. Anadahili kwamba, lugha ni kielelzo cha mamlaka na huchangia katika mahusiano ya kimamlaka. Anaeleza kuwa, katika jamii nyingi wanaume wanafanywa kutukuza na kushabikia ishara zenye sifa za kiume hasa zile za wanyama wenye nguvu kama vile fahali, kifaru, nyati, simba na kadhalika. Isitoshe, wanahimizwa kuwa wajasiri au majahili siku zote mpaka mwisho.

Sifa kama hizi hupitishwa kwa wanaume wakati wa sherehe za kitamaduni kama vile tohara ambapo wahusika hupitishwa kwenye hali zenye ugumu na uchungu na ambapo wanatarajiwa kuzipitia bila uoga kwani hicho ndicho kinachomfanya mwanaume kuwa mkamilifu.

Maoni ya Onyango ni kuwa, katika jamii nyingi zenye misingi ya ubabedume nchini Kenya, sifa muhimu ya mwanamume hudhihirika kupitia kwa ngono. Mathalan, anaeleza kuwa katika baadhi ya miktadha ya kijamii, kuna misemo inayoonekana kuwahimiza hata wale walioambukizwa magonjwa ya zinaa kuendelea kushiriki ngono. Amebainisha misemo kama vile:***Mwanamume ambaye hajaambukizwa homa hajawa mwanaume***. Homa hapa ikiwa na maana ya ugonjwa wa zinaa kama vile kisonono.***Fahali hufa akiwa na nyasi mdomoni***. Kitendo cha fahali kula nyasi hadi kufa kinanasibishwa na kitendo cha mwanaume kushiriki ngono hadi kufa.***Dawa ya moto ni moto***. Hii ni methali yenye maana: Moto huzimwa kwa moto (Onyango, 2007). Misemo kama hii ya Kiswahili huakisika zaidi katika tabia za wahusika na hivyo kuwezesha VVU kuenea kwa kasi.

Kuhusu masuala ya ngono, misemo kama vile, ***Hata paka mzeee hunywa maziwa*** husikika katika baadhi ya miktadha ya kijamii. Kwa mujibu wa Nyawira (2008), ingawa misemo kama hii inaweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali, jambo lililo wazi ni kwamba inawahimiza wanaume kuwa na uhuru wa kushiriki ngono na wanawake wowote na wa kila umri hususan wenye umri mdogo. Wanaume wengine huamini kuwa wanawake wanafaa kutawaliwa kinyama kupitia kwa ngono. Wanaamini kuwa ngono yenye mparuzo ni njia ya pekee ya kumthibitishia mwanamke nguvu zake za kiume pamoja na utu uzima wake. Mathalan, miongoni mwa Waluhyia, matumizi ya neno '***okhukhunda***' humaanisha kumparuza mwanawake wakati wa kitendo cha ngono (Onyango, 2007).

Kuhusu kujamiiana kwa njia salama ambapo wahusika wanafaa kujikinga na baa la UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa, kauli kama vile "***Mtu hawezikula ndizi na maganda yake***" na "***Mtu hawezi kula peremende kwa karatasi yake yakufungia***" huwa maarufu katika miktadha mingi ya kijamii. Kauli hizi zinaashiria upeo wa

ridhaa ambao nao unakuwa upeo wa hatari ya kuambukizwa VVU. Mintaarafu ya kauli hizi, ni wazi kuwa wanawake hawana uwezo wa kudhibiti masuala ya ngono hasa ngono salama katika jamii zenye misingi ya kuumeni.

Urithi wa wajane na purukushani au utovu wa staha ni baadhi ya desturi zingine za kitamaduni zinazochangia kuenea kwa VVU nchini Kenya. Desturi hizi zingali zinakubalika miongoni mwa baaadhi ya jamii. Urithi wa wajane unahusu kupitishwa kwa wajane, watoto wao na mali kwa kakaze marehemu au kwa jamaa kutoka aila husika. Katika baadhi ya jamii mume mmoja anaweza kurithi wajane zaidi ya mmoja. Mathalani, miongoni mwa Wanandi, mjane angerithiwa na kaka mdogo wa marehemu au aliyemfuata kwa umri ikiwa yule mdogo hakuwa amekomaa kiumri. Langley katika Nyawira (2008) anaeleza kuwa desturi hii ililenga kumtunza mjane kwa kukidhi mahitaji yake ya kimsingi na ya kijamii pamoja na ngono kwa ajili ya kuendeleza uzazi. Ni wazi kuwa katika hali kama hii ikiwa marehemu alikufa kutokana na UKIMWI huenda mjane anayerithiwa akawa na VVU pia. Kuna uwezekano mkubwa basi wa mrithi au anayerithiwa kuambukzwa na hatimaye kuwaambukiza wanaume na wanawake wengine pamoja na watoto wao kabla ya kuzaliwa.

Kuoa wake wengi ni desturi na mfumo wa maadili katika jamii nyingi za Kiafrika. Mwanamume anaruhusiwa kuoa wake wengi kadri ya uwezo wake hususan kwa ajili ya uzazi. Dini ya Kiislamu pia huridhia desturi hii. Katika jamii nyingine, mwanaume aliheshimiwa kulingana na idadi ya wake na watoto aliokuwa nao. Miongoni mwa Wakalenjin kwa mfano, kama mume angehitaji mke mwingine kwa sababu moja au nyingine angeomba kibali kutoka kwa mke wa kwanza ambaye alitambuliwa kama mke mkuu.

Desturi ya wanaume zaidi ya mmoja kushiriki ngono na mwanamke mmoja ni kitendo cha kawaida miongoni mwa jamii za wafugaji hususani Wamaasai. Ni desturi ya kubadilishana wanawake ambapo mwanamke aliye katika ndoa anaweza kushiriki ngono na wanaume wengine mbali na mume wake wa ndoa. Mathalani, miongoni mwa Wamaasai, mkuki uliochomekwa ardhini nje ya nyumba iliashiria kuwepo kwa mwanaume kwenye nyumba hiyo akifanya ngono na mwanamke asiye mkewe. Kuibuka kwa UKIMWI kumefanya desturi hii kuwa tisho kwa wanajamii husika. Haya ni kwa mujibu wa Nyawira (2008).

Tohara kwa wavulana na ukeketaji kwa wasichana pamoja na wanawake bado ni hatua inayothaminiwa ya mpito wa maisha miongoni mwa jamii nyingi. Ni hatua ya kitamaduni ambayo kwayo wavulana kwa wasichana huingilia utu uzimani. Ingawa utafiti wa kisayansi unaonyesha kuwa upashaji tohari kwa wanaume hupunguza uwezekano wa kuambukizwa VVU, kuna hatari zaidi ya maambukizi kupitia tohara za kitamaduni au za kiasili. Ingawa kuna kampeini za serikali na mashirika yasiyokuwa ya serikali kuhusu mbinu salama za upashaji tohara, hasa hospitalini, bado kuna baadhi ya jamii zinazoshikilia kwamba watoto watahiriwe kitamaduni. Katika tamaduni nyingi, kipindi hiki muhimu cha mpito wa maisha huambatanishwa na sherehe ambapo kuna karamu, uchezaji densi, uimbaji na kitendo chenyewe cha kutahiriwa. Miongoni mwa jamii nyingi ambazo hushiriki tohara, wale wasiotahiriwa hudharauliwa, huchekwa na kutokubaliwa kuoa na hatimaye imani ya kutowapata watoto huwaandama (Kariuki na wenzake 2006).

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa kupashwa tohara kulikuwa jambo la lazima kwa kila mwanaume na mwanamke ili kupata kuheshimiwa na kuwa na nafasi katika jamii. Masharti haya yalikuweko hata katika jamii zisizoshiriki tohara kama vile

Wajaluo ambao walingoa meno sita ya chini. Katika jamii zilizoshiriki tohara kama vile Wakikuyu, Wakalenjin, Wamaasai na kadhalika, tohara iliambatanishwa na utobolewaji wa masikio kama ishara ya kutofautisha waliotahiriwa na wasiotahiriwa. Watahiriwa waliunda jeshi la jamii husika. Mpaka miaka michache iliyopita, na kufuatia kampeini za kijamii dhidi ya tohara za kitamaduni, ngariba alikuwa akitumia kisu kimoja kwa watahiriwa wengi, jambo ambalo liliongeza uwezekano wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Ingawa siku hizi watahiriwa wanaweza kutahiriwa hospitalini, bado kuna jamii zinazoshikilia mbinu za kiasili. Katika baadhi ya jamii nyingine, baada ya kutoka jandoni watahiriwa walikubaliwa kushiriki ngono na wasichana ambao hawakuwa wametahiriwa Nyawira (2008). Tabia kama hii ikiwa bado ipo, basi inaweza kuchangia hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI katika jamii husika.

Ukeketaji wa wanawake ni desturi iliyokita mizizi katika jamii nyingi za Kiafrika na za Mashariki ya Kati. Msichana alichukuliwa kuwa amehitimu kuolewa pindi baada ya kukeketwa. Kulingana na Sobania katika Nyawira (2008), tohara kwa wanawake huchukuliwa kama kitendo kinachomsitiri mwanamke pamoja na jamaa yake ili aweze kuolewa kwa njia ya kisawasawa.

Kulingana na Nyawira (2008), Wakenya wengi wanaiona desturi hii kuwa ya kishenzi na iliyopitwa na wakati. Maoni haya yana misingi yake katika Ukristo, elimu na usasa. Hata hivyo, baadhi ya jamii kama vile za Kaskazini Mashariki mwa Kenya bado zinashiriki desturi hii. Sobania katika Nyawira (2008) anashadidia kuendelezwa kwa desturi hii kwa kumnukuu mwanamke mmoja aliyekuwa ametahiriwa akiongea na mzungu mmoja kutoka Ulaya:

> *“Ni vibaya kwa kuwa wanawake hawatahiriwi nchini mwenu, mtoto atakayezaliwa na mwanamke kama huyo ni binadamu kweli? Hapa kwetu ni vibaya kwa mwanamke ambaye hajatahiriwa kujifungua mtoto. Lakini wajua wanaume wa hapa kwetu hupenda wanawake waliotahiriwa”. (Sobania, 2003) katika Nyawira (2008:57-58).*

Wengine hushikilia desturi hii kama kaida ya kidini. Na kwa kuwa ni desturi ya mpito wa maisha namna inavyoshughulikiwa huongeza uwezekano na hatari ya wasichana wadogo kuambukizwa virusi vya UKIMWI na maambukizi mengine hatari kutokana na ukosefu wa elimusiha au usafi. Katika jitihada zake za kuikomesha desturi hii, serikali ya Kenya imejaribu mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwashika na kuwashtaki wazazi wa wasichana waathiriwa. Hata hivyo, ufanisi umekuwa mdogo kwa sababu mabadiliko yanayohusiana na desturi zilizokitwa katika utamaduni huanza na wanajamii husika wenyewe. Kwa kuwa hakuna hospitali au zahanati ya umma iliyo na kibali cha kuwakeketa wasichana na wanwake, desturi hii aghalabu hufanywa nyumbani kisiri na mkeketaji wa kiasili ambaye mara nyingi hutumia visu na nyembe zisizo salama kuwatahiri wasichana kadhaa. Hali hii huongeza uwezekano wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Desturi zingine za kitamaduni zinazodhiti ngono na hasa zinazoongeza hatari ya maambukizi ya VVU ni pamoja na ndoa za mapema, ambapo baada ya kukeketwa, msichana mdogo huozwa mwanamume mzee ambaye aghalabu huwa na wake wengine. Desturi ya pili ni ndoa za mwanamke kwa mwanamke, ambapo mjane au mwanamke tasa anakubaliwa kumwoa mwanamke ambaye ni mdogo kwake kiumri. Mwanamke huyu humzalia watoto na mwanaume nje ya ndoa au yule ambaye hajaoa. Kuolewa nyumbani ni desturi nyingine inayosababisha hatari ya kuambukizwa. Aina hii ya ndoa hutokea katika jamii ambapo watoto wa kike peke yake ndio waliozaliwa. Baada ya kuolewa kwa dada zake, msichana kitinda mimba hubaki kwao nyumbani

kwani kidesturi haolewi. Mwanamke huyu huwa na uhuru wa kutembelewa na mwanaume kutoka nje ya aila yake na kupata watoto naye. Mwanaume husika anaweza kuwa na mwanamke au wake wengine wa ndoa.

### 2.2.6 Dini

Nchini Kenya dini zinatekeleza wajibu muhimu katika kubadilisha misimamo, maoni na tafakuri za wanajamii kuhusu janga la UKIMWI. Amuyunzu-Nyamongo (2001) anadhukuru kuwa, baadhi ya imani za kidini zimechangia kuwepo kwa mawazo yasiyo sahihi kuhusu habari zinazohusiana na ngono na afya ya uzazi. Kutokana na hayo, mawazo yasiyo sahihi yamekuwa vizuizi katika kukabiliana na UKIMWI/VVU. Baadhi ya mafundisho na kanuni fulani za dini haziruhusu matumizi ya dawa na bidhaa za kuzuia uzazi, uambukizwaji wa UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Mathalan, Wakatoliki na Waislamu hupinga matumizi ya kondomu. Madhehebu mengine kama vile Mungiki yanashikilia imani na desturi za kitamaduni zilizopitwa na wakati kama vile kutotafuta matibabu, kuoa wake wengi, ukeketaji wa wanawake na kitendo cha wanaume kadhaa kushiriki ngono na mke mmoja. Desturi hizi zinawaweka waumini na wanajamii kwa ujumla katika hatari kubwa ya kuambukizwa VVU. Nyimbo zilizochanganuliwa katika tasnifu hii zina vipande vya simulizi vinavyopinga mawazo kama haya kwa kuwashauri waathiriwa watumie dawa za kupunguza makali ya VVU na matumizi ya kondomu. Aidha kuna vipande au simulizi ndogo ndogo zinazopinga uwezekano wa dini kuleta suluhu kwa tatizo la VVU/UKIMWI. Hii ndiyo sababu ya wasanii wa nyimbo za dini kutunga nyimbo zenye mada hii.

### 2.2.7 Wanajamii Walio katika Hatari ya Kuambukzwa VVU

Ingawa kila mmoja ako katika hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI kuna wanajamii ambao wako katika hatari zaidi ya kuambukizwa kuliko wengine. Ripoti za NACC (2006) na NACC (2008) zinatambua makundi yaliyoko katika hatari zaidi ya kuambukzwa nchini Kenya kuwa watumiaji wa mihadarati ya kujidungia, wasenge au mabasha, madereva wa matrela au malori wanaoshiriki ngono ya malipo pamoja na vijana. Isitoshe watoto wakimbizi, wasiojiweza na wanawake pia wamo katika kikundi hiki. Kulingana na NACC (2005) maambukizi mengi hutokea miongoni mwa wanajamii walio na umri kati ya miaka kumi na mitano na arobaini na tisa (15-49). Kwa kuwa utafiti huu unahusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI, ninaamini kuwa nyimbo husika zinalenga makundi yote yaliyotajwa. Mikakati iliyowekwa na serikali inalenga kuzuia kuenea kwa VVU katika makundi yote ya kijamii.

## 2.3 Athari za VVU/UKIMWI Nchini Kenya

Tangu kuibuka kwa janga la UKIMWI nchini Kenya katika miaka ya 1980, athari zake zimehisika katika kila sekta ya maisha kijamii. Hata hivyo sekta mbili kuu zilizoathirika zaidi ni zile za kijamii na kiuchumi kama vile elimu, afya, kilimo, viwanda na usalama wa kitaifa.

### 2.3.1 Athari za Kijamii na Kiuchumi

Kenya ni nchi yenye mapato ya chini kiuchumi. Uchunguzi unaonyesha kuwa ufanisi katika sekta ya uchumi umetatizwa kwa kiwango kikubwa na VVU/UKIMWI ambao umechangia kuongezeka kwa umaskini miongoni mwa wanajamii pamoja na taifa kwa ujumla (NACC, 2006). Kuongezeka kwa wagonjwa na vifo miongoni mwa wafanyakazi wenye ujuzi na wasio na ujuzi kumeendelea kuwa mojawapo ya vipingamizi vinavyokwamisha na hata kurudisha nyuma uchumi wa nchi.

Sekta ya elimu nayo imeathiriwa kwa njia nyingi. Kenya ina kiwango cha juu cha watu wanaojua kusoma na kuandika. Kulingana na Amuyunzu-Nyamongo (2001), kiwango hiki kilikuwa asilimia sabini na sita (76%) wanaume na asilimia sitini na saba (67%) kwa wanawake. Inavyoelekea ni kwamba, huenda viwango hivi vimeimarika hasa baada ya kuanzishwa kwa elimu ya shule ya msingi bila malipo na mafundisho ya kuruzuku katika shule za upili nchini mwaka wa elfu mbili na tatu (2003) na elfu mbili na tano (2005) mtawalia. Hata hivyo, janga la UKIMWI linaendelea kurudisha nyuma viwango vya kujiunga na shule na pia kukamilisha mafunzo kwa njia mbalimbali. Kwanza, watoto wanaoambukizwa kabla ya kuzaliwa huenda wakafa kabla ya kufikia umri wa kujiunga na shule.

Pili, wengi wa watoto wanaojiunga na shule huenda wakaacha kushiriki masomo kutokana na sababu mbalimbali zinazohusishwa VVU/UKIMWI. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na kuachiwa jukumu la kuwatunza jamaa na ndugu walioathiriwa na VVU/UKIMWI, kuachwa mayatima baada ya wazazi kufariki kutokana na UKIMWI na kukosa pesa za matumizi shuleni kwa kuwa pesa zote zinatumika kuwatunza walio wagonjwa nyumbani. Tatu, kuwapoteza walimu wengi wenye ujuzi na tajriba kutokana na magonjwa na vifo vinavyohusishwa na UKIMWI. Aidha huduma za walimu shuleni hukosekana kwa sababu ya kukosa kwenda shuleni kwa kuwa wagonjwa au kwa kuhudhuria mazishi ya walimu wenzao ( Ministry of Health, 2001).

Uchunguzi katika sekta ya afya unabainisha kuwa, sekta hii pia imeathiriwa na janga la VVU/UKIMWI. Kwa mujibu wa wizara ya afya, kuna matumizi ya kupita kiasi ya rasilmali zilizopo ambazo ni pamoja na uhaba wa dawa na vifaa vya kutumiwa kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya VVU katika viwango vya utoaji wa huduma toshelevu za ubainishaji katika viwango vyote vya ukuaji wa UKIMWI. Baadhi ya

huduma hizo ni pamoja na kutoa na kudumisha zana za kuchujia damu, kuongeza vituo vya afya ili kupunguza msongamano wa wagonjwa pamoja na kutoa vitendanishi vya kutosha vya kubainisha VVU (NACC, 2006; Ministry of Health 2001). Utoaji wa huduma hizi unahitaji nyongeza ya gharama kwa upande wa serikali na sekta ya afya. Pamoja na hayo, sekta hii inahitaji kupambana na suala la kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wanaolazwa hospitalini kutokana na maambukizi yanayohitaji kushughulikiwa katika vituo vya afya. Sekta hii pia imepoteza wafanyakazi wake wengi wenye ujuzi na tajriba kwa sababu ya VVU/UKIMWI.

Sekta ya kilimo ambayo kwa miaka mingi imekuwa uti wa mgongo wa uchumi wa taifa hili haijasazwa na athari za VVU/UKIMWI. Wakenya wengi hutegema kilimo katika maisha yao. Kuna wakulima wanaozalisha mazao ya kutumiwa kama chakula huku wengine wakizalisha mazao ya kuuzwa na hivyo kuwezesha nchi kupata mapato ya kigeni. Kilimo cha uzalishaji wa chakula na kilimo cha biashara vimekuwa mihimili au nguzo za uchumi wa Kenya kwa muda mrefu. Kuna mashamba yenye rutuba ambayo hayatumiki kutokana na uhaba wa wafanyakazi. Uhaba huu unasababishwa na magonjwa, haja ya kuwatunza wagonjwa pamoja na vifo (NACC, 2005). Kutokana na sababu hii, sekta hii imewapoteza wafanyakazi wake wenye ujuzi na hivyo kugharamika kuajiri wafanyakazi wapya na kuwapa mafunzo. Pia, kuna gharama za pensheni, ruzuku za kustaafu na mazishi. Kwa upande mwingine, ukulima wa kuzalisha mazao ya chakula uanendelea kuchukua nafasi ya ukulima wa mazao ya kuuzwa ili kutosheleza mahitaji ya wagonjwa ( Ministry of Health, 2001).

Viwanda vya uzalishaji mali pia vimepigwa na athari za VVU/UKIMWI. Mbali na kuwapoteza wafanyakazi wataalamu na wasio wataalamu, sekta hii inakumbwa na matatizo mengine yanayohusiana na VVU/UKIMWI. Matatizo hayo ni kama vile

wafanyakazi kukosa kufika kazini kwa sababu ya maradhi; jambo linaloathiri kiwango cha uzalishaji kwa siku, gharama za matibabu na za mazishi. Hatimaye, uzalishaji mali katika sekta ya viwanda utahasiriwa kwa sababu mahitaji ya bidhaa zilizoundwa viwandani hupungua wakati wanajamii wanapotumia fedha kuwatunza wagonjwa wao (NACC, 2005).

Sekta nyingine ambayo imepata pigo kubwa kutokana na janga la VVU/UKIMWI nchini Kenya ni ile ya usalama wa kitaifa. Sekta hii inajumuisha jeshi na vikosi vingine vya usalama kama vile polisi na magereza. Hii ni sekta muhimu sana tunapozingatia usalama wa taifa kwa ujumla. Majeshi ya usalama kote ulimwenguni yameathiriwa na janga la UKIMWI. Hii ni kutokana na sababu kuwa askari wengi huwa vijana ambao hufanya kazi mbali na familia zao na aghalabu huhamishwa kutoka eneo moja hadi lingine. Kuhamishwa huku kunawaweka katika hatari ya kushiriki ngono kiholela na hivyo kuongeza uwezekano wa kuambukizwa na kuathiriwa na VVU/UKIMWI (Nyawira, 2008).

**2.3.2 Mayatima na Watoto wasiokuwa na Usalama**

Kulingana na Wizara ya Afya, yatima wa UKIMWI ni mtoto aliye chini ya miaka kumi na mitano na ambaye aliwapoteza wazi wake kutokana na kifo kinachonasibishwa na janga la VVU/UKIMWI ( Ministry of Health, 2001). Idadi ya watoto mayatima na wasio na usalama almaarufu OVC imeongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na VVU/UKIMWI ( NACC, 2006).

Watoto kama hawa hukosa utunzaji na usimamizi wanouhitaji katika hatua hii muhimu ya maisha yao; hatua ya upeo wa matatizo yao. Kutokana na kufiwa na wazazi wote, watoto katika hatua hii hutunzwa na wanajamii wengine kama vile nyanya, shangazi na kadhalika. Kutokana na sababu ya umaskini, mara nyingi

watunzaji hawa hawana nguvu za kifedha ili kukidhi mahitaji ya watoto inavyostahili. Katika sehemu zingine, watoto walio na umri mdogo wa hata miaka kumi (10) huwa viongozi au vichwa vya nyumba ambapo wanachukua jukumu la kuwalea ndugu zao kufuatia kifo cha wazazi kutokana na VVU/UKIMWI (NACC, 2005). Katika hali kama hii, mtoto yatima hayuko salama kwa sababu anaweza kudhulumiwa kimapenzi katika jitihada zake za kutafuta pesa za kukidhi mahitaji ya wakongwe pamoja na ndugu zake.

## 2.4 Mikakati ya Serikali katika Vita dhidi ya VVU/UKIMWI

Serikali ya Kenya ikishirikiana na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali pamoja na wanajamii imeibuka na mikakati anuwai yenye lengo la kupunguza kuenea kwa VVU/UKIMWI na hatimaye kuumaliza kabisa ugonjwa huu. Watu binafsi wenye uwezo na ari ya kuwasaidia Wakenya walioathiriwa wamejitokeza na kuibua na kuendeleza kampeini kabambe zinazolenga kukomesha maambukizi mapya. Mfano mzuri ni mkewe rais wa Kenya Bi. Margaret Kenyatta anayeendesha kampeini inayowalenga kina mama waja wazito na watoto almaarufu *Beyond Zero Campaign*.

### 2.4.1 Uongozi na Uratibu wa Programu zinazohusu VVU/UKIMWI

Ikilinganishwa na utepetevu wa serikali kukabiliana na janga la UKIMWI katika miaka ya themanini, leo hii kuna msukumo na nia dhabiti ya kisiasa ya kupambana na UKIMWI nchini Kenya. Mwishoni mwa miaka ya tisini, serikali na wanasiasa mahususi walilizungumzia janga hili la UKIMWI kwa udhabiti zaidi. Serikali ya Kenya, wakati huo ikiongozwa na Daniel arap Moi ilitambua haja ya kuibua miongozo dhahiri ya sera, mikakati na mifumo ya mipangilio ambayo ingesaidia kukabiliana na janga la UKIMWI. Mswada wa Sera ya Kitaifa uliwasilishwa bungeni na kuidhinishwa tarehe ishirini na nne Septemba mwaka wa elfu moja mia kenda

tisini na saba (1997) kama Mswada wa Kikao Nambari 4 ya 1997 kuhusu UKIMWI nchini Kenya. Lengo la mswada huu lilikuwa kutoa sera tekelezi ambayo ingeongoza jitihada za kuzuia na kudhibiti UKIMWI katika kipindi cha miaka kumi na mitano iliyokuwa inakuja. Wizara ya Afya (2001) imeorodhesha malengo mahususi ya mswada huo kama yafuatayo:

Kwanza, kutoa mwongozo wa namna ya kushughulikia maswala yanayoelekea kuleta mabishano kwa kuzingatia hali zilizopo pamoja na miktadha ya kijamii. Pili, kuiwezesha serikali kuwa katika mstari wa mbele katika shughuli zote zinazolenga kuzuia na kudhibiti UKIMWI; mwelekeo wa kutumia mbinu anuwai uliowaleta na kuwahusisha washiriki wengi tofauti tofauti katika vita dhidi ya UKIMWI.Tatu, kupendekeza mwongozo mwafaka wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi pamoja na uratibu wa shughuli au programu zote zinazohusiana na UKIMWI.

Kuidhinishwa kwa maswada huo, kuliashiria nia ya serikali ya kusimamia shughuli zenye matokeo yanayotarajiwa katika kudhibiti kuenea kwa VVU, kulinda haki za waathiriwa pamoja na kuwatunza walioambukizwa na waliohasiriwa na janga la UKIMWI (Ministry of Health, 2001). Hatua hii ilifuatiwa na aliyekuwa rais kutangaza VVU/UKIMWI kuwa janga la kitaifa. Tangazo hili liliwavutia wahisani wengi wa kimataifa ambao walitoa misaada ya bidhaa na ya kitaaluma. Naye aliyekuwa rais wa tatu Mwai Kibaki alipochukua hatamu za uongozi mwaka wa elfu mbili na mbili (2002) mojawapo ya shughuli zake za kwanza ilikuwa kutangaza vita kamili dhidi ya UKIMWI (Total War on AIDS). Tangazo hili lilienda sambamba na kauli mbiu ya *Pomoja Tuangamize UKIMWI*; wito uliomlenga kila mtu. Matangazo haya yalikuwa viashiria vya kuonyesha kujitolea kwa serikali kuondolea mbali UKIMWI nchini Kenya.

Isitoshe, maafisa mashuhuri serikalini pamoja na wafanya biashara wamekuwa katika mstari wa mbele katika vita dhidi ya UKIMWI katika maeneo mbali mbali nchini. Mathalan, marehemu Mama Lucy Kibaki aliyekuwa mkewe rais wakati huo alipinga sera ya serikali juu ya matumizi ya kondomu. Shirika la habari la BBC iliripoti tarehe kumi na tisa Mei mwaka elfu mbili na sita (19/5/2006) kuwa Bi Kibaki alipinga msimamo wa serikali kuhusu matumizi ya kondomu kwa kuwashauri wanafunzi kujizuia kushiriki ngono badala ya kutumia mipira ya kondomu.

Kujizuia ni njia mojawapo ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU. Wakereketwa wa UKIMWI kwa upande wao nao wanahisi kuwa, matumizi ya kondomu ni njia ya pekee ambayo kwayo vijana wanaweza kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU. Hii ni kwa sababu wengi wao hushiriki ngono wakiwa na umri wa miaka kumi na minne na wengi hushindwa kujizuia. Hatua kama hizi kutoka kwa viongozi huenda zimechangia kupungua kwa maambukizi.

Kujitolea kwa afisi ya rais mwaka wa 1999 kukabiliana na UKIMWI kulipelekea kuanzishwa kwa baraza la kitaifa la kudhibiti UKIMWI (NACC). Baraza hili lilibuniwa kupitia kwa sheria za kubuni mashirika ya umma na Agizo la Kisheria la rais Nambari mia moja na sabini (170) lililotolewa tarehe 26/11/1999 (NACC, 2006). Hili lilionekana kuchipuza kutokana na mapendekezo ya Mswada wa Kikao Nambari Nne (4) juu ya UKIMWI. Lengo kuu la baraza hili ni kuongoza mwitikio wa kitaifa na kuhudumu kama chombo cha serikali cha uratibu. Majukumu yake ambayo yanaakisi malengo ya mswada huu yanajumuishwa katika kauli-wito ya NACC (1999) isemayo " Kutoa sera na mwongozo wa mikakati kwa ajili ya ukusanyaji na uratibu wa mali kwa lengo la kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuwatunza na kuwasaidia watu walioathiriwa na waliohasiriwa nchini Kenya" (Ministry of Health, 2001).

Hata hivyo shughuli ya uratibu katika kiwango cha taifa wakati mwingine huwa ngumu. Hii ni kwa sababu ya kuwepo kwa washiriki watendaji wengi wanaohusika na uratibu wa shughuli au programu za UKIMWI. Tatizo hili liliwaleta pamoja maafisa wote wanaohusika na UKIMWI kote ulimwenguni, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wale wa sekta ya kibinafsi kwenye mkutano wa kimataifa kuhusu UKIMWI na magonjwa ya zinaa. Matokeo ya mkutano huu ni kukubaliana juu ya kanuni tatu za kuongoza uratibu wa mikakati ya kukabiliana na UKIMWI. Kulingana na NACC (2006), kanuni hizo tatu ni:

Kwanza, mwongozo mmoja wa utekelezaji unaokuwa msingi wa uratibu wa shughuli za washiriki wote.Pili, kuwepo kwa shirika moja la kitaifa lililo na mamlaka ya kuratibu na lililo na mwelekeo wa kutumia mbinu anuwai na zilizopanuliwa.Tatu kuwepo kwa kiwango kimoja cha kitaifa chenye mfumo wa usimamizi na utathmini. Hatua hii ililipatia NACC nafasi yake faafu kama shirika moja la kitaifa lenye mamlaka ya uratibu. Shirika hili linafanya kazi katika mfumo changamano wa mipangilio na mitandao ambayo kwa pamoja hushirikiana kutekeleza makabiliano dhidi ya janga la UKIMWI nchini Kenya.

Mnamo mwaka wa elfu mbili na tatu (2003) serikali iligatua NACC katika kiwango cha eneo bunge. Mashirika gatuzi yaliitwa Baraza la Eneo Bunge la Kudhibiti UKIMWI maarufu kama Constituency Aids Control Councils (CACC). Lengo la ugatuzi huu lilikuwa kuwashirikisha wanajamii katika utekelezaji na kurahisisha kujumuishwa kwa mikakati ya kitaifa katika viwango vya mashinani.

### 2.4.2 Mikakati iliyopo Sasa

Kulingana na The Kenya National HIV and AIDs Strategic Plan (KNASP), mwongozo wa kuzuia kuenea kwa UKIMWI hujumuisha kutoshiriki ngono,

kuchelewesha kushiriki ngono ya mara ya kwanza, kuzuia maambukizi kutoka kwa mama hadi mtoto, kuhakikisha usalama wa damu, usalama wa sindano za kudungwa, tohara kwa wanaume, tiba ya haraka baada ya kushuku uambukizwaji, kuzoea kutumia kondomu na kwa njia sahihi, kupunguza idadi ya watu wa kushiriki ngono pamoja na mtu kujua hali yake ya VVU (NACC 2005). Yaelekea kuwa mwongozo huu wa (KNASP) umetambuliwa na kukubaliwa na serikali, mashirika ya kutetea haki za binadamu, Mawakala wa Umoja wa Mataifa, washirika wa kimaendeleo na sekta za umma zinazojihusisha na vita dhidi ya UKIMWI nchini Kenya. Uratibu wake wa kitaifa hutekelezwa na NACC. Mikakati yake ni mingi lakini hapa chini tumezungumzia michache tu.

### 2.4.3 Huduma za Unasihi na Upimaji wa Hiari (UUH)

Watu wanapozijua hali zao za VVU kupitia kwa kujipima, huenda wakabadilika kitabia na hivyo kukubali ushauri unaohusu namna ya kuzuia maambukizi. Kwa kufanya hivi, wanaweza kufanya maamuzi yanayofaa kuhusu maisha yao hasa kuhusiana na suala la ngono na hivyo kuepuka kuambukizwa tena au kuwaambukiza wengine. Vituo vya huduma za Unasihi na Upimaji wa Hiari almaarufu VCT, hutoa ushauri unaohitajika kwa wanajamii kabla na baada ya kujipima.

Kulingana na ripoti ya NACC (2008), lengo lilikuwa kupimwa kwa watu milioni mbili kila mwaka kati ya mwaka wa 2005-2010. Kati yao, watu laki tano walitarajiwa kupimwa katika vituo vya UUH huku milioni moja unusu wakipimwa hospitalini katika shughuli za matibabu na huduma zinazolenga kina mama wajawazito. Mkakati huu wa Unasihii na Upimaji kwa Hiari pia unahusisha matumizi ya vituo vya kuhamishwahamishwa, vituo vya kujipima usiku hasa usiku wa mbalamwezi, vituo vya kutumia ngamia hasa miongoni mwa wafugaji wa kuhamahama, huduma za nyumba hadi nyumba na uchunguzi wa mapema kwa watoto.

Vituo vya UUH huwawezesha wanajamii kupata usaidizi wa kisaikolojia, utunzaji na matibabu. Katika miaka ya hivi karibuni, vituo hivi vimekuwa vikiongezeka kwa kasi. Mathalan, kulikuwa na vituo vitatu tu kote nchini mwaka wa 2000 idadi ambayo imeongezeka na kufikia vituo elfu moja mwaka wa 2007 (NACC, 2008). Kipindi hicho pia kilishuhudia ongezeko la idadi ya watu waliovitembelea vituo hivi kutoka elfu moja hadi laki tano ( NACC, 2008). Hii ni kutokana na juhudi za serikali, wafadhili wa kimataifa, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali pamoja na mashirika ya kidini. Vituo vya UUH huchangia kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa kuwahimiza watu kujua hali zao. Wale waliopimwa na kugunduliwa kuwa na Virusi Vya UKIMWI hupata usaidizi zaidi kwa njia za ushauri, utunzaji na matibabu. Hata hivyo uchunguzi uliofanywa na Kenya Demographic Survey 2003 unaonyesha kuwa, licha ya kuongezeka kwa vituo vya UUH nchini idadi inaonyesha kuwa asilimia kumi na tatu (13%) ya wanawake na asilimia kumi na nne (14%) ya wanaume walikuwa wanajua hali zao za VVU/UKIMWI. Aidha, kulingana na ripoti hii, theluthi mbili hawakuwa wameendakupimwa ili wajue hali zao.

Mintaarafu ya ripoti hii, inabainika kuwa kuna haja ya serikali na watu binafsi kuimarisha kampeini za kuwahimiza watu kujua hali zao za UKIMWI/VVU na kampeini za kuzuia kuenea kwa maambukizi. Kuna sababu kadha wa kadha zianzowafanya watu kutotumia vituo vya UUH kikamilifu. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja na kuogopa kifo, unyanyapaa na ubaguzi kwa misingi ya kuwa na VVU/UKIMWI (NACC 2008, NACC 2006; NACC 2005).

### 2.4.4 Kuzuia Uambukizaji kutoka kwa Mama hadi kwa Mtoto

Kukosekana kwa mikakati ya kudhibiti hali hii, kina mama wajawazito walio na virusi vya UKIMWI wana nafasi ya asilimia kumi na tano (15%) hadi asilimia thelathini na tano (35%) ya kuwaambukiza watoto wao. Katika hali hii, mtoto

anaweza kuambukizwa akiwa tumboni, anapozaliwa au wakati wa kunyoyeshwa (NACC 2006). Hata hivyo, siku hizi kuna mbinu mwafaka ambazo zinaweza kutumiwa kuzuia maambukizi ya aina hii. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI almaarufu ARVs, usimamizi thabiti wa ukunga au uzazi na matumizi ya lishe mbadala almaarufu formula badala ya unyonyeshaji. Kwa sasa, kuna zaidi ya vituo elfu moja (1000) vya kuwahudumia kina mama wajawazito almaarufu ANCs humu nchini. Vituo hivi vinatoa huduma zianzolenga kuzuia maambukizi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto.

Uchunguzi uliofanywa na NACC (2005) unakadiria kuwa, asilimia sitini (60%) ya wanawake wajawazito wanaotembelea kliniki kabla ya kujifungua wanafaidi huduma za UUH kubainisha hali zao za UKIMWI. Uchunguzi huu unabainisha kuwa, matumizi ya ***Nevirapine*** aina mojawapo ya ARV miongoni mwa watoto yalikuwa asilimia hamsini na nane (58%) (NACC, 2006). Mbali na kutumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, huduma nyingine kama vile za mpango wa uzazi na ambazo ni za hiari hutolewa kwa kina mama wajawazito ili kuzuia mimba zisizotarajiwa na hivyo kupunguza uambukizaji unaotoka kwa mama hadi kwa mtoto.

### 2.4.5 Tahadhari za Mfumo wa Afya na Usalama wa Damu

Imethibitishwa kuwa mbali na ngono, VVU huambukizwa kupitia kwa damu yenye virusi vya UKIMWI, sindano zisizosafishwa na njia nyingine za kimatibabu zisizo salama. Usalama wa damu ni suala linalopewa umuhimu wa kwanza katika sekta ya Kitaifa ya Afya ya Umma. Sera inayoongoza utoaji wa damu nchini Kenya ilibuniwa mwaka wa 2001 kufuatia ongezeko la mahitaji ya damu iliyo salama na ya kutosha (NACC 2006). Madhumuni ya sera hii ni kulinda na kukuza afya ya wanaotoa damu na wanaoipokea. Sera hii inasisitiza kuwa damu yote inayotolewa ni sharti ichujwe kubainisha kuwepo au kutokuwepo kwa virusi kama vile vya UKIMWI, Homa ya

Manjano aina ya B, Kaswende, Kisono na kadhalika. Damu isiyo na virusi vyovyote vinavyoweza kupitishwa kwa njia ya upaji damu ndiyo inayoweza kutumiwa.

### 2.4.6 Kuhimiza Matumizi ya Kondomu

Ngono bila kinga katika mkabala wa janga la UKIMWI inaweza kusababisha uharibifu na maangamizi makubwa. Matumizi ya kondomu ni muhimu sana katika kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU na magonjwa mengine ya zinaa. Nchini Kenya, usambazaji wa kondomu za wanaume umeongezeka kwa kiwango kikubwa tangu mwaka wa elfu mbili na nne (2004) (NACC 2005).

Kulingana na ripoti ya NASCOP katika NACC (2006), kunadiwa kwa kondomu katika miktadha ya kijamii kumechangia kupanda kwa mahitaji na matumizi ya kondomu zote za kiume na za kike. Ripoti hii inaonyesha kuwa, ingawa aina zote mbili za kondomu zinapatikana, zile za kike hutumiwa kwa kiwango cha asilimia 05% pekee. Kampeini zinazoendelezwa na vyombo vya habari zimesaidia kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na kondomu na hivyo kuchangia kuhitajika kwake, kupatikana kwake pamoja na kutumika kwake kupanda.

Pamoja na hayo ni kwamba, juzi juzi ilipogunduliwa kwamba wengi wa watu wanaombukizwa Virusi Vya UKUMWI wako kwenye ndoa, kukatolewa tangazo *" Wachana na mpango wa kando la sivyo weka kondom mpangoni."* Tangazo hili lilizua ubishi mkubwa hasa kutoka kwa viongozi wa kidini wanaopinga matumizi ya kondomu kama kinga dhidi maambukizi na kupigia upatu mbinu za kujinyima ngono na kuwa mwaminifu katika ndoa.

### 2.4.7 Kutibu Magonjwa ya Zinaa

Kama ilivyotajwa awali katika sura hii, magonjwa ya zinaa ni mojawapo ya vipengele vielekezi vinavyochangia maambukizi na kuenea kwa VVU/UKIMWI. Kutokana na

sababu hii, kuyazuia, kuyadhibiti na kuyatibu magonjwa haya ni muhimu sana katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI nchini Kenya (Nyawira, 2008). Kulingana na (NACC 2006), UKIMWI ulienea kwa asilimia ishirini na tatu 23% miongoni mwa wanawake waliokuwa na ugonjwa wa zinaa na asilimia 37% miongoni mwa wanawake waliokuwa na vidonda katika viungo vya uzazi. Kuenea kwa VVU/UKIMWI miongoni mwa wanaume kulikuwa asilimia ishirini na mbili 22% kwa waliokuwa na vidonda kwenye viungo vya uzazi. Ripoti hii inaonyesha umuhimu wa kuyatibu na kuyadhibiti magonjwa ya zinaa. Ni kutokana na sababu hii ambapo NASCOP hutoa chati zenye michoro na itifaki za mafunzo zinazoongoza katika udhibiti wa magonjwa ya zinaaa kwenye vituo vyote vya umma vya afya nchini. Wizara ya Afya nayo hutoa hamasisho juu ya dalili za magonjwa ya zinaa (NACC, 2006).

### 2.4.8 Kuhimiza Utambuaji

Serikali ya Kenya imeweka jitihada kubwa katika kuwaelimisha na kuwajuza wananchi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kwa lengo kuu la kuwahimiza kubadilika kitabia. Kubuniwakwa shirika la kitaifa linalotoa habari kuhusu UKIMWI mwaka wa 2005 kumesaidia pakubwa kwa kuibua arafa zinazolenga kupunguza unyanyapaa unaohusishwa na VVU/UKIMWI. Shughuli za shirika hili la kitaifa pia zimegatuliwa kiameneo.

Kuhusiana na haya, aliyekuwa rais wa Kenya, Mwai Kibaki alikuwa katika mstari wa mbele katika kuibuka na kauli mbiu ya***"Pamoja Tuangamize UKIMWI".*** Wizara ya elimu nayo ikishirikiana na NACC imehusisha mada ya VVU/UKIMWI kwenye mtaala wa shule. NACC imefadhili kampeini nyingi kuhusu utambuaji wa magonjwa ya zinaa pamoja na VVU/UKIMWI kupitia vituo vya matangazo na kampeini za ana kwa ana.

Kufuatia dhihirisho kwamba watumiaji wa mihadarati na pombe wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa, kuambukizana wenyewe kwa wenyewe pamoja na kuwaambukiza wasio watumiaji ama kwa kujua au kutojua, serikali ya Kenya ilitambua haja ya kuwahusisha katika mikakati ya kitaifa ya kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI. Mathalan, kufuatia kongamano la 42 la kila mwaka la mawaziri wa afya kanda ya Afrika Mashariki lililofanyika Mombasa Februari 2006, iliafikiwa kuwa masuala yote yanayohusiana na pombe yahusishwe katika mipango ya kitaifa kuhusu VVU/UKIMWI. Aidha, iliafikiwa kuwepo kwa sera za kufaa kuhusu pombe na VVU/UKIMWI, kuwepo kwa miongozo na mipango pamoja na kuunda makundi tekelezi ya kitaaluma yatakayoongoza utekelezaji wa mipango inayohusiana na pombe na UKIMWI (NACC, 2006). Jitihada hizi zinaonekana wazi kupitia tangazo maarufu lililovuma kwenye vituo vya televisheni Kenya likisema ***"Unavyokunywazaidi ndivyo unavyoteleza zaidi"*** (Nyawira, 2008).

Mikakati mingine inayoweza kutumiwa kuzuia au kupunguza kuenea kwa maambukizi miongoni mwa watumiaji wa mihadarati ni pamoja na kampeini za kupinga matumizi ya sindnano moja kwa watu wengi, kuhimiza udungaji ulio salama, kuongeza idadi ya vituo vya UUH, kutumia mbinu ya upimaji yenye kutoa matokeo ya haraka kwenye madanguro, vyumba vya kuogea, makao yasiyokuwa nyumbani, mitaa inayotembelewa zaidi na wahusika na kadhalika.

### 2.4.9 Kuwatibu na Kuwatunza Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI

Huduma za matibabu kwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI almaarufu PLWHA ni suala ambalo serikali ya Kenya imelipatia kipaumbele. Tangu mwaka wa 2005, dawa za kupunguza makali zimekuwa zikitolewa bila malipo (NACC, 2008). Kulingana na ripoti ya (NACC, 2005), watu hamsini na nne elfu walikwua

wanatumia dawa hizi kufikia Septemba 2005. Serikali ya Kenya ililenga kuongeza idadi hii kufikia asilimia sabini na tano (75%) ifikapo mwaka wa elfu mbili na kumi (2010). Repoti hii inabainisha kuwa kwa sasa hospitali zote za mikoa na wilaya wakati huo zilikuwa zinatoa huduma za utunzaji, ushauri, kuzuia maambukizi na matibabu kwa kutumia dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI. Ingawa dawa hizi zinatolewa bila malipo, imeripotiwa kuwa, wakati mwingine wateja hukosa kuzichukua kwa sababu ya kitomudu kulipa huduma zingine zinazoambatana na matibabu haya kama vile kununua chakula maalum, dawa zingine za kutibu magonjwa mengine, kugharamia usafi na kadhalika. Kulikuwa na haja ya mfumo wa usaidizi kwa wanaotumia dawa husika uwe wa bila malipo (NACC, 2008). Shirika la NASCOP pia liliandaa mkakati wa kuongoza matibabu ya watoto walio na virusi. Ripoti zaonyesha kwamba, kufikia Septemba 2005, watoto elfu tatu mia tano walikuwa wanatumia dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (NACC, 2005).

Ni rahisi kwa wagonjwa wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kudhulumiwa haki zao. Mathalani,wanaweza kubaguliwa, kunyimwa haki ya kumiliki mali na haki ya urithi hususani wanawake na watoto Izumi (2006) katikaNyawira (2008). Watu hawa aghalabu hukosa kupata utunzaji, makaazi, elimu na chakula. Ingawa serikali ya Kenya haina sera na miongozo dhidi ya dhuluma hizi, imeweka sheria inayolinda makundi ya watu waliotengwa wakiwemo waathiriwa wa VVU/UKIMWI.

Mkakati mwingine uliowekwa na serikali kuhakikisha watu wanaoishi na VVU/UKIMWI wanatunzwa vizuri ni kuimarisha utunzaji wa kinyumbani. Huu ni mkakati unaokidhi mahitaji ya kiasili, kimatibabu, kiroho na za kijamii kwa wagonjwa husika. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na NASCOP imeandaa miongozo inayohusu utunzaji wa kinyumbani ikiwemo miongozo kuhusu lishe bora

na VVU/UKIMWI (NACC, 2006). Nyimbo nilizozichanganua zinazungumzia vipengele na hali hizi kwa njia moja au nyingine.

Maelezo yaliyotolewa hapo juu yanaonyesha radhi na jitihada zilizowekwa na serikali ya Kenya, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali pamoja na watu binafsi ili kumaliza kuenea kwa VVU/UKIMWI nchini Kenya, Afrika na ulimweguni kwa jumla. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa, VVU/UKIMWI ni suala changamano, lenye ncha nyingi na linalohitaji mbinu na mikakati anuwai ili kufanikisha vita dhidi yake. Hii ni kwa sababu kuna njia tofauti tofauti za kupata maambukizi jinsi makundi tofauti tofauti yalivyo kwenye hatari ya kuambukizwa na njia tofauti tofauti za kuzuia maambukizi.

### 2.5 Hali ya VVU/ UKIMWI Nchini Kenya

Kulingana na ripoti tangulizi ya Kenya AIDS Indicator Survey (2012), asilimia sifuri nukta tisa0.9% ya watoto walio na umri kati ya miezi kumi na minane (18) na miaka kumi na minne (14) wameambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Asilimia hii ni sawa na karibu watoto elfu mia moja na nne(104,000) walioambukizwa katika taifa zima. Kulingana na ripoti hii idadi hii haijumuishi watoto walio na umri wa chini ya miezi kumi na minane (18) pamoja na watoto kutoka eneo la Kaskazini Mashariki mwa Kenya. Kwa upande wa watu wazima, ripoti hii inaeleza kuwa, kwa jumla, asimilia tano nukta sita 5.6% ya watu wazima wenye umri kati ya miaka kumi na mitano (15) na sitini na nne(64) walikuwa wameambukizwa VVU. Asilimia hii ni sawa na kadirio la watu milioni moja, elfu mia moja tisini na mbili (1,192,000) waliokuwa wakiishi na VVU/UKIMWI kabla ya mwaka huo wa 2012. Hali hii ni kinyume na ilivyokuwa mwaka wa 2007 ambapo KAIS ilikadiria kuenea kwa VVU/UKIMWI katika kitengo hiki kwa asilimia saba nukta mbili 7.2%. Kwa mara nyingine, makadirio haya hayakujumuisha Kaskazini Mashariki mwa Kenya.

### 2.5.1 Maambukizi ya VVU Miongoni mwa Wanawake na Wanaume

Takwimu za kijinsia zinaonyesha kuwa wanawake ndio walioathirika zaidi. Ripoti hii inabainisha kuwa, katika kitengo cha umri kati ya miaka kumi na mitano (15) na sitini na nne (64) asimilia 6.9% ya wanawake walikuwa wameambukizwa. Hii ni idadi kubwa ikilinganishwa na asilimia 4.4% ya wanaume walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI mwaka huo wa 2012. Hali kama hii ilibainika katika KAIS (2007). Kwa ujumla, kupungua kwa maenezi ya maambukizi kulishuhudiwa kati ya mwaka 2007 na 2012 miongoni mwa wanaume na wanawake.

Kiumri, ripoti hii inabainisha kuwa, kulikuwa na tofauti kimaenezi kutoka umri mmoja hadi mwingine. Ilibainika kuwa, maambukizi yaliongezeka kadri umri ulivyoongezeka, hivi kwamba maenezi ya juu kabisa yalishuhudiwa miongoni mwa watu wazima waliokuwa na umri kati ya miaka arobaini na tano hadi hamsini na nne (45-54). Maambukizi na maenezi yalishuka kwa kiwango kikubwa miongoni mwa wale waliokuwa na umri kati ya miaka hamsini na mitano na sitini na nne (55-64). Kulingana na KAIS (2007), maambukizi yalikuwa juu miongoni mwa wale waliokuwa katika kitengo cha umri wa miaka ishirini na mitano hadi thelathini na nne (25-34).

### 2.5.2 Maambukizi ya VVU/UKIMWI Kimaeneo

Ueneaji wa VVU/UKIMWI kimaeneo ulionyesha kutofautiana katika taifa zima. Eneo la Nyanza liliongoza kimaambukizi kwa asilimia kumi na tano nukta moja (15.1%) huku eneo la Kaskazini Mashariki likiwa la mwisho kwa asilimia mbili nukta moja (2.1%). Aidha maambukizi yalipungua kwa kiasi kikubwa yakilinganishwa KAIS 2007. Mathalani, kupungua kwa maambukizi kulishuhudiwa Nairobi kwa asilimia arobaini na nne (-44%), Pwani kwa asilimia arobaini na saba (-47%) na Bonde la Ufa kwa asilimia arobaini na moja (-41%).

Ripoti hii pia ilibainisha kuwa, kimakaazi, maambukizi yalikuwa juu mijini ikilinganishwa na vijijini au mashambani. Kulingana na ripoti hii, karibu asilimia sitini na tano (65%) ya watu wengi walioambukizwa huishi  mashambani wakati wa kufanywa kwa uchunguzi huu. Ilidhihirika kwamba, VVU/UKIMWI ulienea kwa asilimia sita nukta tano (6.5%) mijini na kwa asilimia tano nukta moja (5.1%) mashambani. Isitoshe, ripoti hii inaonyesha kuwa, miongoni mwa watu walio na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi sitini na nne (15-64), kulikuwa na uwezekano wa wanawake wengi kuambukizwa kuliko wanaume iwe mijini au mashambani. Mathalani, asilimia nane (8.0%) ya wanawake wanaoishi mijini walikuwa wameambukizwa ikilinganishwa na asilimia tano nukta moja (5.1%) ya wanaume wanaoishi mijini. Aidha, asilimia sita nukta mbili (6.2%) kutoka mashambani walikuwa wameambukizwa ikilinganishwa na asilimia tatu nukta tisa (3.9%) ya wanaume wakaazi wa mashambani.

**2.5.3 Maambukizi  ya VVU/UKIMWI na Viwango vya Elimu**

Kulingana na Kenya National Bureau of Statistics (2012), maambukizi ya VVU/UKIMWI yalikuwa ya juu miongoni mwa wanaume na wanawake katika viwango vyote vya elimu. Usambazaji ulikuwa wa kiwango cha asilimia nne (4.0%) miongoni mwa wanaume na asilimia mbili nukta nne (2.4%) ya wanawake wasiokuwa na elimu ya shule ya msingi. Isitoshe, ripoti hii yaonyesha kuwa, usambazaji wa VVU miongoni mwa wajane ulikuwa wa kiwango cha juu sana. Kwa mfano, asilimia ishirini nukta tatu (20.3%) ya wajane wa kiume walikuwa wameambukizwa huku asilimia kumi na tisa nukta mbili (19.2%) ya wajane wa kike wakiwa wameambukizwa. Maambukizi yalikuwa ya kiwango cha chini miongoni mwa wale ambao hawakuwa kwenye aina yoyote ya ndoa.

Kujipima katika vituo vya UUH kunahitajika ili mtu ajue hali yake ya VVU/UKIMWI na kupata huduma za utunzaji na matibabu. Kulingana na NASCOP(2010), asilimia sabini na mbili (72%) ya watu wazima waliokuwa na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi sitini na nne (15-64) waliwahi kupimwa. Hili lilikuwa ongezeko kubwa likilinganishwa na asilimia thelathini na nne (34%) mwaka wa 2007. Ripoti hii yaonyesha kuwa kulikuwa na uwezekano mkubwa kwa wanawake wengi kupimwa kuliko wanaume. Idadi ya wanawake waliowahi kupimwa ilikuwa asilimia themanini (80%) ikilinganishwa na asilimia sitini na tatu (63%) ya wanaume. Miongoni mwa waliopimwa, idadi kubwa ya asilimia hamsini na sita (56%) walipimwa katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyokuwa imepita. Miongoni mwao, asilimia sitini na saba (67%) walikuwa wamepimwa angalau mara moja maishani mwao huku asilimia thelathini na tano (35%) wakiwa waliowahi kupimwa pamoja na mshirika wa ngono.

Miongoni mwa watu walioambukizwa, asilimia arobaini na saba (47%) waliripotiwa kuwa na VVU, huku asilimia thelathini na saba (37%) wakiripoti kuwa hawakuwa na VVU. Aidha, asilimia kumi na sita (16%) walikuwa wamepimwa lakini hawakuwahi kupata matokeo ya kupimwa kwao. Idadi ya watu waliojua kuwa walikuwa na VVU ilikuwa imeongezeka mara tatu kutoka asilimia kumi na sita (16%) mwaka wa 2007 hadi asilimia arobaini na saba (47%) mwaka wa 2012.

### 2.5.4 Maambukizi Miongoni mwa Walio kwenye Ndoa

Mintaarafu ya Kenya National Bureau of Statistics (kama hapo juu), kati ya watu elfu nne mia mbili ishirini na sita (4,226) waliokuwa kwenye ndoa au waliokuwa wanakaa kinyumba, asilimia arobaini na saba (47%) walikuwa na matokeo ya kupimwa kwao. Asilimia thelathini na tano (35%) walikuwa na matokeo ya mshirika au mwenzi mmoja huku asilimia kumi na nane (18%) wakikosa matokeo ya washirika au wenzi

wote wawili. Miongoni mwa wanajamii ambapo wenzi wote wawili walipimwa na matokeo kujulikana, asilimia tisini na mbili (92%) hawakuwa na VVU. Asilimia tatu (3%) zilionyesha kuwa wenzi wote wawili walikuwa na VVU, huku asilimia tano (5%) zikionyesha kuwa mwenzi mmoja alikuwa na VVU huku mwingine akikosa kuwa navyo.

### 2.5.5 Maambukizi na Suala la Tohara kwa Wanaume

Kuhusu uhusiano kati ya UKIMWI na tohara, ripoti hii inaeleza kuwa, wanaume waliotahiriwa wana kiwango cha chini cha hatari ya kuambukizwa VVU. Mathalani, ripoti za KAIS (2007; 2012) zinaonyesha kuwa, maambukizi miongoni mwa wanaume waliopashwa tohara yalikuwa chini yakilinganishwa na wale ambao hawakutahiriwa. Vile vile ripoti ya KAIS (2012) inaonyesha kuwa, maambukizi miongoni mwa wasiotahiriwa yalikuwa mara tano ya wale waliotahiriwa. Idadi ya wanaume waliotahiriwa iliongezeka kutoka asilimia themanini na tano (85%) hadi asilimia tisini na moja (91%) KAIS (2012). Ongezeko hili lilishuhudiwa kote nchini huku Nyanza ikiongoza kwa kupata ongezeko la kutoka asilimia arobaini na nane (48%) hadi asilimia sitini na sita (66%). Nyanza ilifuatiwa na Nairobi iliyoshuhudia ongezeko la kutoka asilimia themanini na tatu (83%) hadi asilimia tisini na mbili (92%). Tohara katika maeneo haya mawili yaliwahusisha wanajamii ambao kiutamaduni huwa hawashiriki upashaji tohara.

### 2.5.6 Maambukizi Miongoni mwa Walioshiriki Ngono

Kuhusu kitendo cha kushiriki ngono, asilimia saba (7%) ya vijana waliokuwa na umri kati ya miaka kumi na miwili na kumi na minne (12-14) waliripoti kuwahi kushiriki ngono. Miongoni mwa watu wazima waliokuwa na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi miaka ishirini na minne (15-24), asilimia sitini na sita (66%) ya wanawake na asilimia hamsini na tisa (59%) ya wanaume walikuwa wamewahi

kushiriki ngono. Miongoni mwa hao, asilimia ishirini na moja (21%) waliripoti kushiriki ngono kwa mara ya kwanza kabla ya kutimiza umri wa miaka kumi na mitano (15). Miongoni mwa wale waliokuwa na uwezo wa kushiriki ngono na waliokuwa na umri wa miaka kumi na mitano hadi miaka ishirini na minne (15-24), asilimia nne (4%) ya wanawake na asilimia thelathini (30%) ya wanaume walikiri kushiriki ngono na wenzi zaidi ya mmoja katika miezi kumi na miwili iliyokuwa imepita. Asilimia hamsini na saba (57%) ya wanawake na asilimia thelathini nanane (38%) ya wanaume waliripoti kuwa walijua hali ya VVU ya mwenzi wake wa ngono. Oguya na wenzake katika NACC (2009).

### 2.5.7 Maambukizi na Matumizi ya Kondomu

Kuhusu matumizi ya kondomu, Oguya na wenzake (kama hapo juu) wanaongeza kuwa, asilimia arobaini na tatu (43%) ya wanaume waliripoti kuzitumia wanaposhiriki ngono na watu ambao hawakuwa na uhakika kuhusu hali yao ya VVU. Miongoni mwa wale waliokuwa na umri wa kati ya miaka ishirini na mitano hadi sitini na minne (25-64) na ambao walikuwa na uwezo wa kushiriki ngono, asilimia tatu (3%) ya wanawake na asilimia kumi na saba (17%) ya wanaume waliripotiwa kushiriki ngono na wenzi wengi katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyokuwa imepita. Asilimia arobaini na nane (48%) ya wanawake na asilimia sitini na moja (61%) ya wanaume walikuwa na habari kuhusu hali ya VVU ya wenzi wao wa ngono. Katika kitengo hiki, asilimia tano (5%) ya wanawake na asilimia kumi na nne (14%) ya wanume waliripoti kutumia kondomu wakishiriki ngono na wenzi ambao hawakuwa na uhakika juu ya hali yao VVU.

### 2.5.8 Maambukizi Miongoni mwa Walio katika Hatari ya Kuambukizwa

Kuhusu wanajamii walioko kwenye hatari ya kuambukizwa, KAIS (2012) inaeleza kuwa, asilimia sifuri nukta moja (0.1%) ya wahojiwa walikuwa wamewahi kutumia mihadarati ya kujidungia. Asilimia moja (1%) ya wanaume waliripoti kushiriki ubasha. Asilimia tatu (3%) ya wanaume waliripoti kushiriki ngono ya malipo ambapo pesa, zawadi na mpendeleo mengine yalitolewa kugharamia ngono. Aidha, asilimia nne (4%) ya wanawake waliripotiwa kuwahi kushiriki ngono ya mwanamke kwa mwanamke. Kwa upande mwingine, kulikuwa na idadi kubwa ya wanaume; asilimia kumi na saba (17%) walioripoti kutoa pesa, zawadi au mapendeleo ili kulipia ngono. Asilimia tano (5%) kati yao waliripoti kufanya hivi ndani ya kipindi cha miezi kumi na miwili iliyokuwa imepita.

### 2.5.9 Maambukizi kutoka kwa Mama hadi kwa Mtoto

Mojawapo ya mikakati iliyowekwa hasa na taasisi za afya katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI ni kuzuia visa vya maambukizi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto yaani *Prevention of Mother To Child Transmission*(PMTCT). Kulingana na World Health Organization (WHO, 2010), miongoni mwa wanawake wenye umri kati ya miaka kumi na mitano na hamsini na nne (15-54) waliripoti kujifungua salama. Kati ya mwaka wa 2007 na 2012, asilimia tisini na sita (96%) walihudhuria kliniki za kuwahudumia kina mama wajawazito. Asilimia tisini na mbili (92%) kati yao walipimwa kubainisha hali yao ya VVU. Hali hii iliimarika ikilinganishwa na ilivyokuwa KAIS (2007), ambapo asilimia sitini na tano (65%) ya wanawake waliohudhuria kliniki hizi walikuwa wamepimwa kubainisha hali yao ya VVU, hii ikiwa mojawapo ya huduma zinazotolewa kwa kina mama wajawazito kabla ya kujifungua almaarufu ANCs. Asilimia tatu (3%) walijitangaza binafsi kuwa na VVU na asilimia tisini (90%) kati yao walipata huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa

mama hadi kwa mtoto. Asilimia themanini na tatu (83%) ya watoto waliozaliwa na kina mama waliopata huduma za PMTCT walipimwa kubainisha hali yao ya VVU walipopelekwa kwa chanjo mara ya kwanza. Asilimia kumi na sita (16%) ya watoto hawa waliripotiwa na mama zao kuwa na VVU.

### 2.5.10 Maambukizi na huduma za Afya

NASCOP (2011) inabainisha viwango vya matumizi ya huduma za matibabu na utunzaji kwa walio na VVU. Inaeleza na kupendekeza kuwa, kila mtu aliyepimwa na kubainika kuwa na VVU anafaa kuanza kutumia dawa zinazopunguza vifo vya mapema vinavyosababishwa na magonjwa nyemelevu kama vile malaria, kifua kikuu na tumbo la kuendesha. Aidha, dawa hizi huwaepushia waathiriwa dhiki ya kutembelea hospitali mara kwa mara kwa ajili ya matibabu. NASCOP (kama hapo juu) yaonyesha kuwa, asilimia themanini na tisa (89%) ya watu waliojua hali yao ya VVU walikuwa wanatumia dawa hizo. Idadi hii iliimarika kutoka asilimia sabini na sita (76%) ya mwaka wa 2007.

Mbali na hayo, viwango vya matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI pamoja na matibabu ya kitaaluma almaarufu Antiretroviral Theraphy (ART) viliongezeka. Hii ni kwa sababu miongozo ya kitaifa kwa sasa inapendekeza utolewaji wa huduma hii kwa watu wazima na vijana waliobaleghe ikiwa kinga yao iko chini ya kiwango kinachohitajika. Miongoni mwa wanajamii walio na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi sitini na nne (15-64) walioambukizwa VVU, asilimia hamsini na nane (58%) walihitimu kiwango cha kuanzishiwa matibabu ya ART. Asilimia sitini na tatu (63%) waliripoti kufaidi matibabu hayo ya ART. Miongoni mwa watu wote walioambukizwa VVU katika kitengo hiki na ambao walistahiki matibabu ya ART, asilimia themanini na nane (89%) walikuwa wanapata matibabu hayo. (NASCOP, 2011).

### 2.5.11 Viwango vya Ufanisi Vilivyoafikiwa

KAIS (2012) aidha, ilichunguza viwango vilivyofikiwa katika jitihada za kukomesha kuenea kwa VVU miongoni mwa waathiriwa. Kulingana na ripoti hii, matibabu ya ART yatachukuliwa kuwa yamefaulu yakiweza kutimiza na kudumisha ukomeshaji wa ueneaji wa VVU miilini mwa walioambukizwa. Kulingana na ripoti hii, asilimia arobaini (40%) ya waathiriwa waliokuwa na umri kati ya miaka kumi na mitano hadi sitini na nne (15-64) walikuwa wamefaulu kukomesha kuenea kwa VVU miilini mwao. Hata hivyo, ukomeshaji wa maenezi ya VVU miongoni mwa watu waliofaidi matibabu ya ART ulikuwa umefaulu kwa kiwango cha asilimia sabini na nane (78%), kiwango sawa na kile kilichoshuhudiwa katika mataifa yaliyoendelea.

Isitoshe, uchunguzi wa KAIS (kama hapo juu) uliangazia mwendelezo wa huduma ya utunzaji wa waathiriwa wa UKIMWI wenye umri kati ya miaka kumi na mitano hadi sitini na nne (15-64). Ripoti ya uchunguzi huo inabainisha kuwa, ingawa utunzaji unaohusisha waathiriwa wa VVU ulikuwa wa kiwango cha juu miongoni mwa waliokuwa wanajua hali zao za VVU, ni asilimia arobaini na tatu (43%) pekee waliobainishwa kuwa na VVU na kuwekwa chini ya mpango wa utunzaji. Pengo hili la utunzaji miongoni mwa walioambukizwa linaangazia umuhimu wa mtu kujua hali yake ya VVU ili atafute huduma za utunzaji.

Watoto ni sehemu muhimu ya jamii. Wao pia huathirika kutokana na maambukizi ya VVU kwa njia moja au nyingine. KAIS (2012) ilichunguza hali ya utunzaji na matibabu miongoni mwa watoto walioambukizwa VVU. Ripoti yake inabainisha kuwa, miongoni mwa watoto wenye umri wa kuanzia miezi kumi na minane hadi miaka kumi na minne, asilimia arobaini na moja (41%) waliripotiwa kuambukizwa VVU kabla ya KAIS (2012). Miongoni mwao, asilimia mia moja (100%) walikuwa wanapata huduma za utunzaji zinazolenga wanaoishi na VVU. Miongoni mwa watoto

waliokuwa wanapata huduma hizi, asilimia mia moja (100%) walikuwa wanatumia dawa za kupunguza kuenea kwa VVU almaarufu CTX, huku asilimia sabini na moja (71%) wakinufaika kutokana na huduma za ART. Asilimia arobaini (40%) ya wale waliotumia ART walikuwa wamefaulu kukomesha kuenea kwa VVU.

Takwimu hizi za hivi karibuni zinazoonyesha hali ya VVU/UKIMWI nchini Kenya kwa sasa zinatupa taswira tatu. Mosi, zinaonyesha kuwa maambukizi na maenezi ya VVU kitaifa yamepungua kutoka asilimia saba nukta mbili (7.2%) katika KAIS (2007) hadi asilimia tano nukta sita (5.6%) katika KAIS 2012. Pili, jitihada za serikali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali hazijafaulu katika kuangamiza VVU/UKIMWI nchini kabisa kabisa. Isitoshe, takwimu hizi zinaonyesha kuwa, mikakati ya kisayansi peke yake kwa sasa haitoshi katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI na hivyo kusawiri hali ambayo bado inatamausha. Ili kushinda vita dhidi ya VVU/UKIMWI, watu binafsi, serikali na mashirika mengine yanafaa kuchunguza mchango wa utamaduni kwani ndio kikwazo kikubwa zaidi. Vipengele vya utamaduni wa wanajamii kama vile desturi zao, mienendo yao ya kiutamaduni, itikadi zao na kadhalika vinafaa kushirikishwa katika kubuni mikakati, mbinu na sera za kukabiliana na VVU/UKIMWI.

Mradi wa Milenia wa Umoja wa Mataifa unapendekeza kuwa, iwapo mabadiliko ya kitabia yanayotarajiwa kutoka kwa jamii mbalimbali nchini Kenya kuhusiana na kumaliza janga la VVU/UKIMWI yatadumu, kaida na desturi zilizokita mizizi katika utamaduni zinafaa kushughulikiwa haraka iwezekanavyo. Mabadiliko ya kudumu yanaanza na wanajamii wenyewe. Chambilecho wahenga, fimbo iliyo mkononi ndiyo inayoua nyoka. Desturi za kitamaduni zinazotumiwa na wanajamii kujieleza kama vile nyimbo, muziki na sanaa nyinginezo za kiutendaji huenda zikawa fimbo iliyo mkononi inayoweza kutumiwa kushinda vita dhidi ya VVU/UKIMWI. Vipengele hivi

vya utamaduni vina uwezo mkubwa wa kuwasilisha ujumbe na hivyo kuathiri mwenendo wa wanajamii (Nyawira, 2008).

## 2.6 Mapitio ya Maandishi kuhusu Nyimbo na Makabiliano ya UKIMWI

### 2.6.1 Nyimbo kama njia ya Kuwaunganisha Watu

Ahmadi (2005) amefanya utafiti kuhusu muziki na UKIMWI miongoni mwa wahasiriwa wa ugonjwa huu kule Afrika Kusini. Utafiti wake umeonyesha kuwa muziki unaweza kutumiwa kuwaunganisha watu pamoja hasa wale walioambukizwa na VVU/UKIMWI. Anaeleza kuwa sanaa katika muziki husababishwa na uwezo wake wa kiubunifu. Anadai kuwa mtagusano kati ya muziki na mteja hutokea pale ambapo mteja anahisi kuwa ametambulika.

Ahmadi (2005) anaona muziki kama tiba lakini akimrejelea Ruud (1998) anaeleza kuwa tabibu wa kimuziki hutumia muziki kutekenya sehemu ambazo hazijaathiriwa ili kutumiwa kimuziki na hivyo kuleta matumaini badala ya utamaushi. Anaeleza kuwa ugonjwa wa UKIMWI ni zao la kijamii na mbali na matumizi ya dawa za kupunguza makali (ARVs), hali ya afya inafaa kuboreshwa. Anasema kuwa muziki, kwa kuwa una sifa ya kidayolojia una uwezo wa kupunguza upweke na kuwafanya wagonjwa wajieleze na hivyo kujitathmini tena.

Pengo lililopo ni kuwa Ahmadi hajabainisha ni muziki wa aina gani anaozungumzia. Aidha hajaeleza ni vipengele vipi katika muziki vinavyouwezesha kuwa na sifa za kidayolojia. Ingawa utafiti wake ulilenga kuonyesha namna muziki unavyokuwa tiba fulani kwa wahasiriwa wa UKIMWI, sifa zinazowezesha hali hii hakuzibaini. Ingekuwa bora kama angetoa mifano ya nyimbo husika kisha azichanganue na kubainisha sifa zinazosababisha kuwepo kwa dayolojia na mshikamano.

### 2.6.2 Nyimbo kama njia ya kukabiliana na UKIMWI

Nyawira (2008) alichunguza diskosi katika nyimbo pendwa za Kenya kwa lengo la kubainisha mchango wake katika vita dhidi ya UKIMWI. Alijiwekea upeo wa Nairobi kisha kuchunguza nyimbo pendwa nne za wasanii mbalimbali.Mbali na kuchunguza nyimbo husika, kisauti pia alizichunguza kimuziki. Kwa kufanya hivi, alibainisha namna wasanii wa muziki pendwa wanavyotumia lugha kuwasilisha habari zinazohusiana na UKIMWI. Aidha kinyume na alivyofanya Ahmadi, Nyawira alitupatia nyimbo husika.

Utafiti huu basi utachangia utafiti wa Nyawira hasa kwa kupanua upeo wa nyimbo, hadhira na muktadha. Hii ni kwa sababu, pale ambapo Nyawira alijikita katika muziki pendwa, unaolenga hadhira ya vijana, nyimbo nilizozichunguza zinalenga hadhira pana ya Wakenya wasioenda makanisani na wale wanaoshiriki makanisani pamoja na vijana pia. Hii ni kwa sababu niliziteua nyimbo zisizokuwa za dini na zile za dini ambazo zimeimbwa kwa lugha za kiasili na kwa Kiswahili.

Njogu (2003) anapendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa kukabiliana na masuala ya kiafya huku zikiburudisha. Anasisitiza kuwa sanaa huwa na dhima muhimu katika kuhakikisha kuwepo kwa afya nzuri hususan miongoni mwa vijana. Isitoshe, anapendekeza kuwa, kwa sababu janga la UKIMWI ni tisho kubwa kwa jamii, mikakati yote ya kiafya itafute njia muafaka za kukabiliana nalo. Anaeleza kuwa janga hili huwaathiri zaidi wanawake na wasichana barani Afrika kwa sababu yaumaskini unaozidi kila kuchao, ubaguzi wa kijinsia, uhaba wa vifaa vya kiafya vinavyovutia kwa vijana na ukosefu wa miundo misingi hasa katika makaazi ya mabanda naya mashambani. Kwa mujibu wa Njogu, matatizo changamano yanayosababishwa na janga la UKIMWI yanahitaji mwelekeo wa kutumia mbinu anuwai ili kuyatatua. Nyimbo ni mojawapo ya njia zinazowavutia wanajamii.

Mapendekezo ya Njogu ni kuwa, pamoja na kutumia tiba za kitaaluma, inafaa pia kutumia utamaduni na burudani. Imani yake ni kuwa mbinu hizi zitachangia pakubwa katika kuzuia kuenea kwa VVU. Isitoshe nyimbo husika ni kipengele cha utamaduni na hutumiwa kuburudisha huku zikishiriki vita dhidi ya UKIMWI. Diskosi za kijamii zilizomo katika nyimbo husika zinahusu suala laUKIMWI. Aidha, azma yake ya kutumia lugha ya Kiingereza na zile za kiasili katika sanaa ya komedi kuwasilisha habari kuhusu UKIMWI inaafikiana na uamuzi wangu wa kuteua nyimbo za Kiasili kwani lugha hizi ni miongoni mwa lugha za kiasili alizolenga Njogu. Uamuzi wake ulitokea baada ya kuwasilisha habari kuhusu VVU/UKIMWI kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika komedi ya 'Ushikwapo Shikamana'.

Mboya (2009) alichunguza nyimbo mbili za Benga zilizosanifiwa na Okatch Biggy. Katika uhakiki wa nyimbo hizi, Mboya alichukua mtazamo wa kisiasa na kubainisha jinsi msanii alivyosawiri masuala ya ngono, UKIMWI na siasa za kikabila. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa, UKIMWI umetumiwa kama silaha ya kisiasa. Silaha hii kulingana na msanii imetumiwa kuwadhulumu Wajaluo kisiasa, kwamba ni watu wapenda raha, muziki, dansi, pombe, mavazi na ngono. Kwa sababu hii hawawezi kuzingatia mambo mazito ya 'maendeleo' na hivyo hawapaswi kupewa nafasi ya kuongoza Kenya. Mboya hakubainisha vipengele vya lugha vinavyohusika katika kuwasilisha ujumbe. Aidha, alizichanganua nyimbo za Dholuo. Utafiti huu umechukua mtazamo wa kuchanganua nyimbo za kiasili na za Kiswahili. Katika kufanya hivyo nimeonyesha namna vipande vya simulizi vilivyomo katika nyimbo vinavyoweza kuwasilisha habari kuhusu UKIMWI.

Mutembei (2009) alichunguza kuibuka na kuenea kwa UKIMWI nchini Tanzania kwa kujikita katika uchanganuzi wa mashairi yenye mada ya UKIMWI.Mutembei

anaeleza kuwa, utafiti wa ushairi katika tiba hasa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia unabainisha kuwa, njia hiyo huondoa wasiwasi kwa wagonjwa ambao hukaribia kufanyiwa upasuaji, husaidia kupunguza kiwango cha nusu kaputi ambacho hupewa wagonjwa wanaosubiri kupasuliwa, na hupunguza hitaji la madawa wapewayo wagonjwa baada ya kupasuliwa. Anaendelea kueleza kwamba ushairi ukitumika na taswira zinazoundwa katika mawazo ya mgonjwa ambapo mgonjwa hutengenezewa jazanda za kumliwaza, basi ushairi huweza kuondoa maumivu sugu aliyokuwa nayo mgonjwa. Aidha, muziki ambao huwekwa katika kanda za redio na kuendelea kuimbwa kwa muda umeonekana kupunguza uchungu wa uzazi kwa akina mama wajawazito.

Maelezo ya Mutembei (kama hapo juu) yalinifaa kwa kuwa ushairi anaouzungumzia una ukuruba na nyimbo au muziki kwani zote zinaweza kutazamwa kama tanzu za fasihi simulizi. Ikiwa taswira zinaweza kuundwa katika mawazo ya mgonjwa na jazanda za kumliwaza zikaundwa kupitia ushairi, hali hii inawezekana pia kupitia kwa nyimbo. Nyimbo zilizoshughulikiwa katika tasnifu hii zina taswira na huunda jazanda za kuwafariji walioambukizwa VVU/UKIMWI na hivyo kuondoa uchungu sugu pamoja na wasiwasi walionao. Isitoshe, anaeleza kuwa nyimbo hurudisha thamani na kuumba upya utu wa mtu kwani hugusa fikra za mwimbaji na pia za msikilizaji. Hali hii inabainika katika nyimbo zilizochanganuliwa katika tasnifu hii kwani zinazungumzia masuala kama vile ujinsia, utabaka na unyanyapaa.

Kwa kuwa wanajamii wameliumba upya janga la UKIMWI, hii ina maana kuwa watalijadili janga hili kwa lengo la kupunguza makali yake hasa ikizingatiwa kuwa ugonjwa huu haujapata tiba. Hata hivyo, miongoni mwa jamii nyingi za Kenya, ni mwiko kuzungumzia suala hili moja kwa moja kwa sababu linahusiana zaidi na suala

zima la ngono (Achoka katika Kobia, 2008). Wasemaji wa lugha za kiasili na Kiswahili na vijana wanaotumia Sheng wanakumbwa na pingamizi hili katika maongezi yao ya kawaida. Ni kupitia kwa vipande vya simulizi katika nyimbo ambapo masuala ya UKIMWI yanaweza kuwasilishwa bila pingamizi yoyote.

Shitemi (2012) anaeleza kuwa nyimbo za kuimbwa na kutendwa katika fasihi simulizi hutokea katika miktadha ya kijamii. Nyimbo hizi zimesheheni maudhui, mada na maadili muhimu. Ametoa mifano ya matini ya nyimbo ambayo hutokana na miktadha ya kijamii kama vile, kuzaliwa kwa mtoto, tohara, ndoa, mazishi na kazi. Shitemi anaeleza kuwa nyimbo zimetumika tangu jadi katika jamii za Kiafrika kwenye miktadha ya aina hii. Kutokana na maelezo haya, VVU/UKIMWI inaweza kutazamwa kama mada iliyokitwa katika miktadha ya kijamii.

### 2.6.3 UKIMWI na Ulemavu

Mboya (2005) akitoa mchango wake katika warsha kuhusu UKIMWI na Viziwi anapendekeza kuwa, ili viziwi waweze kufaidika kutokana na matangazo yanayohusu UKIMWI, matangazo husika yanafaa kutumia ishara vizuri.Aidha anapendekeza matumizi ya mbinu anuwai za uoni. Kwa kufanya hivi, viziwi hawataendelea kutengwa kwa sababu ya kutopata habari muhimu kuhusu UKIMWI. Hii ni kwa sababu hata wao wanaathirika kutokana na ugonjwa huu kama wanajamii wengine.

Mukasa (2005) akitoa mchango wake kwenye warsha hiyo hiyo anaeleza kuwa, Muungano wa kitaifa wa Umoja wa Viziwi Uganda (The Uganda National Association For The Deaf – UNAD) umeweka mikakati anuwai kuhakikisha kuwa viziwi wanahusishwa vilivyo katika masuala ya UKIMWI. Mojawapo ya mikakati hiyo ni matumizi ya teknolojia ya habari, mawasiliano na elimu pamoja na drama, nyimbo na mawasiliano ya video. Maoni haya ya Mboya na Mukasa (kama hapo juu)

yalinifaa katika utafiti huu kwa sababu, yalikuwa mwongozo kwangu na kwa wanavikundi katika kutoa ufafanuzi kuhusu mwingiliano wa matini na ishara zinazohusiana na VVU/UKIMWI tulizoziona kwenye nyimbo zilizochezwa kwenye video au runinga.

### 2.6.4 Uigizaji kama njia ya kukabiliana na UKIMWI

Barz (2006) alifanya utafiti na kuibuka na mbinu mpya za kuuelewa ugonjwa wa UKIMWI katika miktadha ya kijamii. Utafiti wake ulijikita katika kuchunguza uhusiano kati ya kupungua kwa maambukizi na jitihada za wananchi mashinani walioshiriki drama na muziki kwa lengo la kuwabadilisha watu kitabia nchini Uganda. Kulingana na Barz, mbinu hii, ambayo inavutia ina uwezo sawa na kampeini za chanjo kwa asilimia themanini(80%). Barz anaeleza kuwa, kwa sasa mbinu hii ni faafu zaidi kuliko matumizi ya dawa. Kama alivyoeleza, jambo lililo muhimu katika vita dhidi ya UKIMWI ni kubadilika kwa watu kitabia. Mabadilikohaya yanasababishwa na waigizaji na wala sio kutokana na vyombo vya habari. Ni wazi kuwa vyombo vya habari anavyovizungumzia Barz ni magazeti kwa sababu anaendelea kusema kuwa; watu wanaweza kukataa kusoma mabango, lakini kamwe hawawezi kukwepa mvuto wenye nguvu ulioko kwenye uigizaji uliojikita katika utamaduni.

Akizingatia sifa za utendaji kama tiba, Barz anaeleza kuwa, kupitia kwa nyimbo ugonjwa unapewa maana. Anaeleza kuwa wanawake nchini Uganda hujifunza kupitia njia asilia za mawasiliano ambazo ni muziki, dansi na uigizaji. Aidha, anazungumzia dhana ya ulughaishaji wa UKIMWI kijamii. Maneno kama vile ‘silimu’, mdudu au mnyama katika kisahani cha chakula yameainishwa kuwa ya kurejelea na kueleza UKIMWI ni nini. Utafiti huu wa Barz ulikuwa wa manufaa kwa utafiti wangu kwa

sababu ulitoa mwanga wa kubainisha sitiara zilizotumiwa na wasanii wa nyimbo zilizoteuliwa kurejelea VVU/UKIMWI, ngono na sehemu za siri za mwili.

Wenje na wenzake (2011) wana maoni na mapendekezo kama yale ya Barz. Hii ni kwa sababu wanapendekeza mbinu asilia zinazokubalika katika miktadha ya tamaduni za Kiafrika zitumike katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI badala ya mbinu za Kimagharibi za mawasiliano kama vile redio, magazeti na runinga. Mbinu za mawasiliano walizopendekeza wataalamu hawa ni zile za kiusimulizi na kiuigizaji au kiutendaji. Mbinu hizo ni pamoja na utambaji hadithi, methali au misemo na nyimbo.

Mbinu hizi za mawasiliano ni mwafaka zaidi kwa hadhira za Kiafrika kuliko zile za kimagharibi ambazo huzikengeusha na kuzinyima nafasi ya kushiriki katika mchakato mzima wa mwasiliano.

Wataalamu hawa wanasisitiza, na ninakubaliana nao, kuwa ili kupiga hatua katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI barani Afrika, kuna haja ya kushirikisha mikakati inayozingatia tamaduni za Kiafrika na ambayo inasisitiza kushirikishwa kwa wanajamii katika kutafakari na kuchukulia suala la VVU/UKIMWI kama tatizo linalowahusu. Ingawa mbinu hizi za kiusimulizi na kiuigizaji hazijatambuliwa katika fasihi nyingi za Kimagharibi kama zana muhimu za kuelimisha katika miktadha mingi ya maisha ya mwafrika, ufaafu wake katika kubadlisha watu kitabia hasa mashambani ni jambo lililo wazi kabisa. Jamii nyingi za mashambani zikiwemo Wakalenjin na Wamaasai ambao nyimbo zao ni baadhi ya zile nilizozichanganua zina utajiri mkubwa wa mbinu pendwa za mawasiliano kama vile methali, utambaji hadithi, dansi, drama, ukariri wa mashairi na nyimbo.

Utafiti wa wataalamu hawa ulijikita katika nyimbo mbili za jamii moja ya Wajaluo. Wimbo wa kwanza uliimbwa na wanafunzi wa shule ya msingi huku wa pili ukiimbwa na kikundi cha waigizaji. Utafiti wangu ulipanuka kiupeo kwani, mbali na kuchunguza nyimbo nne za jamii hiyo ya Wajaluo, ulichunguza nyimbo za jamii nyingine za Kenya kama vile Wakalenjin, Wamaasai na nyimbo za Kiswahili zinazosikizwa na Wakenya wengi kupitia vyombo vya habari.

### 2.6.5 Dini, Utamaduni na UKIMWI

Barz (2006) amechunguza namna suala la UKIMWI linavyoshughulikiwa na jamii zenye misingi ya kidini. Anaeleza kuwa baadhi ya jamii huona UKIMWI kama adhabu kutoka kwa Mungu. Dhana hii imekuza unyanyapaa na kutengwa kijamii kwa waliohasiriwa. Mchango wa makanisa na madhehebu mengine katika muktadha huu hauwezi kupuuzwa. Hii ni kwa sababu tiba na utendaji wa kidini huchukua nafasi muhimu katika miktadha ya kijamii. Nyimbo za dini zilizoteuliwa ziliangazia nafasi ya dini katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI katika muktadha wa Kenya.

Rafiq (2008), akielezea nafasi ya Hip-Hop katika vita dhidi ya UKIMWI nchini Tanzania, anasema kuwa kituo cha utangazaji cha Aang Serian Community Studio hujihusisha na kurekodi na kucheza nyimbo za Hip-Hop. Nyimbo hizi zimewasilishwa kwa namna ambavyo zinaakisi mazungumzo ya kawaida yanayotokea hata barabarani.Lugha inayotumiwa ni ya Kiswahili pamoja na mitindo na midundo ya Hip-Hop yenye misingi ya Kimarekani. Mazungumzo yaliyomo ni ya kuwavutia vijana kwa sababu yamejikita katika utamaduni wa nyimbo za Kiswahili kama vile Taarab au kuimbana ambapo msanii anazungumza moja kwa moja na hadhira yake. Rafiq anaendelea kueleza kuwa mazungumzo ya aina hii yana ukuruba zaidi na vijana kuliko mbinu nyingine za kuwasilisha habari kuhusu UKIMWI kama

vile Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOs), Serikali ama makundi ya kidini. Asemavyo Rafiq mashirika kama haya hujihusisha na utoaji wa takwimu za kiafya na usambazaji wa mipira (kondomu) tu. Aidha kuna tofauti za kiuchumi, kijamii, kimaeneo na kielimu kati yao na vijana.

Rafiq (2008) anaeleza kuwa ni kupitia kwa Hip-Hop ambapo vijana wanaweza kuchangia kupunguza kwa kiwango kikubwa kuenea kwa janga la UKIMWI nchini Tanzania. Aidha anaeleza kuwa, vijana nchini humo waliweza kumuktadhaisha Hip-Hop na kuitumia kama chombo cha kuwasilisha matatizo yao kwa jamii na serikali. Kwa kiasi kikubwa wamejihusisha sana na mbinu hii katika kujieleza kiasi kwamba baadhi ya watu nchini humo wametambua Hi-Hop kama kipengele cha utamaduni.

Utafiti huu ulijikita katika muktadha wa taifa la Kenya na kuchunguza iwapo nyimbo za kiasili na za Kiswahili zinaweza kutumiwa kupiga vita janga la UKIMWI. Kwa kufanya hivyo tulilenga kubainisha namna nyimbo hizi zilivyomuktadhaishwa na wahusika huku tukichunguza vipande vya simulizi vilivyomo. Asemavyo Rafiq (2008), nyimbo za Hip-Hop huwa na hadithi za kutahadhrisha na kupitia kwa mtindo huu unaoiga maongezi ya kawaida, vijana nchini Tanzania wameweza kukuza ukuruba na hadhira yao. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa, ni katika miaka ya hivi karibuni tu ambapo baadhi ya taasisi za kiutawala, raia na wazee kwa ujumla wametambua Hip-Hop kama njia ya mawasiliano na utamaduni wa vijana nchini Tanzania. Wanachanganya Hip-Hop, lugha na misemo ya kiutamaduni katika kuwafahamisha wanajamii kuhusu suala la UKIMWI. Mazungumzo yaliyomo ndani ya nyimbo hizi za Hip-Hop yanayozungumgumziwa na Rafiq yanaweza kutazamwa kama mfano wa simulizi zisizokuwa na uaushi na za kila siku ambazo zinajadili maswala muhimu ya VVU/UKIMWI, sawa na ilivyo katika utafiti huu.

Wanyama na Okong’o (2011) walichanganua nyimbo tatu za wasanii watatu kutoka jamii ya Wajaluo. Utafiti wao ulibainisha jinsi wasanii wanavyozingatia kwa kina masuala muhimu ya kiafya nchini Kenya. Kilicho muhimu zaidi ni jinsi wasanii wanavyotumia istilahi za lugha za kiasili pamoja na utamaduni pendwa kama vile muziki wa kiasili kuweka wazi hatari na uhalisia wa maambukizi ya VVU katika Afrika Mashariki. Mapitio ya utafiti wao yalinifaa kwani walifafanua maana ya maneno ya Dholuo yanayorejelea UKIMWI kama vile *Mayaka* lenye maana ya kinachofagia au kinachoharibu. Wimbo mmoja kati ya nyimbo nne za Kijaluo nilizozichanganua una anwani ya neno lilo hilo *Mayaka.*

Nyandiba (2013) alifanya utafiti juu ya mikakati ya kiisimu ya mawasiliano katika diskosi za VVU/UKIMWI miongoni mwa Abagusii. Utafiti wake ulibainisha kuwa jamii husika huwa na maneno mahususi yanayotumiwa kurejelea masuala yanahusu VVU/UKIMWI, kujamiiana, sehemu za siri za mwili na kadhalika. Kulingana na mtafiti huyu, maneno hayo yanalenga kupunguza aibu. Lugha inayotumia maneno hayo mahususi ameiita lugha ya upole. Ingawa utafiti wa Nyandiba ulikuwa wa kiisimu, mapitio ya kazi yake yalikuwa na natija kwa utafiti wangu kwani nyimbo za kibaadausasa nilizozichanganua zina mikakati yenye upekee wa kurejelea masuala yale yale ya VVU/UKIMWI, ngono na sehemu za siri za mwili.

Sambai (2014), akitafiti kuhusu namna wanajamii wanavyounda jumbe za VVU/UKIMWI kutokana na kutazama filamu za *Makutano Junction* na *Siri* anaeleza kuwa, hadhira hushiriki katika kuunda jumbe za VVU/UKIMWI kwa kuongozwa na matamshi na ishara zinazotumiwa na waigizaji. Utafiti wake uligundua kuwa, hadhira haiwi hadhira pokezi tu bali huwa hadhira tendaji kwani huweza kusimbua misimbo iliyotumiwa kufumba na kuwasilisha jumbe zinazohusu ngono, sehemu za siri za mwili, masuala ya kijinsia na ya kitamaduni. Maoni haya ya Sambai yalinifaa kwani

yaliniongoza katika kutafakari, kuchanganua na kutolea maana jumbe za VVU/UKIMWI, ngono, sehemu za siri za mwili, zinazowasilishwa na waimbaji wa nyimbo za kibaadausasa nilizozichanganua. Aidha, maoni ya Sambai (kama hapo juu) yanaonyesha mitazamo ya wanajamii wa jinsia na matabaka mbalimbali kuhusu VVU/UKIMWI, ngono salama; mitazamo ambayo inapata mwangwi katika nyimbo za kibaadausasa.

Taasisi na mashirika yanayojishughulisha na suala la UKIMWI nchini Kenya kama vile Wizara ya Afya ya Umma na Afisi ya Rais kwa kushirikiana na Baraza la Kitaifa la Kudhibiti UKIMWI ( NACC, 2000) hutoa ripoti za mara kwa mara kuhusu hali ya UKIMWI nchini Kenya. Ripoti hizi huwa na takwimu zinazoonyesha viwango vya ufanisi vilivyofikiwa na serikali katika vita dhidi ya UKIMWI. Ripoti ya NACC (2000) kwa mfano, ni juu ya mpango maalumu wa kitaifa kuhusu UKIMWI.

Kijitabu cha data kuhusu UKIMWI cha NACC (2005) pamoja na ripoti za baraza hilo za 2006 na 2008 zilizowasilishwa katika kikao maalumu cha Umoja wa Mataifa kuhusu VVU/UKIMWI zinatoa mwanga na mwelekeo kuhusu utafiti na kusema kwamba vita dhidi ya VVU/UKIMWI mpaka sasa havijashindwa. Hivyo basi kunahitajika mkabala wa mbinu anuwai za kijamii; nyimbo zikiwemo. Nyimbo katika viwango mbalimbali zina ishara maalum zinazoweza kudhihirika kupitia usemi na utendaji. Ishara hizi huingiliana na miktadha ya kijamii na kujenga diskosi kuhusu masuala ya kijamii.

Suala la UKIMWI ni suala la kijamii linaloweza kuchunguzwa kupitia vipande vya simulizi vilivyomo katika nyimbo. Hii ni kwa sababu nyimbo zina uwezo wa kuwasilisha jumbe mbalimbali zinazohusiana na suala la UKIMWI na suala zima la mapenzi au ngono bila pingamizi. Masuala haya hayajadiliwi kwa uwazi na

wanajamii kupitia mazungumzo ya kawaida kwa sababu ya miiko, mipaka ya kiumri, kitamaduni na kijinsia. Nyimbo huvuka mipaka hii kwa kusheheni simulizi ndogo ndogo na simulizi kuu za mada ya VVU/UKIMWI. Utafiti huu ulichanganua simulizi za maadili, faraja, maonyo na unyanyapaa kuhusu VVU/UKIMWI na waathiriwa kwa kujikita katika nyimbo za kiasili na za Kiswahili.

## 2.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Baadausasa, hasa mitazamo ya Michel Foucault, Jean–Francois Lyotard na Richard Rorty ambao kwa pamoja walipinga madai ya wanausasa juu ya kuwepo kwa ushabihi kweli. Nadharia hii inapendekeza kuwa ukweli na maarifa hazitokani na matini husika peke yake bali huweza kupatikana nje ya matini au katika matini nyingine. Kilichopo basi ni tofauti za kimaoni kuhusu uhalisi na hivyo kuwepo kwa uhalisi wingi kulingana na maoni ya watu tofauti tofauti ambapo kila mmoja ana fasiri tofauti ya uhalisi. Msimamo wa nadharia hii ni kwamba mtu mmoja hawezi kudai umiliki juu ya ukweli halisi na hivyo maoni ya kila mtu yafaa kuheshimiwa na kwamba mbinu anuwai za ujitambuaji na wingi masimulizi husisitiza upendelevu.

Wegesa na Macharia (katika Ogechi na wenzake, 2008) wanadai kuwa, kwa sasa jamii zetu zinajipata katika hali ambapo misingi yake inasukumwa kuelekea maeneo yaliyopuuzwa hapo awali. Mabadiliko ya kijamii si swala la uteuzi tena na wala haielekei kudhibitiwa na msingi wa desturi uliozoeleka. Badala yake, mabadiliko haya yaelekea kutokea kwa kasi, bila mpango na yenye upekee wa kimsingi kabisa. Kutokana na mabadiliko haya, matini au simulizi kuu zinachunguzwa na kutupiliwa mbali na nafasi yake kuchukuliwa na matini au simulizi ndogo ndogo. Kwa sababu hii, maana inaweza kupatikana siyo tu kupitia lugha bali pia katika muktadha wa

kijamii ambamo ishara za lugha zinatumika. Mathalan, Bakhtin anasisitiza kuwa lugha yafaa kuzingatiwa katika muktadha wa kijamii, kwamba kila tamko lina uwezo wa kuwa uwanja wa mvutano, kila neno litumiwalo linasababisha diyalojia na hivyo kuwa na ufasiri wa kujadiliwa au kudahiliwa. Kwa maoni yake, jamii daima ni sehemu ya mchakato mzima wa mapambano na miingiliano ya wanajamii.

Deleuze na Guattari (katika Rivkin & Ryan, 2000) wanadai kuwa hata matini iliyovunjwa kabisa yaweza kuwasilishwa kama kazi iliyotimia. Ninayaunga mkono maoni haya kwa sababu vipande vya simulizi navyo huwa vikamilifu. Matini, sentensi na maarifa si lazima yachukue muundo wa mstari laini bali zinaweza kuchukua muundo wa mviringo na wakati huo huo kudumisha mshikamano. Ukoka waweza kukatikia popote lakini huanza kukua upya kuanzia mistari ya awali au mistari mipya. Kwa hivyo, matini yaweza kusomwa kuanzia mahali popote na inaweza kuwa na mahusiano na matini nyingine yoyote. Mtazamo kama huu unazungumziwa pia na Kleist, Lenz na Büchner (katika Bressler (2007) wanaopendekeza kuwa utalii wa matini uanzie katikati, upitie katikati kwenda mbele na kurudi nyuma badala ya mbinu iliyozoeleka ya kuanzia mwanzo kuelekea mwisho.Wanapendekeza kuondolewa kwa kitovu, ubatilishaji wa miisho na mianzo ili kufikia upragmatiki.

Wanabaadausasa wanapendekeza matini itazamwe kutoka juu, chini, kushoto na kulia na wala sio kutoka katikati peke yake. Kutokana na maoni haya, janga la UKIMWI nalo linafaa lisitazamwe kwa jicho la kisayansi pekee, bali kwa kutumia mbinu nyingine nyingi, nyimbo zikiwemo. Aidha, wanajamii wote washirikishwe katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI na wala si wale tu walioko katika hatari ya kuambukizwa.

Foucault katika Rivkin na Ryan (2000), anaeleza kuwa diskosi zinaumbwa na ishara lakini huvuka mipaka ya matumizi ya ishara hizi kuwakilisha vitu. Ni matumizi haya

yanayozifanya zisibanwe katika lugha (*langue*) na usemi. Ni matumizi haya ya ziada ambayo ubaadausasa unapania kuyabainisha na kuyaeleza.

Bressler (2000) anadai kuwa, wanabaadausasa wa miaka ya kati ya 1960 wakiongozwa na mtazamo wa Jacques Derrida kuhusu Baada Umuundo walipinga maoni ya wanausasa kuhusu ushabihi kweli na uhalisi. Wanapinga ufananishaji wa diskosi na ramani; ufananishaji uliofanywa na wanausasa na badala yake kuifananisha na picha itengenezwayo kwa kugandishwa vipande vipande vya karatasi, nguo, vyuma na kadhalika. Kinyume na ramani ambayo inaruhusu ufasiri mmoja tu wa uhalisi, picha hii hurusu kuwepo kwa maana nyingi huku kila mtazamaji au msomaji akiibuka na taswira yake pendelevu ya uhalisi. Hali hii hutokana na uwekaji sambamba.

Vita vya kwanza na vya pili, kufifia kwa uwezo wa kidini, kukua kwa ubinafsi pamoja na mdahalo kuhusu uwepo wa Mungu zilichangia pakubwa kupuuzwa kwa kuwepo kwa ushabihi kweli na mamlaka ya msimulizi anayejaribu kuvumbua uhalisi usiopingika. Mambo haya yaliwafanya Jacques Derrida, Michel Foucault, Jean – Francois Lyotard na Richard Rorty kudai kuwa usasa ulishindwa kutatua matatizo ya wanajamii kwa sababu ya kutegemea Mungu, mantiki, sayansi na kadhalika.

Kutokana mawazo ya wataalamu hawa, msimamo wangu ni kuwa, suluhisho la tatizo la UKIMWI lisitafutwe tu kwenye uwanja wa kisayansi pekee bali nyanja nyingine zihusishwe. Wanabaadausasa wanashikilia kuwa, wanajamii watapata ufanisi tu iwapo wote watashirikiana. Aidha, wanashikilia kuwa enzi za mtaalamu wa kisayansi kujifungia maabarani kufanya uchunguzi zimefika kikomo. Wanahimiza ushirikiano miongoni mwa wataalamu kutoka nyanja na taaluma mbalimbali. Siku za ubinafsi zimepita. Siku za kudai ushindi pia zimepita kwani sasa ni wakati wa kustahamiliana,

kuelewana na kushirikiana. Kutokana na haya, maoni yangu ni kwamba, mkabala wa kijumla utumiwe katika vita dhidi ya UKIMWI. Kwa mfao, mkabala huu uhusishe nyimbo za kutoka jamii mbalimbali kwani zina uwezo kuvunja mipaka na kuwasilisha ujumbe kwa urahisi.

Wamitila (2002) anatumia neno Usasaleo kurejelea dhana ya baadausasa. Akirejelea maelezo ya Abrams, anaeleza kuwa, msingi wa sifa za kibaadausasa ni kule kujitenga na misingi ya jadi ya sanaa na utamaduni wa kimagharibi zilizozoeleka. Waasisi wa tapo hili walidadisi misingi ya miundo ya kijamii, kidini, kimaadili (Kisayansi) na mitazamo ya kijadi kumhusu binadamu kama kiumbe. Kushindwa kwa taasisi hizo kulisababisha kutafutwa kwa njia, mbinu na hata miundo tofauti ya kuangazia au kutazamia na kuelezea kushindwa huku.

Msimamo wangu ni kuwa, njia za kisayansi pekee ambazo zimezoeleka hazijashinda kabisa vita dhidi ya UKIMWI. Kutokana na msingi huu kuna haja ya kutumiwa kwa mbinu anuwai zikiwemo za kijamii na kiutamaduni katika vita dhidi ya UKIMWI. Nyimbo ni mojawapo ya mbinu hizo na hasa ikizingatiwa kuwa zinaweza kuwasilisha jumbe zinazohusu mapenzi, sehemu za siri za mwili, ngono, matumizi ya kondomu na VVU/UKIMWI kwa urahisi huku zikiburudisha. Aidha nyimbo zinatoa nafasi ya kuingiliana kwa matini huku kila matini ikitoa mchango wake kimaana. Katika mwingiliano huu kuna uwezekano wa kuwepo kwa vipande vya simulizi vyenye kukuza unyanyapaa na zile ambazo zinaupinga.

Sifa nyingine zinazohusishwa na mwelekeo wa kibaadausasa ni kukatizwa kwa mkondo wa kiusimulizi, kupuuzwa kwa kaida na kanuni za kimsingi za usawiri wa wahusika, muundo wa msuko, matumizi ya mandhari, udhihirishaji na uendelezaji wa wahusika na swala la uhamasishaji. Panakuweko na mabadiliko katika muundo wa

lugha pamoja na uwiano wa lugha kisimulizi. Waandishi wanaoegemea misingi ya mawazo ya kibaadausasa huitumia mitindo mipya ya kisanii pamoja na kuyashughulikia masuala ambayo yamepuuzwa kwa kiasi kikubwa. Msimamo wangu ni kuwa kupuuzwa kwa wanajamii wengine na mbinu za kijamii zikiwemo nyimbo kumechangia kutofanikiwa kwa vita dhidi ya VVU/UKIMWI.

Mwelekeo wa kibaadausasa unarejelea hali ya kijumla ya maisha ya binadamu na jamii yake. Mwelekeo huu unayahusisha maisha, utamaduni, sanaa na itikadi katika kuiangazia hali ya binadamu. Katika mkabala huo, haiwezekani kutenganisha itikadi na umbuji katika vita dhidi ya janga la UKIMWI. Kupuuzwa kwa mbinu za kiutamaduni kama vile nyimbo zinazoimbwa na vijana pamoja na zile za dini katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI na kutegemea zaidi mbinu za kisayansi kunazifanya nyimbo kuwa na nafasi katika muktadha wa Kenya ya kibaadausasa. Nyimbo ni kipengele muhimu katika muktadha huu.

Aidha, kutokana na mtazamo wa wananadharia wa baadausasa kuwa matini yaweza kugawanywa na kuwasilishwa kama kazi timilifu, ninaamini kuwa vipande vya simulizi katika nyimbo ni vikamilifu. Pamoja na hayo, kwa kuwa nyimbo ni matini zinazoweza kuchanganuliwa jinsi zilivyo matini nyingine, nyimbo husika zilitazamwa kutoka juu, chini, kulia na kushoto pamoja na kutafuta maana nje ya matini jinsi wanavyopendekeza wananadharia hao.

Isitoshe, wagonjwa walioambukizwa VVU/UKIMWI na ambao huenda wametengwa na wanajamii wengine wanapata nafasi katika nyimbo. Ni kupitia kwa vipande vya simulizi vilivyomo kwenye nyimbo ambapo hisia zao na za wanajamii wengine kuwahusu zinawasilishwa. Hisia hizi zinaweza kuwa hasi na zenye kuendeleza unyanyapaa au chanya na hivyo kupiga vita unyanyapaa. Nyimbo pia zina uwezo wa

kukiuka taratibu zilizozoeleka za kisayansi na hivyo kuwasilisha habari kuhusu VVU/UKIMWI bila ya pingamizi yoyote. Kwa msingi huu basi nyimbo zinaafiki mitazamo ya wananadharia wa kibaadausasa kwamba ukweli haupatikani kupitia kwa njia za kisayansi pekee bali kupitia njia nyingine nyingi zikiwemo za kijamii. Ingawa nadharia ya baadausasa ina mihimili kadhaa, utafiti huu uliegemezwa kwenye baadhi ya mihimili yake mahususi ambayo ni pamoja na : mwingilianomatini,uigaji, urejeleaji, ukiukaji, kukosekana kwa mshikamano na kukosekana kwa uaushi au uhalisi.

### 2.8 Hitimisho

Sura hii imejadili na kuhakiki maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Kwa hivyo katika sehemu ya kwanza ya sura hii, nimejadili vipengele vielekezi vinavyochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI nchini. Vipengele hivyo ni pamoja na umaskini, magonjwa ya zinaa, matumizi ya pombe na mihadarati, mizozo na vita vya kikabila pamoja na dhana na desturi za kitamaduni.

Katika sehemu ya pili nimejadili athari za VVU/UKIMWI zikiwemo za kijamii na za kiuchumi. Sehemu ya tatu ya sura hii imeshughulikia mikakati ilyowekwa na serikali, mashirika yasiyo ya serikali na watu binafsi katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI. Baadhi ya mikakati hiyo ni uongozi na uratibu, huduma za UUH, UMMM, matumizi ya ARV, na kadhalika. Katika sehemu ya nne, nimejadili hali ya VVU/UKIMWI nchini Kenya kwa kuangazia takwimu za hivi punde. Katika sehemu ya tano ya sura hii, nimepitia na kuhakiki maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu nyimbo na VVU/UKIMWI. Hatimaye nimejadili misingi ya nadharia ya Ubaadausasa ambayo iliongoza utafiti huu. Sura inayofuata inajadili baadhi ya mikakati ya kibaadausasa inyotumiwa katika nyimbo zilizoteuliwa.

# SURA YA TATU

# MIKAKATI YA KIBAADAUSASA KATIKA NYIMBO ZA VVU/ UKIMWI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha baadhi ya mikakati inayohusishwa na ubaadausasa na kujadili namna ilivyotumiwa katika katika nyimbo za kibaadausasa zinazozungumzia VVU/UKIMWI. Mikakati hiyo aidha inatumiwa kuwasilisha jumbe zinazohusiana na VVU/ UKIMWI kama vile ngono, sehemu za siri na mahusiano ya kijinsia. Mambo haya matatu yanahusiana moja kwa moja na VVU/UKIMWI kwani VVU husambazwa zaidi kupitia ngono. Aidha, ngono huhusisha watu wawili wa jinsia tofauti au jinsia sawa. Pamoja na hayo, mikakati inarejelea matumizi ya kondomu na dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI yaani ARVs. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na, upingwajiwa mawazo ya usasa, ukiukaji, ukosefu wa mshikamano na nafasi yake kuchukuliwa na vipandevidogo vidogo vya simulizi. Sura hii pia imeangazia matumizi ya mwingilianomatini, misemo na au misimu inayoodhihirisha ukosefu wa aushi.

## 3.2 Mikakati Inayopinga Usasa

Baadhi ya wataalamu wanaouona ubaadausasa kama mwondoko unaopinga usasa ni Morgan (2001) na Barry(2002). Upinzani huu ulianza kudhihirika mwanzo kabisa katika sanaa ya majengo ambapo usasa ulikataa marembesho au nakshi katika kuta za majengo ya aushi. Waashi walilazimika kufuata mtindo mmoja maalum katika ujenzi wa nyumba husika (Morgan, 2001). Mathalan usasa ulipendekeza mtindo mmoja wa kiujenzi ambapo majengo yote yalizingatia umbo la mstatili. Kulingana na Barry (2002), kuibuka kwa ubaadausasa kuliwafanya wasanii wa majengo wayarejelee marembesho yaliyokuwa yamekataliwa na usasa. Isitoshe, mitindo ya kizamani na ya

kisasa ilirejelewa na hivyo kuchipuza maumbo tofauti ya ujenzi yaliyozingatia mchanganyiko huu. Mathalan, wanaubaadausasa walipendekeza kuundwa upya kwa kazi za sanaa kwa kutumia uigaji na mchanganyiko wakimitindo hususan katika ujenzi. Mambo haya ndiyo yaliyokuwa yamekataliwa na wanausasa (Barry, 2002). Hali hii inaonyesha kuwa ubaadausasa ulipinga usasa hasa katika uashi.

Kwa mujibu wa Sim (2001) na Carter(2006). Ubaadausasa unapinga mawazo ya kimagharibi pamoja na njia zao za kimaisha zinazohusiana na usasa. Kwa mfano, wanapinga imani za usasa kuhusu maendeleo ya lazima katika hatua za maisha ya binadamu na yasiyojali athari zake kwa mazingira. Wanaubaadausasa wanapendekeza maendeleo yanayozingatia uhifadhi wa mazingira.

Tunapozingatia fasihi kama sanaa, tunaona kuwa ubaadausasa ulikuwa na lengo la kuiondoa mipaka iliyokuwepo kati ya tamaduni za chini na zile za juu. Mipaka hii haikusisitizwa tu bali ilidumishwa na wanausasa (Worfreys na wenzake, 2006). Kulingana na wataalamu hawa, wanausasa walishikilia kuwepo kwa mipaka dhahiri kati ya tamaduni hizo mbili husika. Wanaubaadausasa nao walipuuza kuwepo kwa mipaka hiyo na hivyo kupinga usasa.

Akielezea kuhusu riwaya za kisasa na zile za kibaadausasa, Khamis (2005) anadai kuwa riwaya husika zinatofautiana kimtindo ambapo za kisasa zinazingatia  mtindo wa kiuandishi wa uhalisia huku za kibaadausasa zikiukiuka. Ukiukiaji huu ulisababishwa na kushindwa kwa uhalisia kutoa ufafanuzi kamili kuhusu ulimwengu uliochangamanika. Vilevile, kazi nyingi za kihalisia zilionyesha  matumizi makubwa ya hali kuimarika na kuwa bora licha ya matatizo yaliyoyatinga nchi nyingi barani Afrika.

Hali kama hii inasawiriwa katika baadhiya nyimbo za kibaadausasa zilizochanganuliwa katika tasnifu. Awali wasanii wa nyimbo mbalimbali walitarajiwa kuibuka na nyimbo ambazo zilitakiwa kuheshimu mipaka ya kiumri na kiuana. Aidha walitarajiwa kuimba nyimbo za kuimarisha jamii kimaadili na pia kutumia lugha ya heshima na wala siyo lugha chafu. Wasanii wa nyimbo za dini nao walitakiwa waimbe nyimbo za kumtukuza Mungu na za kueneza injili peke yake. Korir(2013) anadai kuwa, baadhi ya wamishonari walipinga matumizi ya ala za Kiafrika wakati wa kuimba nyimbo za dini. Aidha wasanii hawakuruhusiwa kutumia semi/misemo ya lugha za kiafrika pamoja  na mavazi asilia ya Kiafrika, kwani utamaduni wa mwafrika ulihusishwa na ushetani. Utafiti unazingatia kuwa, nyimbo zilizoimbwa kwa kufuata mtindo huu zilikuwa za usasa. Hizi ni nyimbo zilizosawiri uhalisia jinsi riwaya za kiuhalisia zilivyofanya.

Baadaye, uchangamano wa maisha uliwalazimisha wasanii wa nyimbo wakiuke masharti ya awali na kuibuka na nyimbo ambazo zilizingatia matumizi ya semi/misimu ya lugha za kiafrika, maudhui yaliyotenga matatizo ya kijamii na mchanganyiko wa mitindo mbalimbali huku zikitopea vipengele vya utamaduni wa Mwafrika. Sehemu inayofuata inajadili namna ukiukaji kama mkakati wa ubaadausasa unavyodhihirika katika baadhi ya nyimbo zilizoteuliwa.

### 3.3  Ukiukiaji kama Kipengele cha Ubaada Usasa

Kulingana na Barry (2002) na Klages (2003), kuna mwingiliano wa vipengele vilivyopatikana katika kazi za usasa na vile vya baadausasa. Wanaendelea kueleza kwamba, licha ya kuwepo kwa mwingiliano huu, kuna tofauti za kimielekeo kuhusiana na vipengele husika. Mathalan, wanausasa wanalalamikia ukosefu wa mshikamano katika maisha ya binadamu huku wanabaadausasa wakiusherehekea

ukosefu huo. Maoni ya wanabaadausasa ni kwamba, ulimwengu hauna maana na sanaa yoyote ile haitaleta maana hiyo. Kulingana na maoni yao, kukosekana kwa mshikamano ni njia ya kujikomboa kutokana na mifumo ya awali ambayo haikuruhusu mabadiliko. Kwao, hakuna ukweli halisi kwa hivyo kazi za sanaa za kibaadausasa zikiwemo nyimbo zinawapa wasanii nafasi ya kujaribu mitindo mipya kwa njia ya kiubunifu bila kuhukumiwa kuwa mitindo hiyo mipya imekiuka kanuni,mitindo au kaida zilizowekwa na kuzoeleka.

### 3.3.1 Ukiukiaji na Kimtindo

Morgan (2001) anaeleza kuwa kuna wakati kipindi cha ubaadausasa kilishuhudia kurejelewa kwa marembesho yaliyokuwa yamekataliwa katika kipindi cha usasa hususan katika majengo. Maumbo tofauti ya ujenzi yakashirikisha mchanganyiko wa mitindo ya kizamani na kisasa.

Aina hii ya ukiukiaji inadhihirika waziwazi kupitia wimbo Rat torosta(*Funga nepi*) wake Joel Kimetto. Huu ni wimbo wa kikristo lakini wimbo wenyewe umechanganya mitindo miwili ya rap na hiphop. Mitindo mipya pia inadhihirika kupitia nyimbo kama vile *Wee kamu, Vuta pumzi,Juala* na *Si lazima.* Nyimbo hizi zinadhihirisha mitindo ile ya rap na hiphop inayohusishwa zaidi na vijana. Mitindo hii haingeruhusiwa kutumika katika nyimbo za usasa hasa zile za dini. Hii ni kwa sababu simulizi kuu ilikuwa imeshikilia kuwa nyimbo, hususan za Kikristo zilifaa kuchukua mtindo fulani uliokuwa umezoeleka. Kuingiza mitindo mipya katika nyimbo hizi ni ukiukaji wa kimtindo.

### 3.3.2 Ukiukiaji wa Kimaudhui

Maudhui ya nyimbo hasa zisizo za Kikristo zilizokitwa katika kipindi cha usasa yalihusu tabia njema na hivyo nyimbo husika zilitarajiwa kwasilisha jumbe za

maadili. Aidha wasanii walitarajiwa kuibua nyimbo zilizozungumzia masuala kama vile maendeleo ya kijamii. Nyimbo hizi pia zilitakiwaziwahimize watu wawe na bidii kazini na hivyo kuupinga uzembe. Nyimbo za kibaadausasa zinazohusu VVU/Ukimwi zinaonyesha kukiuka utaratibu huo uliokuwa umezoeleka kwa kujikita katika maudhui nyeti kama vile ngono, sehemu za siri, VVU/UKIMWI, dawa za kupunguza makali ya VVU/Ukimwi, matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume kama vile *Viagra* na matumizi ya kondomu kujikinga dhidi ya VVU. Kutokana na uchangamano wa ugonjwa wa VVU/UKIMWI, baadhi ya wasanii wanauzungumzia kwa njia ya mafumbo huku wengine wakitumia lugha iliyo wazi na ya kuogofya kwa lengo la kuchochea hisia za kuwatia wasikilizaji wasiwasi na huzuni. Hii ni njia ya kuwashawishi wajitume na watafute suluhisho la tatizo hili la VVU/UKIMWI.

Mawazo haya yanaafikiana na ya Khamis (2005) ambaye anaelezea mtindo wa kibaadausasa katika fasihi kama mbinu ambayo kwayo waandishi hulenga kuchochea hisia za kuwatia wananchi wasiwasi na huzuni kama njia ya kuwashawishi wainuke na watafute suluhisho la matatizo yao.

Hali kama hii inadhihirika katika nyimbo za kibadaausasa ambapo wasanii hutumia lugha ya moja kwa moja, iliyo wazi na inayotia wasiwasi mno. Mathalan, Princess Jully katika wimbo *Dunia mbaya* ubeti wa kwanza anatumia maneno yafuatayo yanayotia wasiwasi.

**Mf 1**

*Utakufa mbaya, Ukimwi iko*
*Wacha raha, Ukimwi haijui mtu,*
*Ukimwi hakuna huruma (Nduru)*
*Na dawa ya Ukimwi hakunaaa*
*Utakufa mbaya, utakufa kama mbwa.*

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Maelezo kuhusu kufa kifo kibaya, UKIMWI kutobagua, UKIMWI kutokuwa na huruma kwa yeyote na kufa kama mbwa ni maelezo yanayoogofya. Pia kuna kupiga nduru katika ubeti huu kunakotisha. Ni maelezo yanayosawiri hali ambayo mwanadamu mwenye urazini hangependa hatima yake iwe hivyo. Pamoja na hayo, anawauliza wasikilizaji wake walipo watu wawajuao ambao walikufa kifo hiki kibaya. Katika ubeti wa pili kuna maswali ya kutisha kama vile:

**Mf 2**

*Aleni mwana wa Ochieng ako wapi?*
*Hosea ako wapi*
*Agwambo ako wapi?*
*Wapi Onyango Billy?*
*Ohula yuko wapi. Ohula yuko wapi? Yuko?*
*Wapi? Steve yuko wapi? Yuko?*

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Kutokana na maswali kama haya, huenda wasikilizaji wakachochewa na hivyo kuibua kumbukumbu za jinsi waliotajwa walivyokumbana na mauti. Hali hii huenda ikawafanya wasikilizaji wawe na huzuni na wasiwasi na hivyo kuamua kutafuta suluhisho.

Katika ubeti wa tatu wa wimbo huu pia, mtunzi ametumia maneno ya kuzua wasiwasi kwenye mabano mwishoni mwa kila mshororo. Maneno hayo yanalenga kumfanya msikilizaji ajisaili ili asije akawalaumu wengine endapo hatazingatia ushauri. Baadhi ya mistari inayotumia maneno "Shauri yako" katika ubeti huu ni:

**Mf 3**

*Shauri yako, (shauri yako)*
*Ni wewe utakufa (shauri yako)*
*Ni kichwa nauma (shauri yako)*
*Ni tumbo nauma (shauri yako)*
*Baridii baridi (shauri yako)*

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Lugha hii ya kutia wasiwasi imetumiwa pia na wasanii Ferooz na Profesa Jay katika ubeti wa mwisho wa wimbo Starehe. Baadhi ya maneno aliyotumia daktari akimshauri mgonjwa yanatia huzuni na wasiwasi siyo tu kwa mgonjwa bali hata kwa wasikilizaji. Mistari ifuatayo inashadidi maelezo haya:

**Mf 4**

*Ni kweli vipimo vinaonyesha umeathirika,*
*Starehe mnazipenda, ila mwisho wake mbaya,*
*Wengi wameteketea kwa kuendeleza umalaya.*

(Kutoka: *Starehe*.Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Wasikilizaji wanatiwa wasiwasi na matumizi ya maneno kama vile: umeathirika, starehe mwisho wake huwa mbaya na wengi wameteketea. Haya ni maneno yanayoweza kumtanabahisha msikilizaji.

Katika wimbo Juala wa Circute na Jo-El, wasanii wametumia maneno yanayoibua huzuni na wasiwasi jinsi walivyotumia wasanii waliotangulia. Matumizi ya maneno haya yanadhihirika katika sehemu ya mwisho ya ubeti wa kwanza jinsi inavyoonekana hapa chini.

**Mf 5**

*Lakini hebu tua, lipi linalojiri?*
*Una kondomu? Una kondomu?*
*Ama utaishia kuangalia darini mochari*
*Kama mjinga! Ati nini? Kama mjinga.*

(Kutoka: *Starehe.* Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Katika ubeti huu, maswali kama vile lipi linalojiri? Na Una kondomu? Yanaweza kumtabahisha msikilizaji. Aidha, maelezo katika mistari miwili ya mwisho katika ubeti huu yanatoa taswira ya mochari, taswira ambayo inatisha na pia kuhuzunisha. Wasikilizaji huenda wakapata wasiwasi kutokana na usawiri wa maiti inayoangalia darini. Kutokana na taswira hii, wasikilizaji huenda wakachukua hatua za kuepukana na maambukizi ya VVU/UKIMWI. Aidha, hawangetaka waonekane wajinga.

Longombas sawa na wasanii tuliowazungumzia hapo juu wametumia lugha inayotia huzuni na wasiwasi katika wimbo wao Vuta pumzi ubeti wa pili kama ilivyo hapa chini.

**Mf 6**

*Na mjinga usiyojua kujichunga*
*Hebu jichunge kijana utakuja kufa*
*Tukuzike Langata.*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Katika ubeti huu, wasanii wametuchorea taswira ya kijana asiyechukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya VVU/UKIMWI. Hatima yake ni kifo na kuzikwa kwenye makaburi ya umma kule Langata. Hii ni hali ya kutisha na inayoweza kumfanya msikilizaji awe na wasiwasi na huenda akabadilika ili aepukane na hatima kama hii.

## 3.4 Udhihirikaji Wa Mwingilianomatini katika Nyimbo za Kibaadausasa

### 3.4.1 Dhana ya Mwingilianomatini

Mwingilianomatini hutokana na neno la Kilatini "intertexto" iliyomaanisha "kuchanganya ukifuma". Katika fasihi, mwingilianomatini ni dhana inayohusishwa na mtaalamu Julia Kristeva ambaye alikuwa mwanafalsafa mwenye asili ya Bulgaria na Ufaransa. Ni mhakiki wa kisaikolojia aliyeasisi dhana ya mwingilianomatini 1966 akirejelea nadharia ya Usemezano ya Mrusi Mikhail Bakhtin.

Mwingilianomatini ni dhana inayotumiwa kuelezea kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya kisanaa. Matini huhusiana na kazi zingine na si kazi ya msanii mmoja tu. Marejeleo ya matini fulani humpa msanii wajibu wa kuunda au kubuni matini yake ambayo anaiunga mkono mara kwa mara kwa kurejelea matini nyingine. Matini ni utanzu wa nukuu ambapo msanii anaweza kuiga kitendo kilichoko japo si cha asilia. Wasanii wana ujuzi na uwezo wa kutumia matini

nyingine kubuni kazi inayovutia yenye maswala yahusuyo jamii (Barthes, 1981). Kutokana na maelezo haya basi, matini si kazi asilia bali huumbwa na kuzaliwa kutokana na matini nyingine, na pia hutokana na mchanganyiko wa mambo.

Halliday (2003) anaeleza matini kwa jumla kama athari ya kuwepo kwa matini za awali katika utunzi wa matini husika. Mwingilianomatini unaonyesha uhusiano wa ndani uliopo baina ya matini moja na nyingine.

Kristeva (1980) alipinga mawazo ya Ferdinard de Saussure aliyezingatia matini za kifasihi pekee bila kuhusisha muktadha wa kijamii. Anasisitiza kuwa maana hutokana na maingiliano ya wazungumzaji katika jamii na maana tofauti ya viashiria.

Wakimrejelea Bakhtin (1895 - 1974), Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kwamba kazi ya fasihi huwa na sauti mbalimbali zinazoingiliana na kuiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na zitakazokuja baadaye. Kulingana na Kristeva, matini yoyote ni msuko wa vigae vya nukuu, dondoo athari na badiliko la nyingine. Msanii huumba matini mpya kutokana na anayopata katika matini aliyoyapitia awali. Hufanya hivi kwa kurejelea miktadha ya tamaduni za sanaa za awali pamoja na kukopa matini na nukuu ili kusisitiza manaa ya kazi yake. Haya ni kwa mujibu wa Kristeva (1980) na Tyson (2006). Kimsingi basi, sanaa yoyote ni ya kimwingilianomatini, yaani inahusiana na kurejelea kazi zingine. Hivyo basi nyimbo kama utanzu wa fasihi haziwezi kuepuka sifa hii ya kimsingi.

### 3.4.2 Mbinu ya Unukuzi/ Kiwango cha Sanaa na Miktadha

Kama mkakati wa kibadaausasa, Mwingilianomatini hudhihirika kwa njia mbalimbali katika kazi za sanaa zikiwemo nyimbo. Mwingilianomatini hujitokeza katika viwango mbalimbali kama vile vya simulizi, dhamira, ishara (sitiara) usawiri na uendelezaji wa wahusika. Mbinu kuu zinazowezesha utokeaji wa Mwingilianomatini katika fasihi ni

ubandikaji (pastiche) na wigobezo (parody). Kupitia kwa mbinu hizi, matini asilia huweza kutambulika kwa kuwa kuna kurejelea, kudondoa, majibizano na miigo.

Nyimbo mbili za Joel Kimetto *Kichigili* (Yachunguzwa) na *Rat Torosta* (funga nepi) zinadhihirisha Mwingilianomatini kati yao na matini zingine. Tukianza na wimbo Kichigili (Yachunguzwa), tunaona kwamba kuna kuingiliana kwake kimatini na matini za dini hususan Bibilia na zile za kitamaduni. Msanii amechukua na kueleza taarifa za Bibilia pamoja na utamaduni anazozijua au alizozipata awali ili kuwasilisha maudhui ya kisasa ambayo yanahusiana na VVU/UKIMWI na ngono. Kwa mfano suala la mapenzi kati ya mwanamke na mwanaume linalozungumziwa na msanii katika wimbo huu lina asili yake katika matini ya Bibilia kitabu cha Mwanzo. Hii ni matini inayoeleza kuhusu kuumbwa kwa binadamu wa kwanza Adamu na Hawaa. Maelezo hayo yanarejelewa na msanii jinsi inavyoonekana katika ubeti ufuatao na hivyo kuufanya kuwa mwangwi wa maelezo ya Kibibilia.

**Mf 7**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| ***Kichigili*** | ***Yachunguzwa*** |
| *Kiyai Jehovah en taunet wee* | *Hapo mwanzo Jehova aliwaumba wee* |
| *Muren ak tie* | *Mume na mke* |
| *Ak kondechi mugulelwekwaak* | *Kisha akawawekea nyoyoni mwao* |
| *Kiit aap komonut* | *Kitu cha thamani* |
| *Ngotuiyo konyeek  ko mi kiy* | *Macho yanapokutana kuna kitu* |
| *Moeet ne lelen waa* | *Tumboni kinachofanya waa* |
| *Ne ngokeer age age wee baba* | *Mmoja amwonapo mwenzie wee baba* |
| *Ko sipeshel* | *Yu spesheli* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Maelezo kuhusu hatari ya mapenzi bila tahadhari yanatolewa pia katika wimbo huu. Maelezo haya ni mwangwi wa matukio yaliyotokea kama yanavyoelezwa vile vile katika matini za Kibibilia. Mafungu ya Bibilia yanayorejelewa ni pamoja na kitabu cha Hesabu na kile cha Wafalme. Katika mafungu ya vitabu hivi, kuna kutajwa kwa

wahusika kama vile Dina, Schechem, Samson na Delilah ambao waliathirika kutokana na mapenzi yasiyokuwa ya dhati.

Wahusika hawa wanafanana kitabia na wanaume na wanawake katika ulimwengu wa uhalisia ambao wameathirika kutokana na ugonjwa wa VVU/UKIMWI hasa kutokana na kutokuwa waangalifu katika masuala ya mapenzi. Maelezo hayo yanadhihirika katika beti za tatu (3), nne (4) na tano (5).

**Mf 8**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Kigose akobo Shechem werit aap Amoth* | *Twasikia kuhusu Shechem mwanawe Amoth* |
| *Ne kiicham Dina* | *Ambaye alimpenda Dinah* |
| *Kolen kwo kooito keba kelenji mie keyaatita* | *Alipopeleka posa aliambiwa akubalikutahiriwa* |
| *Kiiba biik tumdo wee kiiba wee ee ee* | *Watu walitahiriwa we walitahiriwa wee ee ee* |
| *Maata agot kobwaat kole* | *Hata hawakutafakari kuwa* |
| *Kinyolchin kwo chiito agenge* | *Mtu mmoja tu ndiye alifaa kutahiriwa* |
| *Ne kiicham chepto wee kiiba wee he he* | *Aliyempenda msichana wee walitahiriwa wee hee ee* |
| *Betut aap somok kemongchi bichoon ak kebar kobek* | *Siku ya tatu watahiriwa walivamiwa na wote wakauawa* |
| *Kigon hasara chamyonoton kibar biik wee* | *Mapenzi hayo yalileta hasara yaliua watu wee* |
| *Kigorom chamyet* | *Mapenzi yalikuwa hatari* |
| *Chamyet aap Dina* | *Mapenzi ya Dinah* |
| *Kiikiyaatita biik, Kiiba wee hee ee* | *Watu walitahiriwa, walitahiriwa wee hee ee* |
| *Kiiba biik tumdo* | *Watu walitahiriwa* |
| *Biik aap Shechem oh* | *Watu wa Shechem* |
| *Tumdaap murenik, Kiiba wee hee ee* | *Tohara ya wanaume, walitahiriwa wee hee ee* |
| *Soman Kirwoogik wee taman ak muut* | *Soma Wafalme wee kumi na tano* |
| *Koiitet aap lo soman ak ites tai* | *Mstari wa sita na uendlee mbele* |
| *Kigosei akobo Samson ak Delila* | *Tunasikia kuhusu Samsoni na Delila* |
| *Kinereech Samson wee ko beel Hekalut* | *Samsoni alikasirika wee akachoma Hekalu* |
| *Woi korom chamyet wee bele emeet wee* | *Woi mapenzi ni hatari wee yachoma nchi wee* |
| *Ribeen gei chamyet wee ne konu hasara* | *Jihadhari na mapenzi hatari wee yaletayo hasara* |
| *Kigingaal Samson wee kongangta siri* | *Samsoni alidanganywa wee akafichua siri* |
| *Keebol konyeekyik wee koraat chamyet* | *Akatolewa machow wee mapenzi ni mapofu* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Janga la UKIMWI linalozungumziwa na msanii wa wimbo huu ni *mwangwi* wa ugonjwa mbaya uliozuka katika jamii ya Wayahudi na kuua watu maelfu kwa maelfu; ugonjwa unaotolewa maelezo katika kitabu cha Hesabu 25:1. Ugonjwa huu una sifa sawa na zile za Ukimwi kwani yote yanahusishwa na zinaa na kusababisha maafa mengi. Haya yanadhihirika katika ubeti wa sita (6) wa wimbo huu.

**Mf 9**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Keer en Kaitosiek 25 inameen 1*<br>*Kingeet koroito ne kiibar biik elipusiek che chaang*<br>*Nda mo Phineas kogereen ng"otit ko kibegu biik*<br><br>*Kergei ak UKIMWI ne kagotar biik ongemween wee wee.* | *Tazama Hesabu 25 uanzie 1*<br>*Ugonjwa mbaya ulizuka ukawaua maelfu*<br>*Kama si Phineas kuuzuia kwa mkuki wengiwangeangamia.*<br>*Sawa na UKIMWI unaomaliza watu tuutoroke* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Ili kuwasilisha ujumbe wa kuepukana na maambukizi ya VVU/UKIMWI, msanii anarejelea matini ya Bibilia tena. Kifungu kinachorejelewa kinapatikana katika kitabu cha Wakorinto 1 mlango wa 6 mstari wa 1 na kuendelea, ambapo mwili wa binadamu unalinganishwa na Hekalu ambayo ni mahali patakatifu katika muktadha wa Wayahudi. Ujumbe ni kwamba, mwili wa binadamu unafaa kutunzwa na kutakaswa kwani ni Hekalu la roho mtakatifu.

**Mf 10**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *En Korintoek 1 kurgat 6 inameen 1*<br>*Soman itestai en yooto asi iguiyie*<br>*Nai ile bortangung ko Hekalut aap tomirmiriet*<br>*Nebo Jehovah ara riip anyun kotililiit wee*<br>*Kainai iile ma kilabotyin ngalechono wee*<br>*Kichigili* | *Katika Wakorinto 1 Sura ya 6 uanzie 1*<br>*Soma kuanzia hapo ili uelewe*<br>*Ujue mwili wako ni Hekalu ya roho*<br>*Ya Mungu hivyo uutakase*<br>*Umejua hayo si maneno ya kukimbilia*<br>*Yachunguzwa* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

### 3.4.3 Mbinu ya Urejelezi

Pamoja na kuingiliana kimatini na matini za Bibilia, wimbo huu pia unaingiliana na matini ya Kijamii hasa utamaduni unaohusu tohara. Katika jamii ya msanii, kitendo cha kutahiriwa kinanasibishwa na adhabu. Kwa misingi hiyo, watu hasa wanaume hutaniana kwa kuambiana "nitakutahiri" kwa maana ya "Nitakuadhibu". Msanii basi katika ubeti wa 4 ametumia tohara kama sitiara. Kimsingi basi, tohara ile ya Kibibilia inaingiliana kimatini na tohara ya Kikalenjini. Hata hivyo, katika muktadha huu,

tohara inayorejelewa ni adhabu wanayoipata wanaume kutokana na VVU wasipochukua tahadhari. Ni "kutahiriwa na VVU/UKIMWI".

Wimbo wa pili unaodhihirisha Mwingilianomatini kama sifa ya kibaadausasa, ni Rat Torosta (Funga Nepi). Wimbo huu unadhihirisha kuigiliana kimatini na miktadha ya kijamii inayobainisha tamaduni na masimulizi ya maadili. Pamoja na hayo, wimbo huu unadhihirisha Mwingilianomatini kimtindo. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu, utamaduni unaorejelewa na mtunzi ni ule wa ufugaji wa mifugo hasa ng'ombe.

**Mf 11**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Ye kiin kobaraa emeet* | *Nchi ilipokuwa pana* |
| *Ye kiin kobaraa emeet* | *Nchi ilipokuwa pana* |
| *Kiogeete tuga kolenge* | *Ng'ombe walikula popote* |

(Kutoka: *Rat Torosta*. Msanii: Joel Kimetto)

Utamadunihuu umetumiwa kulingana na nyakati mbili ambapo wakati wa kwanza unahusu ng'ombe kulishwa popote. Huu ni wakati ambapo janga la VVU/UKIMWI halikuwa limeibuka. Mafunzo yanayolenga kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI kama vile kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja yanapata mwangwi katika ubeti wa pili. Katika ubeti huu, mtunzi anazungumzia ufugaji wa kisasa almaarufu 'zero grazing' ambapo ng'ombe hulishwa ndani ya chumba chake maalum.

**Mf 12**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Ko ra kominginiit emeet* | *Lakini siku hizi nchi imekuwa ndogo* |
| *Woi ra kominginiit emeet* | *Woi siku hizi nchi imekuwa ndogo* |
| *Ko kooba biik zero grazing* | *Watu wameelekea malisho ya ndani* |

(Kutoka: *Rat Torosta*. Msanii: Joel Kimetto)

Katika ubeti wa nne pia, muktadha wa ufugaji hususan ufugaji wa kondoo unarejelewa. Kuzuiliwa kwa kondoo dume kupanda majike kwa kutumia 'Torosta'

kunaapata mwangwi wake kutokana na himizo kwa watu wajizuie katika masuala ya ngono ili kuzuia kuenea kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI.

**Mf 13**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Ko ra kogoyaiit emeet* | *Lakini siku hizi nchi imekuwa mbaya* |
| *Oyie kigoyaiit emeet* | *Jameni nchi imekuwa mbaya* |
| *Kogogeer tiondo bereekwek* | *Mnyama ametamalaki malishoni* |
| *Kiile Nondin aam kerebengung* | *Mnandi alisema kula toka sahani mwako* |

(Kutoka: *Rat Torosta*. Msanii: Joel Kimetto)

Katika ubeti wa tatu, semi za Kikalenjin pamoja na mtindo wa usimulizi zinarejelewa. "Nchi kuwa mbaya" na "Nchi kuwa ndogo" “mnyama kutamalaki malishoni” ni misemo inayotumika katika jamii ya mtunzi kuelezea hali ya kuwepo kwa VVU/UKIMWI. Aidha, maonyo yanayotolewa kwa wasikilizaji kwa kukumbushwa yale yaliyosemwa na wahenga. Mianzo ya usimulizi "Kiile" na "kole" vinaweza kuchukuliwa kuwa visawe vya mianzo ya masimulizi katika jamii nyingine kama vile Kiswahili ambapo tunapata mianzo kama vile "wahenga walisema" au "wahenga hawakukosea". Mbinu kama hii imetumiwa katika wimbo *Yee Beek che miTereng’ung* (Yanywe Maji Yaliyomo Mtungini Mwako)

Isitoshe, kuna Mwingilianomatini wa kimtindo unaodhihirika pia kupitia kwa wimbo huu. Wimbo huu umeiga mitindo ya rap na hip hop kama inavyoonekana na kusikika kupitia kanda ya CD ingawa mwingiliano huu wa kimtindo unakuwa dhahiri katika wimbo mzima, ukweli ni kwamba, unadhihirika zaidi katika ubeti wa tano (5); ubeti unaoongozwa na kijana. Hali inashereheshea kuwa mitindo husika inahusishwa zaidi na vijana.

Nyimbo mbili zilizojadiliwa hapo juu zinadhihirisha kiwango cha Mwingilianomatini ambapo matini za kisanaa kama vile nyimbo zinaingiliana na matini za miktadha ya

kijamii au matini simulizi. Mwingiliano huu humwezesha msanii kuumba kazi mpya zinazomwezesha kuwasilisha maudhui au jumbe nyeti ambazo hangeziwasilisha kwa urahisi katika miktadha ya mazungumzo ya kawaida.

Katika nyimbo hizi, Mwingilianomatini umejitokeza katika viwango vya simulizi, dhamira, matumizi ya ishara (sitiara) na usawiri wa wahusika hivyo kuafiki maelezo ya Wamitila (2008).

### 3.4.4 Mwingilianomatini Kiwango cha Sanaa

Kwa mujibu wa Walibora (2010), wataalamu wanaoegemea ufaafu wa Mwingilianomatini wanaonekana kufuata maoni ya Plato kwamba binadamu hawezi kueleza kitu kilivyo hasa, bali anaweza tu kueleza jinsi kitu kilivyofanana na kingine. Moja huwa mwangwi wa nyingine. Huu ni msingi mpana wa Mwingilianomatini na msingi wake finyu ni pale ambapo kazi ya sanaa husika kama vile wimbo unahusiana na kuingiliana na wimbo mwingine unaojulikana. Katika utafiti huu, tumeuita kiwango hiki cha Mwingilianomatini kiwango cha sanaa na sanaa. Kiwango hiki cha Mwingilianomatini hutokana na matumizi ya mbinu ubandikaji (pastiche) na Simulacra hali inayofanya kazi mbili zifanane kwa njia mbalimbali.

Mwingilianomatini kiwango cha sanaa na sanaa unadhihirika kupitia nyimbo mbalimbali zilizoteuliwa. Katika kijisehemu hiki, nimeshereheshea aina hii ya Mwingilianomatini kwa kutoa mifano ifuatayo ya ushauri kuhusu kuzingatia matumizi ya dawa, lishe bora, kufanya mazoezi ili mtu aliyeambukizwa VVU aendelee kuishi. Mathlan, ushauri huu unatolewa na msanii wa wimbo Merimela katika ubeti wa tisa (9) na wa mwisho wa wimbo pale anapoimba:

**Mf 14**

*Usilie, usilie (Mela mama)*
*Usilie mwana mama usilie (Mela mama)*
*Una nafasi ya kuishi (Mela mama) usilie (Mela mama)*
*Una nafasi ya kuishi (Mela mama) usilie (Mela mama)*
*Fanya tizi (Mela mama), kula vizuri (Mela mama)*
*Meza madawa (Mela mama), tuliza roho (Mela mama)*

(Kutoka: *Merimela*. Msanii: Uncle Ckoniah)

Ushauri kama huu umetolewa katika wimbo Vuta Pumzi ulioimbwa na Longombas na hivyo kusababisha Mwingilianomatini kidhamira kati ya nyimbo hizi. Katika ubeti wa pili wa wimbo huu wao, wasanii wanamshauri na kumpa matumaini mtu aliyeambukizwa VVU/UKIMWI. Wanafanya hivyo kwa kutumia mtindo na maneno yanayolandana na yale ya Merimela hapo. Katika ubeti huu wasanii wanaimba:-

**Mf 15**

*Na kama unayo si mwisho ya maisha*
*Ni ugonjwa tu kama Malaria*
*Meza dawa, piga tizi, kula vizuri, utaishi fiti*
*Maisha utayasukuma*
*Maisha utayasukuma.*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Katika beti hizi mbili basi kuna Mwingilianomatini ambapo katika kila ubeti tunapata simulizi ndogo ndogo juu ya matumaini ya kuishi hata kama mtu ana VVU/UKIMWI. Aidha kuna himizo kuhusu matumizi mazuri ya dawa, kula vizuri, kufanya mazoezi na hivyo kuendelea kuishi.

Nyimbo mbili tulizozijadili hapo juu zinahusiana na kuingiliana kimatini na wimbo Starehe. Mwingilianomatini huu, unadhihirika kwa karibu zaidi kati ya wimbo Vuta Pumzi na Starehe. Mathalan, ushauri unaotolewa na wasanii wa wimbo Starehe kupitia kwa daktari ni sawa na ule unaotolewa katika nyimbo mbili zilizotangulia. Kwa mfano, katika ubeti wa tano (5) na wa mwisho wa wimbo huu, ushauri unatolewa na daktari kwa kijana aliyeambukizwa VVU/UKIMWI:

**Mf 16**

*Usikate tamaa*
*Inaweza ukakonda kwa Typhoid au TB*
*Ni kweli vipimo vinaonyesha umeathirika*
*Starehe mnazipenda, ila mwisho wake mbaya*
*Wengi wameteketea kwa kuendekeza umalaya*
*Kula vizuri, fanya mazoezi pumzisha mwili wako*
*Ukizingatia hayo, utaishi kwa matumizi*
*Sasa jaribu, muda bado unao*

(Kutoka: *Starehe*. Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Kutokana na Mwingilianomatini kiwango cha sanaa na sanaa, nyimbo hizi zinaelekea kufanana kidhamira na kimtindo. Maneno mengi yaliyotumiwakuunda mistari ni kama yaliyotolewa au kunukuliwa kutoka wimbo mmoja na kupachikwa kwa wimbo mwingine.

### 3.5 Ukosefu wa Mshikamano katika Nyimbo za Kibaadausasa

Asili ya neno ushikamano ni neno la Kilatini 'cohaerentia' linalotokana na "Cohaerens" lenye maana ya upangaji wa kimantiki wa sehemu za kitu. Ni kitu chenye mantiki au kisichobadilika badilika na ambacho huleta maana kikiwa kizima. Ni uhusiano wa kimaana kati ya sehemu zote za matini (www.yourdictionary.com.) Hivyo basi kukosekana kwa mshikamano ni kukosekana kwa maana katika matini. Kulingana na ensaiklopedia huru ya wikipedia, muziki wa kibaadausasa ni ama muziki unaohusishwa na kipindi cha ubaadausasa au muziki unaozingatia mielekeo ya ujumi wa falsafa za kibaadausasa. Muziki wa kibaadausasa hushirikisha sifa za sanaa za kibaadausasa kama vile kukosekana kwa mshikamano.

Kukosekana kwa mshikamano ni sifa inayohusishwa na kazi za sanaa za kibaadausasa. Hali hii husababishwa na ukiukaji wa mtindo uliozoeleka wa kihalisia. Mathalan, Wamitila (2003) na Khamis (2005) wanaeleza kazi za kibaadausasa kama zile zilizokiuka mtindo uliozoeleka, zenye ploti isiyozingatia mfuatano uliokubalika

wa vitushi na matumizi ya vipande vidogo vidogo vya visa, hali ambayo imeleta upya katika ulingo wa fasihi. Mawazo haya yanaunga mkono yale ya Barry (2002) na Khamis(2003) wanaoeleza kuwa, katika sanaa ya ubaadausasa kuna matumizi ya ujirejeleaji, ukosefu wa mshikamano na mtiririko maalum wa hadithi na badala yake tunapata vipande vipande tu vya hadithi. Mathalan, Alper (2004) anaeleza kuwa nyimbo za kibaadausasa hutumia mikakati kama vile mchanganyiko wa tanzu, ucheshi, wigobezo na kinaya.

Nao Manuel, Bilby na Largey (1995) wanafafanua kwamba, ujumi wa kibaadausasa, ukiwemo wa nyimbo umekuja kutambuliwa kama kipengele au sifa muhimu ya utamaduni pendwa. Nyimbo pendwa zinazotokana na vijitamaduni (subcultures) zinaweza kuakisi mchanganyiko wa sifa au vipengele vya kibaadausasa na vile vya kitamaduni au kiasili. Anaendelea kueleza kwamba, muziki wa Punk, rock na rap unaweza kushirikisha matumizi ya mikakati ya kibaadausasa kama vile ubandikaji (pastiche), bricolage na mzaha ulio wazi. Katika kijisehemu hiki, nyimbo nne zimetumiwa kushereheshea hali ya kukosekana kwa mshikamano katika nyimbo zinazohusiana na VVU/UKIMWI.

Wimbo wa kwanza unaonyesha ukosefu wa mshikamano ni *Si Lazima*. Huu ni wimbo ambao beti zake za mwanzo mwanzo zinaelekea kuhimiza ugunga au kitendo cha mtu kujizuia kushiriki ngono. Mawazo haya yanatokana na msingi wa matumizi ya kitenzi “Kuchill” kinachotumiwa hasa na marafiki wa kiume kwa kike kupiga vita maambukizi ya VVU. Maana ya kitenzi hiki ni kuwa marafiki wa kuaminiana hususan kuhusu suala la ngono. Kitenzi hicho hurejelea tabia ya kuwajibika katika kitendo cha ngono kwa kuzingatia ngono salama.

Inatarajiwa kuwa, wimbo huu ungehimiza kitendo cha “Kuchill” kwa wahusika kutoka mwanzo hadi mwisho kwani mwimbaji anasema:-

**Mf 17**

*Si lazima tu do*
*Si lazima eti kila wakati ni kukuundress*
*Tunaweza kwenda home na tuchill to do*

(Kutoka: *Si Lazima*.Wasanii: P- Unit)

Hata hivyo, katika ubeti wa mwisho wa wimbo huu, inadhihirika kuwa wahusika huenda walikosa “kuchill” au kutoshiriki ngono. Hii ni kwa sababu, katika mstari wa mwisho wa wimbo huu, mmoja wa wahusika anakiri kushindwa kujizuia. Anasema:

**Mf 18**

*Nimekuwa wet*
*Nimetokwa*
*Ah temptation kibao joh!*

(Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P- Unit)

Hali hii ya ukosefu wa ushikamano inadhihirika vile vile katika wimbo *Nyambizi* wake Dully Sykes. Wimbo huu, sawa na *Si Lazima* unatarajiwa kupiga vita maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa kuhimiza matumizi ya kondomu ikiwa mtu hawezi kujizuia au kugunga kushiriki ngono. Kukosekana kwa mshikamano kunadhihirishwa mwishoni mwa wimbo huu ambapo mwimbaji anaimba:-

**Mf 19**

*Usiku huo ilikuwa bila zana*
*Ngoma dry, ajali kitandani*

(Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Ukosefu wa mshikamano unadhihirika pia katika wimbo *Wee Kamu*. Katika wimbo huu, kuna mistari inayoonyehsa kukosekana huku kwa mshikamano. Tazama mistari hii namna inavyosababisha kupotea kwa mantiki katika wimbo huu:

**Mf 20**

*Naeza tembea kwa chupa zimevunjika miguu tupu?*
*Nijifanye sugu sabu yako tu. Sabu yako tu?*
*Zile tembe zangu za viagra vipi?*
*Nimbariki na juala*
*Juala nimenunua kibao*
*Bora leo niache nizame vimbichi*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Katika wimbo huo mistari miwili ya kwanza inachora taswira ya mwanaume anayekataa kushiriki ngono bila kinga. Taswira hii inashadidiwa katika mstari wa nne na wa tano ambapo mhusika anaonekana kuchukua tahadhari kwa kununua kondomu nyingi na kuziweka chumbani mwake. Hata hivyo, mstari wa tatu unatuchorea picha tofauti na ile ya awali. Picha tuipatayo kutokana na mstari huu ni ya mwanaume anayeshabikia ngono na hivyo kujiwekea dawa za kusisimua misuli kwa ajili ya kitendo hicho. Hatimaye katika mstari wa mwisho, mhusika anaonekana kutupilia mbali matumizi ya kinga na kutaka akubaliwe kushiriki ngono bila kutumia kondomu ambazo tayari ako nazo. Hali hii inadhihirisha ukosefu wa mshikamano wa hali ya juu.

Kutokana na maelezo haya, imebainika kuwa, nyimbo za kibaadausasa zina sifa ya ukosefu wa mshikamano. Wasikilizaji wa nyimbo za aina hii hupata taklifu kubainisha mipaka ya uhalisia na udhahania. Hata hivyo, kutokuwepo na mipaka ya kisanaa ni sifa muhimu ya kazi za kibaadausasa na nyimbo zilizojadiliwa hapo zinabainisha hali hii.

### 3.6 Kukosekana Kwa Uaushi

Jameson (1991) akizungumzia ubaadausasa kama hatua mojawapo ya ubepari, anaeleza kuwa hatua ya tatu na ya mwisho ya ubepari ni wakati wa sasa. Anaeleza kuwa hiki ni kipindi kinachohusishwa na maendeleo makubwa ya kiteknolojia.

Msisitizo katika kipindi hiki upo katika jinsi ya kuuza na kutumia bidhaa na wala siyo katika namna ya kuzitengeneza. Kwake Jameson, hatua hii ya mwisho ya ubepari huhusishwa na ubaadausasa. Jameson anaeleza kuwa, uundaji wa kazi za kisanaa unalinganishwa na utengenezaji wa bidhaa nyingine zozote. Selden, Widdowson na Booker (2005). Hivyo basi, utamaduni wa kibiashara ni sehemu ya sanaa ya ubaadausasa.

Kutokana na hali hii, ubaadausasa unasababisha kukosa kwa uhalisi na kuunda kazi chapwa jinsi waundaji wa bidhaa wanaohusishwa na kipindi hiki wavyoibuka na bidhaa ghushi. Kutokana na ukosefu wa uhalisi wa kihistoria kupitia kile alichokiita Jameson ‘uwanja wa mitindo’ usiongozwa na kanuni yoyote nafasi ya wigobezo inachukuliwa na hali ya uigizaji usio na usanifu.

Kulingana na Baudrillard (1980), ulimwengu wa ubaadausasa ni ulimwengu wa Simulacra ambapo hatuwezi kubainisha tofauti kati ya uhalisi na maigizo. Kwake Baudrillard hakuna tofauti kati ya ishara na uhalisi katika vyombo vya kiteknolojia. Anaeleza kuwa ishara haziwakilishi uhalisi bali zinajiwakilisha zenyewe. Aidha msimamo wa Baudrillard ni kwamba ulimwengu wa sasa una viasharia visivyo na viashiriwa. Jambo hili hutupatia ulimwengu wenye uhalisia usio wa kawaida. Huu ni ulimwengu unaodhihirishwa na baadhi ya nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa katika tasnifu hii. Ulimwengu huu hudhihirika kupitia misimu na au misemo isiyodumu na kuonyesha kukosekana kwa uaushi, uhalisi na ukweli halisi.

### 3.6.1 Misimu/Misemo Inayoonyesha Kukosekana kwa Uaushi

Misimu/misemo iliyotumika katika nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa katika tasnifu hii zinarejelea VVU/UKIMWI, ngono, sehemu za siri na hata vifaa vya kinga kama vile kondomu. Hata hivyo, misimu na au misemo husika inadhihirisha hali ya kukosekana kwa uashi kwani inatumika kuwasilisha ujumbe kisha inapotea na nyingine kuibuka.

Mathalan, msemo wa "kukwachua mimba" uliotumiwa katika wimbo *Merimela* ulitumika wakati wa mashindano ya kuwania shilingi milioni moja yaliyodhaminiwa na kampuni ya mawasiliano; Safaricom. Msimu huu unatokana na neno "kwacha" linalomaanisha pesa za Zambia. Msimu huu unahusishwa na pesa nyingi. Mtu aliyejishindia shilingi milioni moja basi alisemekana "kukwachua" yaani kujipatia. Hii ni kutokana na lugha iliyotumiwa "kwachua milioni". Msanii wa wimbo wa Merimela alitunga wimbo wake katika kipindi hicho cha mashindano husika na akatumia msimu huo kumaanisha kupata mimba. Tangu kuisha kwa mashindano ya kukwachua milioni na baada ya msimu huu kutumiwa katika wimbo huu, misimu mingine imekuja ikienda. Kwa mfano, kumekuweko na mashindano yaliyodhaminiwa na kampuni iyo hiyo ya Safaricom kama vile: Chomoka na Pickup, Dunga Mili, Dosika na pickup na kadhalika.

Mfano mwingine ni msemo "kuvunja mifupa" uliotumiwa katika wimbo ule ule wa *Merimela*. Msemo huu ulitumiwa mwanzo kabisa na mwimbaji Samba Omar Mapangala katika wimbo wake "Vunja mifupa wakati ungali na meno" ambao ulivuma katika miaka ya 1980. Maana ya msemo huu ni kufurahia maisha, kustarehe na hasa kufanya mapenzi mtu akiwa bado ana nguvu. Yaelekea kuwa msemo huu nao umepotea kwani hausikiki ukitumiwa siku hizi.

Msimu unaorejelea mtambo wa kiteknolojia wa kutoa huduma za pesa almaarufu ATM Machine na kadi yake ni msimu unaoenda sambamba na matumizi ya vyombo vya kiteknolojia hasa katika karne hii ya ishirini na moja; kipindi ambacho kinatambuliwa kama kipindi cha dijitali. Pamoja na misemo inayorejelea vyombo vingine vinavyohusishwa na kipindi hiki kama vile ‘kuwa daladala, kuwa dustbin’, msemo wa ‘kuwa daladala umetumiwa katika wimbo wa *Merimela* na ule wa *Starehe* kurejelea mtu hasa mwanamke anayeshiriki ngono na wanaume zaidi ya mmoja.

Katika miaka ya kitambo, mtu aliyeambukizwa ugonjwa wa zinaa alikuwa akisemekana ‘kuchomwa’ na huo ukawa msimu wa nyakati hizo. Enzi ya VVU/UKIMWI ilikuja na misimu na misemo inayoelezea hali hii ya VVU/UKIMWI. Misimu na misemo hii imekuwa ikiibuka na kutumiwa kuwasilisha ujumbe kisha kupotea na mingine kuibuka. Mathalan, katika wimbo *Starehe*, “kukimbilia moto” na “dalili za umeme” ni misemo inayorejelea kuambukizwa VVU. Kwa mfano, mtu akishukiwa kuwa na VVU/UKIMWI, utasikia watu wakisema “amepata moto mkubwa” au amekanyaga waya wenye stima (live wire). Moto huchoma jinsi waya wenye stima unavyochoma. Kuambukizwa huku kumeelezwa na msemo “kupata ngoma” katika wimbo *Starehe* na “kupata kichaa cha mbwa” katika wimbo *AjaliKitandani*. Aidha kuna “ngoma dry” na “ajali kitandani” katika wimbo *Nyambizi.*

Msimu “kuchill: uliotumiwa katika nyimbo *Merimela* na *Si Lazima* una misingi yake katika kampeni za kupiga vita dhidi ya VVU/UKIMWI nchini Kenya hasa wakati wa utawala wa aliyekuwa rais mstaafu Mwai Kibaki (Nyawira, 2008). Ilivyo ni kwamba, msimu huu hausikiki ukitumiwa siku hizi na ikiwa unatumiwa, huwa ni kwa nadra basi.

Pamoja na hayo, kuna misemo na misimu iliyotumiwa kurejelea watu wanaoaminika kuwa wanakufa kutokana na UKIMWI. Katika wimbo *Vuta Pumz,* kuna misemo kama vile “wanachora” na “ku-go”. Kuchora ni kule kuandika wosia mtu anapojua ameambukizwa VVU huku “ku-go” ukimaanisha kufa pole pole. Pia wanawake wenye makalio makubwa makubwa wanarejelewa kwa msimu “kujaza nyuma”. Mtu akiwakimbilia anaweza kuambukizwa. Hali hizi zinazohusishwa na walioambukizwa VVU.

Msimu “mpango wa kando” ni wa hivi karibuni zaidi. Msimu huu unarejelea hali ya mtu, mwanaume au mwanamke aliye kwenye ndoa kuwa na mpenzi mwingine wa nje au kando ya hiyo ndoa. Msimu huu ulitumika zaidi katika mwaka wa 2013 na kwenda nyuma. Ni msimu ambao uliwahi kuzua mjadala mkali wa kijamii ulipotumiwa kutangaza umuhimu wa kutumia kondomu kama kinga wakati wa kushiriki ngono. Wahusika katika tangazo hilo walikuwa wanawake walioonekana kuwa wameolewa huku wakihimiza matumizi ya kondomu wakati wa kushiriki ngono na mpenzi wa nje. Tangazo lilikuwa: “…lakini kumbuka kuweka kondomu mpangoni.”

Hatimaye tangazo hili lilitolewa hewani baada ya makundi ya kidini hasa ya Kikatoliki kulalamika kwamba lilikuwa linawahimiza wanajamii hasa waliokuwa kwenye ndoa kuanza kushiriki ngono za kiholela kinyume na mafundisho ya dini.
“Sooh”, “ashu”, “doo” na “ngiri” ni misimu inayotumiwa kurejelea pesa. Misimu hii imetumiwa katika wimbo *Juala* na *Ajali kitandani*. Katika muktadha huu, “sooh” huwa mia, ‘ashu’ huwa shilingi kumi na ‘ngiri’ huwa elfu moja. “Doo” hurejelea pesa kwa jumla.

Misimu na au misemo iliyojadiliwa katika kijisehemu hiki inabainisha kuwa hakuna kitu kilicho na uaushi. Aidha inaonyesha kuwa hakuna ukweli ulio halisi kwani kama

ungekuweko, misimu na au misemo haingebadilikabadilika au hata kupotea kabisa hususan ikiwa inarejelea hali ile ile moja.

### 3.7 Hitimisho

Katika sura hii nimejadili jinsi baadhi ya mikakati ya Ubaadausasa inavyotumika katika nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa katika tasnifu hii. Kutokana na mjadala huu, imebainika kuwa kazi za kibaadausasa zina mikakati maalum inayozipambanua kazi hizi kutoka kwa kazi nyingine kama vile za Usasa. Baadhi ya sifa hizo zinazodhihirika katika nyimbo zilizochanganuliwa katika tasnifu ni pamoja na ukiukaji, mwingilianomatini, urejelezi, ukosefu wa mshikamano na kukosekana kwa uaushi. Hivi vikiwa ni baadhi ya vipengele muhimu vinavyopambanua Ubaadausasa.

# SURA YA NNE

# NYIMBO NA SUALA LA UNYANYAPAA

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii nimechanganua simulizizinazohusu VVU/UKIMWI na unyanyapaa. Kwa jinsi hiyo, nimefafanua maana ya unyanyapaa athari zake na aina za unyanyapaa. Uchanganuzi huu pia, umepania kubainisha na kufafanua simulizi kuu na ndogo za VVU/UKIMWI zinazokuza na zile ambazo zinaupinga unyanyapaa. Nimefanya hivyo kwa kubainisha hadhira zinazolengwa, miktadha ya kijamii inayohusika na namna lugha ilivyotumiwa kuwasilisha simulizi na jumbe zinazohusiana na ngono, sehemu za siri za mwili wa binadamu na VVU/UKIMWI. Nyimbo husika ni za Kikristo na zisizokuwa za Kikristo na zilizoimbwa kwa Kiswahili, Kimaasai, Kikalenjin na Kijaluo. Ninyimbo zilizotungwa na kurekodiwa na wasanii binafsi au makundi mbalimbali na zinasikika katika sehemu nyingi nchini Kenya.

## 4.2. Maana ya Unyanyapaa

Unyanyapaa una maana tofauti tofauti kwa watu tofauti tofauti. Goffman (1974) anaeleza kuwa unyanyapaa ni sifa ya kuaibisha na ambayo humfanya mtu aonekane mwenye doa na hivyo anayefaa kuadhiriwa kulingana na mielekeo iliyokita katika jamii. Anaendelea kueleza kuwa asili ya neno hili ni Ugiriki ambapo lilikuwa na maana ya chale aliyowekwa mtu kwa kufanya kitendo cha kuhatarisha au cha kuponza. Madhumuni ya alama hiyo ilikuwa ni kumtambulisha mtu aliyekuwa na dosari, ila au waa. Stein (2010) anaeleza kuwa, kadri muda ulivyoendelea, istilahi hii ilifungamanishwa na ukengeushi pamoja na tabia zisizokuwa za kawaida hasa zinazoleta hisia hasi hususan kutowajibika kingono.

Kulingana na Kamusi ya TUKI(2010) unyanyapaa ni fedheha au mtwezo unaohusishwa na chochote kisichokubalika katika jamii. Ni hali ya kuwepo kwa hisia za "sisi na wao" ambapo watu walionyanyapaa wanatiwa alama ya kuwafanya kuwa tofauti na wanajamii wengine na kulaumiwa kwa ajili ya tofauti hiyo.

Katika jamii zetu kwa mfano, watu wengine wanaposikia kuwa mtu ana Virusi Vya UKIMWI, humwona kama mtu anayekufa polepole au aliyekufa huku akiishi. Awali, mtu wa aina hii hangeguswa au kugusana na mwingine asije akawaambukiza. Hii ni kwa sababu UKIMWI ni ugonjwa ambao huwaogofya watu wengi hasa kutokana na kutopata habari zilizo sahihi kuuhusu. Aidha wanajamii wengi huwa na hisia pendelevu au hasi juu ya UKIMWI.

### 4.3 Athari za Unyanyapaa

Matokeo ya unyanyapaa ni kutukanwa, kukataliwa au kutengwa, kufitiniwa na kutoshirikishwa katika shughuli za kijamii kwa walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Hofu juu ya tabia hizi huwafanya watu walio na Virusi Vya UKIMWI kuogopa au kuwa na mfadhaiko wa kutangaza au kufichua hali yao ya VVU/UKIMWI. Aidha huwafanya kukwepa kujumuika na watu wengine. Hali hii huenda ikawafanya wateseke katika unyamavu badala ya kufaidi msaada wanaouhitaji. Isitoshe, unyanyapaa huwafanya watu wasadiki yanayosemwa na watu wengine kuhusiana na VVU/UKIMWI. Mathalan, wanaweza kuamini kuwa VVU/UKIMWI ni hukumu ya kifo kwao au kuwa wote walio na UKIMWI ni wazinzi au wasiowajibika.

Kulingana na ***mobile.aidsmap.com***, unyanyapaa aghalabu hufungamanishwa na vitu au hali zinazoogofya. Kwa mfano, tangu kuripotiwa kwa kesi za kwanza za ugonjwa huu katika miaka 1980s, watu walio na UKIMWI wamekuwa wakifedheheshwa kwa sababu:

i. UKIMWI ni hatari; ni ugonjwa unaotishia maisha au uhai na hasa ikizingatiwa kuwa, kuna historia ndefu ya kufedheheshwa kwa wagonjwa wa Saratani, Kifuakikuu na Ukambi.

ii. Watu wasiojua namna Virusi Vya UKIMWI vinavyoambukizwa huhofia kuambukizwa kupitia mitagusano ya kijamii.

iii. Watu wengine wana mitazamo au misimamamo mikali kuhusu kitendo cha ngono. Wenye misimamo kama hii huchukulia kuwa, kuna nyakati na miktadha ambamo ni hatia au kosa ama watu fulani hawafai kuwa na tabia fulani fulani.

iv. Fikra za watu kuhusu UKIMWI hutegemea namna wanavyochukulia makundi ya kijamii yanayoathirika zaidi kutokana na ugonjwa huu. Wengine tayari wana hisia hasi kuhusu wanawake, mabasha, watu weusi, watumizi wa dawa za kulevya na kadhalika. Hali hizi zinadhihirika katika baadhi ya nyimbo tulizozichanganua. Ni hali na tabia zinazopingwa na wanabaadausasa.

### 4.4 Aina za Unyanyapaa

Ubaguzi dhidi ya watu walio na VVU/UKIMWI huchukua sura mbalimbali ambazo ni pamoja na kukataliwa, kubaguliwa, kutengwa, kuwakwepa walioambukizwa, kuchunguzwa damu bila kujuzwa, kukosa kuweka siri au kutangaza hali ya UKIMWI

ya mtu, kuingiliwa kwa nguvu au bila kuzingatia sheria, kuwekwa karantini na kunyimwa urithi mtu anapofiwa. Vurugu zinazofungamanishwa na unyanyapaa au hofu ya kuingiliwa kwa nguvu huwazuia watu wengi kujichunguza, kurudi kuchukua matokeo au kupata matibabu na hivyo kugeuza ugonjwa hatari ambao ungetibiwa kuwa hukumu ya kifo na kukuza kuenea kwake.

Kuna aina nne za unyanyapaa unaofungamanishwa na VVU/UKIMWI.:

i. Unyanyapaa wa kiufugamano au kiuhusika. Huu ni unyanyapaa unaofungamanishwa na ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Ni akisiko la hofu inayohusishwa na ugonjwa wowote hatari na wa kuambukizana.

ii. Unyanyapaa wa kimfumo au kiishara. Huu ni unyanyapaa unaotumia UKIMWI kueleza mielekeo kuhusu makundi fulani ya kijamii yanayohusishwa na ugonjwa wenyewe.

iii. Unyanyapaa wa kifadhila au kiustahiki. Huu ni unyanyapaa unaoelekezwa kwa watu kama vile makahaba na matajiri wanaohusishwa na suala la VVU/UKIMWI au watu walioambukizwa VVU.

iv. Unyanyapaa wa kibinafsi. Huu ni unyanyapaa unaoendelezwa na mtu aliyeaambukizwa dhidi ya nafsi yake baada ya kugundua ameambukizwa. Ni unyanyapaa unaomfanya mgonjwa ajitenge na wanajamii wengine. Wataalamu wa afya niliowahoji wanadai kuwa, huu ni unyanyapaa unaosababisha vifo vingi zaidi vinavyohusiana na VVU/UKIMWI.

Aghalabu, unyanyapaa au ubaguzi unaohusiana na VVU/UKIMWI huelezwa mintaarafu ya aina moja ya unyanyapaa au zingine hasa zile zinazohusishwa na mabasha, wafanya ajira ya ngono, wanaotumia mihadarati ya kujidungia, wazinzi, huntha na kadhalika. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba, unyanyapaa hupelekea watu kutochukuliwa kwa hadhi na heshima zinazohusiana na ubinadamu.

Kufedheheshwa, kubaguliwa au kutengwa aghalabu huwa sehemu mbaya zaidi ya maisha kwa wale walio na VVU/UKIMWI. Wengi husema: “Siwezi kugeuka na kuwaambia nina VVU/UKIMWI kwa sababu ninajua watakavyonichukulia”. Haya ni mawazo yanayopingwa na wanabaadausasa.

## 4.5 Nyimbo na Simulizi kuhusu Unyanyapaa

Katika wimbo *Merimella,* msanii Ckoniah anaanza kwa kusimulia juu ya maisha ya mhusika Merimela akiwa katika shule ya msingi madarasa ya chini. Msanii anaeleza kuwa, Merimela alikuwa rafiki yake wa karibu walipokuwa shuleni. Anasimulia sifa alizokuwa nazo msichana huyu alipokuwa shuleni na wakiwa wadogo. Sifa hizo ni kwamba, Merimela alikuwa mpole, mwenye adabu, mwerevu, mrembo na alikuwa mshindi kila mara masomoni. Sifa na urembo wake zilienea kote na kila alipopita kulikuwa na ***whispers***, yaani minong’ono**.**

Kwa kutanguliza wimbo wake na simulizi kuhusu sifa alizozidokeza,pamoja na kujikita katika muktadha wa shule ya msingi, msanii alikuwa na lengo la kupinga simulizi kuu kuwa watoto wadogo na hasa wa kike hawakuwa wanashiriki ngono na hivyo hawangeambukizwa VVU/UKIMWI. Hizi zilikuwa dhana potofu. Mintarafu ya habari hizi za kupotosha, wanaume waliokuwa wameambukizwa VVU/UKIMWI waliwakimbilia wasichana wadogo wadogo hasa mabikira kwani iliaminika kuwa, kushiriki kitendo cha ngono na msichana bikira kungemponya mwanaume aliyekuwa na VVU/UKIMWI.

Isitoshe, awali kulikuwa na simulizi kuu kwamba, watu ‘wazuri’ ambao walikuwa wapole, wenye heshima, wenye adabu na werevu hawangepata VVU/UKIMWI. Lakini kwingineko katika wimbo huu, tunasimuliwa kwamba Merimela aliambukizwa VVU/UKIMWIlicha ya kuwa na sifa zilizochukuliwa na wanajamii kuwa za mtu

'mzuri'. Urembo pia ni sifa inayoendana sana na masuala ya mapenzi, ngono na magonjwa ya zinaa ukiwemo VVU/UKIMWI. Wasichana warembo huwavutia wavulana au wanaume kimapenzi. Aghalabu mvuto huu hatimaye huwaingiza wahusika katika kitendo cha ngono kabla ya ndoa na hata bila ya kuwa na mipango ya ndoa. Kupitia kwa kitendo cha ngono bila kinga, wahusika wanaweza kuambukizana VVU/UKIMWI. Ingawa msanii hajataja VVU/UKIMWI mwanzoni mwa wimbo huu, ni dhahiri kuwa ujumbe anaouwasilisha ni kwamba yeyote anaweza kuambukizwa VVU/UKIMWI katika umri wowote maishani. Hili linakuwa wazi hasa tunapofikia tamati ya wimbo huu kwani mhusika mkuu Merimela mwishowe aliambukizwa.

Masimulizi yanayofuata katika ubeti wa pili yamekitwa katika muktadha ule ule wa shule ya msingi lakini madarasa ya juu kwani msanii anasimulia kuwa ni katika darasa la saba ambapo Merimela alianza kugeuka. Mabadiliko yanayosimuliwa na msanii ni kwamba, badala ya kuendelea kuwa msichana mpole na mwenye adabu jinsi jamii ilivyomtarajia, Merimela alianza kushiriki ngono na***machali mbalimbali***yaani vijana tofauti tofauti wa kiume pamoja na walimu wake. Alijihusisha na mapenzi bila tahadhari huku akipuuzilia mbali ushauri kutoka kwa waliokuwa karibu naye. Katika hali hii, Merimela amefananishwa na kinywaji aina ya ***quencher***. Kwa kawaida, kinywaji hiki hutumiwa kuzima kiu hasa ya maji. Aidha hutumiwa kujiburudisha nyumbani au wakati wa sherehe. Hata hivyo, katika muktadha wa wimbo huu**,** ***machali*** na walimu walimfanya Merimela kuwa ***quencher*** na wala si ya kuwazimia kiu ya maji bali ya mapenzi, nyege au ashiki. Lugha iliyotumiwa inaanza kukuza unyanyapaa kwani binadamu anafananishwa na kinywaji kitamu kama ***quecher***.

Isitoshe, msanii anaeleza kuwa, alijaribu kumwonya Merimela lakini hakuzigatia maonyo yake. Mathalan, alipomshauri achunge sana maisha na abadilishe mwenendo,

alipuuza ushauri na kudai kuwa alikuwa akiyafurahia maisha; ***waenjoy*** maisha na alikuwa ***yuavunja mifupa***. Mwimbaji anaendelea kueleza kuwa, Merimela baadaye alipata mimba***; ukakwachua*** mimba. Kulingana na msanii, baada ya mhusika kupata mimba, alitafuta ushauri. Ushauri alioupata ulikuwa kwamba atoe kitu kidogo kwa madhumuni ya kufanya ***abortion***; kuavya mimba hiyo. Pamoja na hayo, hakupewa ushauri kuhusu njia salama ya kuavya mimba. Aidha, msanii anamkumbusha kuwa, aliposhauriwa awe na mpenzi mmoja**'*uchill,*'** alisema hiyo ilikuwa ni ndoto; yaani haingewezekana. Alipoambiwa atumie mipira naye akajibu "si tamu" na aliposhauriwa kupanga uzazi akajibu "ni ***hectic"***; yaani ni maisha yenye msisimko na shughuli nyingi. Kuhusu wokovu, alishikilia kuwa ilikuwa ni mapema kuokoka. Katika sehemu hii, msanii anatumia viingizi katika uimbaji wake ili kuendeleza mazungumzo yake. Viingizi hivyo ni pamoja na: ***that's a dream, haina ladha, vipi? na mambobado, wokovu bado***.

**Mf 21**

*Kwa darasa la saba kipenzi Merimela ukaanza geuka*
*Machali mbalimbali hata nao walimu wakakufanya quencher*
*Nawe ukakubali ingilia mapenzi ya kiholela holela*
*Na ukawachukia walokuwa karibu wakikupa ushauri ee*

(Kutoka: *Merimela*. Msanii: Uncle Ckoniah)

Tangu mwanzo hadi hapa, msanii anawakilisha wanajamii wanaowalaumu waathiriwa wa VVU/UKIMWI. Merimela analaumiwa kwa masaibu yaliyompata. Hapa ndipo tunaweza kusema ya kwamba, wimbo huu unakuza simulizi kuu kuhusu unyanyapaa kwa njia moja au nyingine. Merimela analaumiwa kuwa, aliambukizwa kwa sababu hakuzingatia ushauri. Hiini simulizi kuu kuhusu VVU/UKIMWI unaotawala katika jamii. Kwa kiasi kikubwa basi, wimbo huu unaafikiana na msimamo wa wanajamii kuhusisha urembo, ngono na VVU/UKIMWI hasa kwa upande wa jinsia ya kike. Ni msimamo unaochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI kwa sababu ya kutolaumiwa kwa jinsia ya kiume licha ya kitendo cha ngono kuhusisha watu wa jinsia zote mbili. Ni

simulizi kuu inayopingwa na wanabaadausasa kwa kuwa haumpi mwanamke nafasi ya kutoa simulizi yake, kutoa hisia zake na hivyo kujitoa lawamani. Hata hivyo, kwenye wimbo huu kuna simulizi ndogo inayobainishwa na matamshi ya Merimela akiwawakilisha wale waliotengwa au kunyanyapaa kwa kutwikwa lawama kuhusu kuenea kwa VVU/UKIMWI. Mathalani, anaposema kuwa, ***yuaenjoymaisha*** na ***yuavunja mifupa***, anarejelea kitendo cha ngono ambacho kimsingi hawezi kukitenda peke yake. Isitoshe, utamu wa ngono, kitendo cha ***kuchill*** kuwa ndoto, mpango wa uzazi kuwa ***hectic*** na kutookoka mapema si maswala yanayowahusu wanawake peke yao bali yanawahusu wanaume pia hasa vijana.

Simulizi katika ubeti wa nne kuhusu maisha ya Merimela umekitwa katika miktadha ya shule ya upili na chuo kikuu ambapo aliendelea na mwenendo ule ule wa shule ya msingi. Aliendelea na kushiriki mapenzi ya kiholela, jambo lililomfanya apate mimba kila mwaka na kuziavya. Katika chuo kikuu raha zilipanda na akawa ***anavunja mifupa***. Alishiriki raha hizi pamoja na ***wadosi*;** yaani wenye pesa na vyeo pamoja na mafukara.Wote aliwaonja na mimba ikawa jambo la kawaida. Ili kuwasilisha habari zinazohusu ngono, viungo vya uzazi, uasherati na uwezekano wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI, msanii ametumia lugha ya sitiara. Amemfananisha Merimela na ***dustbin*** yaani jaa la kutupiwa takataka ambapo takataka yaweza kuwakilisha shahawa zilizo na Virusi Vya UKIMWI huku sehemu ya uzazi ya mwanamke ikilinganishwa na jaa. Aidha, viungo vya uzazi vya mwanamke na mwanamume vimefananishwa na vyombo vya teknolojia ambavyo vijana wanavijua. Mathalan, viungo hivi vimetajwa kama ***ATM machine*** na kadi mtawalia. Kila kadi kuweza kuingizwa kwenye mashine ya ***ATM*** ni jazanda ya kitendo cha mwanamke mmoja kushiriki ngono na wanaume wengi.

Mbali na hayo, msanii pia amemfananisha Merimela na gari la kusafiria almaarufu daladala. Kimsingi, daladala ni gari ambalo hutumiwa na umma kusafiria kwa kulipa nauli . Mtu yeyote anaweza kuabiri daladala almuradi tu awe na nauli. Mwimbaji amemlinganisha mwanamke na daladala, huku usemi *kila mtu* ukirejelea wanaume. Kitendo cha kila mtu kupanda daladala ile ile moja kinarejelea kitendo cha wanaume wengi kushiriki ngono na mwananamke mmoja. Katika muktadha wa kushiriki ngono katika jamii nyingi, mwanamke ndiye anayepandwa. Maoni yangu ni kwamba, simulizi zinazomlinganisha mwanamke na jaa, ATM na daladala ni simulizi za kukuza unyanyapaa.

**Mf 22**

*Ukakuwa ni dustbin, ya kutupa takataka*
*ATM machine (Aii), kila kadi yaingia*
*Ukakuwa daladala, kila mtu akupanda (kila mtu)*

(Kutoka: *Merimela*. Msanii: Uncle Ckoniah)

Katika ubeti wa tano, msanii anasimulia maisha ya Merimela akiwa ametoka chuoni. Baada ya kuhitimu masomo ya chuo kikuu, Merimela aliandaa harusi kanisani ambapo siku hiyo ya harusi ilikuwa ya furaha, fivijo na nderemo. Kulikuwa na maombi na zawadi zikawa zinatolewa pia. Almuradi kila mtu alifurahia harusi hiyo.

Kwenye ubeti wa mwisho, kuna simulizi kuhusu maisha ya mhusika baada ya kuolewa. Katika jamii za Kiafrika, simulizi kuu ni kwamba, mwanamke anatarajiwa apate mtoto baada ya kuolewa. Tarajio hili si kwa mwanamke husika peke yake bali ni kwa mumewe, wakwe na jamii nzima kwa ujumla. Mtoto anapokosa kupatikana, mwanamke ndiye wa kulaumiwa na kupigiwa makelele. Katika jitihada za kupata mtoto basi, mwanamke hulazimika kufanya kila mbinu ikiwemo kwenda kwa waganga wa kienyeji, madaktari hospitalini na kwenye maombi. Hivyo ndivyo alivyofanya Merimela lakini bila mafanikio. Simulizi inayohusu unyanyapaa hapa inadhihirika msanii anapoeleza kuwa, furaha ilikwisha ikabaki huzuni, mawazo ya

kila siku na majuto. Simulizi hii inakuwa wazi zaidi msanii anapoingiza maelezo aliyotoa dakitari kwake Merimela kwamba hangebeba mimba kwa sababu ya kuharibika kwa mfuko wa mtoto na kugunduliwa kuwa alikuwa amepata virusi. Ingawa msanii hajaeleza virusi hivi ni vya ugonjwa gani, uteuzi na matumizi yake ya maneno yanabainisha kuwa virusi ni vya UKIMWI. Msanii ametumia maneno kama vile ***Uchungu wamachungu*** na ***Kama ungejua tu ungetahadhari mapema***. Kauli kama hizi zinahusishwa zaidi na ugonjwa wa UKIMWI kuliko magonjwa mengine.

Simulizi inayofuata inapinga unyanyapaa na hivyo kutoa matumaini ya kuishi kwa walioambukizwa. Msanii anamshauri Merimela asilie kwani licha ya kuambukizwa virusi, bado alikuwa na nafasi ya kuishi. Anampa matumaini ambayo hangepewa na wanajamii kwani wangemhukumu hukumu ya kifo tu. Anamshauri afanye mazoezi; ***fanya tisi*** na ale vizuri. Aidha, anamshauri **amezedawa** na ***atulize roho***. Hizi ni simulizi ndogo katika wimbo huu zinazopinga unyanyapaa. Ingawa msanii hakufafanua kwa uwazi umuhimu wa ***kufanyatis***i, ***kumezadawa*** na ***kutulizaroho***, ni wazi kuwa huu ni ushauri nasaha unaotolewa mara kwa mara kwa walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Dawa anazoshauriwa kuzimeza ni zile za kupunguza makali ya UKIMWI almaarufu ARVs ingawa hili halitajwi moja kwa moja. Ushauri kuhusu kufanya mazoezi, lishe bora na kuwa na utulivu wa roho unaenda sambamba na maoni ya wanabaadausasa kwamba, matatizo yanayomkumba binadamu hayawezi kusuluhishwa kikamilifu kwa kutegemea mbinu za kisayansi peke yake. Kufanya mazoezi, kuzingatia lishe bora na kutokuwa na mfadhaiko ni tabia ambazo zinaweza kuimarisha kinga mwilini na hivyo kupunguza kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI. Simulizi hii pia inapinga unyanyapaa na hivyo kudhihirisha umuhimu wa nyimbo katika vita dhidi ya UKIMWI pamoja na unyanyapaa.

**Mf 23**

*Usilie mwana mama uslie (Mela mama)*
*Una nafasi ya kuishi (Mela mama), usilie (Mela mama)*
*Fanya tizi (Mela mama), kula vizuri (Mela mama)*
*Meza madawa (Mela mama), tuliza roho (Mela mama)*

(Kutoka: *Merimela.* Msanii: Uncle Ckoniah)

Kutokana na uteuzi na matumizi ya maneno kama vile ***fanya tisi***, ***uchill***, ***kwachua, waenjoy, wadosi, machali*** pamoja na kuchanganya ndimi kama vile ***whispers, hectic, abortion, quencher***na kadhalika**,** ni wazi kuwa, hadhira inayolengwa ni ya vijana wasomi. Hawa ni wanafunzi wa shule za msingi, shule za upili na vyuo. Aidha, walioko kwenye ndoa pamoja na wale walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI pia wamelengwa na msanii. Miktadha ya kijamii inayobainika ni kama vile, shule ya msingi, shule ya upili na vyuo vikuu. Mathalani, mwishoni mwa wimbo, msanii anawatunuku wimbo wake wanafunzi wote wa vyuo vikuu kutoka Arusha, Kampala, Nairobi na Maseno. Pia kuna miktadha ya harusini, kwa waganga, kazini, hospitalini na mahali pa kufanyia mazoezi. Kuna kuingiliana kwa matini kama vile za kidini, kiteknolojia, usafiri na kadhalika. Aidha, wimbo huu unaingiliana kimatini na wimbo ***Vunja Mifupa KamaMeno Bado Ipo***, ulioimbwa na Samba Omar Mapangala na hivyo kuwa mwigo wake.

Ujumbe unaowasilishwa kupitia kwa wimbo huu ni kwamba, Virusi Vya UKIMWI vinaweza kumpata mtu yeyote. Si wanafunzi wa shule za msingi, si wanafunzi wa shule za upili, si wale wa vyuo vikuu au walio kwenye ndoa, wote wanaweza kuambukizwa. Hii ni simulizi ndogo inayochukua nafasi ya simulizi kuu inayodai kwamba, wanaoambukizwa tu ni wale wanaoshiriki biashara ya ngono, wanaotumia mihadarati na walio nje ya ndoa. Taasisi za elimu pia zinafaa kushughulikiwa katika vita dhidi ya UKIMWI kwani umdhaniaye siye kumbe ndiye.

Msanii wa wimbo *Nimeupata Vipi?* ni Faddy Daddy. Anatanguliza wimbo wake kwa kuangua kilio huku akitangaza kuwa yualia. Kilio chake kinasababishwa na hali yake iliyodhoofika. Anasimulia kuwa, kila anapokaa anawaza, kisha anawaambia wasikilizaji wake wamtazame namna alivyokonda. Majibu aliyopewa kuhusu hali yake ni ya kumtisha na kumchosha. Ingawa msanii hajataja VVU/UKIMWI katika utangulizi wa wimbo wake, maoni yangu ni kuwa, kilio, kukonda, kuwa na mawazo mazito na kutishika kwake ni mambo yanayohusishwa aghalabu na VVU/UKIMWI.

Katika ubeti wa pili, msanii anasimulia kuwa, yeye amepimwa na kuambiwa kuwa ameathirika licha ya kuwa hajashiriki ngono. Katika simulizi hii pia, msanii hajabainisha mwathiriwa ameathiriwa na nini na vipi. Ingawa hivyo, simulizi zinazohusishwa na VVU/UKIMWI ni kama vile ***nimepimwa, nimeathirika na sijafanya ngono***. Msanii katika ubeti wa tatu anaendelea kutusawiria kimasimulizi hali ya mtu aliyeambukizwa. Mtu kama huyo anahisi maumivu, anawaza na kufikiria. Fikra kama hizi zinatokana na namna wanajamii wanavyomchukulia mtu aliyeambukizwa VVU. Mathalani, ndoto za aliyeambukizwa kama vile masomo hazionekani kutimia tena. Aidha mtu kama huyo hutengwa na wanajamii kwa kuhusishwa na uasherati licha ya yeye kuambukizwa kupitia njia nyingine.

**Mf 24**

*Kila siku Faddy mi fikiria*
*Wazazi wangu mi ntawaeleza nini*
*Wakati wanajua mi niko nasoma*
*Kwa kile walichonituma*
*Kila wakati nakaa, nawaza,najiuliza Faddy*
*Mimi nitasema kwamba nimepimwa*
*Nimeambiwa kuwa virusi ninavyo*

*Moyoni naumia, nachanganyikiwa*
*Ni vipi UKIMWI umenipata*
*Wakati zinaa sijawahi fanya*
*Maswali mengi najiulizaa*
*Mi naomba msijenitenga*
*Kwa sababu nimeathirika*
*Skupata ngoma sababu ya zinaa.*

(Kutoka: *Nimeupata Vipi?*. Msanii: Faddy Daddy)

Katika ubeti wa nne, msanii anabainisha simulizi zinazohusu VVU/UKIMWI kwa kujiuliza maswali ambayo mtu aliyejipima na kugundua kuwa ana Virusi Vya UKIMWI hujiuliza hasa anapojua fika kwamba hajashiriki ngono. Mathalani, katika mstari wa kwanza, anajiuliza ni wapi UKIMWI nimeupata? Kwa kuwa hajashiriki ngono, anaanza kushuku usalama wa damu aliyoongezewa na usalama wa saloni anakoenda kunyolewa. Simulizi hizi zinapatikana katika mstari wa pili na wa tatu mtawalia. Msanii anaubwaga ubeti huu kwa kauli kuwa bado jibu hajalipata. Ni katika ubeti huu ambapo neno UKIMWI linatajwa kwa mara ya kwanza. Mbali na hayo, mtu aliyeambukizwa hukabiliwa na maswali chungu nzima kutoka wanajamii wengine kuhusu hali yake mbaya ya afya. Aidha, wanajamii husika badala ya kumshugulikia mgonjwa kwa kumpeleka hospitali, wanaanza kumtenga kwa kumpeleka kijijini kama inavyodhihirika katika ubeti ufuatao.

**Mf 25**

*Wadogo ndugu zangu wananiuliza*
*Mbona Faddy Daddy unazidi konda?*
*Mwili mzima upele umejaa*
*Kila wakati unashika tama*
*Kama hivyo twende zetu Tanga*

(Kutoka: *Nimeupata Vipi?.* Msanii: Faddy Daddy)

Kwenye ubeti wa tano, msanii anaeleza kuwa, kila mara yuafikiria atawaambia nini wazazi kuhusu hali yake ilhali walikuwa wamemtuma kwenda kusoma. Anaogopa kuwaelezea kuwa, amepimwa na kuambiwa kuwa ana Virusi Vya UKIMWWI. Uoga alionao mtu aliyeambukizwa si wa kuhusu hali yake bali unahusu watu wengine wa karibu naye ambao huenda wasielewe namna alivyoambukizwa. Mifano ya watu hao ni ndugu na wazazi kama ubeti nambari 26 hapa chini inavyoonyesha. Huu ni uoga alionao kila mwathiriwa wa VVU/UKIMWI kwani wanajamii watamhukumu kuwa yeye ni asherati na hivyo kumtenga na pia kumnyanyapaa.

**Mf 26**

*Nikifikiria mama, nalia*
*Nikifikiria baba, nalia*
*Nikifikiria ndugu zangu nawapenda sana.*

*Baba na mama wamenisomesha kwa shida*
*Kutoka msingi hadi chuo naingia*

(Kutoka: *Nimeupata Vipi?*. Msanii: Faddy Daddy)

Msanii katika ubeti wa sita anaeleza anayoyapitia kutokana na hali yake. Anaeleza kuwa, ana maumivu moyoni na amechanganyikiwa kwani ana Virusi Vya UKIMWI na hajui alivipata vipi. Yaelekea kuwa, kwa wanajamii njia ya pekee ya kupata maambukizi ni ya ngono; kitendo ambachohajajihusisha nacho. Hii ndiyo simulizi kuu miongoni mwa wanajamii. Pamoja na hayo anawaomba wanajamii wasimtenge kwa misingi ya kuwa na Virusi Vya UKIMWI. Anateta kwamba hakupata ngoma kwa sababu ya zinaa**.**Utetezi wake unakuwa simulizi ndogo inayopinga simulizi kuu kwamba njia ya pekee ya kuambukizwa VVU ni ya ngono. Vipande vinavyohusu VVU/UKIMWI katika ubeti huu ni pamoja na maumivu ya moyoni na kuchanganyikiwa. Maoni yangu ni kwamba, msanii ametumia sitiara ya ***ngoma*** kumaanisha VVU/UKIMWI na ***zinaa*** kumaanisha ngono bila kinga au za kiholela.

**Mf 27**

*Mimi ndio mtoto wanaotegemea*
*Lakini ndoto zangu nimezizuia*
*Najiuliza UKIMWI nimeupata vipi?*
*Wakati Faddy sikushiriki kwa uasherati*

(Kutoka: *Nimeupta Vipi?*. Msanii: Faddy Daddy)

Simulizi kuu za VVU/UKIMWI katika ubeti wa saba ni pamoja na kuzidi kukonda, mwili mzima kujaa upele, kushika tama kila wakati, kujitenga na kulia. Kushika tama kila wakati, kujitenga na kulia ni ishara za mtu aliyejinyanyapaa mwenyewe. Ndugu zake msanii wanashangaa, mbona Faddy Daddy ***anazidi kukonda, mwili mzima upele umejaa*** na ***kila wakati anashika tama***. Wanapendekeza kuwa, ikiwa hali itakuwa hivi

basi wampeleke kwao Tanga; ***kama hivyo twendezetu Tanga***. Huu ndio mwanzo wa kutengwa na kunyanyapaaiwa na wanajamii wengine.  Msanii anatamatisha kwa kueleza kuwa, analia anapofikiria juu ya wazazi na ndugu zake anaowapenda. Haya masimulizi yanayoonyesha hali ya kutamauka, hali inayosababishwa na mtu kujinyanyapaa binafsi au kunyanyapaaiwa na wanajamii wengine.

**Mf 28**

*Ndoto zangu zishapotea*
*Kusoma sitasoma tena*
*Dunia imenitenga mimi.*
*Moyoni naumia nachanganyikiwa*
*Ni vipi UKIMWI nimeupata?*
*Wakati zinaa sijawahi fanya*
*Maswali mengi najiuliza*
*Mi naomba msijenitenga*
*Kwa sababu nimeathirika*
*Sikupata ngoma sababu ya zinaa.*

(Kutoka: *Nimeupata Vipi?*. Msanii: Faddy Daddy)

Katika ubeti wa nane, msanii anawakumbuka wazazi wake waliomsomesha kutoka shule yamsingi hadi sasa anapokuwa chuo kikuu. Anasimulia kuwa, yeye ndiye mtoto wanaomtegemea. Simulizi zinazohusu VVU/UKIMWI katika ubeti huu ni pamoja na ***mtoto wanaomtegemea***, ***ndoto zangu nimeziua***, ***UKIMWI nimeupata vipi?, sikushiriki uasherti*** na ***nilijilinda sana***. Simulizi hizi zimeendelezwa katika stanza ya tisa ambapo msanii anasema kuwa, ***ndoto zanguzishapotea, kusoma sitasoma tena*** na ***dunia imenitenga mimi***. Hizi ni simulizi kuu za wanajamii kuhusu mtu aliyeambukizwa VVU. Imani ni kwamba, mtu aliyeambukizwa hupoteza matumaini ya kuishi na hata kuendelea na shughuli zake za kila siku. Aidha, ndoto walizonazo hupotea.

Ubeti ya kumi ni marudio ya ubeti wa sita ambapo msanii anarudia maelezo ya hisia zake za maumivu ya moyoni na kuchanganyikiwa, ni vipi aliupata UKIMWI bila kushiriki ngono na ombi lake kuwa asitengwe kwa sababu ameathirika kwani

UKIMWI hakuupata kupitia kwa ngono. Kwa ujumla, simulizi ndogo zinazobainika katika wimbo huu ni pamoja na : ***zinaa sijawahi fanya, mi naomba msijenitenga kwa sababu nimeathirika, sikupata ngoma sababu ya zinaa, wakati Faddy sikushiriki uasherati na nilijilinda sana.*** Simulizi hizi zinaafikiana na maoni ya wanabaadausasa kwani wanapinga kutengwa kwa baadhi ya wanajamii kwa misingi yoyote ikiwemo ya kiafya.

Ujumbe unaowasilishwa kupitia simulizi tulizozidokeza ni kwamba, ngono siyo njia ya pekee ambayo kwayo mtu anaweza kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Mtu anaweza kuambukizwa kupitia njia nyingine kama vile kuongezewa damu isiyo salama, ala zenye makali kama zile zitumiwazo katika saloni na vinyozi na kadhalika. Aidha, msanii anapinga unyanyapaa kwa kutumia simulizi kama vile ***Mi naomba msijenitenga kwa sababu nimeathirika***. Msanii pia amedhihirisha kuwa, mtu anaweza kutegemewa licha ya kuwa na Virusi Vya UKIMWI. Hii ni kwa sababu katika ubeti wa nane mshororo wa tatu, msanii anasimulia: ***Mimi ndio mtoto wanaomtegemea.*** Miktadha ya kijamii inayobainika katika wimbo huu ni pamoja na matangani alipoongezewa damu, saloni kwenye kunyoa, nyumbani kwa mwathiriwa, shule ya msingi na chuo kikuu.

Katika ubeti wa kwanza wa wimbo *Si Lazima*, msanii Nonini anawatambulisha wasanii alioshirikiana nao katika kusanifu wimbo husika. Wasanii hao ni Gabu, Frasha na Bonnie. Aidha, anwani ya wimbo inatajwa kuwa Si Lazima. Wimbo huu unawahusu vijana wawili mmoja wa kike na mwingine wa kiume. Wimbo wenyewe una simulizi ndogo ndogo kuhusu suala la ngono ambalo nalo linahusishwa na VVU/UKIMWI. Ingawa VVU/UKIMWI haujatajwa popote katika wimbo huu, kuna maneno yaliyotumiwa ambayo yanahusishwa na vita dhidi ya VVU/UKIMWI.

Katika ubeti wa pili, kuna simulizi kuhusu suala la kushiriki ngono ambapo mmoja wa wahusika anaeleza kuwa wanaweza kwenda nyumbani na si lazima wafanye mapenzi. Ili kuwasilisha ujumbe huu, wasanii wametumia maneno kama vile:

**Mf 29**

> *Si lazima tu do, tunaeza endahome na tuchill tu do* na *tunaeza enda home na tuchill tu aah*.
>
> (Kuoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Simulizi hizi zaendelezwa katika ubeti wa tatu ambapo mhusika mmoja ambaye kwa maoni yangu ni wa kiume anasimulia kuwa, wanaweza kwenda nyumbani kwanza kisha waende sokoni kununua mboga kwani nyumbani mwake hamkuwa na cha kupika siku hiyo. Kitendo cha watu wa jinsia tofauti, hasa vijana kuwa pamoja kila wakati aghalabu huibua fikra, hisia na mitazamo tofauti tofauti miongoni mwa wanajamii. Mara nyingi, wengi hufikiria kwamba, kila wanapokuwa pamoja, wahusika hushiriki ngono tu. Mara nyingi, wahusika huhukumiwa visivyo na wanajamii na ndiyo maana wahusika kupitia kwa wimbo huu kwamba si kila wakati ni ngono tu. Kwa mfano, mmoja wa wahusika katika wimbo huu anatamatisha kuwa, si kwamba kila wakati ni kumvua mwenzake nguo. Ujumbe wa kutoshiriki ngono unawasilishwa kupitia matumizi ya maneno kama vile:

**Mf 30**

> *kuenda kwanza kejani, tuende baby tupate majani leohakuna cha kukaanga ndani, si eti kila saa ni kukuundress* na *kukucarress*.
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Katika ubeti wa nne, msimulizi bado anashikilia kuwa kitendo cha kujamiiana si cha lazima. Aidha anamwambia mwenzake kuwa yuajua kwamba yeye anataka na yeye msimulizi anasema kuwa, hata yeye huwa kuna wakati anataka lakini leo hatamani

kwa sababu ana maumivu ya kichwa na tumbo. Hata hivyo, anahitimisha simulizi hii kwa kauli inayodhihirisha kumtamani mwenzie. Simulizi hizi ndogo ndogo zinazopatikana katika wimbo huu zinasawiri ukweli wa mambo yanayotokea wakati watu, hasa vijana wa jinsia moja wanapokuwa pekee yao. Ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe huu, wasanii wametumia kauli zifuatazo:

**Mf 31**

> *Si eti kila saa ni mambo ya sex, najua baby unataka, pia ni matime huaga nataka, leo manze sijisikii, kichwa kinaniuma, tumbo inakokotanaskia kukuokotaa*.
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii:P - Unit)

Mstari wa kwanza na wa pili katika ubeti unaofuata inaonyesha kuwa msimulizi anaelekea kusalimu amri licha ya kusisitiza kuwa si lazima *tu do* asemavyo katika mstari wa tatu na wa nne. Katika mstari wa pili anajivua nguo tayari kwa kitendo anachodai kuwa si lazima, kisha katika mstari wa mwisho wa ubeti huu, anakiri kuwa huku kulikuwa ni kujifanya kwake tu. Maneno yaliyotumiwa katika ubeti huu ni kama vile:

**Mf 32**

> *Naskia kukuokota, ngoja kwanza nivue hii mbuta, tukachill tuhuku najidoo kwa kona*.
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Msimulizi katika ubeti wa mwisho anamweleza mwenzie kuwa, hata akimtekenya tu na hayuko radhi kufanya mapenzi, wanaweza kuongea tu. Lakini anadai pia kuwa vazi alilovaa mwenzie ambalo ni suruali ndefu linamfanya amtamani. Kumtamani huku kumemfanya atokwe na shahawa licha ya kutaka kushiriki kitendo cha ngono. Anadai kutaka kulala lakini mwenzie ambaye kwa maoni yetu ni wa kike tayari ashamvua shati. Katika mstari wa mwisho, msimulizi anakiri kuwa hilo lilikuwa

jaribio kubwa na kwamba hakuwa na bahati. Maoni yangu ni kwamba, huenda kile kitendo ambacho hakikuwa cha lazima hatimaye kilifanyika. Maneno yaliyotumiwa kuwasilisha ujumbe husika ni kama vile:

**Mf 33**

> *Nikikudhiki tu, ka sijisikii jo tunaeza bonga, nikiangalia trao tu hivinimetokwa wet, ushavua*
> *ngotha,.....umevaa inanimaliza, nataka kulala jo ushanivua shati* na *temptation kibao jo sina bahati*.
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Wimbo huu unamnyanyapaaisha mwanamke kwa kumsawiri na kumshutumu kama kiumbe anayemletea mwanaume majaribu. Mazungumzo yaliyomo katika wimbo huu, hasa yanayoonyesha uzabzabina wa wahusika ni simulizi zisizokuwa na uaushi zinazotumiwa na vijana kila siku kujadili maswala ya VVU/UKIMWI.

Miktadha ya kijamii inayobainika katika wimbo *Si Lazima* ni pamoja na nyumbani kwa msimulizi ambapo msimulizi na mwenzake wanaongea huku wakitazama filamu. Haya yanabainika kupitia matumizi ya maneno kama vile: ***Tunaeza enda home, tunaweza kuenda kwanza kejani, najidoo kwa kona na hii movie tunacheki jo manze*** ikiisha. Muktadha wa sokoni pia unadhihirika kupitia kauli kama vile: ***Tuende baby tupate majani.***

Hadhira inayolengwa ni ya vijana. Hii ni kutokana na matumizi ya lugha ya kuchanganya ndimi, lugha ya mtaani, utohozi na Sheng. Kuhusu kuchanganya ndimi, kuna matumizi ya maneno ya Kiingereza kama vile:

**Mf 34**

> *Introducing, home, sex, mind, movie, wet, baby, story* na *temptation*.
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Aidha kuna maneno kutoka lugha nyingine kama ***Mbuta*** kutoka Kijaluo na ***Afrodisiae*** kutoka Kiingereza. Afrodisiac lina maana ya mtu hasa mwafrika mwenye nguvu za kutekeleza kitendo cha ngono. Miongoni mwa Wajaluo, mbuta ni aina ya samaki ambaye baada ya kukaushwa huwa na umbo la koti. Katika muktadha wa wimbo huu basi, msimulizi anavua koti tayari kufanya mapenzi. Hapa panadhihirika mwingiliano matini kati ya lugha ya Kiswahili, Dholuo na kadhalika.

Lugha ya mtaani hukaribiana sana na 'Sheng'. Neno linaweza kuwa la mtaani na wakati huo huo likawa linatumiwa na wasemaji wa 'Sheng'. Hata hivyo katika kuchanganua wimbo huu niliyaainisha maneno yafuatayo kuwa ya mtaani:

**Mf 35**

> *Kejani, majani, huaga, kukuokota, sijisikii, bonga, wanasmanga* na *kibao.*
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Maneno haya yanamaanisha nyumbani, mboga, huwa, kukukumbatia, sina hamu, kuzungumza, husema na kubwa mtawalia. Aidha, kuna neno *ngotha* ambalo ni vazi la ndani la kike yaani chubi. Maneno yaliyotoholewa ni *kona* na *shati* katika mstari wa tano ubeti wa tano na mstari wa kumi ubeti wa mwisho mtawalia. Isitoshe, kuna kitenzi kilichotoholewa;*tunacheki* kinachomaanisha tunaona kwa wasemaji wa Sheng.

Kuna maneno ya Sheng yaliyotumiwa katika wimbo huu. Baadhi ya maneno hayo ni:

**Mf 36**

> *tudo*, *kukuundress*, *kukucaress*, *najido* na *matime*.
>
> (Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P - Unit)

Kulingana na wasemaji wa Sheng waliokuwa katika makundi teule,maneno haya yanamaanisha tufanye, kukuvua, kukupapasa (kwa mahaba), ninajifanya na nyakati zingine mtawalia. Maneno mengine yaliyotumiwa na ambayo yanahusishwa na Sheng

ni kamavile:***Manze, jo*** na ***trao***. Manze na jo ni maneno wanayotumia wasemaji wa Sheng kuitana hasa wanapozungumza. *Trao* ni neno linalotokana na neno la Kiingereza trouser lenye maana ya suruali ndefu. Katika muktadha wa wimbo huu, vazi linalorejelewa ni lile lililovaliwa na mwanaume ingawa linavaliwa na wanawake siku hizi pia.

Simulizi ndogo inayobainika katika wimbo huu ni ile inayopinga simulizi kuu miongonimwa wanajamii kuwa, kila mara watu wa jinsia tofauti wanapoonekana pamoja ni lazima washiriki ngono. Simulizi ndogo inapinga hili kwa kusisitiza kuwa *Si Lazima* na wanaweza kukaa pamoja bila kufanya mapenzi. Neno *tuchill* hutumiwa hasa na vijana katika vita dhidi ya UKIMWI. Maana yake ni kuwa marafiki wanaojizuia kushiriki ngono au wanaoaminiana. Hata hivyo, mwishoni mwa wimbo, msimulizi anaelekea kushindwa kujizuia na hivyo kuafikiana na simulizi kuu inayohusisha ngono na kitendo cha mwanaume na mwanamke kuwa pamoja. Hizi basi zinakuwa simulizi zisizokuwa na uaushi.

Ujumbe unaowasilishwa kwa wasikilizaji kupitia kwa wimbo huu ni kwamba, wasiwashuku watu wa jinsia tofauti kuwa wanashiriki ngono kila wakati wanapokuwa pamoja. Hii ni kwa sababu, kwa kufanya hivyo wanawatenga na kuwahukumu bila ithibati.  Wasanii wanasema kuwa, ***Si Lazima tudo, si eti kila saa ni kukuundress, si eti kila saa nikukucaress, si eti kila saa ni mambo ya sex, tunaweza kuchill tu*** na kadhalika. Mbali na ujumbe huu, kuna ujumbe wa tahadhari unaowasilishwa pia. Ujumbe huu unawatahadharisha wanajamii hasa vijana dhidi ya kujidai kuwa wana uwezo wa kujizuia. Tahadhari ni kwamba, wawe waangalifu sana kwani majaribu wakati mwingine huwa mazito na mtu anaweza kusalimu amri. Hili ndilo lililomfikia msimulizi kwani mwishoni mwa wimbo anatoa kauli zinazoonyesha kushindwa kwake kujizuia. Kauli hizo ni pamoja na ***Temptationkibao jo*** na ***Sina bahati.***

Katika wimbo Vuta Pumzi, ulioimbwa na Longombas kuna simulizi zinazokuza unyanyapaa pamoja na zile zinazoupinga. Mathalan, katika ubeti wa kwanza, wanaume kwa wanawake walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI wamesawiriwa kama watu wenye afya nzuri. Wanawake wamesifiwa kuwa warembo, wenye marasa, wenye mapaja na weupe. Wanaume nao wamechorwa kama wenye vifua, warefu na wenye nguvu. Kijuujuu, wote wanaonekana wazuri; yaani ***ni wazuri kinyama***. Kukuzwa kwa unyanyapaa kunaanza pale ambapo watu wanaoonekana kuwa na siha nzuri wanaanza kushukiwa kuwa na Virusi Vya UKIMWI. Vipande vya simulizi vinavyokuza unyanyapaa katika ubeti huu ni kama vile:

**Mf 37**

> *Lakini tujichunge,*
> *pengine wanao mdudu,*
> *wanatuacha na wana-go.*
>
> (Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Katika simulizi hii, walio na virusi vya UKIMWI wanasemekana kuwa na mdudu. Katika miktadha mingi ya kijamii, mdudu hutumiwa kiistiara kumaanisha VVU. Matumizi ya sitiara ya mdudu ni mwigo wa sitiara katika tafiti zaMutembei (2009),Kobia (2012) na Lang'at (2013). Aidha, katika muktadha wa wimbo huu,kitendo cha mtu kuwaacha wengine kinarejelea kifo kisababishwacho na UKIMWI. Kwa kawaida mtu anapofariki, wanajamii hutumia usemi ***ametuacha*** kumaanisha amekufa. ***Wana-go*** ni neno la 'Sheng' lenye maana ya wanaenda. Katika muktadha wa wimbo huu, kitendo cha kwenda kinamaanisha kufa kunakohusishwa na UKIMWI.

Isitoshe, kwenye sehemu ya mwisho ya ubeti huu, kuna simulizi zinazokuza na kuendeleza unyanyapaa. Mathalani, watu wanaoshukiwa kuwa na VVU wamesawiriwa kama waliojaza nyuma, waliorembeka na wenye pesa. Mbali na watu

hawa kuwa na sifa zinazothaminiwa kama hizi, wasanii wanawanyanyapaa kwa kusema:

**Mf 38**

*Usimwone amejaza nyuma,*
*ukadhani ako poa,*
*usimwone amerembeka*
*ukadhani umefika,*
*usimwone ana pesa,*
*ukadhani umefika,*
*pengine anatuacha, kesho anachora.*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Mijadala yetu katika kundi teule ilibainisha kuwa ***poa*** ni neno la msimu lenye maana; **-zuri**, **umefika** ni kitenzi kinachomaanisha kutokuwa na haja na kingine baada ya mtu kupataalichokuwaanatafuta huku kitenzi **anachora** kikimaanisha anaandika.

Katika muktadha wa ubeti huu basi, wale waliojaza nyuma, warembo na wenye pesa wanashukiwa kuwa na VVU na ndiyo maana wasanii wametumia maneno kama vile: pengine anatuacha, usidhani ni poa na anachora. Kulingana na mijadala katika kundi moja teule, kitendo cha kuchora ni kuandika wosia. Kwa hivyo, ina maana kuwa, mtu aliyeambukizwa VVU anatayarisha wosia kwa kuwa anatarajia mauti. Simulizi kama hizi zinakuza na kuendeleza unyanyapaa unaoendelezwa dhidi ya walioambukizwa VVU, jambo linalopingwa na Wanabaadausasa.

Katika ubeti wa pili, wasanii wanawasilisha simulizi ndogo ndogo zinazowapa matumaini walioambukizwa VVU na hivyo kupinga simulizi kuu kuhusu unyanyapaa. Simulizi hizi ni kama vile:

**Mf 39**

*Na kama unayo,*
*si mwisho wa maisha,*
*ni ugonjwa tu kama malaria,*
*meza dawa,*
*piga tizi,*
*kula vizuri,*
*utaishi fiti,*
*maisha utayasukuma.*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Simulizi kama hizi hutolewa na wataalamu wa afya kwa walioambukizwa VVU kama ushauri nasaha ili waweze kuishi maisha marefu na ya maana. Kwa hivyo, kutolewa kwa ushauri huu na wasanii kunashadidia ukweli kuwa, nyimbo zinaweza kutumiwa kuwasilisha habari zozote kwa hadhira tena kwa urahisi. Isitoshe, simulizi hizi zinaafiki misimamo ya wanabaadausasa kwamba, hakuna mtu au kikundi cha watu kinachoweza kudai umiliki wa maarifa yote na kwamba wanasayansi wanapaswa kuacha kujifungia maabarani, watoke nje na washirikiane na wanajamii wengine katika kutafuta suluhisho kwa tatizo la UKIMWI.

Hadhira inayolengwa na wasanii ni ile ya vijana, hasa wa mijini na walioambukizwa VVU. Hii ni kwa sababu ya uteuzi na matumizi ya maneno ya Sheng kama vile: ***piga tizi*** kumaanisha fanya mazoezi na ***utaishi fiti*** kumaanisha utaishi vizuri. Aidha kuna kutajwa kwa Langata, eneo lililoko jijini Nairobi ambapo kuna makaburi ya umma.

Wimbo *Starehe* ulioimbwa na Profesa Jay akishirikiana na Ferooz unaweza kugawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inajumuisha betimbili za kwanza pamoja na ubeti wa nne na wa tano zinazoimbwa na Ferooz ambaye anaigiza sehemu ya kijana aliyeambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Sehemu ya pili nayo inajumuisha beti za tatu na sita zinazoimbwa  na Profesa Jay akimwigza dakitari.

Wimbo huu unadhihirisha unyanyapaa wa kibinafsi ambao unaendelezwa na mtu dhidi ya nafsi yake anapogundua kuwa ana Virusi Vya UKIMWI. Katika hali hii, mtu hujilaumu, hujuta na hutamauka. Katika ubeti wa kwanza na wa pili, kuna simulizi zinazoonyesha kujifedhehesha kwa mtu aliyeambukizwa Virusi Vya UKIMWI. Baadhi ya simulizi hizi ni pamoja na:

**Mf 40**

*mimi nipokitandani*
*starehe zimeniwekamashakani,*
*kupona tena mimi haiwezekani,*
*kumbe nilikuwa naukimbilia moto*.

(Kutoka: *Starehe*. Wasanii: Ferooz & Profesa Jay)

Aidha, kauli ya kuwaaga wanajamii wengine inadhihirisha kujitenga nao na hivyo kutamauka. Isitoshe, katika ubeti wa nne, Ferooz anamsimulia dakitari kuwa ameenda kwake kujipima ili kupata uhakika kuhusu hali yake kabla hajafariki kwani dalili zilionyesha kuwa alikuwa ameambukizwa VVU. Hana matumaini ya kuishi tena kwani anasema kuwa hiyo ndiyo ilikuwa mara yake ya mwisho. Katika ubeti wa tano, anamweleza dakitari aone namna alivyokonda, mwili wake ulivyojaa vidonda, kutapika mara sitini na mbili kwa wiki na jinsi nywele zake zilivyonyonyoka, hizi zote zikiwa simulizi za mtu kujidharau baada ya kujishuku kuwa na VVU. Anahitimisha simulizi yake kwa kusema hizo zote zilikuwa dalili za ***umeme.***

Dalili zilizotajwa na mwimbaji katika simulizi yake bado zinahusishwa na VVU/UKIMWI miongoni mwa baadhi ya wanajamii. Mtu aliyeonyesha dalili moja au dalili hizi zote alihesabiwa kuwa alikuwa na UKIMWI. Hii ni simulizi kuu miongoni mwa wanajamii wengi. Kwa kuwa VVU/UKIMWI hauna tiba, mtu aliyeonyesha dalili hizi angejihukumia kifo. Katika hali kama hii, mtu hujitenga na wanajamii wengine kwa kuhofia unyanyapaa kutoka kwa hao wanajamii wengine bila kujua

kwamba, kwa kufanya hivyo anakuza na kujiendelezea aina unyanyapaa ambao ni wa kibinafsi. Mintaarafu ya majadiliano katika kikundi teule cha madakitari, aina hii ya unyanyapaa ndio hatari zaidi na ndio unaohusishwa na vifo vingi vya waathiriwa wa VVU/UKIMWI.

Simulizi ndogo inayopinga unyanyapaa wa kibinafsi imo katika ubeti wa mwisho na ni simulizi inayotolewa na professor Jay akimwigiza dakitari. Hii ni simulizi ndogo inayopinga simulizi kuu katika jamii; simulizi ambayo huchukulia kwamba yeyote anayeonyesha dalili za kukonda, ukurutu wa ngozi, vidonda mwilini na kadhalika ana VVU/UKIMWI. Wasanii wa wimbo huu wanakariri ushauri nasaha unaotolewa na wataalamu wa matibabu kwa wanajamii kwamba, mtu kukonda si kipimo cha kuonyesha kuwa mhusika ana UKIMWI. Hii ni kwa sababu mtu anaweza kukonda kutokana na magonjwa mengine kama vile Homa ya Matumbo na Kifua Kikuu. Simulizi hii inawapa matumaini walioambukizwa kuwa, bado wana nafasi ya kuishi kwani kuambukizwa si hukumu ya kifo. Lakini kuendelea kuishi huku kutategemea namna mgonjwa atakavyojitunza kwa kuzingatia kula vizuri, kufanya mazoezi na kupumzisha mwili. Huu ni ushauri nasaha unaotolewa katika vikao vya ushauri kwa wanaougua UKIMWI na unapitishwa kwa wanajamii wote kupitia wimbo huu. Hata hivyo, katika ubeti huu wa mwisho, kuna kipande cha simulizi kinachoelekea kukuza unyanyapaa kwa kuchukulia kuwa wale wanaoambukizwa ni wapenda starehe na umalaya. Hii ni simulizi kuu ya jamii. Hata hivyo ukweli ni kuwa, yeyote anaweza kuambukizwa kupitia njia nyingine zilizobainishwa katika sura ya pili ya tasnifu hii.

**Mf 41**

*Kwaherini, kwaherini, kwaherini*
*Masela wangu ndugu zangu wote wa gheto buriani*
*Kwaherini kwaherini kwaheini Nagongo na Jitauni kwaherini*
*Watanzania kwaherini,sasa naaga*

(Kutoka: *Starehe.* Wasanii: Ferooz & Profesa Jay)

Hadhira inayolengwa na wimbo huu hasa ni vijana na yeyote aliye na Virusi Vya UKIMWI. Hii ni kwa sababu lugha iliyotumiwa ni rahisi kueleweka na ni maneno machache tu ya Sheng yaliyotumiwa.

Katika wimbo *Wee Kamu*, wasanii Nonini na Jua Cali wanabadilishana zamu za kuimba huku wakijibizana. Nonini ndiye anayetanguliza wimbo kwa kutaja Calif ambapo ni studio ya kurekodi nyimbo zao. Aidha anataja mtindo wao wa muziki Genge Remix na kusema kuwa, watu wa Kenya wana tabia mbaya akiwemo yeye na msanii mwenzake. Tabia mbaya inayozungumziwa na msimulizi ni ile ya kushiriki ngono. Hii ni kwa sababu maneno haya hutumiwa na wanajamii kurejelea masuala yanayohusiana na kitendo cha kufanya mapenzi. Simulizi zinazohusiana na VVU/UKIMWI zinazobainika katika ubeti wa kwanza ni kama vile:

**Mf 42**

> *vile iko poa jako yako*
> *na trao kila kitu toa,*
> *kuna style mpya,*
> *hebu kwanza inua mguu juu,*
> *ntainua polepole jo sababu minashuku,*
> *naeza tembea kwa chupa zimevunjika mguu tupu*
> *nijifanye sugu sababu yako tu*.
>
> (Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Katika kiitikio, simulizi kuhusu VVU/UKIMWI ni ***kwa hivyoukitaka we we we kamu***. Simulizi hizi zote zinahusu kitendo cha kufanya mapenzi ambacho nacho huhusishwa na kuenea kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI. Mathalani, msimulizi anamwambia mwenzie avue kila kitu ili wafanye mapenzi kwa kutumia mtindo mpya. Aidha anamshuku mwenzake kuwa na VVU/UKIMWI kwa sababu shingo lake ni nyembamba kama la kuku. Wanajamii huhusisha kukonda na kuwa na UKIMWI. Simulizi ndogo inayobainika ni kuwa, msimulizi anaridhia kufanya mapenzi na aliyeathirika lakini kwa kutumia kinga. Hii ni kwa sababu amesema hawezi kutembea

miguu mitupu kwenye chupa zilizovunjika. Maana yake ni kuwa hawezi kujifanya bingwa kwa kushiriki ngono bila kuwa na kinga.

Ubeti wa pili inawasilishwa na msanii Jua Cali baada ya mwenzake kumpisha kwa maneno: ***Jua Cali Ushaichota mtoto kwa haga.*** Katika ubeti huu simulizi zinazobainika zinazungumzia suala la ngono kwa uwazi. Msanii ametumia maneno mengi ya Sheng ambayo yanamwezesha kuzungumzia suala hili bila ya aibu na bila kuwaachia wasikilizaji nafasi kutafakari na kujaribu kujifumbulia wenyewe. Isitoshe, simulizi hizi zinahimiza matumizi ya kondomu na matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume. Hata hivyo kuna simulizi zinazohimiza ngono bila kinga. Kwa kufanya hivi, msanii anashabikia kitendo cha ngono na wakati huo huo kukuza uwezekano wa kuenea kwa VVU/UKIMWI miongoni mwa vijana. Hii ni kwa sababu vijana wanaosikiliza wimbo huu, wanaweza kushawishika kuweka wanayoyasikia kwenye majaribio. Simulizi inayohimiza matumizi ya kinga na hivyo kuwasawiri vijana kama watu walio katika mstari wa mbele katika vita dhidi ya VVU/ UKIMWI ni kama vile ***Nimbariki na juala stakimtaani kuwe na mazishi***. Hata hivyo, kuna simulizi nyingi zinazoshabikia ngono na hivyo kendeleza uwezekano wa kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI. Simulizi hizo ni pamoja na:

**Mf 43**

*.....ni make sure bado inaeza steady,*
*inaeza ingiza ata ka ameketi,*
*tembe zangu za viagra vipi?,*
*boraleo uniachie nizame vimbichi*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Maelezo haya yanahusu dhakari na kitendo cha ngono. Aidha kuna simulizi kuhusu matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume na kitendo cha kushiriki ngono bila kinga yaani ***kuzama vimbichi***.

Katika ubeti wa tatu simulizi inayowasilishwa na Nonini ni ile ile ya kushabikia ngono. Matumizi ya maneno kama vile:

**Mf 44**

*usivae jeans imekushika,*
*usikuje peke yako*
*kuja na beshte zako,*
*leo nataka combi*
*sikutaki we peke yako,*
*nikifunga mlango tu hivi nipate ushatoa,*
*tulianikafungue mlango*
*kuna mzungu ana ngoja,*
*ana moto jo anataka ku to to to ka*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Simulizi hii inatufafanulia jinsi vijana wanavyochukulia mapenzi na ngono. Inadhihirika kuwa, huenda vijana wanashiriki ngono za shirika kwani msanii anamwambia mpenzi wake asiende peke yake bali aandamane na wasichana wengine kwani yaelekea kutakuwa na mashindano ya kufanya mapenzi. Ndiposa msanii anasema, ***usikuje peke yako kuja na beshte zako, leo nataka combi sikutaki peke yako***.

Msimamo wa utafiti huu ni kwamba, wimbo huu mzima ni simulizi ndogo. Hii ni kwa sababu, takriban maneno yake yote ni ya kutongozana na mazungumzo ya aina hii hayatolewi hadharani. Ni kwa kupitia nyimbo za aina hii ambapo vijana wanaweza kupata sauti ya kuelezea hisia zao. Vijana hufanya hivyo kwa kutumia lugha iliyosheheni matumizi mazito ya maneno ya Sheng ili kuwasilisha ujumbe bila ya aibu yoyote. Hata hivyo, katika wimbo huu, ni taklifu kuweka mpaka kati ya habari zinazopiga vita dhidi ya VVU/UKIMWI kwa dhati na zile za kimzaha. Mathalani, Jua Cali katika ubeti wa pili anahimiza matumizi ya kinga na wakati huo huo kuhimiza tabia zinazochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI anaposema: ***Najuala staki mtaani***

***kuwe na mazishi*** na ***uniachie nizame vimbichi.*** Nonini naye katika ubeti wa tatu wa wimbo huu huu anaonekana kuhimiza matumizi ya kinga kama vile kondomu anaposema: ***Juala nimenunua kibao, tape za nyundo ninazo***na kadhalika.Simulizi inayohimiza matumizi ya kinga na wakati huo huo kuhimiza matumizi ya dawa za kusisimuua misuli ni simulizi inayotumiwa na vijana kujadili swala la ngono na VVU/UKIMWI na zinaonyesha kukosekana kwa uaushi.

Hadhira inayolengwa na wimbo huu ni ya vijana. Hii ni kwa sababu wimbo mzima umesheheni matumizi ya maneno mengi ya Sheng. Isitoshe, kuna maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kiingereza kama vile kamu kutokana na *come* lenye maana ya kuja na fiti kutokana na *fit* kumaanisha sawa. Mbali na hayo, kuna matumizi ya lugha isiyozingatia kanuni za sarufi pamoja na tahajia, kuchanganya ndimi pamoja na misimu. Kwa muhtasari, baadhi ya misamiati inayohusika ni:

**Mf 45**

*kunicheki, bonga, beshte, budako, masako, manzi* na *noma.*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Maneno haya yanamaanisha kuniona, sema, rafiki, babako, mamako, msichana na shida mtawalia. Misamiati hii inabainisha lugha inayotumiwa na vijana ili kuwasilisha hisia zao wenyewe kwa wenyewe na wakati huo huo kuwafungia wengine kama wazazi wao nje ya mazungumzo yao. Maneno yaliyoendelezwa visivyo ni kama vile:

**Mf 46**

*ukaskia,wasee, inaeza, sabu, supuu, skuma, zko* na kadhalika.

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Katika mazungumzo yao kila siku, vijana hutumia lugha ya kuchangannya ndimi za Kiswahili na Kiingereza. Matumizi ya lugha ya aina hii huwatenga na wanajamii

wengine hususan wale ambao hawakupata kisomo. Katika hali kama, wale wsioielewa lugha hii hujiona kama waliotengwa au hata kujitenga wenyewe. Katika wimbo huu, kuna kuchanganya matumizi ya maneno ya Kiswahili na Kiingereza kama vile:

**Mf 47**

> *ni make sure, kwa coach, na gate, ya blue, baby boy lazima,*
> *cheza kwa speaker* na kadhalika.
>
> (Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

## 4.6 Hitimisho

Katika sura hii, nimechanganua nyimbo zinazokuza na zinazopinga unyanyapaa unaofungamanishwa na wanajamii wanaohusishwa na VVU/UKIMWI kwa njia moja au nyingine. Nyimbo husika ni zile zilizoimbwa kwa Kiswahili. Sura imeanza kwa kufafanua dhana ya unyanyapaa, aina za unyanyapaa na athari za unyanyapaa. Katika sura hii pia, imechanganua nyimbo kwa kubainisha simulizi zilizomo na ambazo zinakuza au kupinga unyanyapaa. Uchanganuzi huu unaonyesha kuwa, nyimbo za kibaadausasa zinaweza kuwa simulizi kuu na ndogo ndogo zinazopingana. Hali hii inaweza kudhihirika kupita wimbo mzima au vipande vya simulizi. Pamoja na hayo nimeonyesha jinsi wasanii wa nyimbo wanavyotumia lugha kuwasilisha jumbe ambazo hazingewasilishwa katika mazungumzo ya kawaida. Aidha, nimebainisha hadhira za kulengwa na pia miktadha ya kijamii inayohusika.

# SURA YA TANO

# UKIMWI NA SUALA LA MATABAKA

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii nimechanganua nyimbo zilizoteuliwa kwa lengo la kubainisha mchango wa matabaka katika kueneza maambukizi ya VVU. Kwa jinsi hiyo nimefafanua maana ya matabaka kasha kujadili namna yanavyojitokeza katika nyimbo zilizoteuliwa. Ilivyo ni kwamba matabaka haya yana misingi katika utajiri, umaskini na mamlaka, uwezo au nafasi aliyonayo mtu katika jamii. Hali hizi huchangia kuenea kwa VVU kwa njia tofauti. Nadharia ya Ubaadausasa inapinga kuwepo kwa mipaka kama hii katika jamii, mipaka inayodhihirisha kuwepo kwa utamaduni wa juu wa chini na inayofanya watu wengine watengwe na hata kulaumiwa mintaarafu ya VVU/UKIMWI.

## 5.2 Dhana ya Utabaka

Kwa mujibu wa Kamusi ya Oxford (2005), tabaka ni kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo wa kiuchumi ambao hugawa watu. Ninaongezea kuwa, dhana ya utabaka inahusiana kwa karibu sana na nadharia ya Umarx iliyoasisiwa na Karl Marx na Friedrich Engels.

Mwamzandi(2002),akimrejelea Lenin (1975) katika andiko lake la *TheABC of Dialectical and Historical Materialism* anafafanua kwamba makundi ya watu hutofautiana kwa sababu ya nafasi wanayoishikilia katika mfumo wa kihistoria ambao ni wa kiuzalishaji mali. Maelezo haya yalinifaa katika kubainisha makundi yanayodhihirika katika nyimbo nilizozichanganua na kuonyesha namna mahusiano kati ya walio na nafasi na wasiokuwa nayo yanavyochangia kuenea kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI nchini Kenya.

### 5.3 Matumizi ya uwezo wa Kifedha

Nyimbo nilizozichanganua zinadhihirisha kuwa kuenea kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI kunapata msukumo kutoka kwa wanajamii walio na uwezo wa kifedha. Wanajamii hawa hutumia pesa walizonazo kuwavuta wenzao wachochole na kununua mapenzi au ngono kutoka kwao.

Mathalani, katika wimbo Merimela, usimulizi kuhusu mhusika Merimela ambaye kulingana na wimbo huu alishiriki mapenzi na watu kutoka matabaka au makundi kadha wa kadha katika jamii. Msanii anasimulia kuwa Merimela alishiriki mapenzi na wadosi waliomtumia kuzima kiu ya mapenzi. M(wa)dosi ni neno linalotumiwa na wasemaji wa Kiswahili hasa mitaani nchini Kenya kumaanisha mtu au watu wenye uwezo hasa wa kifedha. Baadhi ya matajiri hutumia utajiri wao kuwapumbaza wasichana wadogo wadogo na hata wanawake maskini ili kuwakidhia haja zao za mapenzi.

Mbali na kutumia utajiri kununua mapenzi au ngono, wahusika pia hutumia fedha zao kugharamia uavyaji mimba pindi itokeapo. Msanii katika ubeti wa sita anasimulia kuwa, akiwa katika shule ya upili alishiriki mapenzi ya kiholela yaliyomfanya aziavye mimba kila mwaka. Aidha, asimulia kuwa, Merimela aliwaonja wadosi kwa mafukara na mimba ikawa jambo la kawaida kwake. Kuhusiana na matajiri kugharamia uavyaji mimba, msanii katika ubeti wa tatu mstari wa tatu anasimulia kuwa, mhusika baada ya kupata mimba alizunguka kote akitaka ushauri juu ya mimba na akadanganywa atoe kitu kidogo ili afanyiwe uavyaji.

Mijadala katika makundi teule yalibainisha kuwa, aghalabu hicho kitu kidogo, yaani malipo ya kuavya mimba hutolewa na tajiri husika. Merimela anawakilisha wasichana na wanawake wa tabaka la chini au masikini huku wadosi wakiwakilisha tabaka la matajiri. Usimulizi wenyewe ni kama ufuatao:

**Mf 48**

*kila mwaka ni mimba*
*kila mwaka abortion*
*na we ukadanganywa*
*toa kitu kidogo*
*ukafanye abortion*

(Kutoka: *Merimela.* Msanii: Uncle Ckoniah)

Katika wimbo Dunia Mbaya, kuna simulizi zinazoonyesha kuwa matajiri huweza kuathiriwa na VVU/UKIMWI. Mathalani, katika ubeti wa tatu, msanii anawataja wadosi na kuwaambia wachunguze. Anafanya vivyo hivyo katika ubeti wa saba. Simulizi hizo ni pamoja na:

**Mf 49**

*wadosi (chunguzee)*
*Ni wadosi nakufa.*
*Wewe sir, tumia condom.*

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Dully Sykes naye katika wimbo 'Nyambizi' anadokeza kuwa si matajiri wa kiume peke yao wanaohusika katika ununuzi wa ngono/mapenzi. Katika wimbo huu kuna simulizi za mhusika aliyepewa jina Nyambizi. Huyu ni mwanamke aliye na pesa na anatumia uwezo huo wa kifedha kumteka kimapenzi kijana anayewakilishwa na Sykes mwenyewe. Nyambizi anawakilisha tabaka la wanawake akiwemo rafiki yake Winnie ambao wanatumia utajiri wa pesa kununua mapenzi, kutoka kwa vijana. Sykes naye anawakilisha tabaka la wanaume hasa vijana ambao ni maskini na wasio na kazi. Mahusiano ya makundi haya kimapenzi yanaweza kuchangia kuenea kwa virusi vya Ukimwi.

Simulizi ndogo zilizomo katika wimbo huu zinapinga simulizi kuu katika jamii. Mathalani, simulizi kuu katika jamii ni kwamba, katika masuala ya mapenzi mwanamume ndiye humtongoza mwanamke. Katika wimbo huu mwanamke

amechorwa kwa namna ambavyo anaonekana kumtongoza mwanamume. Kwa mfano, yeye ndiye anayemwalika Sykes wakutane kilabuni FM Club Kinondoni Jumapili saa kumi. Kwa kawaida mwanamume ndiye hutekeleza shughuli hii.

Isitoshe, katika wimbo huu mwanamke ndiye amelewa na ndiye anayemwongoza mwanamume apange chumba cha kulala na kufanya mapenzi. Aidha, yeye ndiye anayemtuma mwanamume azime taa wanapokuwa chumbani. Simulizi kuu katika jamii ni kwamba, mwanamke aliyemteka mwanamume kimapenzi ndiye anayesema huyo mwanamume hamwachi, hasikii wala haoni. Nafasi ya simulizi hii kuu inachukuliwa na simulizi ndogo pale mwanamume asemapo:"waseme hadi asubuhi. Nyambizi haniachi, hasikii wala haoni."

Katika ubeti wa mwisho, kuna masimulizi yanayoonyesha uwezekano wa kuambukizana VVU/UKIMWI. Msanii anaeleza kupitia kwa wimbo wake kuwa, usiku huo ilikuwa bila zana, ngoma dry, ajali kazini mpaka kunakucha. Fasiri ya usemi huu ni kwamba, wahusika walishiriki ngono bila kinga (zana). Katika muktadha huu, zana inaweza kuwa kondomu. Aidha, ngoma ni kitendo cha ngono, kwa hivyo ngoma dry ni kushiriki ngono bila kutumia mpira. Isitoshe, ajali kazini inaweza kuwa maambukizi ya VVU kutokana na kutotumia kinga kazini yaani kutika ngono. Matumizi ya neno Sodoma pia huashiria ngono inayohusishwa sana na mabasha na ndiyo huchangia kuenea kwa VVU.

**Mf 50**

*Jimama kote anacheza, hadi sodoma. Japo kanimeza*
*lakini mchezo anauweza.*
*Na sijui wapi mchezo huu aliupokeza. Sababu macho*
*anafumba na kiuno anakilegeza.*
*Nami sitoweza kumuacha, usiku huo ilikuwa bila*
*zana. Ngoma dry ajali kazini mpaka kunakucha,*
*Wwaaa!*

(Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Pamoja na hayo, simulizi ndogo zilizomo katika wimbo huu zinapinga simulizi kuu kwamba, wanawake wanaoeneza VVU ni wale wanaoshiriki katika biashara ya ngono au wale wanaohusishwa na tabaka la chini peke yao. Katika muktadha wa wimbo huu, mhusika Nyambizi ni mwanamke anayefanya kazi katika shirika moja la Benki kama anavyoeleza katika ubeti wa kumi. Kwa jinsi hiyo, yeye si mmoja wa wale wanaoshiriki biashara ya ngono bali anaweza kuhusishwa na tabaka la juu. Hivyo basi, mama Nyambizi anawawakilisha wanawake wenye uwezo wanoshiriki ngono na vijana kama vile Sykes nah ivy kuchangia kuenea kwa maambukizi kama inavyodhihirika katika wimbo huu ubeti wa mwisho.

Kwa kuwa wimbo huu unalenga tabaka la vijana, lugha iliyotumiwa ni ya kuchanganya ndimi. Mathalani kuna matumizi ya maneno kama vile:

**Mf 51**

| | |
|---|---|
| *tunapiga story* | *Ngoma dry.* |
| *OK nakupa promise* | *mfuko wa nylon.* |
| *FM Club* | *siku ya valentine.* |
| *Tukachukua cab* | *upto date empire mjini* |
| *tukaanza na romance* | |
| *semeni mpaka morning* | |
| *ulikuwa umevaa kitop.* | |

(Kutoka: *Nyambizi.* Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Isitoshe, kuna matumizi ya maneno ya mtaani kama vile pozi na dozz. Pamoja na hayo msanii ametumia msamiati uliotoholewa kwa mfano hoteli na benki. Pia kuna matumizi ya nahau kama vile kupiga story, kupiga puchu, kula ndumu na kukutia machoni. Msanii pia ametumia tashbihi na misemo kama vile:

**Mf 52**

*Nilikuwa na mapeni kama Mobutu*
*hasikii wala haoni*

(Kutoka: *Nyambizi.* Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Katika wimbo wa *List ya mazishi*, Msanii anawataja watu ambao wana uwezo wa kifedha na ambao majina yao yalikuwa kwenye orodha iliyoandaliwa na marehemu Eliza. Kuna uwezekano kuwa waliotajwa walitumia uwezo huu wa kifedha kununua mapenzi/ngono toka kwa marehemu ambaye, kulingana na muktadha wa wimbo huu huenda alifariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Wanaotajwa ni pamoja na Dr. Mwachichi, Mwalimu Kibe na Yusufu Taxi Driver. Hawa ni wahusika wanaowawakilisha watu walio na uwezo kifedha katika jamii huku Eliza akiwawakilisha wasiokuwa nayo. Katika mahusiano ya aina hii, masikini aghalabu hawana uwezo wa kukata maamuzi kuhusu maswala ya ngono.

Msanii ametumia lugha inayochanganya ndimi ambapo kuna mchanganyiko wa maneno ya Kiswahili na ya Kiingereza.

**Mf 53**

| **Kiswahili/Kiingereza** | **Kiswahili Sanifu(TY)** |
|---|---|
| *Who can hisi yupi mwenye virusi* | *Nani anaweza kuhisi yupi mwenye virusi* |
| *Kuna list.* | *Kuna orodha* |
| *Kasema you are not allowed in here.* | *Akasema nyinyi hamtakiwi hapa* |
| *Ubishi jo, no.* | *Ubishi bwana, la hasha* |

(Kutoka: *List ya Mazishi*. Wasanii: Mchafuzi & Elyen)

Isitoshe, kuna matumizi ya maneno yaliyotoholewa katika lugha ya kiingereza kama vile:

**Mf 54**

| **Kiingereza** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *List* | *listi.* |
| *Nurse* | *nesi.* |
| *Corner* | *kona.* |
| *Lost* | *potea.* |
| *Pastor* | *pasta.* |
| *Pastors* | *mapasta.* |
| *Story* | *stori/hadithi* |
| *Hospital* | *Hospitali.* |

(Kutoka: *List ya Mazishi*. Wasanii: Mchafuzi & Elyen)

Hadhira zinazolengwa na wimbo huu ni zile za vijana na wanajamii wote kwa ujumla. Hii ni kwa sababu, ile lugha inayotumiwa na mwimbaji akiwalenga vijana ni lugha inayochanganya ndimi za Kiswahili na Kiingereza. Hii ndiyo lugha inayoeleweka zaidi na vijana hasa wenye kisomo. Mbali na kuchanganya ndimi, lugha hii yao husheheni matumizi mazito ya Sheng, lengo kuu likiwa kuzuia habari fulani kufikia watu wengine. Kwa mfano katika wimbo huu, kuna maneno ya Sheng kama vile *Kimatch,* yaani mchezo mdogo ambao kwa muktadha huu ni ngono.

Kwa upande mwingine, lugha inayotumiwa na mamake Eliza (Pokale) ni lugha inayoeleweka na wanajamii wote. Hii ni kwa sababu ni lugha nyepesi na isiyochanganya ndimi kwa wingi. Kwa hakika 'Taxi na Driver' ni maneno ya pekee kutoka lugha ya Kiingeeza yaliyoingizwa katika usemi wa Pokale alipokuwa anasoma orodha. Isitoshe, usemi wake hauna matumizi ya Sheng.Miktadha ya kijamii inayobainika katika wimbo huu ni pamoja na nyumbani kwa Eliza na mamake Pokale, hospitalini na mazishini.

Katika wimbo *Ajali Kitandani,* msanii anatusawiria hali halisi ya mahusiano ya kitabaka ambapo walio na pesa huzitumia kununua mapenzi/ngono.Wanawake

wanaoshiriki biashara ya ngono huinadi kwa kutangaza bei. Kuna wanaohitaji malipo ya shilingi mia moja, wengine wa mia mbili, mia tatu, mia tano hadi elfu moja. Wanawake hawa wamegawika kitabaka. Wale waliokita biashara hii ya ngono katika barabara ya Koinange huwalenga wateja wa tabaka la juu ambao ni matajiri walio na pesa na wa kuendesha magari. Kusimamishwa huku sana sana ni kwa wateja wanaoendesha magari na walio na pesa nyingi.Kwa mfano, katika ubeti wa tatu msanii anasimulia kuwa:

**Mf 55**

| **Kiswahili/Sheng** | **Kiswahili Sanifu(TY)** |
|---|---|
| *Koinange* | *Koinange* |
| *Wanawake wanono* | *Wanawake wanene* |
| *Wabinti wanono* | *Wasichana wanene* |
| *Wanakusimamisha* | *Wanakusimamisha* |
| *Wanakuuliza* | *Wanakuuliza* |
| *Uko na doo ngapi?* | *Una pesa ngapi?* |
| *Uko na ngiri ngapi?* | *Una elfu ngapi?* |

(Kutoka: *Ajali Kitandani*. Msanii: Ratali A. Kibunja)

Wanawake na wanaume wanaoendeleza biashara hii kwenye Barabara ya River Road jijini Nairobi sana sana ni wale wa tabaka la chini. Mathalan, wateja ni wa kutembea miguu kama anavyosimulia mwimbaji katika ubeti wa nne:

**Mf 56**

*Ooh! River Rodi*
*Tembea River Rodi*
*Wanawake warembo*
*Wanakung'ang'ania*
*Wanakuangalia*.

(Kutoka: *Ajali Kitandani*. Msanii: Ratali A. Kibunja)

Kutembea kunakosimuliwa katika mstari wa pili hapo juu ni kule kutumia miguu na wala sio gari.Kuweko kwa wanawake wanaojiuza kwa bei tofauti tofauti iwe katika barabara ya Koinange au ya River Road ni ishara ya kugawika kwao wenyewe

kitabaka. Wale wanaojiuza kwa shilingi mia moja, mia mbili au mia tatu wanaweza kuhesabiwa kuwa wa tabaka la chini huku wanaolipiza mia tano hadi elfu moja huweza kuingizwa katika tabaka la juu.

Mahusiano kati ya matabaka haya yanachangia kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI. Msanii anawahimiza wasikilizaji wake ambao ni kina mama, baba, wazee, vijana na kina dada wajizuie kwani kichaa cha mbwa kimechacha sana barani Afrika. Kichaa cha mbwa kimetumiwa kiistiria kumaanisha Virusi Vya UKIMWI vinavyoenezwa kitabaka.

### 5.4 VVU/UKIMWI na Suala la Mamlaka/Hadhi

Campbell na wenzake (2006) wanaeleza kuwa, katika jamii nyingi za Kiafrika, jinsia ya kuumeni imekwezwa na kupewa mamlaka au uwezo mkubwa huku jinsia ya kuukeni ikitwezwa na kudhalilishwa. Mwanamume amekuzwa kwa namna ambavyo anajiona mwenye nguvu na mamlaka, hali inayompa nafasi ya kumtawala, kumdunisha, kumdhulumu na hivyo kumdhalilisha mwanamke kwa njia nyingi ikiwemo maswala ya ngono. Kimsingi mwanamume hupata nguvu hizi kutokana na itikadi za kijamii, elimu, uchumi, na kadhalika. Katika jamii nyingi za kibabedume, mwanamke hunyimwa haki za kupata elimu, kujiimarisha kiuchumi na hata kufanya maamuzi ya kibinafsi kuhusu jinsi na wakati wa kushiriki ngono ama ndani au nje ya ndoa. Mwanamume ndiye anayemwamulia.

Ukosefu wa elimu, umaskini na kutokuwa na uwezo wa kujifanyia maamuzi hasa kuhusu ngono huwafanya wanawake wengi kukubali kushiriki ngono hata bila kinga na hivyo kuchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU. Baadhi ya nyimbo

tulizozichanganua zinadhihirisha hali hii. Aidha, nyimbo hizi zinabainisha kuwa mamlaka na nafasi walionayo baadhi ya wanajamii huweza kuchangia maenezi ya virusi vya UKIMWI.

### 5.4.1 Tofauti za Kiumri

Tofauti za kiumri kati ya wahusika wanaoshiriki ngono zinaweza kuchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU/UKIMWI. Mathalani, iwapo msichana ana umri mdogo kumshinda mwanamume, ina maana kuwa, msichana hatakuwa na uwezo wa kuamua na kupendekeza matumizi ya kinga kwa ajili ya kujikinga dhidi maambukizi na hata mimba. Kwa mfano, ubeti wa pili na wa sita katika wimbo *Merimela* ni simulizi zinazoshereheshea hali hii. Katika ubeti wa pili mstari wa pili, mwimbaji anasimulia kuwa, akiwa katika darasa la saba, Merimela alishiriki tendo la ngono na wanaume(*machali)* mbalimbali na hata walimu wake. Ninapotafakari juu ya umri wa msichana huyu wa darasa la saba na umri wa mwalimu wake kwa mfano, inakuwa dhahiri kwamba, hawa ni watu wawili walioachana kiumri. Hii ni kwa sababu, kimsingi, umri wa mwalimu wa shule ya msingi huwa mkubwa kuliko wa mwanafunzi wake.

**Mf 57**

*Kwa shule ya upili mwendo ni ule ule mapenzi kiholela*
*Kila mwaka ni mimba kila mwaka abortion ikakuwa mtindo*
*Hata chuo kikuu raha ikapanda vunja vunja mifupa*
*Wadosi na fukara ukaonja Merimela na mimba ni kawaida*

(Kutoka: *Merimela*. Msanii: Uncle Ckoniah)

Kutokana na ubeti wa pili basi, tunaweza kusema kwamba, *machali* na walimu walitumia uwezo wao wa kiume na kiumri dhidi ya Merimela ambaye alikuwa msichana asiyekuwa na nguvu kama za wanaume *(machali*) na aliyekuwa na umri

mdogo kuliko wa walimu wake. Katika hali hii, Merimela hangekata uamuzi kuhusiana na swala la ngono na hivyo kukumbana na mvurugiko wa kimapenzi akiwa mdogo.

Kwa mujibu wa Campell na wenzake (2006), mvurugiko wa kimapenzi katika umri mdogo huwa msukumo unaompelekea mhusika kushiriki mapenzi ya kiholela au mapenzi bila kinga hapo baadaye akiwa na umri pevu na hivyo kuwa katika hatari ya kuambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwemo VVU/UKIMWI. Ukweli wa maoni ya wataalamu hawa unadhihirika katika beti zinazofuata hasa ubeti wa nne, tano, sita na wa saba. Mathalani, katika ubeti wa tano mwimbaji anasimulia kuwa Merimela alikataa ushauri wa kuzingatia ngono salama. Matokeo yake yakawa kudungwa mimba na hatimaye kuambukizwa VVU/UKIMWI kama inavyobainika katika ubeti wa nne na wa tisa. Aidha, matokeo ya mvurugiko wa kimapenzi yanadhihirika katika ubeti wa sita ambapo Merimela alishiriki ngono na wanaume waliomzidi kiumri kama vile *wadosi*. Msimamo wa utafiti huu ni kwamba, umri wa mtu anayetajwa kuwa mdosi ni mkubwa kuliko ule wa msichana wa shule ya upili kama Merimela wa wimbo huu.

Simulizi ndogo kuhusu ngono kati ya wahusika waliotofautiana kiumri hasa watoto wa shule na walimu unakinza simulizi kuu kwamba, VVU/UKIMWI ni ugonjwa unaohusishwa na wale wanaoshiriki biashara ya ngono peke yao. Aidha ni simulizi inayopinga simulizi kuu kwamba, mwalimu anapaswa kuwa kama mzazi na kumchukulia mwanafunzi wake kama mtoto wake. Isitoshe, simulizi hii, inabainisha kuwa, baadhi ya walimu katika muktadha wa baadausasa nchini Kenya si wa kuaminika wala kutegemewa kuwaongoza na kuwashauri wanafunzi walio chini yao.

Wanaotumia uwezo wa kiumri kujishindia ngono na hivyo kueneza virusi vya UKIMWI si wanaume peke yao. Wanawake pia hutumia uwezo huu dhidi ya vijana wa kiume ili wapate kushiriki ngono nao. Hali hii inadhihirika wazi katika wimbo *Nyambizi*. Huu ni wimbo wa majibizano kati ya mwanamke aliyepewa jina Nyambizi na kijana wa kiume anayewakilishwa na msanii. Mintaarafu ya mazungumzo yao, inadhihirika kuwa wahusika hawa wametofautiana kiumri. Hii ni kwa sababu katika mstari wa kumi na sita, Nyambizi anajifanya kukataa ombi la kijana ambaye amemwambia kuwa anataka kuwa naye maishani. Anamjibu kuwa: Hilo haliwezekani na anapoulizwa na kijana atoe sababu anamwambia:

**Mf 58**

> "*Unajua Dully wee kiumri bado upo chini".*
>
> (Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Ni kupitia kwa kauli ya kijana ambapo tunapata kujua umri hasa wa mwanamke huyu. Kijana anamwambia:

**Mf 59**

> "*Dah! Nyambizi, japokuwa una miaka arubaini mi nataka uwe nami maishani.***"**
>
> (Kutoka: *Nyambizi.* Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Baadaye Nyambizi ndiye anayemwalika kijana wakutane Jumapili saa kumi jioni FM Club Kinondoni. Katika mazungumzo yaliyofuata kule kilabuni, Nyambizi alikubali ombi la kijana (Dully Sykes). Anamwambia:

**Mf 60**

> "Dully, ombi lako moyoni nimeridhia."
>
> (Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Katika mistari inayofuata, wanashiriki mvinyo, wanalewa, wanachukua teksi kwenda hotelini wanapopanga chumba cha kulala na hatimaye kushiriki ngono; bila kinga. Hili linadhihirika katika mistari miwili ya mwisho Dully Sykes asemapo.

**Mf 61**

“ Usiku huo ilikuwa bila zana. Ngoma dry”

(Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Mahusiano kama haya ndiyo yanayochangia kuenea kwa virusi vya ukimwi hasa miongoni mwa vijana na wanawake. Kutokana na muktadha wa wimbo huu, ninakubaliana na Nyawira (2008) na Gakahu (2010) wanapodai kuwa ulevi huchangia pakubwa kuenea kwa virusi vya UKIMWI.

Ulevi huathiri urazini na tafakuri ya mtu na kumfanya awe wa kutojali na hivyo kushiriki ngono bila kinga na hatimaye kuishia kujuta. Vyombo vya habari kama vile runinga vimekuwa vikirusha matangazo yanayowaonya wanajamii dhidi ya ulevi na kutotumia kinga wakati wa ngono. Matangazo hayo ni kama vile: *Unapokunywa zaidi ndivyo unavyoteleza zaidi* na *Ngono bila majuto* (TY). Hali hii huenda iliwakumba Nyambizi na Dully Sykes.

Nyambizi anawawakilisha wanawake wanaotumia upevu wa umri wao kuwateka vijana ambao hawajakomaa kiumri na kuwahusisha katika mapenzi. Winnie, ambaye ni rafikiye Nyambizi anatajwa katika wimbo huu kwamba alikuwa ameandamana na Nyambizi kilabuni “Up to Date Empire” Dully Sykes alipomwona mara ya kwanza. Hawa wanawawakilisha mashuga mami au mama sukari wanaowafuata vijana mabarobaro wa kiume ili kuwakidhia mahitaji yao ya kimwili hasa ngono.

Simulizi ndogo inayohusu mahusiano kati ya Nyambizi na kijana (Dully Sykes) inapinga simulizi kuu katika jamii kwamba, mahusiano ya kimapenzi ni ya watu

waliokaribiana kiumri. Aidha, inapinga simulizi kuu inayowaruhusu wanaume wazee wawaoe au wawe na uhusiano wa kimapenzi na wanawake au wasichana wa umri mdogo.

Katika wimbo *Listi ya Mazishi*, suala la VVU/UKIMWI na umri linajitokeza pia. Mathalani, katika ubeti wa pili, msanii anasimulia maisha ya awali ya msichana Eliza. Anaeleza kuwa kabla ya kifo chake, msichana huyu alikuwa mrembo. Baada ya babake kufariki, Eliza aliishi na babake wa kambo ambaye pengine ndiye aliyemwambukiza VVU/UKIMWI. Maoni yangu ni kwamba, labda baba huyu wa kambo ni yule aliyetajwa mwishoni mwa orodha ya walioambukizwa na ambaye alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mamake Eliza pia. Huyu ndiye mzee Mwazingo Kilelo.

Isitoshe, wanaotajwa kwenye orodha kuwa walishiriki ngono na Eliza ni watu ambao, kwa maoni yangu, wana umri mkubwa kumshinda. Kwa mfano, kuna Dakitari Mwachichi, Mwalimu Kibe, Yusufu Dereva wa Teksi, mzee Mwazingo, Pasta Wanjala na kadhalika. Hali ikiwa hivi, huenda waliotajwa kwenye orodha walitumia uwezo wao wa kiumri kujishindia ngono kutoka kwa Eliza ambaye umri wake ulikuwa mchanga.

**Mf 62**

> *Majina yenyewe ni kama yafuatayo:*
> *Dr. Mwachichi*
> *Eeeh (Sauti)*
> *Mwalimu Kibe*
> *Eeeh! Oooh! (Sauti)*
> *Yusufu Taxi Driver*
>
> (Kutoka: *List ya Mazishi*. Msanii: Ratai A. Kibunja)

Simulizi ndogo zinazohusishwa na UKIMWI zinakinza simulizi kuu zilizokuwa zinashikiliwa na wanajamii hapo awali. Kwa mfano, madaktari, walimu, wazee na

mapasta hawakuwa miongoni mwa waliohesabiwa kushiriki ngono na hasa ngono za kiholela na kuambukizwa virusi. Hii ndiyo maana jina la Pasta Wanjala linaposomwa, mmoja wa wale waliohudhuria mazishi ya Eliza anashangaa na kuuliza.

**Mf 63**

*"Aaah! Mpaka mapasta pia?"*

(Kutoka: *List ya Mazishi*.Msanii: Ratai A. Kibunja)

Kwa kuongozwa na nadharia ya baadausasa, msimamo wa utafiti huuni kwamba, vita dhidi ya UKIMWI vinapaswa kushirikisha kila kitengo cha wanajamii hasa kiumri. Hii ni kwa sababu, wanaoshukiwa kushiriki ngono na kusambaza virusi si wafanyi biashara ya ngono peke yao. Kupitia kwa wimbo huu msanii anapendekeza vita hivi vielekezwe kwa madakitari, walimu, madereva, wasanii, mapasta, watoto na kadhalika. Almuradi kila sehemu ya jamii ishirikishwe.

### 5.4.2 VVU/UKIMWI na tofauti za Kihadhi

Hadhi au cheo ni madaraka au nafasi ya juu aliyo nayo mtu katika jamii. Angalabu hadhi hufungamanishwa na kazi afanyayo mtu katika jamii. Kwa msingi huu basi, mtu anaweza kuwa na cheo cha udakitari, ualimu, udereva, usanii, ukarani, upadre, ushehe na kadhalika. Mtu hupata heshima na au mtwezo kulingana na cheo anachoshikilia.

Ingawa watu wanaoshikilia nyadhifa za aina hii wanatarajiwa kuzitumia kwa manufaa ya wanajamii, wakati mwingine huzitumia kuwadhulumu wanajamii na hivyo kujinufaisha wenyewe. Nyimbo tano kati ya nyimbo ishirini na tatu nilizozichagua zilibainisha kuwa, UKIMWI huathiri hata wenye vyeo ambao awali hawangefikiriwa kujihusisha na mapenzi ya kiholela. Msimamo wangu ni kuwa, baadhi yao hupata kuambukizwa na kuwaambukiza VVU kwa sababu ya kutumia madaraka kujishindia

ngono. Kwao, nyadhifa hizi zinakuwa mafichoni ambamo hujificha na kushiriki matendo hayo yanayofichuliwa pindi tu mhusika anapobainika kuwa na VVU/UKIMWI. Hapo ndipo wanajamii hutanabahi na kushangaa kuwa kumbe hata wao wamekuwa wakishiriki. Ugonjwa huu basi ni kama mtego wa panya unaowashika waliomo na wasiokuwemo; wasiokuwemo ikiimanisha wasiotarajiwa au wasioshukiwa kushiriki matendo fulani fulani.

Katika wimbo *Merimela* ubeti wa pili, msanii anasimulia kuwa mbali na kushiriki mapenzi na machali mbalimbali, Merimela pia alishiriki mapenzi na walimu wake. Tunapotafakari juu ya tofauti kati ya mwanafunzi na mwalimu kihadhi, inabainika kuwa mwalimu ndiye mwenye cheo, hadhi au madaraka ya juu. Msimamo wetu ni kuwa, huenda walimu walichangia kuambukizwa kwake Merimela (mwanafunzi). Hadhi aliyo nayo mwalimu katika jamii humfanya kuwa mtu wa kuaminiwa na wengi.

**Mf 64**

*Kwa darasa la saba kipenzi Merimela ukaanza geuka*
*Machali mbalimbali hata nao walimu wakakufanya quencher*
*Nawe ukakubali ingilia mapenzi ya kiholela holela*
*Na ukawachukia walokuwa karibu wakikupa ushauri ee*

(Kutoka: *Merimela*. Msanii: Uncle Ckoniah)

Simulizi ya uhusiano wa kimapenzi kati ya mwalimu na mwanafunzi ni simulizi ndogo inayopinga simulizi kuu ya awali ambapo walimu waliaminika na kuachiwa watoto wa kike kuwa chini ya uangalizi wao. Katika jamii nyingi za Kenya hasa katika muktadha wa kibaadausasa, kuaminika huku kwa walimu kumetiliwa shaka. Tunapofikia mwisho wa wimbo huu, mhusika Merimela alikuwa ameambukizwa VVU. Miongoni mwa walioshukiwa kumwambukiza ugonjwa huu ni walimu wake. Hii ni kwa sababu huenda walimu hao walitumia hadhi yao ya ualimu kujishindia mapenzi kutoka kwa Merimela.

Katika wimbo Dunia mbaya, baadhi ya watu wanaotahadharishwa na msanii Princess Jully ni watu wenye vyeo au madaraka. Aidha, baadhi ya waliokufa kutokana na ugonjwa huu wa UKIMWI ni watu waliokuwa wanaheshimika katika jamii. Hii ndiyo simulizi kuu inayopingwa na simulizi ndogo kuhusu vifo vyao vilivyosababishwa na UKIMWI.

Mathalan, katika ubeti wa pili, msanii anauliza na kujibu: “Yu wapi Ohula? Alikufa kwa sababu ya Ukimwi.” Kulingana na majadiliano yetu na wanawake wafanyikazi wa vilabuni, ilibainika kuwa baadhi ya wanaume wanaohudumu katika jeshi la polisi hutumia vyeo walivyo navyo kujishindia warembo dhidi ya raia wa kawaida. Isitoshe, kwa kuwa wao huwa kimbilio la usalama kwa raia hususan wanawake na wasichana wadogo, baadhi ya maafisa hutumia nafasi hiyo kuwadhulumu kimapenzi. Hufanya hivyo kwa kisingizio cha kuwafanyia mambo yao hasa zinazohusiana na kesi kunyooka. Msimamo wa utafiti huu ni kwamba, Virusi Vya UKIMWI vinaweza kuenezwa kupitia kwa mahusiano ya kimapenzi kama haya. Sifa ya uzuri anayopewa Ohula katika wimbo huu ni kwamba, yeye akiwa afisa wa polisi hangetarajiwa kushiriki mapenzi ya kiholela ambayo mwishowe yanamletea maangamizi. Afisa wa polisi anatarajiwa kuwa na heshima pamoja na nidhamu.

**Mf 65**

*Wapi Onyango Billy? Wapi Onyango Billy?*
*Ni Tom yuko wapi?*
*Wapi wa Mombasa?*
*Wapi wa Mombasa?*
*Okoyo yuko wapi? Okoyo yuko wapi?*
*Ohula yuko wapi? Ohula yuko wapi? Yuko*
*Wapi? Steve yuko wapi? Evans yuko wapi*
*Evans yuko wapi? Wapi wa Mombasa,*
*Wapi wa Mombasa?*
*Wapi wa Kisumu? Wapi wa Kisumu*
*Ogweno yuko wapi? Ogweno yuko wapi?*
*Otieno yuko wapi, Tafadhali wacha raha,*
*Utakufa mbaya,*
*Utakufa kama mbwa, utakufa mbaya*
*Tafadhali chunguze*
(Kutoka: Dunia Mbaya. Msanii: Princess Jully)

Katika ubeti wa tatu na nne, msanii anawatahadharisha wanawake dhidi ya kutotumia kondomu wanapojishindia wadosi. Isitoshe, anawaonya wenye suti na wale wanaotajika kama *Sir*watumie kondomu pia. Tasnifu yangu ni kwamba polisi, wadosi wenye suti na kina *sir* ni watu wa kustahiwa katika jamii kwa sababu ya hadhi waliyo nayo. Simulizi ya VVU/UKIMWI kuwahusu inapinga simulizi kuu ya awali kwamba watu wa heshima kama wao hangeshiriki mapenzi ya kiholela wacha kuambukizwa viruzi vya Ukimwi.

**Mf 66**

*Wadosi (chunguzee)*
*Wazee (chunguzee)*
*Kuenda Kisumu, tumia condom.*
*Kuenda Amerika, tumia condom.*
*Wewe Jane, tumia condom.*
*Wewe Rebecca, tumia condom.*
*Wewe sir, tumia condom.*
*Akina Okoth, tumia condom*

(Kutoka: Dunia Mbaya. Msanii: Princess Jully)

Wimbo *List ya mazishi*, unaorodhesha majina ya wanaume waliowahi kushiriki ngono na Eliza ambaye anafariki baada ya kuugua UKIMWI. Wahusika wanotajwa wanawawakilisha watu wanaoheshimika katika jamii; baadhi yao wakiwa watu ambao awali hawangeshukiwa na kuhusishwa na tabia walizonazo na ambazo zingewaweka katika hatari ya kuambukizwa. Maoni yangu ni kwamba Dr. Mwachichi anawawakilisha madakitari, mwalimu Kibe anawawakilisha walimu, Yusufu dereva wa taxi anawawakilisha viongozi wa Kiislamu huku Pasta Wanjala akiwawakilisha viongozi wa Kikristo. Simulizi inayowahusisha waliotajwa na UKIMWI ni simulizi inayopinga simulizi kuu uliowatenganisha na UKIMWI. Mathalani, mmoja wa waliohudhuria mazishi ya Eliza aliposikia jina la Pasta Wanjala kwenye orodha alishangaa na kuuliza.

**Mf 67**

*Aaaah! Mpaka mapasta pia?*

(Kutoka. *List ya Mazishi*. Msanii: Ratai A. Kibunja)

Mshangao huu ni mfano wa simulizi kuu inayopingwa na simulizi ndogo katika wimbo inayoonyesha kuwa, kinyume na ilivyochukuliwa awali, mapasta nao huambukizwa VVU. Msanii wa wimbo huu ametumia aina fulani ya majazi ili kutuchorea taswira ya tabia za wahusika na ambazo zinahusiana na ngono na hata VVU/UKIMWI. Jina "Jipande"linaashiria mtu aliye na tabia ya kushiriki ngono za jinsia moja au usagaji. Hii ni kutokana na matumizi ya kiambishi awali (JI) kwenye jina. Katika lugha ya Kiswahili, kiambishi hiki huleta dhana ya urejelezi. Kama anavyoeleza Nyawira (2008) kitendo cha usagaji kinahusiana na VVU/UKIMWI kwa karibu kwani kikundi hiki cha wanajamii kiko katika hali ya hatari zaidi ya kuambukizwa virusi. Hiki kilikuwa kikundi cha kwanza kuonyesha dalili za kuambukizwa VVU/UKIMWI kule Marekani. Ni kutokana na hali hii ambapo ugonjwa huu ulipata jina lake la kwanza kabisa GRID (Gay Related Disease) yaani ugonjwa unaofungamanishwa na usagaji. Kupitia kwa mhusika huyu basi msanii anawaonya wasagaji kwamba wanaweza kuambukizwa.

Isitoshe, jina Mnyamba, humaanishamtu ambaye ngozi ya mwili wake inanyambuka. Kunyambuka kwa ngozi ya mwili ni dalili mojawapo ya kuambukizwa VVU. Kwa hivyo, msanii ametumia jina hili kimajazi kuelezea hadhira kuwa yule ambaye ngozi ya mwili imeanza kunyambuka huenda ana ugonjwa wa VVU/UKIMWI. Hii ni njia ya mawasiliano inayowasilisha ujumbe bila kumtaja mtu kwa jina lake hasa.

Pamoja na haya jina Shani linamaanisha kitu kinachoshangaza. Aidha, huweza kuwa na maana ya mwenye maisha ya vituko au mpenda vituko; pia mwenye kuthubutu

kushiriki matendo ya hatari. Tukijikita katika wimbo huu ni kwamba, watu wasioogopa UKIMWI ndio wanaoambukizwa VVU. Ujasiri wao unaweza kuwapofusha wasitumie kinga wakati wa kushiriki ngono. Katika hali hii mtu hujihusisha na tukio au tendo lisilokuwa la kawaida na la hatari linaloweza kumfanya aambukizwe virusi. Katika muktadha wa kibaadausasa, tendo la kushiriki ngono bila kinga ni shani. Msanii amempa mwenye ujasiri wa aina hiyo jina Shani Msuba – mtafuta anasa au raha.

Hatimaye, jina la mwisho kwenye orodha ni la mzee. Mzee huyu amepewa jinaMwazingo Kilelo. Msimamo wa utafiti huu ni kwamba, hili ni jina la kimajazi linalomrejelea mtu anayewafuata au kuwatafuta wanawake. Pia huweza kumaanisha mtu asiyetulia mahali pamoja. Mtu wa kubadilika badilika au wa kuzurura bila lengo au wa kuzurura akiwa na lengo au nia mbaya. Jina lake la pili ni kilelo. Msimamo wangu kutokana na mijadala ya kimakundi ni kwamba maana ya jina hili ni kileo au kitu kinacholevya. Kwa msingi huu, tunaweza kusema kuwa jina kilelo linarejelea mtu anayependa kunywa na kulewa mvinyo au kileo. Mwanaume anayependa kuwafuata wanawake huwa katika hatari ya kuambukizwa magonjwa ya zinaa ukiwemo UKIMWI. Isitoshe, wanaotumia pombe na dawa zingine za kulevya pia nao wamo katika hatari hiyo hiyo. Kwa mujibu wa wimbo huu, Mwazingo alikuwa anashiriki mapenzi na Pokale mamake Eliza pamoja na Eliza mwenyewe kabla ya kufariki kwake. Hii ndiyo maana jina lake lilikuwa kwenye orodha ya mazishi, na lilipotajwa, mamake Eliza alionyesha mfadhaiko. Ni dhahiri kuwa huyu alikuwa mtu wa kuwafuata wanawake.

Katika wimbo wa kimaasai, *Enkotoroki*, Msanii Daniel Saning’o katika stanza ya nne anasimulia kuwa nyuki amewauma wabunge, maaskofu pamoja na mapasta. Nyuki

ametumiwa kiistiara kumaanisha mwanamke anayeeneza VVU. Hii ni kwa sababu msanii amempa nyuki sifa za kifeministi kama vile kuwa na macho makubwa (ya gololi) na kuuma kwa kutumia sehemu ya nyuma.

**Mf 68**

| | |
|---|---|
| *Oi torrono olotoroi, amu meire toki* | *Nyuki ni mbaya, kwa sababu hachagui* |
| *Nemeure olkanzolai, nemeure orbungei tapala yie* | *Haimwogopi Diwani au Akitaka kukuchoma Mbunge* |
| *Orbishop, tapala yie orpastai, ore ninye ilkalkal* | *Askofu au pasta* |
| *Ekesulu tosikiria paa keworu olenywa* | *Hata wazee hawabakishwi pia* |
| *Oi torrono olotoroi, etarrue yie olotoroi* | *Nyuki ni hatari, namwogopa nyuki* |
| *Oyie torrono olotoroi* | *Nyuki ni hatari mno* |
| *Eee hoyia* | |

(Kutoka: *Enkotoroki*. Msanii: Daniel Saning'o)

Wahusika wote wanaotajwa katika nyimbo hizi wakiwemo madaktari, walimu, viongozi wa kidini, madiwani, wabunge na kadhalika ni watu walio na vyeo mbalimbali. Simulizi ndogo inayowahusisha na ugonjwa wa UKIMWI inapinga simulizi kuu iliyowatenganisha na ugonjwa huo kitabia. Walichukuliwa kuwa waadilifu, watu walioheshimika na kustahiwa. Simulizi ndogo inaonyesha kuwa, katika muktadha wa kibaadausasa, hali imebadilika kwani waliodhaniwa kuwa sio kumbe wanakuwa ndio.

## 5.5 Hitimisho

Kaika sura hii nimejadili namna suala la VVU/UKIMWI inavyohusiana na utabaka. Sura hii ilianza kwa ufafanuzi wa dhana ya utabaka kisha matumizi ya uwezo wa kifedha kupata ngono na mapenzi. Aidha, nimejadili jinsi wanajamii wengine wanavyotumia mamlaka au nguvu walizonazo ili kukidhi mahitaji ya kimwili hasa ngono. Pamoja na hayo, nimejadili jinsi tofauti za kiumri zinavyochangia kuenea kwa VVU. Hali hizi zote nimezinabainisha katika nyimbo mbalimbali nilizozichanganua. Kutokana na uchanganuzi huu, nimebainisha kuwa, watu walio na fedha wanaweza

kutumia uwezo huo kujipatia ngono. Aidha wale walio na umri mkubwa wanaweza kutimia upevu huo wa umri dhidi ya wenye umri mdogo ili kupata mapenzi na ngono. Wasanii wa nyimbo wamewataja watu kama hao kwa njia moja au nyingine na kusawiri hali zilizowapata kama vile kuambukiza, kuambukizwa na hata kufa.

# SURA YA SITA

# NYIMBO ZINAZOHUSU UKIMWI NA MIKTADHA MINGINE YA KIJAMII

## 6.1 Utangulizi

Katika sura hii nimechanganua nyimbo zilizoteuliwa na kubainisha jinsi zinavyoshughulikia suala la VVU/UKIMWI na masuala mengine yanayohusiana nalo katika jamii. Kwa jinsi hiyo nimejadili vipengele kama vile: UKIMWI na suala la jinsia, nyimbo na malalamishi juu ya ngono bila tahadhari, ulevi, tamaa, starehe na anasa. Hatimaye nimejadili njia nyingine za kuepukana na VVU/UKIMWI kama zinavyopendekezwa na waimbaji na hivyo kuchangia katika vita dhidi ya janga hili.

## 6.2 Dhana ya Jinsia

Kulingana na Roper (2013), istilahi uana na jinsia kwa bahati mbaya hutumiwa kwa kubadilishana na hivyo kuwa kama visawe. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, matumizi ya aina hii si sahihi. Hata hivyo kulingana na American Psychological Association APA (2011), uana ni maumbile ya mtu kibayolojia; hali inayopambanuliwa na viungo vya uzazi vya ndani na vya nje, huku jinsia ikimaanisha mielekeo, hisia na tabia ambazo utamaduni fulani unazifungamanisha na maumbile ya mtu kibayolojia.

Mwanasosholojia Coakley(2009) anapendekeza kuwa, jinsia ni kile kinachofikiriwa kuwa ume au uke katika jamii. Katika mfumo uwili huu wa jinsia, kila mtu huainishwa ama kama mwanamke au mwanamume tu, huku ikidhaniwa kuwa mtoto akizaliwa wa kiume atakuwa na sifa za kiume na akizaliwa wa kike basi atakuwa na sifa za kike. Sifa hizi ni zile zinazotokana na mielekeo, hisia na hulka zenye misingi katika utamaduni. Kategoria hizi mbili hazikufumwa kuwa vinyume tu ila hufasiriwa kuwa kategoria asili ambapo mwanamume na ume ni bora kuliko mwanamke na uke.

Hii ni hali halisi katika tamaduni nyingi ambapo wanaume hudhibiti kwa viwango vikubwa nguvu za kisiasa na malighafi.

Coakley (2009) anaendelea kueleza kuwa inaaminika watu wote walioko katika kategoria ya wanaume kiasili hutofautiana na wale wa kategoria ya wanawake na matarajio ya wanajamii kwao kimaadili hutofautiana mintaarafu ya hisia, fikira na matendo. Uanishaji huu wa jinsia katika kategoria mbili unaathiri pakubwa mwonoulimwengu wa wanajamii kiasi cha kuwafanya kukataa kutafakari kwa kina kuhusu suala la jinsia. Katika hali kama hii, kuna uwezekano wa kutohisi vizuri wakati watu wanapokosa kuingia kabisa katika kategoria ya uanaume au uanamke.

Butler (1990), anafafanua dhana ya jinsia kama utendaji. Anaeleza kwamba, kimsingi jinsia hubainika wakati mtu anapotenda utambulisho wake kama mume au mke. Utendaji huu huhusisha namna anavyovaa, namna anavyozungumza, namna anavyocheza na kadhalika. Isitoshe, Butler anaendelea kufafanua kwamba, katika tamaduni nyingi utendaji wa jinsia si wa hiari; amali za jinsia hupendekeza ni matendo yapi ya kijinsia yapo na yanafaa kutendwa kwa njia zipi. Aliamini kwamba, watu wanaojitambulisha na mtindo fulani usioafikiana na amali za kitamaduni hukataliwa na kutengwa na wanajamii wengi wa jamii husika. Hii ni hali inayowakumba waathiriwa wa VVU/UKIMWI.

### 6.3 KIMWI na Suala la Ujinsia

Yaliyomo katika nyimbo  nilizozichanganua yanatoa taswira juu ya mtazamo wa wanajamii kuhusiana na suala la jinsia na ngono. Kuna nyimbo zinazomsawiri mwanamke kama kiumbe ambaye anafaa kuparuzwa wakati wa kitendo cha ngono. Aidha, baadhi ya nyimbo zinamsawiri mwanamke kama kiumbe hatari anayeeneza VVU na tahadhari zinatolewa kwa jinsia ya kiume kujihadhari naye.

Isitoshe, Mutembei (2009) anaeleza kuwa, katika jamii zenye mfumo wa kibabedume, jinsia ya kike aghalabu ndiyo inayolaumiwa mintaarafu ya maambukizi ya VVU. Nyimbo zinazomsawiri mwanamke kwa jinsi hiizinamtweza huku zikimtwaza mwanamme. Pamoja na hayo, anaongeza kuwa, sitiara zinazorejelea ngono na VVV/UKIMWI kama vile “kula” zinaashiria kuwa, anayeliwa ni mwanamke. Maoni haya yanaafikiana na yale ya Nyawira (2008) aliyeeleza kuwa, miongoni mwa Waluyia, kitendo cha ngono kinanasibishwa na kitendo cha kulima. Simulizi zilizomo kwenye nyimbo nilizozichanganua zinachora picha sawa na hii.

Katika wimbo *Wee Kamu*, maandalizi yote yanayofanywa na msimulizi yanalenga kumparuza msichana katika tendo la ngono atakapomtembelea mwanamumechumbani mwake (*kejani)*. Maandalizi haya ni pamoja na kuhakikisha matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume kama vile Viagra. Isitoshe msimulizi ambaye ni wa jinsia ya kiume anapanga kumtapisha sukuma wiki wakati wa kitendo hicho cha ngono. Aidha, anapanga namna na wapi kitendo hicho kitakapofanywa. Mathalan ananuia kutumia mtindo wa wanyama kama vile ndovu, kucheza ngono kochini, mezani, kucheza ngono ya mdomoni na pia ya ushirika. Hii ndio maana anamwambia aandamane na wasichana wengine marafiki. Katika wimbo huu pia, kuna pendekezo la kucheza ngono bila kinga. Hii ni kwa sababu, katika ubeti wa pili msimulizi anasema: “bora leo uniachie tu nizame vimbichi.”

**Mf 69**

*Na juala staki mtaani kuwe na mazishi!*
*Kwa hivyo wee kamu tu ongeze raha na watu kwa nchi!*
*Bora leo unia chie tu nizame vimbichi,*
*Bora leo uniachie nikushike hivi,*
*Nikupeleke juu, nikupeleke juu mpaka utapike skuma wiki!*
*Elephant run, ningeiskia mpaka kwa coach,*
*Akule itakuwa ibidi!*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Nonini & Jua Cali)

Hali kama hii inadhihirika katika wimbo *Starehe*, ambapo muathiriwa anakiri kushiriki ngono na wanawake wengi kufikia kiwango cha kutowakumbuka. Isitoshe, kuna simulizi za kubainisha kuwa mhusika alishiriki ngono bila kinga kwani aliamini kuwa, kutumia kondomu kungepunguza utamu ndipo akapuuza ushauri aliopewa. Hii ni hali inayowakumba vijana wengi na huchangia pakubwa katika kuenea kwa VVU. Kitendo cha kushiriki ngono na wanawake wengi kinachukuliwa cha kiume. Hudhihirisha ubabedume wao dhidi ya wanawake. Simulizi zilizomo katika wimbo huu zinakosa uaushi na ndizo zinazotumiwa na vijana kujadili swala la ngono na VVU/UKIMWI.

Kulingana na The Norwegian Working Group on HIV/AIDS and Gender (2001), kitendo cha mwanamume kummwagia mwanamke shahawasi kitendo cha lazima kwa ajili ya ridhaa katika ngono, ila ni tarajio la kijamii linalofungamanishwa na ubabedume. Kwa msingi huu, mwanamume anaweza kummwagia mwanamke mahali popote hata kinywani jinsi inavyobainika katika ubeti wa tatu ya wimbo huu.

**Mf 70**

*Mdogo mdogo jo hajui inaeza kunyonga,*
*Umejaza mingi kwa mdomo utashindwa kubonga,*
*Tulia nikafungue mlango kuna mzungu ana ngoja,*
*Ana moto jo ananiambia anataka ku to to to ka.*

(Kutoka: *Wee Kamu*. Wasanii: Nonini & Jua Cali)

Kuna imani miongoni mwa wanajamii wengi kwamba mwanamume lazima ashiriki ngono penyezi ili kudhihirisha ubabe dume. Hili lilijitokeza wazi katika majadiliano ya kimakundi. Ngono za aina hii huchangia pakubwa kuenea kwa Virusi Vya UKIMWI. Hii ni kwa sababu mielekeo ya wanajamii kuhusu tofauti za kijinsia zinazofungaminisha jinsia ya kiume na tabia za kijasiri kama vile kufanya majaribio

ya hatari, matendo ya shani na ujeuri pamoja na kupuuza matokeo haribifu huimarisha mapuuza ya ngono salama na kukuza ngono isiyowajibikiwa miongoni mwa wanaume. Tabia hizo za kibabedume huwapofusha wanaume na hivyo kuwazuia kuelezea kutokuwa na uhakika pamoja na kujaribu tabia za kuhakikisha ngono salama.

Katika wimbo *Kichigili* wake Joel Kimetto, msanii anatubainishia matokeo haribifu yanayofungamana na matendo ya ujasiri hasa wa kibabedume. Katika wimbo huu, kuna usimulizi kutoka kwa Biblia kuhusu Shechem, mwanawe Amoth. Shechem alimpenda Dina, msichana kutoka jamii iliyokuwa inawatahiri wavulana. Jamii yake Schechem kidesturi haikuwa inawatahiri wavulana. Alipopeleka posa kwa wazaziwe Dina, aliambiwa sharti atahiriwe kwanza kabla ya kupewa Dina amwoe. Kwa sababu alimpenda msichana na hakutaka kuonekana mwoga au dhaifu, yeye na wanaume wenzake alioandamana nao walikubali kutahiriwa. Kumbe huu ulikuwa mtego wa kuwaangamiza kwani walivamiwa na wote wakauawa siku ya tatu baada ya kutahiriwa.

Msanii anaeleza kuwa, wale wanaume waliomsindikiza kupeleka posa hawakutafakari kuwa ilikuwa ni mmoja tu aliyepaswa kutahiriwa; yule aliyempenda msichana. Wote walijitosa ulingoni kwa sababu walikuwa ‘wanaume’; hawakutaka waonekane waoga au wadhaifu. Msanii afafanisha hali hii na ugonjwa wa UKIMWI ambapo wanaume wanaoekana kutojali madhara yake. Kitendo hiki cha kutahiriwa kinanasibishwa na maambukizi yanayotokana na kushiriki ngono na wenzi wengi.

Katika wimbo huu pia, Kimetto tofauti na wasanii wengine hajaonyesha mapendeleo ya kijinsia anapozungumzia suala la mapenzi na UKIMWI. Lugha aliyoitumia haimkwezi mwanamume wala kumtweza mwanamke. Mathalan, anaanza wimbo

wake kwa kurejelea Bibilia Takatifu, kitabu cha Mwanzo sura ya 34 ambapo anaeleza kuwa, hapo mwanzo Mungu alimwumba *Muren ak tie* yaani mwanamume na mwanamke. Kwa mujibu wa ubeti wa kwanza ya wimbo huu, Mungualiwawekea wote wawili kitu cha thamani nyoyoni mwao. Kitu hicho cha thamani kulingana na msanii ni mapenzi. Kutokana na mapenzi haya, macho ya mwanamke yanapokutanana ya mwanamume, kila mmoja huvutiwa na mwenzake na humwona huyo mwenzake kama kiumbe maalum. Hii ndiyo maana ya msanii kusema katika ubeti wa kwanza:

**Mf 71**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
| --- | --- |
| *Ak kondechi mugulelwekywak* | *Na akawawekea nyoyoni zao* |
| *Kitaap komonut* | *Kitu cha thamani* |
| *Ngotuiyo konyek komi* | *Macho yanapokutana kuna* |
| *Kiy moet ne lenen waa* | *Kitu tumboni kinachofanya waa* |
| *Ne ingokeer age age wee* | *Mmoja amwonapo mwenzie wee* |
| *Ko sipeshel* | *Ni spesheli.* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Kulingana na msanii si jinsia moja inayovutiwa na nyingine bali jinsia zote mbili zinavutiana. Anapotoa ushauri kwa wanajamii juu ya umuhimu wa mtu kujua hali yake ya UVU/UKIMWI, msanii ana ujumbe kwa kila jinsia. Mathalani kina mama na kina baba wanashauriwa kujipima.

**Mf 72**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
| --- | --- |
| *Kichigili oh mama* | *yachunguzwa oh mama* |
| *Kichigili oh baba* | *yachunguzwa oh baba* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Isitoshe, kuna ushauri huo huo kwa wanaochumbiana. Mchumba wa kike (mureret) ashauriwa ampeleke mchumba wa kiume (sandet) kwa daktari wachunguzwe kabla ya kuanza maisha ya ndoa. Vivyo hivyo, mchumba wa kiume anashauriwa kuwa ampatapo mchumba wa kike, ampeleke kwa daktari wachunguzwe kwanza. Kila mmoja wao anashauriwa kupata habari kuhusu tabia za mwenzie kutoka kwa marafiki na majirani kabla ya kukata uamuzi. Msanii aimba hivi:

**Mf 73**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Kas oh lakwanon* | *Sikiza ewe mtoto (msichana, bi. Arusi)* |
| *Ye inyoru sandet* | *Umpatapo mchumba (bw. Arusi)* |
| *Obe dakitari* | *Muende kwa dakitari* |
| *Si otou mengisiet* | *Kabla ya kuanza maisha ya ndoa* |
| *Kas oh sandanin* | *Sikiza ewe mkaza mwana (bw. Arusi)* |
| *Ye inyoru mureret* | *Umpatapo mchumba (bi. Arusi)* |
| *Obe dakitari* | *Mwende kwa dakitari* |
| *Si kechigil korook wee* | *Ili ichunguzwe kwanza wee* |
| *Tebeen choronok* | *Waulize marafiki* |
| *Ak biikaap kokwet* | *Na majirani* |
| *Ye teptoi chito* | *Jinsi mtu anavyoishi (tabia zake)* |
| *Si yoni ngalechon* | *Kabla hujakubali maneno hayo* |

(Kutoka: *Kichigili.* Msanii: Joel Kimetto)

Hii ni simulizi ndogo inayopinga simulizi kuu inayolimbikiza lawama kwa jinsia moja, hasa jinsia ya kike.

Lugha iliyotumiwa na msanii Chali katika wimbo wake *Miluma* (Tamaa), inaonyesha udhaifu wa jinsia zote. Anasimulia kuwa tamaa inamwandama hata aliyeoa na imewaharibu wanawake, wanaume, wazee na hata watoto. Hata hivyo katika ubeti wa nne, jinsia ya kike ikiwakilishwa na Adhiambo imesawiriwa kama jinsia inayompumbaza mwanaume. Wanawake wanaowakilishwa na Adhiambo ni wenye umri mdogo lakini wanaoshiriki ngono na wazee. Mzee aliyenunua gari na akapumbazwa na Adhiambo anawakilisha mababa sukari wanaofanya mapenzi na

wasichana marika ya wajukuu wao. Swali letu ni je, mwanamke hawezi kupumbazwa na mwanaume? Chali aimba hivi:

**Mf 74**

| **DhoLuo** | **Kiswahil(TY)** |
|---|---|
| *Jaduong' ong'ieo gari* | *Mzee amenunua gari* |
| *Adhiambo okao pache* | *Akapumbazwa na Adhiambo* |
| *Omanyo mbas nyakware* | *Anatafuta Marika ya wajukuu.* |

(Kutoka: *Miluma*. Msanii: Chali)

Katika wimbo *Tang'ne Dendi* (Linda mwili), msanii Ajoji Dume anawashauri watu wa jinsia zote wailinde miili yao dhidi ya VVU/UKIMWI. Mathalani katika ubeti wa mwisho katika wimbo huu, msanii amewalenga wanaume na mabanati na kuwashauri wailinde miili yao. Matendo ya wahusika huchangia pakubwa katika kueneza Virusi Vya UKIMWI na kusababisha maafa mengi. Ubeti wa mwisho ya wimbo huu ndiyo hii hapa:

**Mf 75**

| **DhoLuo** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Thithi sikul tee* | *Wanafunzi wote* |
| *Tang'ne dendi* | *mwili wako* |
| *Chuo te* | *Wanaume wote* |
| *Tang'ne dendi* | *Linda mwili wako* |
| *Thindo ma nyiri* | *Mabanati wote* |
| *Tang'ne dendi* | *Linda mwili wako* |

(Kutoka: *Tang'ne Dendi*. Ajoji Dume)

Msanii Daniel Saning'o katika wimbo wake wa *Enkotorok*i (Nyuki) amemsawiri mwanamke kama kiumbe cha kuvutia hasa kwa macho yake makubwa. Aidha, picha anayotuchorea msanii huyu kumhusu mwanamke ni kuwa yeye ni kiumbe hatari wa kufananishwa na nyuki.

Wanaume wanaonywa kuwa waangalifuwasiumwe/wasidungwe na huyo nyuki anayeuma kwa kutumia sehemu yake ya nyuma hasa wanapokuwa kwenye baa, sokoni na kadhalika.

**Mf 76**

| **Maa** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Entodolu olotoroi, entodolu irkiseyia* | *Muwe waangalifu dhidi nyuki* |
| *Oi eng'ura olotoroi, tenilo ake osokoni* | *Nyie vijana na wa umri wa makamo* |
| *Alo aing'oru enkurma, ena niyaki ng'aturan* | *Ukienda sokoni kutafuta chakula* |
| *Todolu ake olotoroi,tenilo aok bia* | *Tahadhari dhidi ya nyuki* |
| *Tenilo aok bia todolu ake olotoroi* | *Unapokunywa bia uwe mwangalifu* |
| *Amu tesiadi king'or* | *Atakuchoma kwa kutumia nyuma* |
| *Naliki kitamoni, naliki sii musalal* | *Namwomba kila mtu* |
| *Oi entodolu entoki amuu keng'orrisho* | *Atahadhari na nyuki* |
| *Naa tesiadi king'orr, neeta enkiti orii pee* | *Ana sauti tamu* |
| *Kitumoki ailejileja, eee, oooh* | *Itakayokuhadaa* |

(Kutoka: *Enkotoroki.* Msanii: Daniel Saning'o)

Simulizi kuu katika jamii nyingi ni kwamba, wanaume ndio wanaowafuata wanawake wakitafuta ngono ili kudhihirisha ubabedume wao. Hata hivyo, nyimbo tatu kati ya nyimbo zote nilizochanganua zinasheheni simulizi ndogo za kupinga simulizi hii. Nyimbo hizo ni: *Nampenda John, Silazima tudo*, na *Nyambizi.*

Wasanii wa *Wimbo Nampenda* John wametumia nomino John kijazanda kumaanisha dhakari ya mwanamume. Sifa alizopewa huyu John ni pamoja na kuwa ana jicho moja ndogo, hana mikono lakini shughuli anaifanya, anaishi msituni, ni mpenda raha, ana sweta yake maalum, akisalimiwa huona haya, akiona anaowapenda anasisimka. Aidha, haeleweki kwani mara amekwenda kazini, mara amekasirika amekwenda mwezini, ni mpita njia asiyebagua wazee au vijana, maskini au matajiri wote anawapa kinywaji.

Mjadala juu ya sifa za John iliyofanyika katika kikundi kimoja teule, ulibainisha kwamba, sifa hizi ni za dhakari ya mwanamume. Mathalani, jicho lake moja ndogo ni

lile tundu la kupitishia mkojo na shahawa. Shughuli inayosemekana kuifanya licha ya kutokuwa na mikono ni kitendo cha ngono na kule kuishi msituni ni kule kuzingirwa na manyoya ya sehemu ya siri. Kitendo cha kuona haya ni wakati kiungo hiki huwa katika hali yake ya kawaida. Kule kukasirika na kwenda mwezini pia hurejelea hali yake ya kawaida. Kitendo cha kusisimka ni kule kusimama kwa dhakari inapotekenywa tayari kwa ngono. Sifa ya kupita njia na kutobagua ni kushiriki ngono na wanawake wengi, wadogo kwa wakubwa. Kwa Upande mwingine kitendo cha kuwapa kinywaji kikiashiria kule kumwaga shahawa hasa wakati wa ngono penyezi.

Kimsingi, wimbo huu unamtweza mwanamke kwa kumsawiri kama kiumbe ambaye ako pale tu kukidhiwa mahitaji yake ya kimapenzi na mwanamume. Katika ubeti wa pili wasanii wanasimulia kuwa John anapendwa sana na watu wa jinsia moja, ya kike. Aidha, wanaeleza kuwa wanampenda hata kuliko chakula na wengine wakimkosa ndani ya nyumba wananuna. Isitoshe, wanasimulia kuwa, wengi wanavaa vizuri ili wampendeze 'John' na idadi kubwa yao wanapenda akitapika, yaani akimwaga 'kinywaji' kinachorejelea shahawa. Katika ubeti wa tatu, wasanii wanamsawiri mwanamke kama kiumbe anayefaa kwenda kwa mwanamume apewe shahawa tu. Sehemu yake ya siri inarejelewa kama chombo cha kumwagiwa vitu majimaji. Katika mstari wa mwisho wa ubetihuu, wanaimba:

**Mf 77**

*Ukija na container*
*John atakupa kinywaji.*

(Kutoka: *Nampenda John*. Wasanii: Wakimbizi)

Mwananmke katika wimbo huu amedhalilishwa kwa kusawiriwa kama kiumbe asiyeweza kufanya chochote bila kumwona mwanamume karibu naye. Wasanii wanaeleza kuwa John akienda mwezini, maskini kwa matajiri humngojea chini

wakijiuliza atarudi lini? Kwa kufanya hivi, wasanii wanapinga na kubatilisha simulizi kuu kuwa, ni wanaume pekee ambao wamo mbioni kuwafuata wanawake. Wasanii walitumia mbinu ya tashhisi kwa ufanisi mkubwa kuwasilisha habari zinazohusu ngono, mahitaji ya kibayolojia na sehemu za siri.

Jamii nyingi zenye misingi ya kuumeni zimemkuza mtoto wa kiume kwa namna inayomfanya ajihisi na kuonekana shujaa hata pale ambapo maisha yake yamo hatarini. Kukuzwa huku kumemfanya aamini kuwa matendo fulani, licha ya kuwa hatari ni lazima yatekelezwe na mwanaume. Mathalan, katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu wa *Nampenda John* msanii anayeimba ubeti husika ambaye ni Dokta Mark anashangaa kwamba licha ya 'John' kuwaambukiza wengi magonjwa na kuwasababishia madhara, bado anapendwa na kusifiwa kuwa ni mtu mzuri, yaani 'mtu poa.' Maoni yangu ni kwamba magonjwa yanayozungumziwa hapa ni yale ya zinaa ukiwemo UKIMWI. Katika mstari wa mwisho wa ubeti wa kwanza, anamkweza mwanamume kwa kusema:

**Mf 78**

> *Nyumba zote mtakwenda lakini John ndio boss.*
>
> (Kutoka: *Nampenda John*. Wasanii: Wakimbizi)

Maoni yangu ambayo yanaafikiana na ya Sambai (2014) ni kwamba, mwanamume, kutokana na alivyokuzwa na jamii anataka kutambuliwa kuwa mkuu wa nyumba na kushiriki ngono bila kinga hata na mkewe licha ya kujua fika kuwa ana virusi. Wengine hukataa kwenda kupimwa kwani kwao hicho ni kitendo cha uoga na kisichopaswa kutekelezwa na mwanamume. Tabia kama hizi za "John" ndizo zinazorutubisha kuenea kwa virusi vya VVU/UKIMWI katika jamii.

Katika wimbo *Si lazima*, maoni yangu, ambayo yaafikiana na ya wanabaadausasa ni kwamba, kinyume na ilivyo ada, mwanamke ndiye anayemshawishi mwanamume wacheze ngono. Ingawa mwanamume anasisitiza kwamba si lazima wafanye mapenzi, na kwamba yuataka kulala, mwishowe tunamwona akivuliwa shati na mwanamke. Yanayofuata ni kwamba anakubali kuwa amepata majaribu makubwa na kwamba hana bahati. Kwa hivyo kitendo cha ngono kwa muktadha wa wimbo huu unaweza kuanzishwa na mwanamke. Hii basi ni simulizi ndogo inayopinga simulizi kuu kuhusu suala la ngono na jinsia.

**Mf 79**

*Hii movie tunacheki manze ikiisha*
*Nataka kugusa lakini jo sitaki*
*Nataka kulala jo huku ushanivua shati*
*Temptation kibao jo sina bahati*

(Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P- Unit)

Dhana kwamba mwanamume anafaa kutekeleza kitendo cha ngono ili kudhihirisha ubabedume inapingwa katika wimbo *Nyambiz*i. Kwa mujibu wa wimbo huu, mwanamke hatulii tu na kukipokea kitendo hicho bali yeye ndiye mtendaji. Mathalan, ingawa Nyambizi alikuwa jirimu la mwanamke aliyemshinda kijana Dully kwa kimo, aliweza kufanya kitendo hicho kwa urahisi. Hii ndiyo maana ya msanii kuimba:

**Mf 80**

*Jimama kote anacheza, hadi sodoma.*
*Japo kanimeza*
*Lakini mchezo anauweza*
*Na sijui wapi mchezo huu aliupokeza.*
*Sababu macho anafumba na kiuno anakilegeza.*

(Kutoka: *Nyambizi*. Msanii:Abdikadir Ibrahim)

Kwa hivyo, katika kukabiliana na janga la UKIMWI, ni muhimu kushughulikia suala la jinsia hasa kutatua tofautizilizopo na ambazo zinaweza kuelekeza lawama kwa

jinsia moja ilhali suala zima la UKIMWI kwa kiwango kikubwa linahusiana na ngono ambayo huhusisha watu wa jinsia zote.

### 6.4 Nyimbo na Malalamishi

Malalamishi ni matamko anayoyatoa mtu kuonyesha hisia za kudhulumiwa au kuonewa. Malalamishi huweza kutolewa pia pale mtu anapojutia kitendo alichokitenda na kilichomletea madhara; kitendo ambacho kwa maoni ya mlalamishi, angeepukana nacho. Isitoshe binadamu hulalamika anapokabiliwa na jambo linalokuwa nzito kwake kulitatua.

Tangu kuibuka kwa janga la ukimwi, wasanii wa nyimbo za muziki wameibuka na nyimbo zinazobainisha udhaifu wa binadamu katika kukabiliana nalo. Nyimbo hizi kwa kawaida humsawiri binadamu anayeteta juu ya ubaya wa ugonjwa wa UKIMWI. Pia humsawiri binadamu anayeshindwa kujitanzua kutokana na mtego wa ugonjwa huu hasa ikizingatiwa kwamba UKIMWI unafangamanishwa na mapenzi na hasa kitendo cha ngono ambacho ndicho kitovu cha kuendeleza kizazi cha binadamu. Malalamishi yanayobainika katika nyimbo nilizochanganua yanahusiana na VVU/UKIMWI kwa njia moja au nyingine.

#### 6.4.1 Malalamishi juu Ubaya wa UKIMWI

Princess Jully katika wimbo wake *Dunia mbaya*, analalamika juu UKIMWI ambao umewaua watu wa jamii yake. Katika muktadha wa wimbo huu, dunia imetumiwa kama jazanda kumaanisha UKIMWI ambao umeenea dunia kote.

Kama sehemu ya malalamishi yake,anataja majina ya watu waliokufakutokana na UKIMWI.Anauliza wako wapi watu wa Homabay kama vile Aleni, Ochieng, Hosea,Aran, Agwambo, Steve, Obula Majenda na Agina. Isitoshe, katika ubeti wa pili, anauliza yuko wapi Asam kutoka Koyugi, Ohula aliyekuwa polisi mzuri,

Onyango, Billy, Tom, Okoyo, Otieno na Ogweno. Mwishoni mwa ubeti huu wa pili msanii anawaomba wasikilizaji wake waache raha la sivyo watakufa kifo kibaya; kifo kama cha mbwa. Kutokana na maelezo haya, waliotajwa walikufa kwa sababu ya kufuata raha.

**Mf 81**

Wapi Onyango Billy? Wapi Onyango Billy?
Ni Tom yuko wapi?
Wapi wa Mombasa?
Wapi wa Mombasa?
Okoyo yuko wapi? Okoyo yuko wapi?
Ohula yuko wapi? Ohula yuko wapi? Yuko

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Katika wimbo *Nimeupata vipi?*, msanii Faddy Daddy analalamikia hai yake ya kiafya iiydhoofika; hali iliyosababishwa na UKIMWI, ugonjwa ambao hajui aliupata vipi. Kwake yeye jinsi ilivyo kwa wanajamii wengi, njia ya pekee ya kuambukizwa Virusi Vya UKIMWI ni kupitia matendo ya uasherati ambayo hajawahi kuyashiriki. Analalamika kuwa anaumia, analia, anawaza na kufikiria.

Mbali na malalamiko ya msanii, kuna malalamiko ya nduguze wadogo. Katika ubeti wa saba, wao wanamlalamikia Faddy Daddy kwa nini anazidi kukonda, mwili mzima kujaa upele na kushika tama kila wakati. Isitoshe wanalalamika kuwa, ikiwa hali yake itaendelea kuwa hivyo basi itakuwa vyema wampeleke kwao Tanga. Kauli zao zinaonyesha kushindwa kwao kukabiliana na hali hii iliyosababishwa na UKIMWI na hivyo kutamauka.

**Mf 82**

Wadogo ndugu zangu wananiuliza
Mbona Faddy Daddy unazidi konda?
Mwili mzima upele umejaa
Kila wakati unashika tama
Kama hivyo twende zetu Tanga

(Kutoka: *Nimeupata Vipi ?*. Msanii: Faddy Daddy)

Wimbo *Starehe* unabainisha malalamishi na majuto ya kijana aliyeathiriwa na Virusi Vya UKIMWI. Malalamishi haya yanabainika katika beti mbili za kwanza. Mathalani, katika ubeti wa kwanza, mwathiriwa anateta kwamba, amelala kitandani na kupona tena kwake hakuwezekani. Anawaaga wenzake wote wa ghetto. Msimulizi anakiri kwamba starehe alizozipapia ndizo zilizomweka mashakani au matatani.

**Mf 83**

Kwaherini, kwaherini, kwaherini
Masela wangu ndugu zangu wote wa gheto buriani
Kwaherini kwaherini kwaheini Nagongo na Jitauni kwaherini
Watanzania kwaherini,sasa naaga

(Kutoka: *Starehe*. Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Starehe alizozifanyia papara msimulizi zinabainika wazi katika ubeti wa pili anaposema kuwa alibadili wanawake akienda kwa huyu akirudia yule. Kwa mfano anasema kuwa, saa saba ilipotimia, alikuwa ameachana na Jacky na kukutana na Salama. Saa kumi na mbili ana miadi na wanawake wengine wawili mbali na Lily ambaye amempangia saa mbili za jioni. Mwishowe aliwaacha wasichana akashiriki ngono na wanawake wazee. Anasema:

**Mf 84**

*Starehe nilizifania papara*
*Nilibadili mademu kama vidaladala*
*Nikimpenda hiki nikirudie lile*
*Nilitamani starehe zote nizitawale*
*Ubaya ni kwamba condom sikuitambua*
*Idadi ya wanawake ikawa lukulu*
*Wengine nikawa siwakumbuki.*

(Kutoka: *Starehe.* Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Isitoshe, msimulizi anapofika kwa dakitari anaendeleza malalmishi yake kwake. Malalamishi haya yanabainika katika ubeti wa nne na wa tano. Mathalani analalamika kwamba dalili zinaonyesha kwamba ameathirika na kilichobakia ni kifo.

Analalamikia namna alivyokonda, kukohoa, kutapika mara sitini na mbili kwa wiki na nywele kunyonyoka. Anahitimisha malalamishi yake kwa kusema hizo zote zilikuwa dalili za umeme.

Mintaarafu ya ubeti huo hapo juu, ni wazi kwamba msimulizi analalamika juu ya UKIMWI. Ugonjwa huu aliupata kwa kufuata starehe na kushiriki ngono na wanawake wengi bila kutumia kinga. Katika wimbo huu, istiara zinazorejelea VVU/UKIMWI ni pamoja na moto na umeme. Wasanii wanaimba:

**Mf 85**

*Kumbe nilikuwa ninakimbilia moto*
*Hizi zote ni dalili za umeme*

(Kutoka: *Starehe.* Wasanii: Ferooz & Prof. Jay)

Katika wimbo *List ya mazishi*, marafikize Eliza aliyeambukizwa Virusi Vya UKIMWI ndio wanaolalamika. Wanalalamikia kufukuzwa na Pokale, mamake Eliza walipokuwa wamemtembelea kumjulia hali baada ya kuugua na kujifungia ndani asitake watu kujua. Pokale naye analalamika kuwa wao ndio wanaomuua mwanawe. Isitoshe, rafikize Eliza wanalalamikia kufurushwa na muuguzi walipoenda hospitalini kumtembelea Eliza. Malalamishi hayo yanabainika kwenye mfano ufuatao:

**Mf 86**

Mama Eliza: Tokeni hapa. Nyinyi ndo mnamuua mwanangu.

| **Kiingereza** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Nurse: You are not allowed here.* | *Muuguzi: Hamtakikani hapa* |

(Kutoka: *List ya Mazishi*. Wasanii: Mchafuzi & Elyen)

Msanii Joel Kimetto katika wimbo wake *Kichigili* (Yachunguzwa) analalamika juu ya UKIMWI na madhara yake. Mathalani, analinganisha maafa yanayosabishwa na

UKIMWI na maafa yaliyosababishwa na ugonjwa wa zinaa unaozungumziwa katika Bibilia kitabu cha Hesabu sura ya ishirini na tano mstari wa kwanza na kuendelea (Hesabu 25:1-). Kulingana na maandishi haya, ugonjwa huo uliwaua watu maelfu kwa maelfu. Afueni ilipatikana tu baada ya Phineas kuwafuma mkuki na kuwaua mwanamume na mwanamke waliohusika katika kueneza ugonjwa huu. Walifumwa mkuki wakiwa katika kitendo cha ngono. UKIMWI nao umewauwa maelfu.

Malalamishi mengine yanayojitokeza katika wimbo huu ni kwamba, UKIMWI umewafanya wanajamii kutofurahia maisha ya ndoa. Akitumia istiara ya 'siku' msanii alalamika kuwa siku hizi ni mbaya au ni hatari kwani watu wanahudhuria sherehe ya harusi ambapo maharusi wanafunga ndoa na muda si muda watu wanaenda kuhudhuria mazishi yao. Vifo kama hivi hutokea hasa ikiwa maharusi hawakuwa wamejipima ili kujua hali zao; ujumbe ambao ni kiini cha wimbo huu. Msanii anaimba:

**Mf 87**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Yaach betusiechu wee* | *Hizi siku ni mbaya/hatari wee.* |
| *Kiguure harusi* | *Harusi yaandaliwa* |
| *Ak ne matianit wee* | *Na muda si muda weee* |
| *Keeba funeral* | *Mazishi yahudhuriwa.* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto)

Katika wimbo Rat Torosta (Funga Nepi), Joel Kimetto analalamika juu ya athari za VVU/UKIMWI kwa wanajamii. Msanii ametumia istiara za nchi, mifugo na wanyama ili kuwasilisha malalamishi kuhusu UKIMWI na athari zake. Katika ubeti wa kwanza, msanii anatuchorea picha ya jinsi maisha yalivyokuwa kabla ya majilio ya UKIMWI. Anaeleza kwamba, wakati nchi bado ilikuwa pana, ng'ombe walikuwa wanakula nyasi popote.

**Mf 88**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Ye kiin kobaraa emeet* | *wakati nchi ilikuwa pana* |
| *Kiogeete tuga kolenge* | *Ng'ombe walikula nyasi popote.* |
| *Ko ra kominginiit emeet* | *Kwa kuwa siku hizi nchi imekuwa ndogo* |
| *Ko kooba biik zero grazing* | *Watu wamegukia malisho ndani ya nyumba.* |
| *Ko ra kogoyaiit emeet* | *Siku hizi nchi imeharibika* |
| *Kogogeer tiondo bereekwek* | *Mnyama ametamalaki malishoni* |
| *Kole boiyon rat torosta* | *Mzee kasema funga nepi.* |

(Kutoka: *Rat Torosta*. Msanii: Joel Kimetto)

Katika ubeti wa pili, msanii analalamika kuwa, kwa sababu nchi imekuwa ndogo, watu wamegeukia mbinu ya kuwalisha ng'ombe ndani ya vyumba maalum vya malisho. Aidha, katika ubeti wa tatu analalamika kuwa, nchi imeharibika au imekuwa mbaya siku hizi kwani mnyama ametamalaki malishoni.

Mintaarafu ya masimulizi haya, nchi kuwa pana kunamaanisha wakati kabla ya kuibuka kwa ugonjwa wa UKIMWI. Ng'ombe ni istiara ya binadamu ambaye kabla ya kuibuka kwa UKIMWI angefanya mapenzi na yeyote yule bila kuhofia maisha yake na ya wenzie.

Nchi kuwa ndogo kunamaanisha wakati wa sasa; wakati kuna UKIMWI ambapo watu wanahimizwa kuwa na mpenzi mmoja anayemwamini; hali inayorejelewa na ufugaji wa ng'ombe wa kutotoka nje. Katika jamii ya msanii, neno 'tiondo' lenye maana ya mnyama hutumiwa kiistiara kurejelea UKIMWI. Mnyama aliyetamalaki malishoni basi ni Virusi Vya UKIMWI. Kitendo cha kufunga nepi ni kujizuia au kushiriki ngono kwa kutumia kinga.

### 6.4.2 Malalamishi kuhusu Ulevi wa Pombe

Malalamiko ya msanii Paul Kurui katika wimbo wake *Mi Meet Tereet* (Kuna Kifo Mtungini) yanahusu ulevi wa pombe miongoni mwa wanajamii wake. Ni kupitia kwa

ulevi ambapo Virusi Vya UKIMWI vinaweza kuenezwa kwani mtu akilewa uwezo wake wa tafakuri hupungua na hivyo kuathiri vibaya maamuzi yake. Wengine hujasirishwa na kileo kufikia kiwango cha kutojali na hivyo kushiriki ngono bila kinga.

Msanii alalamika kuwa, kifo kinachofungamanishwa na ulevi au kifo kilichomo mtungini ndicho kinawamaliza watu wa jamii yake ya Wakalenjin. Analalamika kuwa mtu huenda kunywa hadi kupoteza fahamu asijue chochote. Katika hali kama hii mtu anaweza kuleta ugonjwa nyumbani; ugonjwa unaokuja kusababisha kifo cha watu wa jamii au familia yake. Msanii ametaja ugonjwa huu kama UKIMWI au 'Kipkenda Bor' yaani kinachokula mwili pole pole jinsi watu wa jamii yake wanavyourejelea ugonjwa huu kiistiari.

Kulingana na wanakikundi waliousikiza na kuutazama wimbo huu, msanii anapendekeza kuwa ili vita dhidi ya UKIMWI vifanikiwe, ni muhimu vianze kwa kupiga vita visababishi vielekezi kama vile ulevi wa pombe. Hii ndiyo maana ya mwimbaji kuimba:

**Mf 89**

| **Kalenjin** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Ara ingoro loeet keetui?* | *Kwa hivyo wapi mtungi tuuvunje?* |
| *Ara ingoro sageet keetui?* | *Kwa hivyo wapi kata tuivunje?* |
| *Ingoro mesengeswet keebel?* | *Wapi mwanzi tuuchome?* |

(Kutoka: Mi Meet Tereet. Msanii: Paul Kurui)

Vyombo vitatu vinavyotajwa katika wimbo huu vinafungamanishwa na pombe pamoja na ulevi.*Loeet au tereet* ni mtungi wa kiasili uilofinyangwa kwa udongo na hutumiwa kupikia na kuhifadhi pombe.*Sageet* ni kibuyu kinachotumiwa kuchotea pombe kutoka mtungini. *Mesengeswet* na nacho ni chombo cha kuhifadhia mirija ya

kunywea pombe. Hetengenezwa kwa kutumia mwanzi. Msanii anapopendekeza vyombo hivi vivunjwe na kuchomwa, kimsingi anawahimiza wanajamii wake waache ulevi na hatimaye wataepukana na janga la UKIMWI.

### 6.4.3 Malalamishi kuhusu tamaa

Katika wimbo *Miluma* (Tamaa), mwimbaji Chali analalamika juu ya tamaa. Akitumia mbinu za takriri na balagha, msanii anauliza tamaa ni nini? Analalamika kuwa inawaandama wanajamii. Katika beti tatu za kwanza, mwimbaji analalamika kuwa tamaa inawaandama na kuwaharibu hata walio kwenye ndoa pamoja na watoto. Kulingana na msanii, tamaa imevuruga mambo katika jamii. Wanaume kwawanawake wameharibika huku watoto na wazee wakipotoka. Msanii aimba hivi:

**Mf 90**

| **Dholuo** | **Kiswahili(TY)** |
|---|---|
| *Miluma to enang'o ?*<br>*Makata ng'at moseko nyombo*<br>*Miluma obaro ndasi* | *Tamaa ni nini?*<br>*Hata aliyeoa!*<br>*Tamaa inamwandama* |
| *Chali miluma to enang'o?*<br>*Makata ng'at moseko nyombo*<br>*Miluma oketho mon*<br>*Jodongo onjaore*<br>*Nyithindo okethore* | *Chali tamaa ni nini?*<br>*Hata aliyeoa!*<br>*Tamaa imewaharibu wanawake*<br>*Tamaa imewaharibu wanaume*<br>*Watoto wamepotoka* |
| *Miluma to enang'o?* | *Tamaa ni nini?* |
| *Jaduong' moti ong'ieo gari*<br>*Adhiambo okao pache*<br>*Omanyo mbas nyakware* | *Mzee amenunua gari*<br>*Akapumbazwa na Adhiambo*<br>*Anatafuta marika ya wajukuu* |

(Kutoka*: Miluma*. Msanii: Chali)

Ingawa msanii hajataja tamaa anayozungumzia ni ya nini katika beti tatu za kwanza, wanakikundi waliosikiza wimbo huu walikubali kwa kauli moja kuwa msanii anazungumzia tamaa ya mapenzi. Maoni yao yalipata mashiko kutokana na masimulizi katika ubeti wa nne. Masimulizi haya yanamhusu mzee ambaye baada ya

kununua gari alipumbazwa na msichana Adhiambo na akawa anawatafuta wasichana wadogo ambao wanastahili kuwa wajukuu wake. Huku ndiko kuharibika na kupotoka kwa wazee kunakozungumziwa na mwimbaji. Tamaa ya mapenzi ni njia mojawapo ambapo Virusi Vya UKIMWI vinaenezwa.

Musa Juma naye katika wimbo *Mayaka* (UKIMWI), analalamika juu ya UKIMWI; ugonjwa ambao anasema umekuwa balaa duniani kote. Msanii anaanza wimbo wake kwa kueleza kuwa, duniani kote UKIMWI ni balaa. Anaendelea kutaja miji na mataifa mbali ili kushereheshea  kuwa UKIMWI umeenea kote na hivyo kuwa balaa. Baadhi ya miji aliyoitaja ni Mombasa, Migori, Homabay, Bungoma na Dubai huku baadhi ya nchi zikiwa Kenya, Uganda na Marekani. Mathalani, katika ubeti wa kwanza mwimbaji anaimba:

**Mf 91**

| **Dholuo** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Piny te*<br>*Ayaki chalo kidi*<br>*Mombasa Kenya*<br>*Ayaki chalo kidi*<br>*Migori Kenya*<br>*Ayaki chalo kidi* | *Duniani kote*<br>*UKIMWI ni balaa*<br>*Mombasa Kenya*<br>*UKIMWI ni balaa*<br>*Migori Kenya*<br>*UKIMWI ni balaa* |

(Kutoka: *Mayaka*. Msanii:Musa Juma)

Katika wimbo *UKIMWI Onego Jater* (UKIMWI Umemwua Mrithi wa Mke) msanii Atomi Sifa analalamikia namna UKIMWI ulivyosababisha madhara katika jamii. Mathalani, analalamika kuwa, UKIMWI umezifanya boma kuwa mahame, umewaangamiza wazazi na kuwafanya watoto wawe mayatima. Aidha analalamika kuwa, UKIMWI unamaliza vizazi. Katika ubeti wa tatu anaeleza kuwa UKIMWI unaua watu Sudan na Kenya na katika ubeti wa nne, anatangaza kutamauka kwake. Kwa mfano ubeti wa kwanza inaenda hivi:

**Mf 92**

| **DhoLuo** | **Kiswahili(TY)** |
| --- | --- |
| *Wololo! Wololo! Wolo!* | *Jamani! Jamani! Jamani!* |
| *Dala dong gunda* | *Boma labaki mahame* |
| *Atomi ayhago piny* | *Atomi nasikitikia dunia* |
| *Ukimwi tieko yawa* | *UKIMWI unatuangamiza* |
| *Ka kigo odonjo epacho* | *Ukiambukizwa ukimwi* |
| *Dala dong gunda* | *Boma labaki mahame.* |

(Kutoka: *UKIMWI Onegi Jater*. Msanii: Atomi Sifa)

### 6.5 Simulizi za Tahadhari

Tangu kuibuka kwa ugonjwa wa UKIMWI nchini Kenya, wasanii waimbaji wamekuwa wakizitunga nyimbo zilizo na jumbe za kuwatahadharisha wanajamii dhidi ya VVU/UKIMWI hasa ikizingatiwa kwamba, ugonjwa huu mpaka sasa hauna tiba kamilifu.

Nyimbo nilizozichanganua zinawasilisha jumbe zinazotoa tahadhari kwa wanajamii waepukane na tabia zinazofungamana na vipengele vielekezi vinavyochangia kuenea kwa VVU kama vile ulevi, tamaa, starehe na kadhalika. Aidha kuna tahadhari kuhusu hatari ya ngono bila kinga au ngono za kiholela. Pamoja na hayo, kuna jumbe za tahadhari kuhusu VVU/UKIMWI na athari zake. Baadhi ya vipengele hivi huwasilishwa kupitia kwa vyombo vya habari na makongamano kama ilivyojadiliwa katika sura ya pili ya tasnifu hii. Kwa kufanya hivyo, nyimbo zinachangia mbinu hizo zilizozoeleka.

#### 6.5.1 Tahadhari kuhusu Ulevi

Needle na wenzake (2006), Deveau na wenzake (2006), wanabainisha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ulevi na maenezi ya virusi vya UKIMWI. Vileo vinavyohusika mintaarafu ya wataalamu hawa ni pamoja na bangi, kokeini, miraa na pombe. Miktadha ya kijamii inayohusika na uuzaji na matumizi ya vileo hivi kama

vile vilabu vya pombe huchangia pakubwa katika kueneza maambukizi ya VVU/UKIMWI. Maoni yangu ni kwamba, hili ndilo lilomfanya msanii Princess Jully katika wimbo wake *Dunia Mbaya*, kawatadharisha wanaofanya kazi kwenye vilabu vya pombe watumie kondomu wanaposhiriki ngono kwa sababu wako katika hatari ya kuambukizwa. Akitumia mbinu ya takriri mstari anawahimiza wasisahau kamwe kuitumia. Ujumbe huu unapatikana kupitia ubeti wa tano kama ifuatavyo:

**Mf 93**

| **Sheng** | **Kiswahili sanifu(TY)** |
|---|---|
| *Ma maid wa bar, tumia condom* | *Watumishi wa baa, tumia kondomu* |
| *Men wa bar, tumia Condom* | *Wanaume wa baa, tumia kondomu* |
| *Waiter wa bar, tumia condom* | *Mhudumu wa baa, tumia kondomu* |
| *Usisahau, tumia condom* | *Usisahau, tumia kondomu* |

(Kutoka: *Dunia Mbaya*. Msanii: Princess Jully)

Dully Sykes naye katika wimbo wake *Nyambizi*anatudokezea miktadha ya vilabuni ambapo wanajamii wanaume kwa wanawake hujumuika kwa ajili ya starehe za pombe na ngono. Vilabu viwili vinavyotajwa katika wimbo huu ni Upto date Empire na FM club Kinondoni. Washiriki katika kikundi kimoja teule walieleza kuwa, majina ya vilabu hivi yanabeba maana zinazohusiana na mapenzi na ngono. Matahalani, mshiriki mmoja alikuwa na haya ya kusema kuhusu siku ya Valentine na kilabu cha Upto date Empire:

**Mf 94**

**Mshr 1**:

*Valentine ni siku ya wapendanao na kwa kawaida huwa mwanaume kwa mwanamke. Ni siku ya kuonyeshana mapenzi kwa kununuliana zawadi ikiwemo pombe. Upto date Empire ni mahali pa kuwekeana miadi ya mapenzi.*

Mshiriki mwingine alieleza kuwa FM katika jina FM Club ni ufupisho wa *Female* na *Male*. Kauli yake ilikuwa :

**Mf 95**

**Mshr 2:**

*Nafikiri F inasimamia* ***Female*** *yaani Mwanamke au Msichana na M inasimamia* ***Male*** *Mwanamume au Mvulana. Kwa hivyo hiki ni kilabu maalum kwa wanawake na wanaume wanaopendana na kupenda raha.*

Hali hii ni sawa na ile inayosawiriwa katika wimbo *Kamata Dame*(Tazama kiambatisho cha 3).Ni mazingira ya kilabu cha pombe ambapo wahusika wa kiume kwa wa kike wanakunywa na kucheza dansi kila mwanamume akiwa na mwanamume. Waimbaji wanawahimiza wanaume wapate wenzi sio tu wa kucheza dansi bali pia kucheza ngono. Maoni yangu ni kwamba, vilabu kama hivi huchangia kuenea kwa VVU/ UKIMWI hasa ikizingatiwa kwamba wahusika huishia kulewa na kushiriki ngono za kiholela au bila kinga. Hali hii inadhihirika katika simulizi zifuatazo kwenye wimbo huu:

**Mf 96**

*Jimama kote anacheza, hadi sodoma*
*Usiku huo ilikuwa bila zana. Ngoma dry, ajali kazini*

(Kutoka: *Nyambizi*. Msanii: Abdikadir Ibrahim)

Katika wimbo *Mi Meet Tereet* (Kuna Kifo Mtungini), msanii Paul Kurui anawasilisha ujumbe wa tahadhari kwa wanajamii wake wa Kikalenjin kuhusu uwezekano wa kuambukizwa na kuwaambukiza wengine Virusi Vya UKIMWI kupitia kwa njia ya ulevi. Msanii anawaonya wasikilizaji wake wautoroke ulevi. Anaeleza kuwa, watu wanapoenda kunywa pombe (komen), baada ya kulewa wanarudi nyumbani wakileta ugonjwa mbaya (koroot) watakaotumia kuwaua wanajamii wao. Kitendo cha kuleta au kubeba ugonjwa ni kuambukizwa VVU huku kitendo cha kuua kikimaanisha mtu

mlevi kuwaambukiza wengine hasa mke wake. Mwishoni mwa ubeti wa mwisho, msanii anawahimiza wanajamii wake wautoroke ulevi. Ubeti wa mwisho unaghanwa hivi:

**Mf 97**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Okas amwaiyuok wee biikyo* | *Sikizeni niwaambie enyi watu wetu* |
| *Iwendi chito, iwe iee* | *Wee mtu unaenda, unaenda kunywa pombe* |
| *Kot Kotoor maingen kiy* | *Hadi ukakosa fahamu* |
| *Kor inyone gaa ko meikertoi* | *Utakapokuja nyumbani huoni* |
| *Iloou koroot konyo gaa* | *Ukaleta ugonjwa nyumbani* |

(Kutoka: *Mi Meet Tereet*. Msanii: Paul Kurui)

Wimbo mwingine unaotoa tahadhari dhidi ya ulevi ni *Tang'ne Dendi* (Chunga mwili) wake Ajoji Dume. Katika ubeti wa kwanza, msanii anarejelea ulevi na ukware kama ibilisi. Baada ya hapo, anawatahadharisha wasikilizaji wake dhidi ya kuandama huo ulevi na ukware.

**Mf 98**

| **DhoLuo** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Berna berna berna* | *Navutiwa navutiwa navutiwa* |
| *Jochiende mag chode* | *Ibilisi wa ukware* |
| *Uwena mamna* | *Msimwandame muhibu wangu* |
| *Jochiende mag mer* | *Ibilisi wa ulevi* |
| *Uwena mamna* | *Msimwandame muhibu wangu* |
| *Wadagi adagi mos* | *Tuishi tu kwa amani* |
| *Orita seche te* | *Alinde nyakati zote* |

(Kutoka: *Tang'ne Dendi*. Msanii: Ajoji Dume)

Daniel Saning'o ana ujumbe wa tahadhari kwa Wamaasai wanaopenda kutembelea vilabu na kunywa pombe. Anawatahadharisha wawe waangalivu wasidungwe na nyuki (*Enkotoroki*). Kama tulivyoeleza kwingineko katika tasnifu hii, nyuki ametumiwa kama istiara ya mwanamke.

### 6.5.2 Tahadhari kuhusu Tamaa, Starehe na Anasa

Tamaa ni tabia ya binadamu kutaka kitu kwa vyovyote vile. Ni utashi uliokithiri na unaoelekea kwenye ulafi; ulafi ambapo yule aliye na tamaa huwanyima wengine nao wasipate. Mtu anaweza kuwa na tamaa ya pesa, cheo, mapenzi na kadhalika.

Aghalabu, binadamu, hutamani vitu na hali anazofikiria kuwa zitamletea furaha lakini tamaa iliyokithiri humletea majuto na maangamizi. Na ndiposa Waswahili wakasema, "Tamaa mbele mauti nyuma".

Kwa mfano, tamaa ya mapenzi iliyokithiri inadhihirika katika nyimbo nne kati ya nyimbo ishirini na tatu nilizochanganua. Wimbo *Miluma* (Tamaa) ulioimbwa na msanii Chali unawaonya wasilikizaji wake waache tamaa iliyokithiri ya mapenzi. Hii ni kwa sababu tamaa huwapotosha watu na kusababisha uharibifu kwa wanajamii. Tamaa ya aina hii huwaharibu wake na waume katika ndoa, huwapotosha watoto na hata wakongwe kama vile nyanya. Isitoshe, tamaa iliyozidi huwafanya wazee wawafuate wasichana marika ya wajukuu ili wafanye mapenzi almuradi tu wana hela za kulipia ngono. Hali hii inadhihirika zaidi katika ubeti wa nne. Mababa sukari kama mzee anayetajwa katika ubeti huo huchangia katika kusambaza VVU.

Katika wimbo *Starehe* ulioimbwa na Ferooz na Prof. Jay, ujumbe wa tahadhari juu ya tamaa ya mapenzi unatolewa kwa vijana. Katika wimbo huu, kijana aliyemtembelea dakitari kutaka kuthibitishiwa hali yake ya VVU/ UKIMWI anakiri kuwa hali yake iliathirika kutokana na kushiriki ngono na wanawake aliowabadilisha kama vidaladala. Mara amekuwa na Jacky,sasa ako naSalama,saa kumi na mbili atakuwa na wengine wawili naLilyatamtamatishia siku mwendo wa saa mbili**.** Yaliyompata huyu kijana kwa sababu ya tamaa yanaweza kumpata mtu yeyote asipotahadhari. Hili ndilo onyo linalotolewa na msanii kwao.

Longombas nao katika wimbo *Vuta Pumz* wanawatahadharisha vijana dhidi ya tamaa ya kutaka kushriki ngono na kila mwanamke mpita njia. Tabia kama hii pamoja na matokeo yake yanadhihirishwa na wasanii katika ubeti wa pili. Matokeo tamaa ya kudunga kila **shimo, kutamani kila paja, kila kifua** na **kila tako** ni mauti. Sehemu za mwili zilizotajwa katika ubeti huu zinamrejelea mwanamke, kwani shimo ni sehemu yake ya uzazi, paja ni sehemu ya mwili baina ya goti na kiuno, kifua hurejelea matiti na matako ni sehemu ya nyuma au makalio. Ubeti huo wa pili una masimulizi kama ifuatavyo:

**Mf 99**

*Kila shimo unaona unadunga*
*Paja asione tu, ashainua*
*Kifua kisipite tu, ashajigonga*
*Tako lisipite tu, mate yashamtoka*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Sehemu za mwili zilizotajwa katika ubeti huu zinafungamanishwa na ngono na huwavutia wanaume. Vijana wanatahadharishwa dhidi ya kutamani kitendo cha ngono kupita kiasi kwani tamaa kama hiyo inaweza kuua mtu asipochunga. Longombas wanaimba:

**Mf 100**

*Na mjinga asiyejuwa kujichunga*
*Hebu jichunge kijana utakuja kufa*
*Tukuzike Langata.*

(Kutoka: *Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Wimbo wa nne unaodhihirisha tamaa ya mapenzi ingawa bila kudokeza matokeo yake ni *Wee Kamu* ulioimbwa na wasanii Nonini na Jua Cali. Katika ubeti wa pili, mhusika anayemgonjea mpenzi wake awasili ili wafanye mapenzi anatubainishia vitendo vinavyoonyesha kuwa ni mwenye tamaa ya ngono. Kwake ameweka tembe

za Viagra zinazoaminika kuongeza nguvu za kiume kwa kusisimua misuli. Aidha, katika ubeti wa tatu mhusika anamwambia mpenzi wake wa kike asimtembelee peke yake bali aandamane na marafikize wa kike ili acheze ngono ya wenzi wengi nao kwa hali ya kushindana.

Maoni yangu ni kwamba, mtu anayetumia dawa za kuongeza nguvu za kiume ili kurefusha kitendo cha ngono ni mtu mwenye tamaa. Vivyo hivyo na anayeshiriki ngono na wenzi wengi. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa ni mtu mwenye tamaa; asiyetosheka na mwanamke mmoja. Ingawa msanii hakudokeza matokeo ya tamaa ya aina hii, maoni yangu ni kwamba, matokeo yake ni mauti kutokana na maambukizi ya VVU na shinikizo la damu linalosababishwa na dawa kama za Viagra. Wengi wamekufa kwa jinsi hii.

### 6.5.3 Tahadhari kuhusu Ngono bila Kinga au ya Kiholela

Kulingana na Ripoti ya KAIS (2012) asilimia kubwa ya maambukizi ya virusi hutokea kupitia kwa ngono kati ya mwanamume na mwanamke. Hali hii inakuwa mbaya zaidi wahusika wanapokosa kuzingatia ngono salama kwa kutotumia kinga na kushiriki ngono na wenzi wengi. Nyimbo kumi na moja kati ya nyimbo ishirini na tatu nilizozichanganua zinawasilisha ujumbe kuhusu matumizi ya kinga na tabia zinazoweza kupunguza kueneakwa VVU. Nyimbo tatu kati ya nyimbo hizo zinahimiza matumizi ya kondomu kwa kutumia lugha ya moja kwa moja ambapo neno "condom" linatajwa moja kwa moja. Nyimbo hizo ni *Dunia mbaya*, *Starehe* na *Wee Kamu*.

Katika beti za nne, tano, na sita za wimbo wake *Dunia Mbaya* Princess Jully anawahimiza wasikilizaji wake watumie kondomu kila mahali na kila wakati wanaposhiriki kitendo cha ngono. Hii ni kwa sababu UKIMWI upo kila mahali.

Mathalan, anawashauri wanaume wakienda Nairobi, Kisumu na Marekani watumie kondomu wanapopata warembo. Warembo nao wanashauriwa wafanye vivyo hivyo wanapopata *wadosi*. Hadhira aliyoilenga msanii kuiwasilishia ujumbe huu unawajumuisha watoto, wafanya kazi mbalimbali, wanawake kwa wanaume, wazee kwa vijana tena wa matabaka mbalimbali. Umuhimu wa Kondomu na matumizi yake unasisitizwa na msanii. Hii ni kwa sababu ya takriri ya kauli "**Tumia condom".**

Ukweli ni kwamba kauli hii imerudiwa mara thelathini na tatu katika beti tatu za wimbo huu. Princess Jully katika wimbo huu ametambua wanajamii ambao awali walitengwa katika vita dhidi ya UKIMWI. Miongoni mwa wanajamii hao ni watoto, *wadosi* na akina *Sir* wanaofanya kazi za ofisi. Kwa kufanya hivi, wimbo wake unaafikiana na maoni ya wanaubaada usasa.

Katika wimbo *Merimella*, msanii anawatahadharisha wasikilizaji wake dhidi ya kupuuza matumizi ya kondomu kujikinga dhidi ya virusi vinavyosababisha UKIMWI. Anafanya hivyo kwa kueleza yaliyompata mhusika Merimella kutokana na mapuuza yake. Badala ya kutumia neno *condom*, msanii ametumia neno mipira.

Wasanii wa wimbo *Starehe* wanatoa onyo kwa wasikilizaji wao dhidi ya kupuuza matumizi ya kondomu kwa kufuata utamu wa ngono kwani wanaweza kuambukizwa VVU. Kijana aliyemtembelea dakitari baada ya kuonyesha dalili za UKIMWI anakiri kwamba, mbali na kushiriki ngono na wenzi wengi, hakuzingatia matumizi ya kondomu. Hii ni kwa sababu alikuwa na dhana potovu kwamba kondomu ingepunguza ladha au utamu wa ngono. Matokeo yake yalikuwa kuambukizwa VVU hali ambayo daktari anamthibitishia kuwa kweli.

Kuna nyimbo zilizozungumzia suala la kondomu na matumizi yake kwa njia isiyokuwa ya wazi wazi au ya moja kwa moja. Katika nyimbo hizi, wasanii wanatoa

maelezo kuhusu kondomu kiistiara au kimafumbo. Circuit na Jo-el katika wimbo wao *Juala* wanasisitiza matumizi ya kondomu ili kuepukana na maambukizi ya VVU na mauti au vifo vinavyosababishwa na UKIMWI. Wanawahimiza wasikilizaji wasicheze na maisha ilhali kondomu ni shilingi kumi tu. Wanasema hivi katika ubeti wa pili:

**Mf 101**

| **Sheng** | **Kiswahili Sanifu (TY)** |
|---|---|
| *Juala ni ashuu tu*<br>*Na bado mnacheza na maisha mandugu* | *Kondomu ni shilingi kumi tu*<br>*Na bado mnacheza na maisha ndugu zangu* |

(Kutoka: *Juala*. Wasanii: Circute & Jo-el)

Katika ubeti ulio hapa chini, wasanii wanatahadharisha wasikilizaji wao wawe na tafakuri kabla ya kushiriki ngono na mwanamke yeyote yule hata awe mrembo kiasi gani. Wanaimba hivi katika ubeti wa pili:

**Mf 102**

| **Sheng** | **Kiswahili Sanifu(TY)** |
|---|---|
| *Hata kama nyarere ni poa aje*<br>*Juala ndio wahitaji* | *Hata kama msichana ni mrembo aje*<br>*Kondomu ndiyo wahitaji* |

(Kutoka: *Juala*. Wasanii: Circute & Jo-el)

*Juala* ni neno la Kijaluo lenye maana ya mfuko wa nailoni au mpira unaotumiwa kubebea bidha kama vile mboga, maziwa, mafuta ya taa, nyanya na kadhalika. Katika muktadha wa wimbo huu, juala ni kondomu kwani ina sifa kama za mfuko husika na hutengenezwa kutokana na malighafi ile ile ya nailoni au mpira. Ashuu ni neno la mitaani lenye maana ya shilingi kumi. Katika muktadha wa wimbo huu, imetumiwa kuwasilisha tahadhari kwamba mtu hapaswi kufa kutokana na UKIMWI ilihali bei ya

kondomu inaweza kufikiwa. Katika jitihada za kupuguza kuenea kwa VVU, siku hizi kondomu zinatolewa bila malipo hususan katika vituo vya afya na kumbi za kijamii. Neno lingine ambalo wasanii wamelitumia badala ya ‘condom’ ni ‘protection’. Katika ubeti wa kwanza na wa pili, kauli kama vile:

**Mf 103**

| **Sheng** | **Kiswahili Sanifu(TY)** |
|---|---|
| *Tutumie protection to avoid the disease* | *Tutumie kinga tuepukane na ugonjwa* |
| *Tumia protection joo* | *Tumia kinga bwana* |
| *Ati you want it bila protection?* | *Ati unataka ngono bila kinga* |
| *Bila protection naringa* | *Bila kinga ninakataa* |
| *Bila juala usichape hizo vitu.* | *Bila kondomu usifanye ngono* |

(Kutoka:*Vuta Pumz*. Wasanii: Longombas)

Hizi ni kauli zinazorejelea kondomu na matumizi yake ili kujikinga dhidi ya kuambukizwa VVU.

### 6.5.4 Nyimbo na njia nyingine za kuepukana na UKIMWI

Nyimbo tano kati ya nyimbo ishirini zilizochanganuliwa zinaunga mkono njia nyingine za kitaaluma ambazo wanajamii wanahimizwa kuzizingatia ili kuepukana na UKIMWI. Mojawapo ya njia hizo ni kugunga au kusubiri, kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja au kutumia kondomu almaarufu ABC. Kulingana na kauli mbiu ya ABC, nyimbo hizi zinapendekeza wasikilizaji wazingatie A na B huku nyimbo zilizotangulia zikipendekeza kuzingatiwa kwa C.

Wimbo *Merimella* unapendekeza kuzingatiwa kwa A na C. Hii ni kwa sababu, msanii alimsharui mhusika kutoshiriki kabisa tendo la ngono. Msanii ametumia neno maarufu “kuchill” linalomaanisha kuwa na mpenzi mmoja wa kushiriki ngono naye. Hili lisipowezekana jinsi ilivyokuwa kwa Merimella, msanii anapendekeza wasikilizaji wake wazingatie C ambayo ni matumizi ya kondomu. Ckoniah anaimba hivi katika ubeti wa tano:

**Mf 104**

Kaambiwa uchilli, ukasema ni ndoto
Utumie mipira, ukasema si tamu

(Kutoka: Merimela. Msanii: Uncle Ckoniah)

Wasanii wa wimbo *Si Lazima*, wanawashauri wasikilizaji wao wawe na subira kuhusiana na suala la ngono. Katika wimbo huu, wasanii wanapendekeza uzingatiaji wa A kwa wasikilizaji wao. Ushauri huu unashadidiwa na kauli kama vile:

**Mf 105**

| **Sheng** | **Kiswahili Sanifu (TY)** |
|---|---|
| *Si lazima tu do.* | *Si lazima tufanye* |
| *Tunaeza enda home na tuchill tu* | *Tunaweza kwenda nyumbani na kugunga tu* |
| *Tunaeza enda home na tuchill tu do* | *Tunaweza kwenda nyumbani na tukaagunga tu* |
| *Tunaeza enda kejani tukachill tuu* | *Tunaweza kwenda chumbani na tukagunga tuu* |
| *Si eti kila saa ni kukuundress* | *Si eti kila wakati ni kukuvua nguo* |

(Kutoka: *Si Lazima*. Wasanii: P-Unit)

Katika wimbo *Yee beek che mi Tereng'ung* (Yanywe maji yaliyo Mtungini Mwako) hadhira inashauriwa kuzingatia B katika kauli mbiu ya ABC. Maana ya B ni kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja. Wanaolengwa hasa ni wanaume wanaoshauriwa kunywa maji kila mmoja kutoka kwenye mtungi wake. Pamoja na hayo, msanii anasisitiza kuwa, mke wa ndoa wa mtu si wa ushirika; si wa ukoo au wa marafiki ila ni wa mume wa ndoa peke yake.

Msanii ametumia sitiara ya mtungi kumwakilisha mwanamke huku kitendo cha kunywa maji kikirejelea kitendo cha mwanaume kufanya ngono. Pamoja na hayo, msanii anapinga matumizi ya kondomu. Anasema kwamba, ingawa watu wengine husema watavaa *'gumboot'* yaani kondomu, hiyo *'gumboot'* inaweza kukatika, maji yaliyo na '*kimitiat'*yaani kiroboto aweza kuingia. Ushauri wake ni kwamba kondomu haiwezi kutegemewa asilimia kwa mia kuzuia kuambukizwa VVU.

Katika wimbo wake wa *Rat Torosta* (Funga Nepi), Kimetto ana ujumbe kwa vijana.

Ujumbe huu ni wa kujizuia kushiriki ngono ili kuepukana na maambukizi ya VVU. Anatumia maigizo na picha za mifugo na vyombo vya upishi ili kuwasilisha habari kuhusu UKIMWI na ngono; habari ambazo hazingewasilishwa kwa kutumia lugha ya kawaida. Mathalani, akitumia maigizo kusisitiza ushauri wa kuwa na mpenzi mmoja, yeye na mwimbaji mwenzake wanaigiza namna kila mtu anavyopaswa kula kilichomo kwenye chombo chake. Kuhusu tabia ya kujizuia, mmoja wa waimbaji anavua koti lake na kulifunga kiunoni. Aidha, kwenye video hiyo tunaonyeshwa kondoo dume aliyefungiwa aina fulani ya ngozi ili kumzuia asiwapande kondoo jike.  Hata kama atafaulu kumpanda kondoo jike, shahawa hazitamfikia kwa kuwa zitazuiliwa na ngozi ile. Pamoja na hayo kauli kuhusu mtindo wa ufugaji wa ng'ombe mmoja nyumbani zinarejelea maadili kama vile kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja. Msanii ametumia vyombo na mifugo; vitu ambavyo vinapatikana na kueleweka katika muktadha wa jamii ya Kikalenjin.

Katika wimbo *Kichigili* (Yachunguzwa), msanii Kimetto anawashauri wasikilizaji wake hasa wale wanaochumbiana kuhusu umuhimu wa kupimwa ili wajue hali zao za VVU/ UKIMWI. Anasisitiza umuhimu wa kupimwa huku ili kuepukana na vifo vinavyotokea pindi tu watu wanapooana kutokana na kutojua hali zao. Msanii anawasilisha ujumbe huu kwa urahisi kwa kutuonyesha picha za wachumnba wawili kwenye kituo cha UUH. Pamoja na hayo, msanii ametumia simulizi kutoka kwa Biblia, simulizi ambazo zinaweza kuwasilisha habari kuhusu mapenzi na ngono kwa kutumia lugha isiyochukiza au kuaibisha.  Kimetto hakutumia mbinu hizo peke yake bali alitumia semi zinazoeleweka na zinazowavutia wasikilizaji wa Kikalenjin. Mathalani, '*kechigil*'na '*keoboi'* ni vitenzi vinavyomaanisha kuchunguza tena kwa makini, kwa kugeuza kitu kinachochunguzwa juu chini, kushoto kulia na katikati ili kuwa na uhakika wa kila sehemu yake.

Akiwatahadharisha wasikilizaji wake, hususan wanaochumbiana dhidi ya kukimbilia mapenzi na ngono, msanii ameteua semi za Kikalenjin ambazo zinavutia zinapotumiwa katika mazungumzo. Semi hizo ni pamoja na:

**Mf 106**

| **Kalenjin** | **Kiswahili (TY)** |
|---|---|
| *Ma kilabotyin* | *Si ya kukimbilia* |
| *Ma kiororyechin* | *Si ya kusepetukia* |
| *Ma kiobobtechin* | *Si ya kuikabili kiujinga au bila tafakari* |

(Kutoka: *Kichigili*. Msanii: Joel Kimetto

Ili kusisitiza umuhimu wa kujipima kwa mtu ili ajue hali yake ya VVU, msanii hakuwalenga wanaochumbiana peke yao bali wanajamii wengine kama vile watoto, kina mama na kina baba jinsi anavyotaja katika wimbo wake. Umuhimu wa vituo vya huduma za UUH unashadidiwa na matumizi ya takriri neno '*kichigili'*. Neno hili liemerudiwa na kiongozi mara kumi huku waitikiaji wakilirudia mara thelathini na tano.

## 6.6 Hitimisho

Sura hii inahusu VVU/UKIMWI na masuala yanayohusiana na ugonjwa huu kwa njia moja au nyingine. Katika sura hii nimejadili vipengele vitatu muhimu ambavyo vinabainika katika nyimbo nilizozichanganua. Vipengele hivyo ni UKIMWI na suala la jinsia, malalamishi na tahadhari. Sura hii imebainisha kuwa kuenea kwa VVU hakuhusishi jinsia moja ilivyo simulizi kuu miongoni mwa wanajamii bali huchangiwa na watu wa jinsia zote. Aidha, imebainisha kuwa jinsia ya kike bado inasawiriwa kihasi mintaarafu ya masuala ya ngono. Isitoshe, baadhi ya wasanii wameibuka na nyimbo zinazopinga usimulizi mkuu kwamba wanaume ndio wa kuwafuata wanawake kwa ajili ya mapenzi na ngono. Inavyoonekana ni kwamba,

katika muktadha wa kibaada usasa, kitendo hiki kinaweza kutekelezwa na wanawake pia.

Kuhusu malalamishi, wasanii wamesawiri jamii yenye udhaifu na kulalamika kuhusu ubaya wa VVU/UKIMWI, ulevi wa pombe na tamaa. Pamoja na hayo, nimejadili simulizi za tahadhari dhidi ya tabia zinazoweza kuchangia kuenea kwa VVU/UKIMWI. Wasanii wametoa tahadhari dhidi ya ulevi, tamaa, starehe, anasa na ngono bila kinga. Hatimaye wamependekeza njia za kuepukana na maambukizi ya VVU/UKIMWI.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho ya utafiti huu uliochunguza nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI katika muktadha wa kibaada usasa nchini Kenya. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi huku sehemu ya pili ikishughulikia muhtasari kuhusu utafiti. Matokeo ya utafiti yamejadiliwa katika sehemu ya tatu huku mchango wa utafiti ukitolewa katika sehemu ya nne ya sura hii. Katika sehemu ya tano, hitimisho kuhusu utafiti huu imefafanuliwa, nayo sehemu ya sita inashughulikia mapendekezo yanayotokana na utafiti huu.

## 7.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulichanganua simulizi za VVU/UKIMWI zilizomo katika nyimbo kwa kujikita katika muktadha wa kibaadausasa nchini Kenya. Nyimbo zilizohusika ni zile zile zilizoimbwa kwa lugha za Kiswahili, Kikalenjin, Kijaluo na Kimaasai. Sura ya kwanza iliweka msingi wa tasnifu ambapo masuala ya kimsingi yalifafanuliwa. Baadhi ya mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika sura hii ni pamoja na usuli wa utafiti, suala la utafiti, azma ya utafiti, nadharia tete, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Masuala mengine yaliyojadiliwa katika sura hii ya kwanza ni mbinu za utafiti, vifaa vya utafiti na hatimaye uchanganuzi wa data.

Sura ya pili inahusu mapitio ya yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti pamoja na misingi ya kinadharia. Katika sura hii basi, nimepitia na kuhakiki maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Mjadala huu umechukuua mtazamo kuwa, VVU/UKIMWI unaweza kujadiliwa kama simulizi kuu ya kitaifa nchini Kenya. Kwa jinsi hiyo basi, vipengele vilivyojadiliwa katika sura hiyo ni pamoja na hali ya

VVU/UKIMWI nchini Kenya na vipengele vielekezi vinavyochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI nchini Kenya. Aidha, mambo mengine muhimu niliyoyajadili ni athari za VVU/UKIMWI nchini Kenya pamoja na mikakati ya serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na ya watu binafsi dhidi ya VVU/UKIMWI. Mjadala kuhusu mambo hayo manne ulikuwa muhimu kwani ulibainisha kuwa mikakati iliyowekwa dhidi ya VVU/UKIMWI haijafaulu kuliangamiza janga hili na hivyo kuufanya utafiti huu kupata ufaafu wake. Katika sehemu ya mwisho ya sura hiyo ya pili, nimejadili misingi ya nadharia ya Ubaadausasa, nadharia ambayo iliongoza utafiti huu. Katika sura za tatu, nne na tano na sita nilijikita katika uchanganuzi wa data.

Sura ya tatu imebainisha jinsi mikakati ya kibaadausasa inavyobainika katika nyimbo zinazohusiana na VVU/UKIMWI. Katika sura ya nne nilijadili suala la unyanyapaa na kubainisha simulizi ndogo zinazopinga au kukuza unyanyapaa. Katika sura ya tano nilichanganua namna matabaka ya kijamii yanavyochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI huku sura ya tano ikifafanua nafasi ya nyimbo katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI kwa kuangazia masuala kama vile VVU/UKIMWI na jinsia, nyimbo na malalamishi pamoja na simulizi za tahadhari. Katika sura ya sita, nilifafanua nafasi ya nyimbo katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI nchini Kenya kwa kujikita katika vipengele vya kimuktadha kama vile mada, wakati, uteuzi wa istilahi na mazingira katika nyimbo husika. Sura ya saba ndiyo mwisho wa tasnifu hii na imeshughulikia muhtasari, matokeo, mchango, mahitimisho na mapendekezo.

### 7.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu uliohusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI katika muktadha wa kibaadausasa nchini Kenya ulikuwa na matokeo kadha wa kadha. Mathalani, kuhusu nyimbo na simulizi za unyanyapaa, utafiti huu ulibainisha kwamba, nyimbo zinaweza

kutumiwa ama kupinga au kukuza unyanyapaa unaofungamanishwa na VVU/UKIMWI. Utafiti ulibainisha kuwa, ni kupitia kwa nyimbo ambapo waathiriwa wa VVU/UKIMWI wanapata sauti ya kujitetea dhidi ya lawama na unyanyapaa unaoendelezwa na wanajamii wengine dhidi yao. Kwa kufanya hivi, tetezi zao zinakuwa simulizi ndogo ndogo ambazo zinatumiwa na wasanii kupinga simulizi kuu zinazotawala katika jamii.Baadhi ya wasanii wamevuka viwango vya unyanyapaa unaohusishwa na matumizi ya kondomu na kuwahimiza wanajamii wote waitumie kujikinga. Hata hivyo, kuna wasanii wengine hususan wale wanaolenga hadhira za vijana ambao nyimbo zao zinaelekea kutukuza kitendo cha ngono bila kinga. Vile vile, utafiti huu uligundua kwamba, kupitia kwa simulizi ndogo ndogo zilizomo kwenye nyimbo, waathiriwa huwasilisha hisia na matarajio yao hasa kuhusu ngono, mapenzi na maambukizi ya VVU. Pamoja na hayo, utafiti huu uligundua kwamba, katika baadhi ya nyimbo, kuna simulizi ndogo ambazo zinawapa matumaini ya kuendelea kuishi wale walioambukizwa na hivyo kupinga simulizi kuu katika jamii kwamba, kuambukizwa VVU ni hukumu ya kifo. Utafiti huo basi uligundua kwamba, kwa kufanya hivi, wasanii kupitia nyimbo zao huchangia mbinu za kimatibabu za kupiga vita unyanyapaa na VVU/UKIMWI kwa ujumla. Mambo haya yamejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu ya tasnifu hii.

Kuhusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI na suala la matabaka, utafiti huu uligundua ya kwamba wanajamii kutoka kwa matabaka mbalimbali huchangia kwa njia moja au nyingine kuenea kwa VVU. Kupitia kwa nyimbo zilizochanganuliwa, wasanii wamedhihirisha kuwa baadhi ya wanajamii hususa wenye nafasi katika jamii hutumia nafasi hiyo kujipatia mapenzi na ngono, matendo ambayo yanafungamanishwa na VVU/UKIMWI. Kupitia kwa nyimbo zilizochanganuliwa, ilibainika kuwa wanajamii walio na uwezo wa kifedha, mamlaka au cheo hutumia

uwezo huo kukidhiwa haja zao za mapenzi na ngono na wale wasio na uwezo kama huo. Mbali na kutumia uwezo wa kifedha na mamlaka au cheo, utafiti huu ulibainisha kuwa wengine wenye umri mpevu hutumia upevu huo wa kiumri kupata ngono kutoka kwa walio na umri mdogo. Watu wa jinsia zote mbili wanahusika na matumizi haya mabaya ya uwezo. Katika hali kama hizi kuna uwezekano wa watu wa jinsia zote kueneza maambukizi ya VVU hasa ikizingatiwa kwamba, wale wasio na uwezo aghalabu huwa hawana nafasi ya kukata maamuzi kuhusu ni lini, wapi, vipi na nani wa kushiriki ngono nao.

Kuhusu nyimbo na nafasi yake katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI, utafiti huu uligundua kwamba wasanii wanaweza kutunga nyimbo zinazoweza kuwasilisha jumbe za kulenga hadhira mbalimbali za jinsia zote. Aidha, iligunduliwa kwamba nyimbo huwasilisha jumbe na simulizi za malalamishi na za tahadhari juu ya tabia zinazofungamanishwa na VVU/UKIMWI bila pingamizi. Baadhi ya tabia hizo ni kama vile ulevi, ngono bila kinga, tamaa, starehe na anasa. Isitoshe, utafiti huu uligundua kuwa, wasanii kupitia kwa nyimbo zao wanapendekeza njia nyingine za kuepukana na VVU/UKIMWI na kwa jinsi hiyo kuchangia zile njia za kitaalumu kama vile ABC; yaani kutoshiriki ngono, kuwa mwaminifu kwa mpenzi mmoja na kutumia kondomu (KMK).

Hali kadhalika utafiti huu ulibainisha matumizi ya mikakati ya nadharia ya baadausasa. Mikakati hiyo ni pamoja na, ukiukaji, urejelezi, mwingiliano wa matini ukosefu wa mshikamano na kukosekana kwa uaushi katika simulizi zinazotumiwa na vijana kila siku kujadili swala la VVU/UKIMWI.

### 7.4 Mchango wa Utafiti

Tasnifu hii inatoa mchango wa kitaaluma kwa njia mbalimbali. Kwanza, uchunguzi wa simulizi ndogo ndogo na hasa katika kitengo cha fasihi ni muhimu hasa katika kupinga simulizi kuu zilizokita katika jamii kuhusu maambukizi ya VVU kwamba ni hukumu ya kifo. Utafiti basi utawasaidia wanajamii waelewe kuwa, kuambukizwa VVU siyo hukumu ya kifo. Aidha, utawawezesha kuwatambua wanajamii waliotengwa na kunyanyapaaishwa kwa misingi ya VVU/UKIMWI. Hii ni kwa sababu nyimbo zimebainisha kuwa ngono siyo njia ya pekee ambayo kwayo VVU husambazwa.

Zaidi ya hayo, tasnifu hii ni mchango kwa taaluma ya matibabu kwani wasanii kupitia kwa nyimbo zao huwasilisha jumbe zile zile zinazowasilishwa na wataalamu wa matibabu na afya. Wasanii huwasilisha jumbe husika kwa njia rahisi na inayofurahikiwa na wasikilizaji. Hii ni kwa sababu nyimbo huelimisha huku zikiburudisha. Mbali na umuhimu wake katika taaluma ya matibabu na afya, tasnifu hii inatoa mchango kwa taaluma nyingine zikiwemo za muziki, isimu, soshiolojia na sayansi jamii miongoni mwa nyingine.

Mbali na hayo, tasnifu ina umuhimu wa kuongeza idadi ya maandishi ya kitaaluma kuhusu fasihi na VVU/UKIMWI. Pamoja na kuongeza maandishi hasa kuhusu nyimbo na VVU/UKIMWI, tasnifu hii ni kichocheo kwa wataalam wengine kufanya tafiti zaidi katika uwanja wa fasihi simulizi ya kijamii iliyofungamanishwa na VVU/UKIMWI. Yote tisa, ya kumi ni kuwa, kwa jumla utafiti huu ni mchango kwa taaluma nzima ya fasihi simulizi hasa uchaganuzi wa matini simulizi.

### 7.5 Mahitimisho

Mintaarafu ya mijadala na uchanganuzi ulioendelezwa katika tasnifu hii, imebainika kwamba nyimbo zilizokitwa katika muktadha wa kibaadausasa nchini Kenya zinadhihirisha matumizi ya mikakati ya kibaadausasa. Baadhi ya mikakati hiyo ni mwingilianomatini, ukosfu wa mshikamano, ukosefu wa uaushi na kadhalika. Aidha, nyimbo hizi zina simulizi ndogo ndogo na simulizi kuu zinazohusishwa na masuala ya VVU/UKIMWI, ngono, sehemu za siri na matumizi ya kondomu. Utafiti huu ulifafanua jinsi simulizi zinazopinga na au kukuza unyanyapaa zinavyodhihirika katika nyimbo zilizochanganuliwa. Aidha, nyimbo zilidhihirisha kuwa wanajamii wa jinsia zote huchangia kuenea kwa VVU na wala si jinsia moja jinsi ilivyokuwa ilivyokuwa imezoeleka hapo awali.

Utafiti ulidhihirisha kwamba, nyimbo zinaweza kuwa jukwaa ambalo kwalo wanajamii waliotengwa na kunyanyapaaishwa kwa misingi ya VVU/UKIMWI wanaweza kuwasilisha hisia zao. Aidha kupitia mjadala ulioendelezwa katika tasnifu hii, imebainika kwamba wasanii wa nyimbo huteua maneno ya kutumiwa kulingana na muktadha, mada na hadhira za kulengwa. Uteuzi huu ndio unaoziwezesha nyimbo kuwasilisha jumbe nyeti kwa urahisi; jumbe ambazo hazingeweza kuwasilishwa katika muktadha wa mazungumzo ya kawaida.

Pia, ilibainika kwamba matabaka huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU kwa njia moja au nyingine. Matabaka yaliyobainishwa na wasanii ni kama vile tabaka la wanaume au wanawake wenye nafasi katika jamii, watu wanaotumia umri mpevu kushawishi kupata ngono pamoja na watu kama vile viongozi wa kisiasa na kidini ambao awali hawakuwa wanashukiwa katika mchakato mzima wa maambukizi na maenezi ya VVU. Aidha utafiti huu ulieleza jinsi nyimbo zinavyoweza kutumiwa kuwasilisha jumbe za tahadhari sio tu juu VVU/UKIMWI bali pia juu tabia na

visababishi vielekezi kama vile umaskini, ulevi, tamaa, anasa na starehe. Uchanganuzi wa nyimbo zilizoteuliwa ulidhihirisha kuwa tabia hizi, ambazo zinazohusishwa na wanaume na wanawake huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU.

Kwa muhtasari, utafiti huu uliangazia masuala kadhaa. Kwanza, ulibainisha na kujadili baadhi ya mikakati ya kibaadausasa iiliyotumiwa katika nnyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa. Pili, ulifafanua jinsi simulizi ndogo ndogo zinazohusu VVU/UKIMWI zinavyojitokeza katika nyimbo zilizoteuliwa na kuchanganuliwa. Aidha utafiti huu ulidhihirisha namna suala la matabaka linavyofungamanishwa na VVU/UKIMWI. Utafiti huu vile vile ulifafanua mchango wa nyimbo za kibaada usasa katika vita dhidi ya janga la VVU/UKIMWI.

## 7.6 Mapendekezo

Utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo:

Kwanza, ni wazi kuwa nyimbo za Kiswahili, Kikalenjin, Kijaluo na Kimaasai zina simulizi ndogo ndogo zinazohusiana na VVU/UKIMWI. Hivyo basi kuna haja ya kuendeleza utafiti zaidi kwa kujikita katika nyimbo za jamii nyingine za Kenya ili kubainisha simulizi zilizomo na nafasi yake katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI.

Aidha, utafiti huu ulihusu nyimbo na simulizi za VVU/UKIMWI. Kwa kuwa swala la VVU/UKIMWI linajadiliwa katika vipera vingine vya fasihi simulizi, kuna haja ya utafiti zaidi kufanywa ili kubainisha simulizi zilizomo katika vipera vingine kama vile ngano, maigizo, vichekesho, majigambo na kadhalika.

Hatimaye, utafiti zaidi ufanywe kwa kujikita katika nyimbo za kizazi kipya ili kubainisha mchango wake katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI nchini Kenya.

**MAREJELEO**


Agawu, K. (1991). *Playing with Signs: A Semiotic Interpretation of Classic Music.* Princeton: Princeton University Press.

Ahmadi, M. (2005). *Music and HIV/ AIDs communities; perceptions, Implications for Music Therapy*. Pretoria. (Haijachapishwa).

Alfaro, M. J. M. (1996). Intertextuality: Origins and Development of the Concept. *Atlantis 18* (1/2), 268-285.

Allison, E. J. Jr. (2011). Nyimbo za EDZI (Songs About AIDS): Using Music to Combat AIDS and other Public Health Issues in Malawi. Katika g. Barz, G. na J. Cohen.*The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts*. New York; London: Oxford University Press, Inc.

Alviso, R. (2011). Tears Run Dry: Coping with AIDS Through Music in Zimbabwe: Katika Barz,G. na Cohen, J. (whr.). *The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts*. New York ; Oxford : Oxford University Press.

Amuyunzu-Nyamongo, M. (2001). 'HIV/AIDs in Kenya: Moving Beyond Policy Rhetoric. Population Council, East and Sourthern African Regions. Naiorbi: Kenya'. African Sociological Reviews 5(20:68-1020).

Baaz, M. E., & Stern, J. (2009). Why do soldiers Rape? Musculinity, Violence and sexuality in the Armed Forces in the Congo DR *International studeis quarterly 53*(2), 495-518.

Baileyshea, M. (2007).Mignon: A new recipe for analysis and recomposition. *Music Theory Online*. (13), 4.

Barry F. (2002). *Beginning Theory*. London : Manchester University Press.

Barthes, R. in Harari, J. V. (Ed). (1979). Textual Strategies: Perspectives in post-Structuralist criticism. Ithaca: Cornell University Press.

Barthes, S. (1981). *Structuralism and After*. London: Cornell University Press.

Barz, G. (2006). *Singing for Life: HIV/ AIDS and Music in Uganda*. London: Routledge.

Barz, G., & Cohen, J. (whr.). (2011). *The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts*. New York: Oxford: Oxford University Press, Inc.

Baudrallard, J. (2009) The Precession of Simulacra. In J. Storey (Ed.), C*ultural Theory and Popular Culture: A Reader* (4th ed.) (pp. 409-415). Harlow: Pearson.

Bauer, M. W. (2004). *Analysing noise and music as social data: A practical handbook*. London: Sage.

Bressler, C.E. (2007). *Literary Criticism: An Introduction to Theory and Practice*. Pearson Education Ltd. London.

British Broadcasting Corporation (BBC) (2006). 'Kenyan First Lady in AIDS Storm'. London: British Broadcasting Corporation (BBC). Kutembelewa 9/7/2012.

Buren, K. J. V. (2011) Music, HIV/AIDS and Social Change in Nairobi, Kenya: Katika Barz, G. na Cohen, J. (whr.) *The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts*. New York: Oxford: Oxford University Press, Inc.

Butler, J. (1990). *Gender Trouble: Feminism and the Subversion of Identity. Thinking Gender*. New York: Routledge.

Cagnolo, C., Wambugu, H., Ngariga, J. M., & Kariuki, P. M. (2006). *The Agikuyu: Their Customs, Traditions and Folklore.* Nairobi: Wisdom Graphics Place.

Campbell, C. A. (1983). Nyimbo za Kiswahili: A Socio-Ethno Musicological Study of Swahili Poetic Form. New York: Washington Press.

Campbell, C., Nair, Y., & Maimane, S. (2006). AIDS Stigma, Sexual Moralities and the Policing of Women and Youth in South Africa. *Feminist Review*, (83), 132-138. Retrieved from http://www.jstor.org/stable/3874387

Carter, A. (2006). *New Critical Readings*.London: Bloomsburg.

Cheryl, D.(2008). Reclaiming Our Lives: HIV and AIDS, Women's Land and Property Rights and Livelihoods in southern and East Africa – Narratives and Responses. *Feminist Economics*,*14*(4),213-216,DOI: 10.1080/13545700802262964.

Coakley, J. (2009). Katika E. A. Roper (mhr.) (2013). Gender Relations in Sport. Rotterdam: Sense Publishers.

Comrie, B. (1981). *Language Universals and Linguistic Typology: Syntax and Morphology*. Oxford: Blackwell.

Covach, J. (1999). Popular Music, Unpopular Musicology. Katika N.Cook & M. Everist(whr.), *Rethinking Music*(190-210). Oxford: Oxford University Press.

Deleuze, G., & Guattari, F. (2007). *A Thousand Plateaus.* Katika J. Rivkin & M.

Deveau, C., Levine B., & Beckerleg, S. (2006). Heroin use in Kenya and Findings from a Community-Based Outreach Programme to Reduce the Spread of HIV/AIDS. *African Journal of Drug and Alcohol Studies 5*(2), 95-106.

Dunbar-Hall, P. (1991). Semiotics as Method for Study of Popular Music. *International Review of Aesthetics and Sociology of Music22*(2), 127-132.

Eller-Isaacs, J. (2011). Singingin the Shadow of Death: African Musicians Respond to A Pandemic with Songs of Sorrow, Resistance, Advocacy and Hope. Katika G. Barz,&J. Cohen,(whr.),*The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts* (pages). New York: Oxford University Press.

Ewens, G. (2006). Heart of Danceness: The Music of Zaire. Katika Broughton, S., Ellingham, M., & Trillo, R. (whr.),*World Music: The Rough Guide. Africa, Europe and the Middle East* (77-102). London: Rough Guides.

Fairclough N. L. (1992). Discourse and Text: Linguistic and Intertextual Analysis within Discourse Analysis. Katika: *Discourse and Society3*, 193-217

Fay, B. (1971). *Life is people.* Nothingbuthopeandpassion.com. Rejelewa 16/9/2013

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press.

Foucault, M. (1970). *The Order of Things*. New York City: Pantheon Books.

Foucault, M. (2000). Archeology of Knowledge. Katika Rivkin, J. na Ryan, M. (whr) *Literary Theory: An Anthology* (2000: 477). New Jersey: Blackwell Publishers.

Frith, S., & Goodwin, A. (1990). From Subcultural to Cultural Studies. Katika S. Frith, & A. Goodwin,(whr.),*On Record: Rock, Pop and the Written Word*(92-117).New York: Pantheon Books.

Gakahu, N. (2010). The Role of Broadcast Media in behavior change and HIV/AIDS communication to the youth: A focus on Kenya's Musi Industry. *Journal of Media and Communication Studies,2(7)*,154-158. Retrieved from *http://www.academicjournals.org/jmcs.*

Garfias, A. (2004). Music: The Cultural Context – UCI School of Social Sciences. Retrieved from http://www.socscie.uci.edu>ser47_chap_01_02.

Garth, A. (2004). *Hip Hops Hostile Gospel: Postsoul theological exploration*. New York: New York University Press.

Goffman, E. (1963/1974).*Frame Analysis: An Essay on the Organization of Experience*. New York: Hamper and Row.

Halliday, M. A. K (2003). *A study of the Effects of intertextuality Awareness on reading Literary texts*.

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary* ($17^{th}$ ed.). New York: Oxford University Press.http://news.bbc.co.uk/2/hi/africa/4997336.stm.

Hymes, D. (1974). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic approach.* Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

IMF (2007). *Poverty Reduction Strategy Paper*. Washington: International Monetary Fund.

Jameson, F. (1991). *Postmodernism, or the cultural logic of late Capitalism*. Durham, NC Duke University Press.

Joint United Nations Programme on HIV/AIDS.(2004).*Report on the Global AIDS Epidemic: Fourth Global Report.* Geneva: United Nations Programme on HIV/AIDS (UNAIDS). Retrieved from http://www.unaids.org/bangkok2004/GAR2004-pdf/UNAIDSGlobalReport2004-en.pdf

Kenya National HIV and AIDS Strategic Plan ( 2009/10-12/13 ). *Delivering on universal access to services.* Nairobi: National AIDS Control Council (NACC).

Khamisi, A. (2005).*Transgression in Swahili Narrative and its Reception*. Berlin: LIT. Verlag.

King'ei, K., & Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Klages,M. (2003). Modernism and Beyond. <http://www.colorado.edu/english/courses/ENG2012 WAGE/POMO.

Kobia, J. (2008). Metaphors on HIV/AIDS Discourse Among Oluluyia Speakers of Western Kenya. *Critical Approaches to Discourse Analysis across Disciplines, 2* (2), 48-66.

Korir, J. (2013). *Appropriation of Kalenjin Idiom in Selected Songs of Joel Kimetto*(Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Kurth, E., & Rothfarb, L. A. (1991). *Selected Writings*. Cambridge: Cambridge University Press.

Langley, S. (1979). *The Nandi of Kenya: Life Crisis Rituals in a Period of Change*. New York: St Martin's Press.

LaRue, J. (1970). *Guidelines for Style Analysis*. New York: W. W. Norton.

Lerdahl, F. (1992). Cognitive constraints on compositional systems. *Contemporary music review, 6*(2), 97-121.

M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni.*Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Manuel, P., Bibly, K., & Largey, M. (1995). *Carribean currents: Carribean Music from Rumba to Reggae.* Philadelphia: Temple University Press.

Matei, (2011). *Misingi ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari na Vyuo.* Nairobi: Oxford University Press.

Matengu, B. (2005). *The Importance of STI Treatment in HIV Prevention: Knowledge and Behaviours of Secondary School Students in Tsumeb, Namibia* (Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa).University of Western Cape, Cape Town, South Africa.

Matteru, M. L. (1987). "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi". Mulika na19. Dar-es-Salaam.TUKI.

Mboya, M. (2005). Linguistic and Attitudinal Obstacles The Deaf People in Accessing HIV/AIDS Information in African Countries: The Case of Tanzania. Katika*: Report on HIV/AIDS Sensitization Workshop for the Deaf Population in Africa. The First Continental-Wide HIV/AIDS Sensitization Workshop for The Deaf Population in Africa*.

Middleton, R. (1990). *Studying Popular Music*. *Milton Keynes*. Philadelphia: Open University Press.

Ministry of Health. (2001). *AIDS in Kenya: Background, Projection, Impact, Interventions and Policy*. (6th edition). Nairobi: Ministry of Health. Retrieved from http://www.nacc.org.ke/downloads/AIDS-in-Kenya.pdf.

Molino, J. (1975). *Music theory musicololgy*. Indianapolis: Indiana University Press.

Morgan, D. (2001). *Postmordernism and Arts*. London: Routledge publishers.

Mukasa, F. N. (2005). *Uganda National Association of the Deaf Struggle to Fight HIV/AIDS Amongst The Deaf People*. Katika: Report on HIV/AIDS Sensitization Workshop for the Deaf Population in Africa. The First Continental-Wide HIV/AIDS Sensitization Workshop for The Deaf Population in Africa.

Mutembei, A. K. (2009). UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili.1982 – 2006. *Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

National AIDS and STI Control Programme. (2013). *Kenya AIDS Indicator Survey 2012 Preliminary Report*. Nairobi: NACC.

National AIDS and STI Control Progrmme. (2007). Kenya AIDS Indicator Survey 2007 Report. Nairobi: NACC.

National AIDS Control Council(1999). Nairobi: NACC. Rejelewa13/5/2012.

National AIDS Control Council NACC (2000). *National HIV/ AIDs strategic plan 2000- 2005*. Nairobi: NACC.

National AIDS Control Council. (2005). *Kenya HIV/ AIDS Data Booklet*. Nairobi: NACC.

National AIDS Control, Office of the President, Kenya. (2006). *United Nations General Assembly Special Session on HIV and AIDS ( UNGASS) 2006 Country Report for Kenya*. Nairobi: NACC.

National AIDS Control, Office of the President, Kenya. (2008). *United Nations General Assembly Special Session on HIV and AIDS ( UNGASS) 2006 Country Report for Kenya*. Nairobi: NACC.

Nattiez, J. (1990). *Music and Discourse: Towards a Semiology of Music*. Seattle: University of Washington Press.

Needle, R. H. na wenzake (2006). Substance Abuse and HIV in Sub-Saharan Africa: Introduction to the Special Issue. *African Journal of Drug and Alcohol Studies*, *5*(2), 83-94.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K., & Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (2003). *Culture, Entertainment and Health Promotion in Africa.* Nairobi. Twaweza Publications.

Ntarangwi, (2001). A Socio-Historical and Contextual Analysis of Popular Musical Performance among the Swahili of Mombasa, Kenya. *Cultural Analysis*, *2*, 1-37.

Nyandiba, C. (2013). *Uchanganuzi wa Mikakati ya Kiisimu ya Mawasiliano katika Diskosi za VVU/UKIMWI miongoni mwa AbaGusii*(Tasnifu ya Uzamifu haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya.

Nyawira, P. M. (2008). *Music as Social Discourse. The Role of Popular Music in the Fight Against HIV/AIDs among Youth in Nairobi*. (Haijachapishwa).

Ogechi, N. O. (2005). The Language of sex and HIV/AIDS among University students in Kenya. *Stichproben Wiener Zeitschrift fur Kritische Afrikastudien Nr. 9/2005, 5 (Jg), 23-49*.

Onyango, J. O. (2007). Discursive Masculinities and the War against AIDS: Kenyan Experience. *Commission for Development for Studies at the Austrian Academy of Sciences* (KEF). Retrieved from http:// www.oeaw.ac.at/kef.

Paterson, D. (2006). Until Morning:The Life and Times of Kenyan Pop. Katika S. Broughton, M.E Ellingham and D. Muddyman (whr.), *World Music: The Rough Guide. Africa, Europe and the Middle East*(337-348).London: Rough Guides.

Rafiq M.Y. (2008). *'' Ni full ile laana'' (It's as rael as it gets): The creative blending of Hip-Hop with Oratory styles to address HIV/AIDS in Tanzania.* http:www.youthmediareporter.org/2008/06. Rejelewa 14/5/2011.

Rieti, R. (1961). *The Thematic Process in Music*. London: Faber & Faber.

Rivkin, J., & Ryan, M. (whr) (2000). *Literary Theory: An Anthology*. Hoboken,NJ:Wiley-Blackwell Publishers.

Roper, E. A. (2013). *Gender Relations in Sport*. Rotterdam: Sense Publishers.

Rotich, A. K. (2009). *Nyimbo za Watoto wa Shule za Chekechea na za Msingi katika Manispaa ya Bomet: Uchunguzi wa Kiuamilifu*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Moi.

Ruud, E. (1998). *Music Therapy: Improvisation, Communication and Culture*. Gilsum, NH: Barcelona Publishers.

Sambai, C. S. (2014). *Framing HIV/AIDS and Sexuality in Television Dramas in Kenya: A Reading of Makutano Junction and Siri.*Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Moi.

Selden, R.,Widdowson, P. & Brooker, P. (2005). *A reader's Guide to Contempoorary Literary Theory* (5th Edition). Harlow, England; New York: Pearson Longman.

Shitemi, N.L. (2002). Rethinking and Mainstreaming African Literature in the Academia, *Journal of Literary Studies, 28(*2), 20-36.

Simandan, V. M. (2010, December 29). *Julia Kristeva's concepts of intertextuality* [Blog post]. Retrieved from http://www.simandan.com/blog/

Sobania, N. (2003). Katika P. Nyawira (2008). *Culture and Customs of Kenya*. London: Greenwood Press.

Stein, J. (2010). HIV/AIDS Stigma: The Latest Dirty Secret. *African Journal of AIDS Research 2(2), 95-101.*

Syambo, B., & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Tagg, P. (2000). 'Analysing Popular Music: Theory, Method and Practice'. Katika Middleton, R. (mhr.): *Reading Pop: Approaches to Textual Analysis in Popular Music.* New York: Oxford University Press.

Taruskin, R. (1982). 'On letting the Music Speak for Itself: Some Reflections on Musicology and Performance'. The Journal of Musicology 1(3): 338-349.

Thonya, L. M. (1978). *Misingi ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam : Black Star Agencies.

Tovey, D. F. (1982. Essays in Musical Analysis. London: Oxford University Press.

Tufte, T. (mhr). (2002). Edutainment in HIV/AIDS Prevention: Building on the Soul City Experience in South Africa. Paris: UNESCO.

TUKI, (2010). *English – Swahili Dictionary*.Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Tyson, N. G. (2006). *Critical theory today: A User- Friendly Guide*: New York: Routledge.

Umberto, E. (1979). *A Theory of Semiotics*. Bloomington: Indiana University Press.

Umeh, D. C. (mhr.) (1997). *Confronting the AIDS Epidemic: Cross-Cultural Perspectiveson HIV/AIDS Education*. Africa World Press,Inc

United Nations Educational Scientific and Cultural Organization (UNESCO)(2008). *Culture,HIV and AIDS-Arts and Creativity*. Retrieved on 12/6/2011 from http://unesdoc.unesco.org/images/0019/001931/193118e.pdf

Walibora, K. (2010). Postmodernism as seen through the Swahili novel: A Reading of Babu Alipofufuka and Dunia Yao. *Journal of African Cultural Studies* (27).

Wamitila K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istalahi na Nadharia.*Nairobi: Focus Publications.

Wamitila K.W. (2008). Point of View in Kiswahili. Narrative fiction: Reading of Shafi Adam Shafi's Vuta N'kuvute *Kiswahili.* 71:84-97. https://www.ajol.info/index.php/ksh/article/view/79021

Wamitila K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fsihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wanyama, M., & Okong'o, J.B. (2011). Confronting AIDS Through Popular Music Cultures in Kenya: A Study of Princess Jully's "Dunia Mbaya", Jack Nyadundo's "UKIMWI" and Oduor Odhialo's "Nyakomollo". Katika Barz, G & Cohen J. M. (whr) *The Culture of AIDS in Africa: Hope and Healing through Music and the Arts*. New York; Oxford : Oxford University Press. .

Wegesa, B., & Macharia, S.N.(2008). Postmodernism or Chaos? Theoretical considerations in reading new directions in some cultural practices in Kenya katika N.O Ogechi (whr) (2008). *Nadharia Katika Taaluma Ya Kiswahili na Lugha Za Kiafrika*.Eldoret: Moi University Press.

Wenje, P., Nyambedha, E., & Muhoma, C. (2011). 'Wende Luo' (Luo Songs) as an intervention tool in the fight against HIV/AIDS among the Luo of Western Kenya. *Journal of AIDS and HIV Research Vol. 3*(8),pp.151-160*http://www.academicjournals.org/jahr*Rejelewa 14/7/2014

Worfreys, J., Robbins, R., & Wamack, K.(2006). Key Concepts in Literary Theory. Edinburgh: Edinburgh University Press

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Mwongozo wa Mijadala katika Makundi Teule

1. Kujitambulisha kwa mtafiti na wanakikundi teule
2. Kufafanua sababu za utafiti kwa kusisitiza umuhimu wa maoni yao kama watazamaji/wasikilizaji na umuhimu wa kujadili waliyoyaona/waliyoyasikia bila uoga
3. Ufafanuzi wa utaratibu wa mjadala, kwamba ni kutazama/kusiliza wimbo ukichezwa kwanza kisha kutoa maoni mintaarafu ya simulizi za VVU/UKIMWI, ngono, sehemu za siri na kadhalika
4. Kipindi cha dakika 15 cha kutazama/kusikiliza wimbo husika
5. Mjadala baada ya kutazama/kusikiliza wimbo ambapo masuala huibuliwa na kujadiliwa kila mshiriki akitoa maoni yake kwa zamu
6. Kutamatisha kwa kuwashukuru wanakikundi kwa kushiriki katika mjadala na kutoa mchango wao wa maoni

**Kiambatisho cha 2: Kidadisi cha maswali kwa Hadhira**

1. Jinsia yako ☐ Mume ☐ Mke
2. Umri wako ☐ 18 – 30 ☐ 30 – 40 ☐ Zaidi ya 40
3. Kiwango chako cha elimu
4. Wataje wasanii wanaoimba nyimbo zinazohusu UKIMWI kwa Kiswahili au kwa lugha yako ya mama

   ____________________________________________

   ____________________________________________

5. Kati ya wasanii uliowataja, ni wepi wanaoshughulikia suala la UKIMWI ipasavyo?

   ____________________________________________

   ____________________________________________

6. Kwa maoni yako, faida za nyimbo za UKIMWI ni zipi? Orodhesha angalau tano.

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   ____________________________________________

**Kiambatisho cha 3. Wasanii na Nyimbo**

| | **Msanii/Wasanii** | **Nyimbo** |
|---|---|---|
| 1 | Joel Kimeto | Kichigili |
| 2 | Joel Kimeto | Rat Torosta |
| 3 | Daniel Kurui | Mi Meet Tereet |
| 4 | Israel Alphine Rono | Yee Beek che mii Tereeng'ung |
| 5 | Ajoji Dume | Tang'ne Dendi |
| 6 | Chali | Miluma |
| 7 | Musa Juma | Mayaka |
| 8 | Atomi Sifa | UKIMWI Onego Jater |
| 9 | Daniel Ole Senei | Etumuta Biitia |
| 10 | Daniel Saning'o | Enkotoroki |
| 11 | Jua Cali & Pilipili | Kamata Dame |
| 12 | P-Unit | Si Lazima |
| 13 | Circute na Jo-el | Juala |
| 14 | Uncle Ckoniah | Merimela |
| 15 | Mchafuzi & Elyen | List ya mazishi |
| 16 | Abdikadir Ibrahim | Nyambizi |
| 17 | Wakimbizi | Nampenda John |
| 18 | Faddy Daddy | Nimeupata Vipi? |
| 19 | Ratali Alias Kibunja | Ajali Kitandani |
| 20 | Nonini & Jua Cali | Wee Kamu |
| 21 | Princess Jully | Dunia Mbaya |
| 22 | Ferooz & Profesa Jay | Starehe |
| 23 | Longombas | Vuta Pumz |

## Kiambatisho cha 4: Nyimbo za Kiswahili

## MERIMELA – UNCLE CKONIAH

Merimela kipenzi rafiki wa karibu tangu hapo zamani ee
Tulipoanza shule nasi tukiwa watoto ulikuwa mpole
Tena mwenye adabu msichana mrembo kila mara mshindi
Sifa nazo urembo zikaenea kote ukipita ni whispers

Kwa darasa la saba kipenzi Merimela ukaanza geuka
Machali mbalimbali hata nao walimu wakakufanya quencher
Nawe ukakubali ingilia mapenzi ya kiholela holela
Na ukawachukia walokuwa karibu wakikupa ushauri ee

Nami nikakuonya, chunga sana maisha
Nawe kashauriwa (Mela) badilisha mwenendo (oh)
Nawe ukapuuza (kwamba) waenjoy maisha
Tena ukakataa (Mela) unavuja mifupa

Ukakosa bahati mrembo Merimela ukakwachua mimba
Ukazunguka kote  ukitaka mawaidha juu ya mimba mpenzi
Nawe ukadanganywa toa kitu kidogo ukafanye abortion
Bila kushauriwa njia gani salama ya kujilinda mrembo

Kaambiwa uchilli, uksema ni ndoto
Utumie mipira, ukasema si tamu
Basi panga uzazi, uksema ni hectic
Heri pata wokovu, kakataa ni mapema
Kaambiwa uchilli, (chill please), kakataa ni ndoto (that’s a dream)
Utumie mipra, (hush) ukasema si tamu (haina ladha)
Basi panga uzazi, ukasema ni hectic (vipi?)
Heri pata wokovu, kakataa ni mapema (mambo bado wokovu bado)

Kwa shule ya upili mwendo ni ule ule mapenzi kiholela
Kila mwaka ni mimba kila mwaka abortion ikakuwa mtindo
Hata chuo kikuu raha ikapanda vunja vunja mifupa
Wadosi na fukara ukaonja Merimela na mimba ni kawaida

Ukakuwa ni dustbin, ya kutupa takataka
ATM machine (Aii), kila kadi yaingia
Ukakuwa daladala, kila mtu akupanda (kila mtu)

Bado ninakumbuka siku ulonialika kwa harusi Merimela
Ukanielezea umekwisha hitimu na umepata mchumba
Kama rafiki yako kanisisitizia nisikose kufika
Kazi umeshapata na mshahara unapata itakuwa sherehe
Mimi kama rafiki (Mela) nilifika kwa mapema (saana)
Ilikuwa ni sherehe (kubwa) na vivijo na nderemo
Ilikuwa ni maombi (Halleluya) na zawadi tele tele (ooh)
Kila uso ni furaha (hahaha), siku hiyo ya harusi
Sasa miaka mitano imepita Merimela hujapata mtoto
Kila siku kelele, kati yako na bwana anataka mtoto
Hata wakwe zako wanapiga kelele wanataka mtoto
Furaha imekwisha imebaki huzuni kila siku mawazo (na majuto)

Kwa waganga umeenda, hujapta mtoto
Kwa maombi umeenda, hujapata mtoto
Dakitari akasema, beba mimba huwezi (mfuko umeharibika)
Na machungu ya machungu (Aii Mela), umepatwa na virusi (Mela mama)
"Kama ungejua tu ungetahadhari mapema, lakini usilie bado una nafasi"
Usilie, usilie (Mela mama)
Usilie Merimela (Mela mama) usilie (Mela mama)
Usilie (Mela mama) usilie (Mela mama)
Usilie mwana mama uslie (Mela mama)
Una nafasi ya kuishi (Mela mama), usilie (Mela mama)
Fanya tizi (Mela mama), kula vizuri (Mela mama)
Meza madawa (Mela mama), tuliza roho (Mela mama)
"This is a dedication to all university students from Arusha, Kampala mpaka Nairobi Kenya hata Maseno kwetu. Haya warembo tahadharini, ladha ya ndoa ni mtoto na ukianza kutoatoa utalia baadaye".

**NIMEUPATA VIPI? – Faddy Daddy.**
Huuh nalia, uuh uuh uuh
Kila napokaa, nawaza nitazame Faddy
Nilivyokonda majibu niliyopewa yanitisha
Yanachosha kabisa
Faddy Daddy nimepimwa
Nimeambiwa kwamba nimeathirika
Wakati ngono sijawahi kufanya
Mi naumia
Mi nalia
Mi nawaza
Mimi nafikiria
Wapi UKIMWI nimeupata?
Ama kwa matanga nilipoongezewa damu?
Ama kwenye saloni kwenye kunyoa?

Kila siku Faddy mi fikiria
Wazazi wangu mi ntawaeleza nini
Wakati wanajua mi niko nasoma
Kwa kile walichonituma
Kila wakati nakaa, nawaza,najiuliza Faddy
Mimi nitasema kwamba nimepimwa
Nimeambiwa kuwa virusi ninavyo

Moyoni naumia, nachanganyikiwa
Ni vipi UKIMWI umenipata
Wakati zinaa sijawahi fanya
Maswali mengi najiulizaa
Mi naomba msijenitenga
Kwa sababu nimeathirika
Skupata ngoma sababu ya zinaa.

Wadogo ndugu zangu wananiuliza
Mbona Faddy Daddy unazidi konda?
Mwili mzima upele umejaa
Kila wakati unashika tama
Kama hivyo twende zetu Tanga

Nikifikiria mama, nalia
Nikifikiria baba, nalia
Nikifikiria ndugu zangu nawapenda sana.

Baba na mama wamenisomesha kwa shida
Kutoka msingi hadi chuo naingia

Mimi ndio mtoto wanaotegemea
Lakini ndoto zangu nimezizuia
Najiuliza UKIMWI nimeupata vipi?
Wakati Faddy sikushiriki kwa uasherati

Ndoto zangu zishapotea
Kusoma sitasoma tena
Dunia imenitenga mimi.
Moyoni naumia nachanganyikiwa
Ni vipi UKIMWI nimeupata?
Wakati zinaa sijawahi fanya
Maswali mengi najiuliza
Mi naomba msijenitenga
Kwa sababu nimeathirika
Sikupata ngoma sababu ya zinaa.

**SI LAZIMA – P-Unit.**

Aahh ha ha ha ha
Isss Nonini…..Yeah aha ah….
Introducing….Bonnies N Frasha na Gabu
Jessie on this
Si Lazima…..eeh….eeh….Si Lazima

Si lazima tu do
Tunaeza enda home na tuchill tu doo
Si lazima tu do, si lazima tu doo
Tunaeza enda home na tuchill tu
Si lazima tu do….
Tunaeza enda home na tuchill tu aahh

Ooh si lazima tu do
Tunaweza kuenda kwanza kejani
Tuende baby tupate majani
Leo hakuna cha kukaanga ndani
Si eti kila saa ni kukuundress
Si eti kila saa ni kukuundress

Si eti kila saa ni mambo ya sex
Si lazima oh ah si lazima
Najua baby unataka
Pia ni matime huaga nataka
Lakini leo manze sijisikii
Ha mi manze kichwa kinaniuma
Tumbo pia naskia ikikokota
Na kuna vyenye naskia kukuokotaa….

Aah….ati naskia ku kuokota
Ngoja ngoja ngoja kwanza nivue hii mbuta
Si lazima tu doo
Tunaeza enda kejani tukachill tuu
Na huku nzi najidoo kwa kona

Nikikudhiki tu
Ka sijisikii jo tunaeza bonga
Wanasemanga mind ndio afradisiae ya kutosha
Nikiangalia trao tu hivi nimetokwa
Tuko story yako wet ushavua ngotha
Man takuwaje jo story zikikatika
Hii movie tunacheki manze ikiisha
Nataka kugusa lakini jo sitaki
Nataka kulala jo huku ushanivua shati
Temptation kibao jo sina bahati.

**JUALA – CIRCUTE NA JO-EL.**

Let me see those hands, me see those hands
Let me see those hands let me see em Cmon
Yeah, Calif Records,Circute and Jo-el
Bursting up your glass
Bringing breaking news…..
**(Chorus )**
Manyake …all sizes
Manyake….kama prizes
Manyake…kaa balloon zina maji
Juala ndo waitaji
Ok, alright, tuongee juu ya Manyake,
Za mchik msawa not za mnyanye
Akipita mbele ya wasee, this is what the
kerende will say:
“Does she have manyarere, does she
does she manyarere?
Mikono juu if she has manyake
Piga nduru if she has manyarere
Kwanza, tutumie protection to avoid the
disease infection injection,
African men wako obsessed, possessed,
dipressed na manyake,
But pause, wazup niki?
Do you have some Juala? Do you have some
Juala?
Ama uta end up ukicheki ceiling ya mortuary,
kaa fala! Ati nini? Kaa fala!
Tumia protection joo

Juala ni ashuu tu
Na bado mnacheza na maisha mandugu,
Hata kama nyarere ni poa aje
Juala ndio wahitaji
Yeeah cheki hizi facts na hizi figures,
Wasee soh tano wanadie daily
Its like wanabondwa na madinga

Ati you want it bila protection?
Are you agrave-digger?
Ah! Ah! Nyoya finga we mjinga,
Bila protection, na ringa
(Usichape hizo vitu bila juala wacheni story za Manyake)

Eeh! Naongea kuhusu manyake na si zile za butcha,
Manyake zikipita mtu anakula kucha,
Si unajua zile zime fura?
Kama zako hazijafura enda ukule mutura alafu
Ungojee. Pengine watu watakupiga kura

Manyake loh! Mtu anaeza ziworship
Manyake. Zinafanya mtu aloose friendship.
Ebu enda club watu wanafight kwa nini?
Watu wanajaribu kuimpress akina nani?
Pastor alikosana na wife kwa sababu ya nini?
Lakini usichanganywe akili kwa sababu ya mwili
Tumia Juala ama uta haribu mwili.
Eeh! Tumia Juala ama utaharibu mwili.
Hiyo ndio ukweli joh!

**VUTA PUMZ – LONGOMBAS.**

**Chorus**
Hee-haa, vuta pumz
We vuta pumz
Longombas wanafanya mambo (vuta pumz)
Longombas wanatetemesha (vuta pumz)

**Verse 1**
Jamani nisikilizeni, mnisikilize
Jamani nisikilizeni, mnisikilize
Kuna wanwake warembo
Wenye marasa, na mapaja, na weupe
Na ni wazuri kinyama
Jamani nisikilizeni, mnisikilize
Jamani nisikilizeni, mnisikilize
Kuna wanaume wengi
Wenye vifua, na warefu, na wenye nguvu
Na ni wazuri kinyama
Lakini tujichunge
Pengine wanao mdudu
Wantuacha, wana-go
Wanatuacha wana-go
Chorus
Hee-haa, vuta pumz
We vuta pumz
Hee-haa, vuta pumz
We vuta pumz

Usimwone amejaza nyuma, ukadhani ako poa
Usimwone amerembeka, ukadhani umefika

Usimwone ana pesa, ukadhani umefika
Pengine anatuacha, kesho anachora
Usimwone amejaza nyuma, ukadhani ako poa
Usimwone amerembeka, ukadhani umefika
Usimwone ana pesa, ukadhani umefika
Pengine anatuacha, kesho anachora

**Verse 2**
Na kama unayo, si mwisho ya maisha
Ni ugonjwa tu kama malaria
Meza dawa, piga tizi, kula vizuri, utaishi fiti
Maisha utayasukuma
Maisha utayasukuma

Na mijinga usiyojua kujichunga
Kila shimo unaona unadunga
Hebu jichunge kijana utakuja kufa
Tukuzike Langata
Paja asione tu, ashainua
Kifua kisipite tu, ashajigonga
Tako lisipite tu, mate yashamtoka
Tako lisipite tu, mate yashamtoka

Chorus
Hee-haa, vuta pumz
We vuta pumz
Hee-haa, vuta pumz

Ayi ndendende…
Usimwone amejaza nyma, ukadhani ako poa
Usimwone amerembeka, ukadhani umefika
Usimwone ana pesa, ukadhani umefika
Pengine anatuacha, kesho anachora
Kesho anachora

**STAREHE-Ferooz & Profesa Jay**

**Ferooz**

Sasa hapa mimi nipo kitandani
Starehe zimeniweka mashakani/matatani
Starehe nilizifanyia papara
Kupona tena mimi haiwezekani
Jamani buriani

**Chorus**
Kwaherini, kwaherini, kwaherini
Masela wangu ndugu zangu wote wa gheto buriani
Kwaherini kwaherini kwaheini Nagongo na Jitauni kwaherini
Watanzania kwaherini,sasa naaga

**Ferooz**
Starehe nilizifanyia papara
Nilibadili mademu kama vidaladala
Nikienda hili nikirudi lile

Saa saba juu ya alama saa nikitazama
Nimeshaachana na Jacky
Sasa napata Salama
saa kumi na mbili nina appointment na madame wawili
Achana na Lily, tutakutana saa mbili.
Nikaja kubadili wasichana nilikubuni,
kutembea na maate wa ghetto na masistado
Ubaya kwamba condom sikuitambua
Kwa kujua kwamba ladha ya mapenzi itapungua
Kumbe nilikuwa ninapotea njia,
Nlioshauriwa mi nikapuuzia.
Idadi ya wanawake ikawa lukuki
Kupita kipindi wengine nikawa siwakumbuki,
Ona sasa haya nolisibu
Kwa dadake Bashir nishamsahau mkutana kimwili
Nilitaka starehe zote nizitawale
Ona sasa hata kumkumbuka Mola wangu ilikuwa ndoto
Kumbe nilikuwa nakimbilia moto
Sasa najuta mwenzenu
Ibilisi amefanikiwa kunivuta
Sasa sijui wa kumlaumu nani
Kati ya nafsi yangu ama shetani.

**Profesa Jay**
Kijana vipi mbona hujagonga mlango?
Jipange kwenye foleni
Mmoja mmoja ndio mpango
Ondoa mashaka tiba bora haihitaji haraka
Subiri watibiwe wenzakonawe utafuata.

**Ferooz**
Dokta nimekuja kufanya hitimisho
Naamini hii ndiyo mara yangu ya mwisho
Dalili zinaonyesha nimeathirika
Na nimekuja pima ili nipate uhakika

Dokta cheki nilivyokonda
Mwili umetapakaa vidonda
Kukohoa, kutapika
mara sitini na mbili kwa wiki
Ona hata nywele zilivyonyonyoka
Hii yote dalili zote za umeme

**Profesa Jay**
Usikate tamaa
Unaweza ukakonda, kwa Typhoid au TB
Ni kweli vipimo vinaonyesha umeathirika
Starehe mnazipenda, ila mwisho wake mbaya
Wengi wameteketea, kwa kuendekeza umalaya
Kula vizuri, fanya mazoezi pumzisha mwili wako
Ukizingatia hayo, utaishi kwa matumaini
Sasa jaribu, muda bado unao.

**NAMPENDA JOHN – Wakimbizi.**

**Verse 1(Mariko)**
Mimi ni Dokta Mark kutoka kwa wakoloni
minashangazwa sana huu jamaa anaitwa Johnny
ametenda madhara na washikaji hawaoni
bado wanafurahia Johnny kumtia machoni
ameongeza idadi kibao tu ya magonjwa
na bado wanamsifu eti Johnny ni mtu poa
aajaribu kujiuliza maswali sipati jibu
mbona humpendi mchana wanampenda tu usiku
Johnny, Johnny kweli wee ni mpita njia
